
# Maazimio ya Kozi ya Omega

**Nyenzo ya Kusaidia**

## Kituo cha Mafunzo kwa Wapanda Kanisa

Imetolewa na Jerry C. Wofford, Ph.D.




# Jinsi ya Kutumia Maazimio ya Wakufunzi

Kozi ya Omega inatoa yaliyo bora ya kuridhisha zaidi kwa kufunza wapanda kanisa na kuwaongoza katika utaratibu wa upandaji kanisa. Kwa kumaliza Mwongozo wa Tatu, kila mwanafunzi mpanda kanisa anatakiwa awe na kanisa mpya lililopandwa kwa kujifunza nyenzo ya somo na kufanya utekelezaji wa azimio mwishoni mwa masomo. Unapotumia kiongozi cha wakufunzi, Miongozo ya Kozi ya Omega inasaidia kama mwongozo wa kuelekezea. Kiongozi cha wakufunzi kimeandaliwa kusisitiza mwingiliano na njia za kufanya warsha kwenye maelekezo ambayo ni ya lazima kwenye kupata matumizi yenye mafanikio ya nyenzo. Kozi ya Omega lazima itumike. Kwa kifupi lazima itumike kama chombo cha kufundishia na kuelekezea katika upandaji hasa wa makanisa mapya ili kuwa ya thamani katika kufatilia Utume Mkuu.

Yaliyomo katika somo kwa wafunzwa yanatakiwa yawe sawa kama hayo ya Kozi ya Omega iwezekanavyo. Kiongozi hiki kinajitwalia kuwa wanafunzi wapanda kanisa hawatakuwa na Kozi ya Omega kuwepo kusomwa. Mara nyingi hili linatokea wakati wanafunzi wanapokuwa wanaweza kusoma tu lugha ambayo Kozi ya Omega inakuwa haijatafasiliwa. Hakika, wakufunzi wanatakiwa wawe wanaweza kusoma Kozi ya Omega ili kujiandaa kwa ajili ya mafunzo. (Viongozi hivi vya Wakufunzi vinaweza pia vikatumika kuwasaidia wakufunzi wa madarasa ambayo wanafunzi wanakuwa na miongozo ya Kozi ya Omega.) Madarasa yanatakiwa yawe madogo, yasiozidi watu thelathini. Kwa darsasa la watu 10 au zaidi, vikundi vidogo vinatakiwa vitumike kwenye majadiliano. Baada ya majadiliano haya, waulize wajumbe wote wa makundi madogo kusema baadhi ya mawazo yaliyoelezewa kwenye majadiliano yao. Kama wanafunzi wanapokea maazimio haya ya mafunzo, wakati majibu yanapotolewa kwenye maswali waulize wanafunzi kuelezea , kutathimini, na kujadili majibu yaliyotolewa.

Anza kujiandaa kwa kusoma Kusudi la Somo, Wazo Kuu, Matokeo Yanayotarajiwa, na Ushauri kwa wakufunzi yanayopatikana mwanzoni mwa kila Somo la Omega. Wakati wote toa agizo kwa utekelezaji wa azimio unaopatikana kwenye kiongozi hiki. Soma Utekelezaji wa Azimio mara kadhaa kuhakikisha kila mwanafunzi anaweza kuandika. Miongozo ya Kozi ya Omega ni viongozi wako waelekezi. Visome kwa uangalifu kabla ya kufundisha kila somo.

Mkazo wa masomo haya ni juu ya mafunzo ya mwingiliano ya Biblia. Wanafunzi wapanda kanisa lazima wawe na Biblia na kuweza kuisoma. Nyenzo katika viongozi hivi vya masomo yaliyo katika visanduku yametolewa kama maelekezo kwa wakufunzi. Mahali inapowezekana wafanye wanafunzi tofauti kusoma mistari ya maandiko kutoka kwenye Biblia zao wenyewe. Hata inapokuwa hakuna swali lililotolewa, waulize wanafunzi kujadili mistari mahali mda unaporuhusu. Wanafunzi wanatakiwa kwa bidii kuandika wakati wa darasa. Vitu vilivyo katika kivuli kwenye nyenzo hapo chini vinatakiwa viandikwe kwenye ubao wa choki au ubao mweupe, au karatasi za kunyofoa ili wanafunzi waweze kuandika vitu hivyo.

Viongozi hivi vya mafunzo vimekusudiwa kutoa mchanganyiko, yanayovutia na yenye ufanisi katika kufundisha. Masomo yanatakiwa yatolewe kwa furaha, shauku na mwingiliano zaidi. Kila somo ni la saa moja. Wakufunzi lazima wawe waangalifu kuanza na kumaliza katika mda.

# Yaliyomo

## MWONGOZO WA KWANZA


MAONO YA KUM ..... 5

SOMO LA 1: "Z" Kufikiri "Z" ..... 5

SOMO LA 2: Utume Mkuu na Upandaji Kanisa ..... 6

SOMO LA 3: Mzunguko wa Upandaji Kanisa ..... 8

SOMO LA 4: Kanuniza Utafiti ..... 10

KANISA

SOMO LA 1: Misingi ya Kibiblia kwa Ajili ya Kanisa ..... 20

SOMO LA 2: Kusudi la Kanisa ..... 20

SOMO LA 3: Mfumo na Kazi ..... 21

SOMO LA 4: Kutafsiri Kanisa la Mtaa ..... 23

TABIA YA KIROHO

SOMO LA 1: Kuhesabiwa Haki kwa Imani ..... 24

SOMO LA 2: Kuishi kwa Injili ..... 25

SOMO LA 3: Kukua kwa Mkristo ..... 26

SOMO LA 4: Nguvu ya Injili Ibadilishayo ..... 27

SOMO LA 5: Kuweka Kumbukumbu za Maisha ya Kiroho ..... 29

MAOMBI

SOMO LA 1, 2: Kongamano la Maombi ..... 30

**SOMO LA 3: Jinsi ya Kuwezesha Maombi ..... 31**

NJIA ZA KUJIFUNZA BIBLIA

SOMO LA 1: Utangulizi Kwenye Njia za Kujifuza Biblia kwa Kufata Neno ..... 32

SOMO LA 2: Kuchunguza Neno la Mungu ..... 33

SOMO LA 3: Warsha ya Uchunguzi ..... 35

SOMO LA 4: Kufafanua Neno la Mungu ..... 36

SOMO LA 5: Warsha ya Ufafanuzi ..... 38

SOMO LA 6: Kulitumia Neno la Mungu ..... 39

SOMO LA 7: Warsha ya Matumizi ..... 41

UINJILISTI

SOMO LA 1: Utangulizi juu ya Uinjilisti ..... 42

SOMO LA 2, 3: Kuandaa Ushuhuda wa Mtu Binafsi ..... 43

## MWONGOZO WA PILI

MAONO YA KUM
SOMO LA 6: Warsha ya Utafiti ........ 44
SOMO LA 7: Kuhamasisha Raslimali Kwa Kupitia Utafiti ........ 45
KANISA
SOMO LA 5: Asili ya Kanisa........ 46
SOMO LA 6: Kazi za Umoja za Kanisa ........ 47
SOMO LA 7: Kuanzisha Maelezo ya Kusudi la Kanisa ........ 48
SOMO LA 8: Falsafa ya Huduma ya Upandaji Kanisa ........ 49
TABIA YA KIROHO
SOMO LA 6: Kuishi Kama Wana Badala Ya Kuishi Kama Yatima ........ 51
SOMO LA 7: Kujifunza Kuwa Wana........ 52
MAOMBI
SOMO LA 4: Kongamano la Maombi ........ 54
UONGOZI
SOMO LA 1: Kanuni za Kibiblia za Uongozi ........ 56
SOMO LA 2: Sura ya Kiongozi ........ 58
VIKUNDI KIINI
SOMO LA 1: Kazi na Faida za Vikundi Kiini........ 61
SOMO LA 2: Kanuni za Uongozi wa Kikundi Kiini........ 62
SOMO LA 3: Kuanzisha kikundi Kiini ........ 69
SOMO LA 4: Uinjilisti wa Kikundi Kiini ........ 72
SOMO LA 5: Onyesho la Kikundi Kiini ........ 73
SOMO LA 6: Falsafa ya Huduma ya Kikundi Kiini........ 74
NJIA ZA KUJIFUNZA BIBLIA
SOMO LA 8: Njia Tofauti Tofauti za Kutumia Kujifunza Biblia kwa Kufata Neno ........ 75
SOMO LA 9: Kuongoza Mafunzo ya Biblia kwa kufata Neno ........ 79
SOMO LA 10, 11: Warsha Juu ya Kuongoza Mafunzo ya Biblia Kwa Kufata Neno ........ 81
UINJILISTI**81**
SOMO LA 4: Uinjilisti na Upandaji Kanisa........ 82
SOMO LA 5: Vizuizi Vya Uinjilisti wa Mafanikio........ 82
SOMO LA 6, 7: Utaratibu Wa Kukata Shauri ........ 83

## Mwongozo wa Tatu

MAONO YA KUM
SOMO LA 8: Kusonga Mbele kwa Mara ya Kwanza........ 86
SOMO LA 9: Asili ya Harakati za Upandaji Kanisa ........ 87
KANISA
SOMO LA 9, 10: Kanisa na Vipawa Vya Kiroho ........ 88
SOMO LA 11: Nguvu za Kijamii za Kanisa........ 89
TABIA YA KIROHO

SOMO LA 8, 9: Sheria na Injili ... 90
SOMO LA 10: Toba Kama Njia ya Maisha ... 91
MAOMBI
SOMO LA 5: Maombi na Kufunga ... 92
SOMO LA 6,7: Kongamano la Maombi ... 93
UONGOZI
SOMO LA 3: Mizunguko ya Uongozi ... 93
SOMO LA 4: Utangulizi Kwa Kazi ya Timu ... 94
SOMO LA 5: Maendeleo ya Timu ... 96
VIKUNDI KIINI
SOMO LA 7: Nguvu ya Majadiliano ya Kikundi Kiini ... 97
SOMO LA 8: Kuwajali Watu Kwenye Kikundi Kiini ... 99
SOMO LA 9: Kuwafunza Viongozi Wapya wa Kikundi Kiini ... 101
UINJILISTI
SOMO LA 8: Uinjilisti wa Kimahusiano ... 102
KUFUASA
SOMO LA 1: Utangulizi Katika Kufuasa ... 103
SOMO LA 2: Jukumu Lako Katika Kufuasa ... 104
SOMO LA 3: Jua Lengo Lako, Jua Watu Wako ... 105
SOMO LA 4: Kuwasaidia Wafuasi Kukua Kiroho ... 106
SOMO LA 5: Mifumo ya Kufuasa ... 108
VITA VYA KIROHO
SOMO LA 1: Kuelewa Mtazamo wa Kidunia ... 112
SOMO LA 2: Nguvu za Vita Vya Kiroho ... 113
SOMO LA 3: Mashambulizi ya Kiroho ... 114

## Omega Mwongozo wa Nne

KANISA
SOMO LA 12: Nguvu ya Kanisa Linaloibuka ... 115
SOMO LA 13: Tabia za Makanisa Yanayokua ... 116
SOMO LA 14: Azimio la Mafunzo ... 117
TABIA YA KIROHO
SOMO LA 11: Upendo Kama Msingi wa Huduma ... 119
SOMO LA 12: Kuuelewa Moyo wa Baba ... 120
SOMO LA 13: Neema ni Kwa Wanyenyekevu ... 121
MAOMBI
SOMO 8,9: Kongamano la Maombi ... 122
UONGOZI
SOMO LA 6: Uongozi wa Kitumishi ... 123
SOMO LA 7: Nguvu za Uongozi ... 124
SOMO LA 8: Mitindo ya Mwingiliano ... 125
SOMO LA 9: Hitaji la Uongozi ... 128
SOMO LA 10: Kuwafundisha Viongozi wapya ... 128
VIKUNDI KIINI
SOMO LA 10: Maswali ya Majadiliano ya Kikundi Kiini na Matatizo ... 129
SOMO LA 11: Kuzidisha kwa Kikundi Kiini ... 130
KUFUASA

SOMO LA 6: Warsha ya Kufuasa ........ 132
UWAKILI
SOMO LA 1: Utangulizi kwenye Uwakili ........ 133
SOMO L:A 2: Uwakili Katika Fedha ........ 134
SOMO LA 3: Usimamizi wa Mda ........ 135
SOMO LA 4: Utaratibu wa Upangaji Kimkakati ........ 136
SOMO LA 5: Warsha ya Utaratibu wa Upangaji Kimkakati ........ 137
FAMILIA
SOMO LA 1: Wajibu wa Kiblia katika Familia ........ 138
SOMO LA 2: Uleaji ........ 139

## Mwongozo wa Tano

MAONO YA kum
SOMO 13: Maono na Kumlika kwa darubini ........ 140
SOMO 14: Kuhamasisha ........ 142
SOMO 15: HATUA ZINAZOFATA ........ 143
KANISA
SOMO 15: Malezi ya Kanisa ........ 144
SOMO 16: Ibada ya Umoja katika kanisa la Mtaa ........ 146
SOMO 17: Jinsi ya Kuongoza Ibada ya Pamoja ........ 147
SOMO 18: Kanisa la Mtaa na Mwili Mkubwa wa Kristo ........ 148
TABIA YA KIROHO
SOMO 14: Huduma ya Upatanisho ........ 150
SOMO 15: Unyoofu wa Maadili ya Wapanda Kanisa ........ 151
MAOMBI
SOMO 10: Maombi ya Kuwezesha kwa Harakati za Upandaaji Kanisa ........ 152
SOMO 11,12: Kongamano la Maombi ........ 153
UONGOZI
SOMO 11: Utoaji Viongozi ........ 154
VIKUNDI KIINI
SOMO 12: Viini Vinavyoenea Kupitia Makanisa ya Mtaa ........ 155
SOMO 13: Usimamizi wa Viini ........ 156
KUHUBIRI
SOMO 1: Kuhubiri Kibiblia I ........ 159
SOMO 2: Kuhubiri Kibiblia II ........ 160
SOMO 3: Kuhubiri Kibiblia III ........ 162
FAMILIA
SOMO 3: Huduma kwenye Familia ........ 163

# Maazimio ya Mafunzo ya Omega
# Mwongozo wa Kwanza

# MAONO YA KUM –Azimio la Mafunzo 1

## "Z" Kufikiri: Nini Mungu anataka?

**I. NINI MAANA YA "Z" KUFUKIRI?**

Soma yafuatayo kwenye darasa:

**"Z"—matokeo ya mwisho ya kile ambacho Mungu hatimaye anataka kwa ajili ya mataifa., eneo, jiji, kijiji, au ujirani.** Z imetumika kwa sababu iko mwishoni mwa alfabeti –mwisho au herufu ya hatima, kama tu Omega inavyoishia na alfabeti ya Kigiriki.

Waulize wanafunzi tofauti tofauti kusoma mistari ya maandiko yafuatayo kwa sauti: **Yohana 3:16, 1 Tim. 2:3-4, na 2 Pet. 3:9.** Kisha uliza maswali yafuatayo kwenye darasa: (KAMA DARASA NI KUBWA KULIKO 9 FANYA KATIKA MAKUNDI MADOGO)

1. Nini mistari yote hii inachotuambia kuwa hatima ya mwisho ya anachotaka Mungu?
2. Ni njia zipi zingine Mungu anazotimizia mwisho wake?
3. Ni nini chombo cha kwanza Mungu anachotumia kutimizia mwisho wake? (jibu: "kanisa lake.")
4. Kuna njia nyingine Mungu anayotumia kwa ufanisi zaidi leo?
5. Ni nini Mungu anataka kwa taifa langu, mkoa, jiji, kijiji, au ujirani? Andika jibu katika sentesi moja.
6. Jinsi gani "Z"inaweza kukamilishwa katika taifa lako, mkoa, jiji, kijiji, na ujirani?
7. Jinsi gani ninachofanya kwa sasa kinavyoonyesha ninachoamini Mungu anataka kufanya?

**II. KUENEZA UPANDAJI KANISA**

Jinsi gani tunaweza kutimiza 'Utume Mkuu'?

Andaa au pata ramani ya jiji au kijiji chako. Onyesha kadiri makanisa mengi ya kiinjili katika jiji lako au kijiji kadiri uwezavyo na onyesha kadiri ya ukubwa wake. Nukuru ukubwa wa jiji au kijiji kwenye ramani. Uliza darasa lote kukusaidia kwenye ramani.

Unafahamu kanisa jingine la kiinjili katika___________(jiji au kijiji) ambalo nimevuka?
Kama umekubali wazo kwamba kunatakiwa kuwa na kanisa moja kwa kila watu 1,000, ni makanisa mengine mangapi unafikiri ________________(jiji au kijiji) kinahitaji kuanzisha?

Fanya mistari yote hapo chini kusomwa na wapanda kanisa.

1. Ni nini mistari hii inatuambia kuhusu mpango wa Mungu kwa kufikia nje kwa injili?
**Isaya 11:9; Marko 13:10; Mathayo 24:14; Luka 24:45-47**
2. Ni nini mistari hii inatuambia kuhusu kazi yetu katika kutimiza haja ya Mungu kwa ulimwengu?
**Mathayo 28:18-20, Matendo 1:8**

**III. BAADHI YA HATUA ZA LAZIMA KATIKA KUFIKIA KWENYE "Z"**

Soma nyenzo hapo chini iliyopigiwa mstari na uliza maswali yaliyotolewa. (KAMA DARASA NI KUBWA KULIKO 9 JADILI MASWALI KATIKA MAKUNDI MADOGO)

A. **Maombi** – Nini tunachotakiwa kuombea katika safari yetu ya kupata "Z"? **2 Nya. 7:14, Mt. 9:38**

B. **Upendo na Umoja** – Kwa nini upendo na umoja ni wa lazima katika kutimiza "Z"? Yohana 1**3:35, Yohana 17:21,23**

C. **Maono** – maono ni kuunda kivuli cha hali ya wakati ujao Mungu alichonacho kwa kila mmoja, vikundi kiini, au kanisa. **Yohana 3:16, 1 Yohana 2:2, Mat. 9:37**

D. **Uinjilisti – (Rum 10:14-15**). Jinsi gani tunaweza kupata nafasi za kushuhudia kwa wasioamini katika eneo letu? Jinsi gani waumini wanafikia kupitia mzunguko wa waumini wengine marafiki kwenda kwa wasioamini?

E. **Upandaji kanisa – Efe. 3:8-11, Efe. 4:11-13** Wakati kanisa mpya linapopandwa watu wanafikiwa kwenye ujirani unaozunguka ambao wasingeweza kufikiwa kwa injili. Ni kwa sababu gani zingine hili linatokea? Kama unajua tukio la kutokea kwa hili liambie kundi juu yake na jadili kilichotokea.

**IV. "Z" KUFIKIRI INAPELEKEA KATIKA "Z" VITENDO**

Vitendo viwili vinavyotokana na "Z" kufikiri ni "Z" utoaji (**2 Kor. 8:7, 2 Kor 9:6-7)** Na "Z"mkakati.

1. Jinsi gani tunaweza kuhakikishiwa kuwa fungu linalohitajika kwa upandaji kanisa litatolewa?
2. Ni baadhi ya maswali yapi ya kimkakati ambayo lazima yajibiwe kwa upandaji kanisa kutokea?
3. Ni baadhi ya mipango ipi inayohitajika kufanywa kadiri kanisa linavyoendelea kuelekea upandaji wa kanisa jipya?

| |
|---|
| Yachunguze maswali mwishoni mwa somo hili kwenye Kozi ya Omega Mwongozo wa Kwanza. Gundua yale ambayo unadhani kuwa ya thamani zaidi kwa kusisimua majadiliano ye msaada. Kama huna mda kwa ajili ya darasa kujadili yote kati ya maswali haya, tumia yele unayodhania kuonekana kuwa na thamani kwa darasa. |

## Utekelezaji wa Azimio (Soma au uandike ubaoni ili kwamba wanafunzi waweze kuuandika)

Anza kufikiria kuhusu mkakati wa kueneza upandaji kanisa ambao unahusisha maombi, umoja na upendo, maono, uinjilisti na upandaji kanisa. Andika baadhi ya mawazo ya awali na mshirikishe mshauri wako au mkufunzi wa somo hili.

Fikiri kuhusu ujirani wako, kijiji, jiji, mkoa au nchi. Fikiria majibu yako kwenye swali, "Nini Mungu anataka_________? Orodhesha vitu vitatu ambavyo utafanya kusaidia "Z" kutokea katika eneo lako.

# MAONO YA KUM – Azimio la Mafunzo 2

## Utume Mkuu na Upandaji kanisa: Kueneza ufuasishaji

**I. KUUELEWA UTUME MKUU**
**Mathayo 28:18-20).**

"Fuasa " ni amri ya kati ya Utume Mkuu. Kubatiza na kufundisha ni mitambo miwili ya kukamilisha hili. Kuwa mfuasi wa Yesu Kristo ni lazima uamini na kutubu (**Marko 1:15).** Ubatizo ni alama na kifungo cha wongofu **(Tit. 3:5, Rum. 6:3-4).**

**A. Agizo: Fanya Wanafunzi**

1. Mwanafunzi ni nini?
2. Ni kwa namna gani tunafanya wanafunzi na ni kwa namna gani hii ni kazi ya Mungu?
3. Ni nini thamani ya ubatizo katika kufanya wanafunzi?
4. Ni yapi baadhi ya masomo muhimu zaidi ambayo tunafundisha tunapokuwa tunafuasa?

**B. Upeo : YOTE**

1. Katika tafasiri halisi hapo juu, kuna "yote" nne. "Mamlaka **Yote** ninepewa mbinguni na dubiani. Kwa hiyo, kwenda, kufanya wanafunzi wa mataifa **yote**, tukiwabatiza kwa jina la Baba na la Mwana na la Roho Mtakatifu, tukiwafundisha kushika **yote** niliyoamru; na, Nipo pamoja nanyi siku **zote,** hata mpaka miisho ya dunia" (tafasiri halisi ya **Mat 28:18-20 )** inaainisha na kujadili umuhimu wa kila moja ya "yote"
2. Jadili na tathimini jinsi Yesu, Paulo na kanisa lililotawanyika walivyofanya wanafunzi kadiri walivyokwenda. Walikuwa wakipangilia kufanya wanafunzi (1) kwa kusudi la kufanya hivyo (**Mat. 24:14)**, (2) kwa utii, (**2 Kor. 5:18-19**) na?au (3) kwa sababu ya mateso (Matendo **8:1**)? Elezea.

3. Jinsi gani ahadi ya Yesu inatoa hakika ya mafanikio yetu katika kufuasa (**Yohana 15:4-5**)?
4. Jinsi gani maneno ya Mtume Paulo kwa kanisa la Wafilipi yanadhihirisha ujasiri wake kwenye ahadi katika **Fl.p 1:6**?
5. Ni shughuli zipi na huduma katika kanisa lako ni za ufanisi zaidi katika kuhudumu kufanya wanafunzi? Zinaheshimu mkazo wote wa Utume Mkuu? Ni jinsi gani zinaweza kufanya hili vyema?
6. Mafundisho au uinjilisti ni kipengele kigumu zaidi cha Utume Mkuu kwa kanisa lako kukamilisha?

**II. UTUME MKUU NA KUENEZA UPANDAJI KANISA**

1. Upandaji kanisa unastahili kipao mbele kinachoendelea kutokana na ukweli kwamba ni kiuongo bora cha Utume Mkuu uliotolewa na Bwana. Wakati **Mat 24:14** inatuambia Utume Mkuu utatimizwa?
2. Uinjilisti unaweza kufanyika kwa upandaji wa kanisa, kwa shughuli zilizoanzishwa katikati ya kanisa na kwa uinjilisti usio wa kanisa. Ni upi unafikiri ni wa ufanisi zaidi katika "Kufuasa?"
3. Kwa ujumla , jinsi gani unaweza kutathimini kanisa lako katika kufanyia kazi Utume Mkuu? Jinsi gani ya ufanisi wa kufundisha , uinjilisti, na kufuasa ?
4. Katika Matendo 1:8, tumeamriwa "kwenda." Ni kwa njia zipi kanisa lako sasa linakwenda? Jinsi gani msisitizo katika upandaji kanisa utaongeza "kwenda" kwa kanisa lako?
5. Kuna mipaka katika maisha ya kanisa lako kwenye upandaji kanisa? Kama ni hivyo, ni mipaka ipi. Ni kwa jinsi gani inaweza kuepukwa?

## Utekelezaji wa Azimio


Soma au uandike ubaoni ili kwamba wanafunzi wauandike

**Anzisha na fuasa kundi la watu kuomba kwa ajili ya taifa lako na kwa ajili ya mataifa mengine, anza kutoa fedha kwenye misheni za kitaifa na za kigeni, na anza hatua ya kwanza ya upandaji kanisa kwa maono ya kufikia mataifa yote.**

# MAONO YA KUM – Azimio la Somo 3

**Mzunguko wa Upandaji kanisa:** Kupata Picha Kubwa

**Mzunguko wa Upandaji kanisa" (Kielelezo 3.1)** Kama inawezekana, pata kopi ya mchoro huu kulionyeshga darasa.




Omba kwa ajili ya hao ambao watasaidia na kwa wewe mwenyewe?

MASWALA YA UFUNGUO (Mda unaweza usiruhusu kujadiliana maswali yote ya ufunguo kwenye awamu ya saba)

- Ni nini shamba langu binafsi la mavuno? Nini Mungu anataka kutoka kwangu katika eneo langu?
- Ni sera zipi za kipekee za wito na maono ambayo Mungu anakupatia?
- Nani atakwenda kusaidia?
- Ni kwa nani utaombea? Nini utakachoombea?
- Ni ombi gani unatakiwa kufanya kwa huduma yako mwenyewe kwa Mungu?

**II. AWAMU YA II—Injilisha 1 Kor. 9:19-23**

SHUGHULI:

Wasiliana na viongozi mashuhuri na anza mahusiano.

Injilisha waliopotea.

Anzisha kundi  la mafunzo ya Biblia ya kiuinjilisti.
Eleleza huduma kwa wakata shauri.
MASWALA YA UFUNGUO:

- Ni njia zipi za kiuinjilisti ni za ufanisi zaidi kwetu kufikia malengo yetu?
- Jinsi gani tunafanya mawasiliano na viongozi mashuhuri? Ni nani hao? Jinsi gani tunawapata?
- Jinsi gani tunawafunza wakata shauri wapya kuwa washuhudiaji kwa marafiki zao na famili?
- Jinsi gani unagundua mitandao ya marafiki zao na kuanza kuwainjilisha?

**III. AWAMU YA III—Fanya Wanafumzi 1 The. 5:11**
SHUGHULI:
Fuasa wakata shauri.
Shauri viongozi wanaoibuka.
Fundisha utii na kujitoa kwa Bwana
Tia moyo kugeuka kuwa kama Kristo
Fuasa wakata shauri wapya kwenye utii kwa Kristo
MASWALA YA UFUNGUO:

- Jinsi gani ya kuanzisha na kufuasa kundi la watu?
- Jinsi gani viongozi wa kikundi kiini wafunzwe na kutolewa?
- Jinsi gani ya kueleleza uongozi wa ufanisi?

**IV. AWAMU YA IV—Kusanyika Pamoja Ebr 10:24-25**
SHUGHULI:
Panua juhudi za uinjilisti kupitia mtandao wa marafiki.
Zidisha vikundi kiini.
Anza kuabudu kunakoendelea kwa mara moja moja.
MASWALA YA UFUNGUO:

- Jinsi gani viongozi wa kikundi kiini wafunzwe na kutolewa?
- Lini tunawabatiza wakata shauri?  Lini na nani anawapatia meza ya Bwana?
- Jinsi gani utaanzisha ‘maisha ya mwili?'  Jinsi gani waumini wapya wanavyohusishwa kwenye mwili?
- Lini tunakusanyika, wapi tunakutana?  Lini tunawaalika watu?
- Ni mifumo ipi tutatumia kufikia kusudi letu linalokusudiwa?  Ni mtindo upi wa kuabudu tutatumia?

**V.  AWAMU YA V—Endeleza viongozi  2Tim. 2:2**
SHUGHUL:
Jenga sura ya viongozi wanaohitajika katika kila eneo la huduma.
Gundua kujaliwa vipawa kwa wajumbe wote.
Funza viongozi wa kikundi kiini.
Pangia na toa viongozi kwenye huduma.

Pangilia muundo na nafasi za huduma unazofikiria kwa ajili ya huduma.
MASWALA YA UFUNGUO

- Jinsi gani tunawafanya wakata shauri wapya kugundua kujaliwa kwao vipawa? Nani atawafunza?
- Ni maeneo yapi ya mafunzo yanayohitajika? Wapi na jinsi gani mafunzo haya yatatolewa?
- Ni akina nani ni viongozi mashuhuri?  Ni nini vipawa vyao na uwezo? Ni waaminifu, kuwahudumia watu?
- Ni wapi hao waliofunzwa watakuwa na huduma?  Ni yapi mahitaji ya msingi na maswala katika eneo hilo?  Lini huduma yao katika eneo hilo itaanza ? Ni kwa nani watatoa taarifa? Ni upi mgawanyo wao wa kazi?

**VI.   AWAMU YA VI—KUZIDISHA MATENDO 1:8**
SHUGHULI:
Fundisha viongozi kuunda timu za upandaji kanisa.
Funza wafanya kazi wa ngazi kadhaa na huduma tofauti tofauti.
Tafiti eneo mpya ambapo unajisikia kuwa tayari kuanzisha huduma.
Panga na endesha juhudi za uinjilisti za kimkakati.
Anzisha na teua viongozi kwenye sehemu ya chama cha kihuduma.
MASWALA YA UFUNGUO

- Ni utafiti upi unahitaji kufanyika?  Nani ataufanya?  Kuna makabila ya wakazi karibu na hapo ambao bado hawajafikiwa kwa injili?  Kuna viongozi maarufu miongoni mwao wanaoweza kufundishwa?

- Ni malengo yapi yanahitaji kuwekwa na kuchapishwa? Nani anasukuma juhudi za maombi kusaidia huduma hii?
- Nani anawapangia na kuangalia huduma zote mpya? Nani atawafunza katika kuendeleza elimu?
- Kuna huduma nyingine ambayo inaweza ikahusishwa kwenye juhudi hizi? Nani anatakiwa kuwaalika kujiunga na nguvu? Ni mchango upi maalumu watakaofanya kwenye juhudi za misheni kwa ujumla?
- Tunahitaji huduma yoyote ya elimu ya juu kufundisha ngazi mbali mbali za uongozi kwa harakati hizi? Nani atafanya mafunzo? Jinsi gani yatafadhiliwa?

**VII. AWAMU YA VII—HARAKATI Isa 11:9**

SHUGHULI:

Funika makazi yote ya makabila ya wakaaji.

Anzisha mipaka ya kutangaza harakati.

Onyesha miradi ya misheni ya mwingiliano wa tamaduni ambazo kundi litafadhili.

Endesha maombi na kusanyika kusifu.

Weka malengo ya kimkoa/au kitaifa.

Anzisha ngazi za juu za mafunzo kwa viongozi mashuhuri wa harakati.

MASWALI YA UFUNGUO:

- Je harakati zinajitangaza zenyewe, kujisaidia na kujitawala? Kama siyo, nini kinahitaji kufanyika kuhakikisha kwamba inakuwa hivyo?
- Ni mikoa ipi au watu ambao bado hawajafikiwa? Ni miradi ipi ya misheni Bwana anatuongoza kuianzisha?
- Ni aina gani ya mafunzo yanahitajika kwa harakati? Jinsi gani yatafadhiliwa?
- Ni akina nani viongozi ni"aina ya mitume" kwa ajili ya harakati? Jinsi gani tunafanya kazi pamoja nao? Jinsi gani tunaweza kuwatia moyo na kuwasaidia? Ni yapi ni mahitaji yao?

## UTEKELEZAJI WA AZIMIO

**Jadili kila moja ya awamu nne hapo juu pamoja na hao unaofanya nao kazi katika juhudi zenu za upandaji kanisa. Waulize maswali kuhusu kila ngazi na jadili maoni yako pamoja nao.**

# MAONO YA KUM--Azimio la Mafunzo 4

Kanuni za Utafiti (Kuweka Ramani Kiroho): Taarifa kwa Ajili ya makusudi ya Kimkakati

**I. NINI MAANA YA UTAFITI (KUWEKA RAMANI KIROHO)?**

**A. Utafiti (Kuweka ramani Kiroho) ni njia ya Kukusanya Taarifa lakini Inatoa Thamani Iliyoongezeka**

**(1) Shamba la mavuno**

**(2) Nguvu ya mavuno**

**B. Utafiti (Kuweka Ramani Kiroho) Ina Msingi wa Kibiblia**

- **Hesabu 1:1-5** Mungu anaamuru kata ya wapiganaji.
- **Hesabu 13:1-4.** Wapelelezi wanatumwa kuchunguza ardhi.
- **Neh 1:3-4; 2:1-6.** Nehemia alitafiti hali ya Yerusalemu kabla hajaanza kazi ya kuujenga upya ukuta wa mji, kisha ari ya watu watakaofanya kazi.
- **Mt 9:35-10:1.** Yesu alikwenda miongoni mwa watu na kuona mahitaji yao kabla ya kutuma wanafunzi wake nje kufanya nao kazi.
- Y**ohana 4:35**. Bwana Yesu aliwaamuru wanafunzi wake “kuangalia kwenye” au “kuchunguza” (Ambayo ina maana ya Kiyunani) mavuno ya mioyo ya watu.
- **Mdo 2:41, 47; 4:4; 5:14** Inatoa taarifa ya idadi ya watu.

**II. WAPI UTAFITI UNATAKIWA UFANYIKE?**

Mkufunzi anatakiwa atoe mfano –kutafuta au kuchora ramani ya eneo linalolengwa, na kupata taarifa kuhusu eneo linalolengwa (mzunguko) katika mfano wako. Fupisha ramani kuonyesha takwimu muhimu kama

vile makanisa yalipo na ni aina gani ya makanisa, vile vile na sehemu zingine muhimu kwa kazi (kwa mfano: vituo vya kidini, siasa, masoko, sehemu za mambo ya kumbu kumbu, etc.).

- Nani anatakiwa kukusanya taarifa?
- Nani anatakiwa afupishe na kutoa taarifa? Wanazionyesha kwa namna kwamba zinaamsha huruma na kujenga ujasiri kwa kile Mungu anachotaka kufanya.

**IV. LINI RAMANI YA KIROHO (UTAFITI) UNATAKIWA KUFANYIKA?**

Kuna angalau sehemu tatu katika mzunguko wa upandaji kanisa ambapo Utafiti unatakiwa ufanyike:

A. Awamu ya Maombi: Katika maandalizi ya kanisa maalumu jipya

B. Awamu ya kukusanyika pamoja: Kutathimini ufanisi wa kanisa

**C.** Awamu ya Kuzidisha na Harakati: Kupata Picha Kubwa

**V. KWA NINI WAPANDA KANISA WANATAKIWA KUFANYA UTAFITI (KUWEKA RAMANI YA KIROHO)?**

A. Taarifa zinachochea huruma Kwa Watu Walio Katika Mzunguko
B. Taarifa Zinazaa maombi
C. Taarifa Zinaamsha Maono ya Kupanda Makanisa
D. Taarifa zinaandaa Nguvu ya Mavuno Kuwa ya Ufanisi Zaidi

**VI. JINSI GANI UTAFITI UNATAKIWA (KUWEKA RAMANI YA KIROHO) UFANYIKE?**

A. Uchunguzi
B. Mahojiano
C. Maswali ya Mazoezi na Ukaguzi
D. Takwimu za Kiofisi za Idadi ya wakazi
E. Kuyarudia Maandishi

MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI

Nini unachofikiria utafiti wako utagundua kuhusu eneo lako lengwa?

Ni faida zipi za kuchukua mda kufanya utafiti katika eneo lako unalolenga? Jinsi gani utafiti utafanya juhudi za upandaji wako kanisa kuwa za ufanisi zaidi?

Ni vipande vipi tano au sita vya taarifa unazojisikia unahitaji kujua kuhusu eneo lako unalolenga ambazo zitazidisha ufanisi wa upandaji wako kanisa?

Unawafahamu watu ambao wanaweza wakafanya vyema utafiti baada ya kuwa umewafunza?

Hao walio katika shamba lako la mavuno wako tayari kusikia injili? Ni baadhi ya uchunguzi upi uliofanya ambao unaonyesha kwako kwamba watu wako wazi au ni wapinzani wa injili?

| |
|---|
| Utahitaji kutoa kopi ya Ziada 4A na 4B kwa kila mwanafunzi mpanda Kanisa. Hili ni agizo la lazima! |

## UTEKELEZAJI WA AZIMIO

Ziada 4A inaagizo la ujuzi wa kimazoezi katika kutafiti eneo linalolengwa. **Fanya marudio ya maagizo katika ziada hii na yamalize kufikia kipindi kijacho cha mafunzo.** Muulize Mungu Kutumia agizo hili kukupa ufahamu mkubwa na huruma kwa watu katika eneo lako linalolengwa. Muulize kutumia utafiti huu kukupa mawazo mazuri ya wapi na jinsi gani ya kuanza huduma yako ya upandaji kanisa katika eneo hili linalolengwa. **Unaweza ukataka kurithi mifano ya maswali ya mazoezi katika Ziada 4B kutumia kama sehemu yako ya utafiti.**

MAONO YA KUM
*ZIADA*
4A

# Kuelewa Eneo Unalolenga

## AGIZO LA UTAFITI

*Kusudi la agizo hili ni kukupa* <u>*uzoefu*</u> *katika kutafiti kwa vitendo kama zana ya ufanisiy kwa upandaji kanisa. Unatakiwa kufanya kila kipengele ulichopangiwa. Unaweza kukuta baadhi ya kazi zikiwa rahisi kuliko zingine. Hata kama ni ngumu au rahisi, Mungu atakuwa na vitu vya kukufundisha kuhusu watu na sehemu unayojaribu kuifikia, kupitia kila aina ya kazi ya agizo hili.*

*Huhitaji kufanya kazi hii uliyoagizwa peke yako. Unaweza kuifanya pamoja na wengine. Hata hivyo inashauriwa kuwa ufanye pamoja na wengine iwezekanavyo. Uwe tayari kumshirikisha uliyoyapata kiongozi wako wa utafiti, mshauri na wengineo. Kazi hii inahitajika mara tu unapopata mwongozo wa pili wa mafunzo.*

*Ukumbusho kwa anayetafsiri: Kumbuka kutengeneza Ziada 4A na 4B katika vijitabu tofauti vidogo ili kwamba washiriki waweze kuweka taarifa zao za utafiti katika sehemu moja.*

**HATUA YA 1: TAMBUA ENEO LAKO UNALOLENGA**

Pata au tengeneza ramani ya mji wako, eneo, au mkoa. Pata ambayo ina mambo mengi zaidi unapoweza kupata vituo vyote vya wakazi, majina ya mitaa, na njia za usafiri. Chora duara kwenye sehemu unayolenga. Hili ni eneo la huduma yako, mkoa ambao unaamini Mungu anakutaka kulifanya jina lake lijulikane, na anapotaka kupanda makanisa.

**HATUA YA 2: KUSANYA TAARIFA ZA NGUVU YA MAVUNO**

Kama ilivyoelezwa katika somo la 4—“Kanuni za Utafiti”—nguvu ya mavuno ni rasilimali zote za Mungu zilizokwisha kuwa kazini katika eneo lako unalolenga. Onyesha ni rasilimali gani zilizopo katika mzunguko wako kwa kujifunza yafuatayo:

**1. Makanisa ya Mtaa Yaliyopo**

a. Weka alama kwenye kila kanisa la mtaa katika ramani yako kwenye mkoa wako. Onyesha ni dhehebu gani kwa kila moja.
b. Kama inawezekana, orodhesha watu wao wazima wanaohudhuria.
c. Onyesha mwaka ambao kanisa lilipandwa au kutumika.
d. Yakinisha ni kundi gani la watu linafikiwa na kila kanisa (M.f. --, vijana, watoto, wasio na makazi maalumu, wazee, wa kutoka mataifa mbalimbali n.k.) Ni namna gani wamefanikiwa katika juhudi zao?
e. Ni aina gani ya muhusiano yaliyopo miongoni mwa makanisa yaliyopo katika mzunguko? Wameungana au wamegawanyika?
f. Watu wanakutana kuomba kwa ajili ya waliopotea katika jamii yao au kwa ajili ya kutuma wamishenari?

1. **Misheni na Makundi ya Makanisa ya Kando Kando**

a. Orodhesha misheni na makundi ya makanisa ya kando kando katika eneo linalolengwa.
b. Kwa kifupi eleza kila huduma ambayo ina (maandishi, wafungwa, huduma ya waislamu, vijana n.k.)
c. Wangependa kushirikiana na wewe au wengine katika uinjilisti na juhudi za upandaji kanisa?

**3. Historia ya Ukristo**

a. Lini ukristo uliletwa kwa mara ya kwanza katika eneo na ni namna gani uliletwa? Watu walilazimishwa au walipenda wenyewe kupokea injili?
b. Eleza historia ya namna ambayo kila dhehebu liliingizwa katika eneo.
c. Ni dini zipi zingine kuu zimeweza kuwa na mguso kwa wingi katika eneo lako unalolenga? Ni dini zipi zingine/ibada zilizopo katika sehemu yako sasa na ni kwa namna gani zinafanikiwa kuvuta wafuasi?
d. Ni namna gani historia hii inaathiri harakati zako za upandaji kanisa?

**HATUA YA 3: KUSANYA TAARIFA JUU YA SHAMBA LA MAVUNO**

Shamba la mavuno ni kundi la watu miongoni ambamo utafanya kazi na sehemu ambayo utapanda kanisa. Shughuli zifuatazo zitakusaidia juu ya shamba la mavuno katika eneo unalolenga.

**1. Habari za Kitakwimu**

a. Idadi ya wakazi
b. Namba na asilimia ya wakazi ambao ni wanaume, wanawake, vijana, watoto
c. Namba ya watu wazima wanaofanya kazi…ikiwa ni pamoja na taarifa za shughuli na kiwango cha mapato.
d. Namba ya waliostaafu na wazee, na wasiojiweza na vilema
e. Asilimia na eneo la jamii ya walio wachache. Ni lugha gani wanaongea?

**2. Habari za Kijiografia**

Alama za kijiografia zinaweza kuwa na mguso makubwa katika harakati za upandaji kanisa. Zinashika nafasi ya jinsi gani na wapi watu wanaishi na kuhusiana na wengine. Kwa mfano, njia ya reli ya magusi inayopita kati kati ya ujirani wa mji. Upande mmoja wa magusi, watu ni matajiri zaidi kuliko upande mwingine. Watu hawako tayari kuvuka njia ya reli ya magusi. Kwa hiyo, magusi ni kizuizi kisichoonekana, na watu wa upande mwingine wa njia ya reli ya magusi wanaonekana kutokuhudhuria kanisa la upande mwingine wa magusi haya. Mfano mwingine unaweza kuwa kwamba kwa sababu mji umezungukwa na milima mizuri, watu mara nyingi wanakwenda nje ya mji siku za jumapili na hivyo kuwa na uwezekano kidogo wa watu kuhudhuria ibada za jumapili.

Ni vitu gani vinagawanya mkoa (mito, njia ya reli, barabara, n.k.)? Ni jinsi gani vitu hivi vinavyogawanya vinagusa mtindo wa usafiri, utajiri, n.k?

Mji unazungukwa na milima? Kuna maziwa, kingo, mbuga za wanyama au sehemu zingine ambazo watu watapenda kwenda kufurahia?

Kama sehemu yako unayolenga ni mkoa au mji, weka alama kwenye ramani yako mahali vilipo viwanda, na mahali wanapoishi watu. Kuna sehemu maalumu za kununulia vitu? Je watu wanaishi karibu na sehemu zao za kazi au kusafiri umbali mrefu?

Pia nukuu njia kuu za usafirishaji. Je, watu wengi wanasafiri kwa gari, basi, reli?

Ni wapi watu wanakwenda kwenye faragha, starehe? Wanakaa kwenye mji na kwenda kwenye mbuga za wanyama? Wanatumia muda wao mwingi wa mapumziko kwenye bustani au kwenye nyumba?

**3. Taarifa za Kijamii na Kiutamaduni**

Kwa kujifunza juu ya mtazamo wa watu wa kidunia na mahitaji yanayowagusa, tunaweza kupata ufahamu katika njia ambazo zinaweza kuwa za maana kuonyesha upendo wa Yesu Kristo. Njia nzuri ya kujifunza

kuhusu watu ni kuwauliza maswali na kuchunguza tabia zao. Nenda katika sehemu yako unayolenga na ongea na watu kama 15-20. Jaribu na jifunze yafuatayo:

Mtazamo kuhusu Mungu

Watu wanamwamini Mungu? Wanaamini nini juu ya Mungu? Wamewahi kusikia juu ya Yesu? Wanajua nini juu ya Yesu? Wanaamini kama kuna mbingu na jehanamu? Wanaamini juu ya malaika, mapepo, au Shetani? Wanapokuwa wanaumwa wanakwenda wapi kupata msaada? Wanaamini katika bahati? Wanaamini kama wanaweza kumudu maisha yao ya mbeleni au kufanya maisha yao kuwa mazuri kwa ajili ya watoto wao? Wanaamini kuwa dhambi ni nini? Wanahudhuria kanisa mara kwa mara? Kama ndiyo ni mara ngapi? Kama siyo ni kwa nini hawahudhurii kanisa?

Zipi ni sikukuu muhimu au siku za mapumuziko katika eneo hilo? Watu wanazisherehekeaje?

Ni nini wanapenda zaidi juu ya maisha yao? Ni kitu gani kimoja wangebadilisha?

Ni kitu gani wanaona kimoja au viwili katika jamii yao kuwa matatizo ya kijamii? (ulevi, mayatima, ukosefu wa huduma za hospitali, wazee wasio na uangalizi, n.k.)

Ni viongozi gani wanakubalika katika jamii? Kwa nini wanaonekana kama viongozi?

Nani wanadhaniwa kuwa mashujaa?

Orodhesha vitu sita ambavyo watu wanathamini kwa wengine? (uaminifu, uhodari, ukarimu, n.k?)

## HATUA YA 4: MCHANGANUO WA HABARI ZA SHAMBA LA MAVUNO NA NGUVU YA MAVUNO

***Ni makanisa mangapi yanahitajika ili kwamba kila mwanaume, mwanamke, mtoto katika eneo lengwa ataweza kuona, kusikia, na kuelewa habari ya injili kwa njia inayofanana na utamaduni wao?***
Mara unapokuwa umekusanya taarifa zako zote, umeandika ufupisho wake, na kutia maelezo kwenye ramani yako, chukua mda kurudia na kutafakari juu ya habari hizi. Muulize Mungu kukupa huruma juu ya watu walio kwenye eneo lako lengwa. Muombe Mungu kukupa ubunifu wa mawazo juu ya namna ya kushirikisha watu upendo wake. Kama sehemu ya utaratibu huu, changanua habari zako kwa kujibu maswali haya:

Ni makanisa mangapi yanahitaijika kukumilisha Utume Mkuu katika eneo unalolenga? Ni makanisa mangapi yanahitajika ili kwamba kila mwanaume, mwanamke, mtoto katika eneo lengwa ataweza kuona, kusikia, na kuelewa habari ya injili kwa njia inayofanana na utamaduni wao? Anza kuomba na kumuuliza Mungu kukuongoza kufanya kile anachotaka ufanye.

Onyesha mugao wako: Ni makanisa mangapi Mungu anataka umwamini kwa ajili ya huduma yako.

Chagua mahali unapoanzia: Ni wapi utaanzia? Ni wapi zaidi watu wanaitikia? Paulo mara nyingi alipata kwanza waliokubali kutoka kwenye sinagogi. Kisha alifanya kazi kuanzia pale kwa mtandao wa mahusiano.

Chagua njia zako: Ni nini ilikuwa moja au mbili ya mahitaji makuu ya watu katika jamii? Ni njia zipi utatumia kukidhi mahitaji ya watu? Ni njia ipi inatumika na kuleta matokeo mazuri zaidi katika makanisa mengine katika sehemu hiyo? Ni rasilimali gani zilizopo kwako kwa njia hizi? Nini kipawa chako na unayoweza kufanya?

Onyesha rasilimali zako: Ni rasilimali zipi zilizopo na shirikisha maono hayo hayo? Kuna wengine ambao unaweza kushirikisha maono haya na kushirikiana katika lengo lililofikiwa? Nani vibarua, fedha, na watu binafisi walio na vipawa wanaopatikana kwa ajili yako? Makanisa katika eneo yana shauku kwa ajili ya uinjilisti na upandaji kanisa? Wako tayari kufanya kazi pamoja au pamoja na wewe katika juhudi zako? Wako tayari kuomba kwa ajili ya uinjilisti na juhudi za upandaji kanisa na kwa Mungu kujidhihirisha katika maisha ya watu katika jamii zao?

Watu wana ueleo au kuamini katika Mungu au Yesu Kristo? Ni katika hatua gani utaanza kushirikisha habari ya injili? (Mf. unaweza kuanza na Yesu Kristo au kuanza na kuwepo kwa nguvu ya juu, Mungu muumbaji?

**HATUA YA 5: MASOMO YALIYOJIFUNZWA KUTOKA KWENYE UTARATIBU WA UTAFITI**

Tathimini uzoefu wako katika kufanya utafiti uliopangiwa. Ni nini Mungu amekufundisha wewe mweneywe kutokana na utafiti uliopangiwa, haja yako ya kushiriki katika upandaji kanisa? Ni mahangaiko gani umepata wakati unafanya utafiti? Ni kwa namna gani umeyashinda? Ni nini kilikuwa rahisi kuhusu utafiti? Kama ingekuwa kwamba urudie utafiti huu, ni nini ungefanya tofauti?

**HATUA YA 6: KUSHIRIKISHA MATOKEO YA UTAFITI**

Katika kipindi kingine cha mafunzo, jiandae kutoa matokeo ya utafiti wako. Taarifa yako inatakiwa kuwa ya wastani wa dakika 10-15 na iwe na mambo yafuatayo:

1. **Sehemu ya Kwanza—Taarifa za Msingi Zilizokusanywa (dakika 5-7)**

Elezea eneo lako unalolenga.

Namna gani umekusanya habari zako (kukagua, kuhoji mtu, uchunguzi/kuweka ramani, utafiti kwenye maktaba, n.k.).

Jadili matatizo au ugumu ulioukuta na namna gani umeweza kuushinda. Nini utahitaji kufanya tofauti wakati mwingine?

**2. Sehemu ya Pili—Uchanganuzi wa Habari za utafiti (dakika 5-8)**

Ukumbusho wa utoaji unatakiwa kukazia juu ya matokeo ya utafiti wako. Utoaji unatakiwa kujibu maswali yafuatayo ya ufunguo:

Ni taarifa ipi uliyojifunza iliyokuvutia juu ya eneo lako unalolenga na watu wanaoishi mahali pale?

Kulikuwa na taarifa yoyote iliyokushangaza?

Ni kitu gani maalumu ulichojifunza ambacho kitakusaidia kuonyesha mkakati wako wa upandaji kanisa katika eneo unalolenga?

Ni nini kimoja cha kweli muhimu kwenye upandaji kanisa ulichodhihirisha kwamba umeshakifahamu juu ya shamba la mavuno?

Ni ugunduzi gani mpya ambao ni muhimu kwa upandaji kanisa uliofanya juu ya shamba la mavuno ambao hukuujua mwanzoni?

Ni nafasi zipi ulizopata kama mlango wazi kwa ajili ya injili?

Ni vipingamizi gani ulivyopata na namna gani vinaweza kudhibitiwa?

Ni utafiti gani ufuatao unaohitaji kufanya ili kuendeleza uinjilisti na mikakati ya upandaji kanisa katika eneo unalolenga?

**MAONO YA KUM**
***ZIADA***
**4B**

# Mfano wa Karatasi ya Mazoezi

*Katika Ziada hii kuna maswali mawili ya mfano wa maswali ya utafiti: ukaguzi wa kanisa la mtaa, na maswali ya utafiti kwa ajili ya kutafiti eneo linalolengwa. Hii ni mifano tu na inaweza kuundwa upya kukidhi malengo yako.*

*Ukumbusho kwa anayetafasiri: Maswali haya ya utafiti yanaweza zaidi kwa uhakika kuchapishwa katika wingi (hasa katika vijitabu vodogo) ili kutengeneza kopi nyingi zaidi zitakazokuwepo kwa ajili ya wapanda kanisa AU kwa viongozi wengine wa kanisa kwa wote wanaotumia lugha hiyo.*

**UKAGUZI WA KANISA LA MTAA**
**A. SURA**

1. Jina la kanisa_____________________________
2. Dhehebu (Wanachoamini) ___________________________
3. Anwani ya kanisa /mahali lilipo_______________________
4. Mahali kanisa linapokutana: Panamilikiwa na kanisa_______ Ni mahali pa kupanga_______
5. Tarehe lilipoanzishwa________Tarehe lilipoandikishwa_________
6. Jina la mchungaji/kiongozi________________ umri________
7. Mchungaji/kiongozi anafanya kazi katika nafasi nyingine? Ndiyo______ Hapana____
8. Lugha kuu inayozungumzwa kanisani__________ Nyinginezo______________
9. Idadi ya waumini kwa wakati huo_____________
10. Wastani wa wanaohudhuria______________

**A. WATU**

Jaribu kujaza idadi ya watu kulingana na makundi haya*:*

| | Wanaohudhuria | | Wanaoamini | | Wajumbe | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Mm | Mk | Mm | Mk | Mm | Mk |
| Umri 0-10 | | | | | | |
| 11-17 | | | | | | |
| 18-24 | | | | | | |
| 25-30 | | | | | | |
| 31-55 | | | | | | |
| 55+ | | | | | | |

*Dhana:*
Waliohudhuria siyo waumini na /au wajumbe.

Idadi ya wanaohudhuria inatakiwa kuwa kubwa kuliko ya waumini na wajumbe.

Mtu anaweza kuhudhuria na kuwa muumini, na si lazima awe mjumbe.

Mjumbe lazima awe muumini.

Idadi ya wanaoamini lazima iwe ndogo kuliko idadi ya wanaohudhuria na kubwa kuliko idadi ya wajumbe.

Idadi ya ubatizo: 92—93—94—95—96—97—98—99—2000
Idadi ya familia (mme/mke wanaohudhuria:__________

**B. Vipindi**

*Angalia kila shughuli iliyotolewa na kanisa na tambua kushiriki katika shughuli hizo*

| Shughuli | Kanisa kutoa | Idadi ya walioshiriki |
|---|---|---|
| Shule ya jumapili ya watoto (kwa umri ) | | |
| Kuabudu | | |
| Vikundi vya vijana | | |
| Vikundi vya watoto | | |
| Kikundi cha wanawake | | |
| Kikundi cha wanaume | | |
| Umishenari | | |
| Uinjilisti | | |
| Mafunzo ya kufuasa | | |
| Kikundi cha kujifunza Biblia nyumbani | | |
| Mafundisho kwa waumini wapya | | |
| Mafundisho ya uongozi | | |
| Mafundisho ya ualimu | | |
| Mkutano wa maombi | | |
| Kwaya | | |
| Huduma ya jeshi | | |
| Huduma ya kanisa jipya | | |
| Huduma ya maandishi | | |
| Huduma kwa njia ya Redio/TV | | |
| Huduma ya wafungwa | | |
| Huduma ya walevi/wavuta madawa ya kulevya | | |
| Huduma ya hospitalini | | |
| Huduma ya watoto yatima | | |
| Huduma ya kutunza wazee | | |
| Huduma ya maombi | | |

**C. MPANGO**

1.Kuna mpango wowote maalumu wa huduma kwa mwaka huu? Ndiyo_______Hapana_______
2.Ni mipango ipi hiyo?

3.Mipango ya mwaka ujao imeanza? Ndiyo_____Hapana____

4.Ni nini mipango hii?

5.Kuna uongozi unaopanga kwa ajili ya kanisa? Ndiyo___Hapana___
6.Kanisa lina hati ya dhumuni? Ndiyo____Hapa____
7.Kanisa lina mipango ya kifedha? Ndiyo____Hapana____
8.Kanisa lina mpango wa kukua kiroho kwa waumini? Ndiyo____Hapana___
9.Kanisa linashirikiana na makanisa mengine? Ndiyo____Hapana____
10.Kanisa linashirikiana na madhehebu mengine? Ndiyo____Hapana____

**ENEO LINALOLENGWA AU UKAGUZI WA "MUZUNGUKO"**

**A. NANI**

1. Kuna kundi lolote maalumu la watu katika kanisa wanaoshawishi mzunguko?

2. Kuna daraja moja la jamii linalotawala zaidi katika mzunguko? Ndiyo___ Hapana

3. kama ni "ndiyo" ni lipi

**B. NINI?**

Ni tabia zipi dhahiri za "mzunguko" wa kanisa?

Ni hitaji lipi la watu linalohitaji ufumbuzi wa haraka katika "mzunguko"?

Kiuchumi____Kiroho____maadili____kijamii____kielimu____kiutamadini____kifamilia____kidini____

Ni kundi gani la kidini lililopo katika "mzunguko" wa kanisa?

Othodox____#____Babtisti____#____Pentekosti____#____Romani Katoliki____#____Lutherani____#____Wapinzani____#____Wasio wa dhehebu____#____ Waislamu____#____makundi ya kimishenari ya nje____(tafadhali nukuru makundi haya yanaweza kuwa yapi:_________________________)

Kanisa linajaribu kugusia mahitaji ya watu? Ndiyo____Hapana____

Kama ndiyo, ni nini hasa kanisa linafanya kuhudumia mahitaji yaliyopo katika "mzunguko" wao?

Maelezo ya kusudi la kanisa yanaonyesha haja ya kugusa mahitaji ya "mzunguko" wao? Ndiyo____Hapana____

Mpango wa huduma ya kanisa unaonyesha kujali kuhudumu kihistoria kwenye mzunguko wao? Ndiyo____Hapana____

**C. JINSI GANI?**

1. Kanisa linajifananisha na mzunguko wake? Ndiyo____Hapana____

2. Kama ni "ndiyo" Jinsi gani?

______________________________________________________________________________
______________________________________________________________________________
____________________________

3.Kama ni "hapana" ni nini kanisa lifanye kuanza kujifananisha na "mzunguko" wao?

4.Shughuli za kanisa zimepangwa katika namna ambayo zinaufikia "mzunguko" wake?
Ndiyo____Hapana____

5.Ni jinsi gani kanisa linalingana na makanisa mengine ya kiinjili ya kiprotestanti katika "mzunguko" wake?

Linaendana vizuri na yote____

Linaendana vizuri na baadhi, lakini si vizuri sana na mengine____

Haliendani vizuri na lolote____

**D. RASILIMALI**

Ni aina gani ya rasilimali zilizopo kwenye kanisa kwa ajili ya "mzunguko" wake?

TV/Radio____Maandishi____Nyumba ya uchapaji____Kibali cha kiofisi cha "kusaidia" huduma____Kushirikiana na makundi mengine ya wakristo wa makanisa ya kiinjili ya kiprotestanti (makanisa mengine ya mtaa____mawakala/mashirika ya kigeni ya kimishenari____Vyama____palipo katikati____miungano____mashirika ya kielimu-____)

Ni makundi gani ambayo kanisa linashirikiana nayo kwa sasa katika mradi maalumu wa huduma?

______________________________________________________________________________
______________________________________________________________________________
__________________________________

Juhudi zimefanywa na kanisa kuzungumza na makanisa mengine yaliyo kwenye"mzunguko" juu ya kufikia wasiookoka kwenye "mzunguko kwa ajili ya Kristo? Ndiyo—Hapana—

Uongozi wa kanisa utakuwa tayari kufanya kazi na makanisa mengine na mashirika kumfikia kila mmoja katika "mzunguko" kwa ajili ya Kristo?

Kama "ndiyo" ni lini watajaribu kukusanya "mzunguko wa rasilimali" kuzungumzia juu ya kutimiza Utume Mkuu katika mzunguko wao?

______________________________________________________________________________
______________________________________________________________________________
_________________________________

"kama hapana," Ni kwa nin Siyo?

______________________________________________________________________________

# KANISA – Azimio la Mafunzo 1

## **Misingi ya Kibiblia Kwa kanisa:** Kanisa katika Mpango wa Mungu kwa Vizazi

**I. MPANGO WA MUNGU KWA VIZAZI**

**Mungu ni mwenyezi juu ya ulimwengu (Zab 29:10; Da 2:20-21; 4:34-35; 5:21).**
**Shetani aliasi (Isa. 14:3-21, Eze 28:11-17).**
**Uasi duniani (Mwa 1:28;2:7).**

| KAMA DARASA NI KUBWA KUPITA 9 GAWANYIKA KATIKA MAKUNDI MADOGO. |
|---|

Ni nini matokeo ya dhambi ya mtu?
Jinsi gani unaweza kuelezea mpango wa Mungu wa ukombozi?
Ni nini mstari hapo juu wa maandiko unachotuambia kuhusu mpango wa Mungu?
Ni nini **1 Yohana 4:16** inachotuambia kuhusu ukweli kwamba Mungu ni pendo?
Ni sifa gani zingine za Mungu zinazoweza kuonekana katika uumbaji wake, uumbaji wake wa mtu kwa mfano wake, kutokea kwa dhambi, na hatima ya mpango wake wa ukombozi?

II. **KUANZISHWA KWA KANISA**

**A. Kutabiliwa kwa Kanisa: Mathayo 16:18-19**

1. Ni nini msingi wa huduma yako ya kanisa?
2. Nini kinachotokea wakati Kristo anapokuwa siyo msingi wa kazi mpya ya kanisa?
3. Kanisa lipo kwa ajili ya ulimwengu (**Efe 3:1-10**). Ni nini muonekano?
4. Kristo ni kichwa cha kanisa. Ni nini muonekano wa kivitendo wa hili? **Efe 1:23; Col 1:18**
5. Jinsi gani tunamruhusu kuwa Bwana na Mfalme kwa ngazi ya kivitendo?

**III. WAJIBU NA ASILI YA KANISA LEO**

**A. Kanisa—WatuWalioitwa kwa Yote Kimtaa na Kujidhirisha Kwa Wote (Efe 1:10)**

Tambua kuwa kanisa la mtaa linaweza kutafasiriwa kwa njia nyingi:

-  **Kanisa la nyumba: 1 Wakorintho 16:19**
-  **Kanisa la jiji: 1 Wathesalonike 1:1 1 Wakorintho 1:2**
-  **makanisa ya mkoa: Wagalatia 1:2** (Makanisa kwa Wagalatia)

**B. kanisa ni Mwili wa Kristo**

**Rum 12:4-5; 1Kor 12:12-31; Efe 1:22-23; 4:4-16**
**Mwili Unategemeana (Rum 12:3-8, 1Kor 12:12-31**
**Mwili Una Kichwa Kimoja -- Kristo (Col 1:18).**

**C. Kanisa ni Chombo Cha Kwanza Cha Mungu Cha Kuenezea Injili (Mt 28:19-20).**

- ✓ Muumini anaweza kuwa sehemu ya kanisa la wote na asiwe sehemu ya kanisa la mtaa?
- ✓ Ina maana gani kwa kanisa kuwa mwenyeji?
- ✓ Jifunze baadhi ya methali zilizotumiwa kuelezea kanisa **(Efe 2:15, 19, 21)**

## UTEKELEZAJI WA AZIMIO

Jinsi gani Mungu alivyo kazini katika nchi yako kutimiza ahadi yake? Ni nini Mungu amefanya kwa mwaka uliopita, miaka 5, au miaka 50, ambacho kinadhihirisha uaminifu wake wa kujenga kanisa**?** **Andika angalau uchunguzi 10 kuonyuesha uaminifu wa Mungu katika mandhali ya nchi yako.**

# KANISA – Azimio la Mafunzo 2

## **Kusudi la Kanisa:** Kwa nini Kanisa Lipo?

Ni nini unachoelewa kuwa makusudi ya kanisa?

**I. KUSUDI LA KANISA**

**A. Kumwinua Bwana -- (Rum 15:6,9; Efe 1:5ff; 2The 1:12; 1Pet 4:11).**

-  Ina maana kwako kumtukuza Mungu?

- Jinsi gani kanisa linamtukuza Mungu?
- Ni jinsi gani Mungu anatukuzwa kati kati yetu?

**B. Injilisha waliopotea -- (Lk 19:10; Yn 20:21)**
**C. Adilisha Watenda Kazi – (Waefeso 4:11-16**)
- Uongozi umetolewa (Efe 4: 11) kuwaandaa watakatifu kwa ajili ya hudum (Efe 4: 12), na siyo tu kufanya kazi ya huduma wao wenyewe. Ni nini muonekano wa ukweli maalumu kwa kazi yako ya upandaji kanisa? Jinsi gani hili litagusa jinsi unavyofanya unachofanya?
- Ni uchunguzi upi unafanya kutoka katika Efe 4:11-16 kuhusu upandaji kanisa?

**II. MAPANA KATIKA KUELEWA KUSUDI LA KANISA**

A. Jinsi gani unaweza kulinganisa kanisa linalozingatia vipindi kwenye Kanisa la Utume Mkuu?
B. Jinsi gani unaweza kulinganisha kanisa kama "Chombo cha Huduma" Ikilinganishwa na kanisa kama "Wakala wa Kuhamasisha?"

**Matayo 28:18-20**
1. Ni faraja gani iliyopo kwenye ukweli kwamba "mamlaka yote" yametolewa kwa Kristo?
2. Kwa kuwa Bwana ni mwenyezi, Nini alichotuomba kufanya?

**Marko 16:15-20**
1. Ni onyo gani unapata hapa kwa wasioamini?
2. Nini kitakuwa kithibitisho kinachofatana na waumini?
3. Jinsi gani bwana alijidhihirisha mwenyewe baada ya kupaa kwake mbinguni?

**Luka 24:45-53**
1. Ni vitu gani wanafunzi wanatakiwa kushuhudia?
2. Ni ahadi gani Kristo alikuwa anafanya kwao?

**Yohana 20:19-23**
1. Yesu alimaanisha nini aliposema, "Amani iwe nanyi"?
2. Jinsi gani hili linaendana na maelezo yake katika vv. 22-23?
3. Ina maana gani kutumwa?

**Matendo 1:1-11**
1. Ni matokeo gani ya asili tunapokuwa na Roho Mtakatifu akifanya kazi kupitia sisi?
2. Ni kwa umbali gani matokeo ya injili yatafika?

**MASWALI YA KUTUMIA**

**KAMA DARASA LINA ZAIDI YA 9 GAWANYIKA KATIKA MAKUNDIMADOGO**

Ni hofu gani ulizonazo zinazohitaji kushindwa kwa kutambua mamlaka makuu ya Kristo? Jinsi gani unaweza "kufanya wanafunzi vyema?"

Jinsi gani injili inaweza kutangazwa "kwa mataifa yote" katika nchi yangu?

Unahudumu kwa nguvu ya Mungu ndani yako? Jinsi gani unaweza kuruhusu nguvu yake kuwa kubwa kwa ajili ya utukufu wake?

Jinsi gani unajali hali ya waliopotea? Jinsi gani hili litagusa jinsi unavyoongoza kanisa unalopanda? Ni tofauti gani linafanya?

# KANISA – Azimio la Mafunzo 3

## Mfumo na kazi: Mtazamo wa Kibiblia na Kiutamaduni

**Kazi=Shughuli zinazotokana na kibiblia ambazo zinahitajika kufanyika.**
**Mfumo=njia inayochaguliwa kufanya kazi.**
**I. Mfumo na kazi katika kanisa**
- Toa mfano wa kazi katika kanisa.
- Toa mfano wa mfumo katika kanisa.

Kwa Kazi, **Maombi**, Baadhi ya mifumo ni (1) kupiga magoti au kusimama, (2) kimya au kwa sauti, (3) kundi dogo au mtu pekee, (4) kabla au baada ya ibada, na (5) toba au kusihi.
Kwa Kazi, **Fundisha neno,** baadhi ya mifumo ni (1) darasa la jumapili (2) mahubiri, (3) kujifunza Biblia katika makundi madogo, na (4) sala ya familia.

Kwa Kazi**, Uinjilisti**, baadhi ya mifumo ni (1) uinjilisti wa kirafiki, (2) mikutano ya hadhara na (3) kukaribisha kanisani.

- Ni ipi badala ya mifumo ya maombi unayotumia zaidi mara nyingi? Ni mifumo ipi inatumika "kufundisha neno?" Ni mifumo ipi unatumia kuinjilisha?
- Unaweza kusema kwamba mfumo mmoja kawaida ni bora kuliko mingine ya maombi, kwa kufundisha neno, na kwa uinjilisti?

Ni baadhi ya mifumo ipi ambayo inaweza kutumika kwa kazi ya utoaji?
Ni baadhi ya mifumo ipi inaweza kutumika kwa kazi ya kuabudu?

Kwa kila moja ya mifumo ifuatayo, nieleze ni kazi ipi inaendana: Kambi ya Vijana, Mkutano wa Maombi wa Kanisa, Kwaya ya Kanisa, Kupitisha Sahani ya Sadaka, Jengo la Kanisa, Mziki Maalumu katika Ibada, kanisa la watoto, Kutaja Mistari Kanisani.

**II. Kanuni Kuhusiana na Mfumo na Kazi**

1. Tazama **Mathayo 9:14-17**. Jinsi gani mafundisho ya Yesu juu ya uvaaji na ngozi ya kugawia divai yanavyoendana na mfumo na kazi? Ina maana gani 'ngozi mpya ya kugawia divai' aina ya kanisa? Ni nini **Mathayo 12:1-8** inachangia kwenye swala hili? Ni mifumo ipi inatumika kwenye uwakili katika kanisa lako? Jinsi gani hii inalingana na **1Kor 16:1-2?**
2. Ni kanuni ya kanisa kwamba mifumo **irithiwe kwenye utamaduni.** Kuna mifumo yoyote kanisani kwako ambayo haiendani tena na utamaduni ambao kanisa lako lipo. Kuna mifumo unayotumia kwenye kuabudu, ubatizo au utawala ambayo isingeweza kufaa vyema kwa baadhi ya makanisa?
3. Unaweza ukafikiria kundi lolote la watu katika eneo lako ambalo linaweza lisiitikie vyema kwa baadhi ya mifumo yako (kuabudu, maombi, kuhubiri, n.k.) ambayo inatumika katika kanisa unalohudhuria? Jadili mifumo hii na nini kinatakiwa kufanyika kama unapanda kanisa kwa watu hawa kama walengwa?

> "Siyo kawaida kwa kijana, ambaye ndiyo anatoka chuo cha seminari au chuo cha Biblia, bila kuwa na uzoefu halisi wa kichungaji, kuwa mchungaji na kufikiri kwamba anajua hasa jinsi kila kitu kinavyotakiwa kufanyika. Ana ufahamu wa nini mifumo kamili ilivyo na anatarajia kubadili kila kitu ili kwamba iendane na mawazo yake. Hana habari na nini watu wanachopenda, wala kujua nini wanachotaka kufanya. Anaweza hata asijue kawa mawazo hayo yalishajaribiwa kabla na matokeo yake. Hii inaweza kupelekea kwenye hali ambapo watu wanaanza kufikiria kwamba mchungaji wao hawathamini isipokuwa kuwaona kama sehemu ya majaribio na kuchukizwa naye. Pia wanajisikia kana kwamba kanisa haliwafai tena na kwamba ama mchungaji aondoke ama wao wataondoka."

- Ni nini kitendo hiki cha mchungaji mchanga hapo juu kinachotuambia kuhusu uongozi wake wa utumishi na upendo wake kwa kusanyiko? Ni nini unachoweza kumwambia kinachoweza kumsaidia kuona kosa lake?

> "Mifumo inatakiwa ibadirishwe tu kusisistiza kazi. Wakati mmoja, ili kusisitiza kuabudu (kazi), mchungaji alianza ibada kwa wimbo wa sifa (kama kawaida) na kisha akatoa mahubiri. Mahubiri kawaida yanakuwa mwishoni mwa ibada baada ya mziki maalumu, kuimba kwa mda mrefu, salaamu na matangazo, lakini mchungaji huyu akachagua kuzungumzia juu ya Mungu na kazi zake za ajabu, na kisha akakaribisha kusanyiko kwenye kuabudu na kumshukuru Mungu kwa maombi, kuimba nyimbo za sifa na chakula cha Bwana. Badiliko lilikuwa la ufanisi. Hii haimaanishi kwamba alifanya hilo kila jumapili. Lilikuwa limefanyika wakati huo mmoja ili kuwafanya watu kuacha na kufikiria katika namna tofauti juu ya sehemu ya kuabudu ya ibada. Kisha walirudi kwenye mfumo wa kawaida."

- Watu katika kanisa lako wanaweza kuridhika na badiliko hili la juma moja katika ibada? Kwa nini na kwa nini siyo?

## Maswali ya marudio, kutafakari na matumizi

**KAMA DARASA NI KUBWA KULIKO 9, GAWANYIKA KATIKA MAKUNDI MADOGO.**

Kwa nini 'mfumo na kazi' ni muhimu sana kwa upandaji kanisa?

Jinsi gani mifumo katika kanisa lako imeendelezwa? Jinsi gani imetunzwa?

Je mifumo katika uzoefu wako wa kanisa inakidhi kusudi/kazi ya kibiblia?

Jinsi gani unaweza kukuza mifumo katika kanisa lako kuendana na utamaduni vyema?

Ni mifumo ipi ni kizuizi cha kuleta injili kwa waliopotea? Kuwaleta wakata shauri wapya katika maisha ya kanisa?

Ni aina gani ya upinzani unaweza kukutana nao kama ungefikiria kuanzisha kanisa mpya kwa mifumo tofauti na makanisa mengine katika utamaduni wako?

Ni kwa njia zipi mifumo yako ni migeni na ya kigeni kwa wakata shauri wapya?

# KANISA – Azinio la Mafunzo 4

## **Kutafsiri kanisa la Mtaa:** "Nini Tunachopanga?"

**I. Ugumu wa Kutafsiri Kanisa**

1. Lini kundi la watu ni kanisa?
2. Ni kigezo gani cha kuamua endapo kama ni kanisa au la?
3. Itikia kwenye hali zifuatazo. Ni kila moja ni kanisa? Kwa nini na Kwa nini siyo?

**II. Mifano ya Tafsiri ya Kanisa**

A. Mfano #1

Tafsiri ifuatayo ni jaribio la kutafsiri kanisa kwa kutumia marejeo maalumu kutoka kwenye maandiko yanayoelezea jinsi watu wa Mungu wanavyotakiwa kuhusiana mmoja kwa mwingine. Tafsiri hii inasisitizia mahusiano ambayo yanatakiwa yawepo kati ya waumini.

"Knisa ni kundi la watu waliojitoa na kutoa mapendeleo kwa mmoja kwa mwingine (Rum 12:10), wanaokubaliana mmoja kwa mwingine (Rum 15:7), wanaojaliana mmoja kwa mwingine (1Kor 12:25), wanaobebeana mizigo (Gal 6:2), wanaosameheana (Efe 4:32), wanaotiana moyo na kujengana (1The 5:11) wanaochocheana juu ya kupenda na matendo mema (Ebr 10:24), kuungama dhambi mmoja kwa mwingine (Yak 5:16), kuombeana (Yak 5:16), kuhudumiana (1Pet 4:10), na kupendana (1Yn 4:11)."

Jinsi gani tafsiri hii itafanikisha au kuzuia utaratibu wa upandaji kanisa?

Ni aina gani ya kanisa linaweza kuzalishwa na kundi la watu waliojitoa kwenye tafsiri hii?

Tafsiri hii inatoshereza? Kwa nini na kwa nini siyo?

B. Mfano #2

"Kanisa la mtaa la Agano Jipya ni kusanyiko lililoandaliwa la waumini waliobatizwa, ambao uwepo wa kipekee wa Yesu Kristo unakaa; wanaokusanyika mara moja moja kwa ajili ya kuabudu, maelekezo, kushirikiana, meza ya Bwana, na kuwabatiza waumini wapya, chini ya utii wa neno la Mungu, wakisimamiwa na wazee wanaosaidiwa na mashemasi wakiweka katika vitendo vipawa vya kuwezesha ambavyo Mungu amewapatia wajumbe wake kujenga kusanyiko hilo la kanisa la mtaa, inayopelekea kushuhudia injili kimtaa na kwa ulimwengu mzima."

Jinsi gani tafasiri hii itafanikisha au kurudisha utaratibu wa upandaji kanisa?

Ni aina gani ya kanisa linaweza kuzalishwa na kundi la watu waliojitoa kwenye tafsiri hii?

Tafsiri hii inatoshereza? Kwa nini na kwa nini sityo?

C. Mfano #3

Tafsiri ifuatayo zaidi ni ya kimapokeo na inaweza kuwa tafsiri utakayoisikia kutoka kwa wastani ya wasioamini mtaani.

"Kanisa la mtaa ni jengo mahali watu wanapokusanyika kupata huduma ya kidini kutoka kwa muhudumu mtaalamu ambaye amefunzwa maalumu kuendesha mikutano kila jumapili asubuhi vile vile na shughuli zingine kwa watu kama vile ndoa na misiba."

Jinsi gani tafsiri hii itafanikisha au kurudisha utaratibu wa upandaji kanisa?

Ni aina gani ya kanisa linaweza kuzalishwa na kundi la watu waliojitoa kwenye tafsiri hii?

Tafsiri hii inatoshereza? Kwa nini na kwa nini siyo?

D. Mfano #4

"Kanisa la mtaa ni mwili uliojipanga wa waumini waliobatizwa, wakiongzwa na mchungaji anayestahili kiroho, akihakikisha uhusiano wao kwa Bwana na kwa mmoja kwa mwingine kwa wanaotimiza kufanya meza ya Bwana mara moja moja, waliojitoa kwenye mamlaka ya neno la Mungu, wanaokusanyika mara moja moja kwa ajili ya kuabudu na kujifunza neno, na kuugeukia ulimwengu kuushuhudia."

Jinsi gani tafsiri hii inafanikisha au kurudisha utaratibu wa upandaji kanisa?

Ni aina gani ya kanisa linaweza kuzalishwa na kundi la watu waliojitoa kweny tafsiri hii?

Tafsiri hii inatoshereza? Kwa nini na mwa nini siyo?

**III. Mipaka katika Kutafsiri Kanisa**

A. Epuka **kusisitiza mifumo**, muundo na vipindi kwenye tafsiri.

B. **Kazia kazi za kibiblia** ambazo kanisa lazima lifanye.

**IV. Uandikaji wa Tafsiri yako ya Kanisa**

Ni kanuni ipi unapata katika kila moja ya mistari hii?

| | | |
|---|---|---|
| **Mdo 2:42-47** | **1Kor 12:28** | **Efe 5:27** |
| **Mdo 14:23** | **1Kor 14:33** | **Ebr 10:24-27** |
| **Mdo 20:7** | **Efe 1:22** | |
| **Mdo 20:28** | **Efe 4:11-16** | |

Waulize wapanda kanisa kufanya yafuatayo kipekee.

Kuandika tafsiri yako ya kanisa.

Fikiria maswali yafuatayo kuhusiana na tafsiri yako.

Tafsiri yako inaeleweka?

Inaendana na maandiko?

Tafsiri yako ni ya msingi vya kutosha kuelezea makanisa yote kila mahali na wakati wote?

Je tafsiri yako inaruhusu kanisa linalozaliana?

Uliza baadhi katika darasa kushirikisha tafsiri zao kwenye darasa

1. Ni vitu gani visivyo vya lazima hasa hasa vinaongezwa kwenye tafsiri ya watu inayofanya kazi ya kanisa?
2. Lini jengo ni la lazima kwa upandaji kanisa? Jinsi gani majengo yanaweza kusaidia au kurudisha nyuma ukuaji wa kanisa?
3. Kwa nini ni makosa kukazania kwenye mifumo unapotafsiri kanisa la mtaa**?**

## Utekelezaji wa Azimio

Pamoja na timu yako ya upandaji kanisa, anzisha na kubaliana juu ya tafsiri ya kanisa ambayo itajulisha utaratibu wenu wa upandaji kanisa. Shirikisha tafsiri yako na wapanda kanisa wengine, mkufunzi wako au mshauri.

# TABIA YA KIROHO—Azimio la Mafunzo 1

### **Kuhesabiwa haki kwa imani:** Msingi Wetu wa Uhusiano na Mungu

Jinsi gani tunaweza kumjua Mungu kwa ukaribu?

Mungu anatukubali kweli kweli?

Ni wapi kukubaliwa kwetu mbele za Mungu kunakotoka?

Jinsi gani tunaweza kuishi maisha yanayompendeza?

Nini kinachotokea tunapofanya dhambi?

**I. Kuhesabiwa haki siyo --**

- **A. Kwa kazi**
- **B. Kusikilizwa**

**II. Kuhesabiwa haki ni**

- **A. Utakatifu wa Mungu: Warumi 3:21-24**
- **B. KubadirishanaKukuu Kor 5:21, Isa 61:10, Rum 4:3-5, 8:1, Efe 4:22-24**

**III. Swala la lazima la kuhesabiwa haki kwa imani**

- A. Tunaweza kujihesabia haki wenyewe?
- B. Tunaweza kuchukua sifa kwa alichofanya Mungu?

Mfano: Fikiria mtu aliyefanya uharifu mbaya sana, na anasubiri adhabu ya kifo. Anapokuwa anasubiri, mmoja wa rafiki zake anakwenda kwa hakimu na kuomba kusikilizwa kwake. Hakimu anajibu, " nitamwachilia, kama utanipa kijana wako kufa badala yake. Rafiki anasema, "Huu ni upuuzi. Jinsi gani naweza kufanya hivi kamwe" lakini hakimu anasema, "Hii ndiyo njia pekee ninayoweza kumwachilia huru." Baada ya maumivu, baba anaamua kuwa atajitoa kutoa kijana wake kwa ajili ya rafiki yake…akijua ndiyo njia pekee. Kwa kutii, kijana anakwenda kwa hakimu na kukubali kufa badala ya rafiki wa baba yake. Siku inayofata hakimu anamunyonga kijana na kumwacha huyu mtu huru. Mara baada ya hili, baba anakuja kusikia majadiliano kati ya mfungwa aliyeachiliwa na rafiki. Alipoulizwa, "Jinsi gani uliwekwa huru kutokana na adhabu yako ya kifo?" mtu aliyeachiliwa anajibu, "Hhu, nilipokuwa ningali jera nilijitunza mwenyewe safi, nikajiheshimu, na kufanya alichoniambia mlinzi. Kisha wakaniachilia kwa sababu ya tabia yangu njema."

Unafikiria nini juu ya kile mtu huyu alichojibu kwa kile rafiki yake alichosema? Jinsi gani mtu huyu anaweza kufikiria kuwa tabia yake ilichangia kwenye kuachiliwa kwake baada ya kijana wake kuachia masha yake kwa ajili yake?

- C. Tunaweza tukamtumaini Mungu kabisa na peke yake?

Andika tafsiri yako ya "kuhesabiwa haki kwa imani."

Ina maana gani tunapoelezea kuhesabiwa haki kwa imani kama "haki ya kutendewa"?

Katika kutembea kwetu kila siku na Bwana, kwa nini ni vigumu sana kwetu tulioanza katika neema kuendelea katika neema, tukitumaini katika kazi iliyomalizika ya Yesu Kristo msalabani?

Jinsi gani kuhesabiwa haki kwa imani kunagusa namna unavyohusiana na Mungu na namna unavyofikiri Anajihusisha kwako?

## Utekelezaji wa Azimio

Mfundishe mtu mwingine tu maana ya kuhesabiwa haki kwa imani, na kisha mfanye kuandika tafsiri yeye mwenyewe. Leta walichoandika kwenye kipindi kijacho cha mafunzo.

# TABIA YA KIROHO—Azimio la Mafunzo 2

### **Kuishi kwa Injili:** Kukataa kujitumainia

Jinsi gani unafikiri kuamini kwako kwa injili kuhusu kuhesabiwa haki kwa imani peke yake kunagusa ukuaji wako katika Kristo leo?

Yesu anazungumzia kuokoka kwa imani katika **Yohana 3:36.** Katika Warumi, Paulo wazi wazi anawakilisha ujumbe wa kuhesabiwa haki kwa imani peke yake: Kufuatana na vifungu hivi vitatu, ni nini matakwa ya kuhesabiwa haki?

**Warumi 1:16, Warumi 4:5, Warumi 10:9-10**

Katika wagalatia, Paulo anathibitisha wokovu kwa imani. **Wagalatia 3:2-5** Katika Wagalatia 3:2-5, Paulo anatoa matokeo mawili ya imani (kuamini). Ni yapi? Ni lengo lipi analorejeza kwake?

Ni nini **Wagalatia 4:15** anatuambia kwamba alikuwa amepotea kwa sababu ya kujaribu kutunza sheria ya kuhesabiwa haki?

Ni nini hatari za kujitumainia? Jinsi gani waumini Wagalatia wameangukia mbali kutoka kwenye injili? Unakubaliana na maelezo haya, "Kutumainia katika rasilimali zetu pengine ndiyo kielelezo cha kutokuamini?"

Kama mfano, ngoja tulinganishe siku mbili katika maisha yako. Jumamosi moja unaamka na kwenda kwenye mkutano wa maombi, kama ilivyo kawaida yako. Ukiwa unakwenda, unakuwa na mazungumzo mazuri mafupi na jirani yako. Unaendelea kwenda kuwa na siku njema ambapo uwepo wa Mungu ni dhahiri kwa njia nyingi. Unaporudi nyumbani, unapata nafasi ya kushirikisha injili kwa mtu flani, na kwa hiyo unamshirikisha Kristo na wokovu wake kwake. Jumamosi inayofata inakuwa tofauti kidogo. Unaamka ukiwa umechelewa, unakosa mkutano wa maombi, na kuongea siyo kwa upole na jirani yako ukiwa unatoka nje. Kwa ujumla siku inajawa na kuchanganyikiwa na Mungu anaonekana kutokuwa karibu. Unaanza kujisikia vibaya kuhusu uliyofanya, lakini kwa kukushangaza, unapata nafasi nyingine kushirikisha injili kwa mtu fulani.

Utapitwa na nafasi hiyo ya kushirikisha injili kwa sababu unajisikia kana kwamba hufai kwa hilo? Unafikri inawezekana Mungu kukubariki katika siku mbaya? Kama siyo, kisha kwa nini siyo?

**Mfano:** Mfano:

Tarehe 21, mwezi wa nane 1544, Martin Luther alimwandikia rafiki mmojawapo mwaminifu na wa kutumainiwa, George Spalatin. Spalatini alikuwa ameshampa ushauri ambao baadaye alikuja kuuona kama dhambi. Alipofikia suluhi hili, alikuwa amezama katika uchungu na hatia. Alikuwa ameshawishika kwamba angelijua vizuri zaidi na kwamba yeye wa watu wote asingelifanya kosa hilo. Hakuweza kushauriwa, Wakati Luther alipojua juu ya hali yake, alimwandikia kumfariji, kwa kusema, "…ombi langu la uaminifu na onyo la upole ni kwamba uungane na kampuni yetu na ushirikiane nasi, tulio halisi, wenye nguvu na waliojaa dhambi. Ni lazima kwa njia yoyote usimfanye Yesu kuonekana kuwa mnyonge na hafifu kwetu, kana kwamba anahitaji kuwa msaidizi wetu wakati tu tunataka kuepukana na kivuli cha kuwazika, majina, na dhambi za kitoto. Hapana! Hapana! Hiyo haitakuwa nzuri kwetu. Ni lazima afadhali awe mwokozi na mkombozi wa uhakika, mkuu, mzito, anayehukumu uovu na uasi, mwenyezi, na kutoka katika dhambi kuu zaidi na za kutisha kupindukia, kuwa na machache, kutoka kwenye dhambi zilizowekwa pamoja katika jumala…" Kutoka: Martin Luther Mwandamizi kwa Wakristo wa Wakati ule.

Tumegeuka kuwa wenye dhambi wadogo tunaohitaji Mwokozi mdogo au tu wenye dhambi halisi tunaohitaji Mwokozi halisi? Elezea.

Nini kinatokea tunapoongeza kingine kwa kile Kristo alichofanya?

Unapoteza hisia yako ya furaha katika Kristo? Kama ni hivyo, kwa nini?
Jinsi gani injili inahusika kwetu kama waumini?
Ni nini tofauti kati ya juhudi za binafsi na imani?
Jinsi gani kuishi kwa imani kunavyogusa kufikiri kwetu kwa kila siku na matendo katika maisha?

# **TABIA YA KIROHO—**Azimio la Mafunzo 3

## **Ukuaji wa Kikristo:** Kumfanya Kristo kuwa Kiini cha Kuangalia Katika Maisha

Jinsi gani tunaweza kujilinda kutokuwa meli iliyovunjika kwa dhambi? Jinsi gani tunaweza kukua katika imani yetu, ili kwamba tuwe na uhusiano nyeti na Yesu Kristo?

**I. Ni nini Ukuaji Kiroho? Ni nini Flp. 2:12-13** inachotuambia kuhusu ushirika tulio nao na Mungu katika ukuaji wetu?

**II. Jukumu la Msalaba Katika Ukuaji Kiroho**

- **A.** Ni nini mistari hii inatuambia kuhusu **Ukuaji katika ufahamu wa Utakatifu wa Mungu? -- Yer. 9:23,24, Yohana 17:3, Flp l. 3:8**
- B. **Kujifunza kuzitambua dhambi zetu – Efe. 3:8, 1 Tim. 1:15**
  1. jinsi gani tunaweza kuutambua vyema udhambi wetu?
  2. Jinsi gani utambuzi wa dhambi zetu unaendana na utu?
- **C. Mwanya Unatokeo kati ya Utakatifu wa Mungu na dhambi zetu--Warumi 8:10; 1 Yohana 1:9**

Ni nini kinaongeza kiwango chetu cha ukuaji kwenye ukomavu?
Ni nini kinapunguza kiwango chetu cha ukuaji?

**III. Vipingamizi Kwenye Ukuaji wa Wakristo.**

A. Ufarisayo ni kuishi kufuatana na matakwa, wajibu, na kujitoshereza (kwa uwezo wetu) –tatizo la kiburi. Ni nini **Luka 10:38-42** inatuambia ni ufunguo kwa ukuaji badala ya kiburi?

Ufarisayo unakuwaje unapokuwa umeonyeshwa kuelekea kwa Mungu? Ufarisayo unakuwaje unapokuwa umeelekezwa kuelekea kwa mwenzi wako? Jinsi gani mwenzi wako atafanya? Toa mfano.

B. Kuachilia – Ukosefu wa Imani – Ni nini **Waebrania 10:14** inatuambia kuwa tunatakiwa kuwa na imani ambayo tutaondoa mwanya kati ya utakatifu wa Mungu na dhambi zetu?

Nini tunachoweza kufanya kushindwa kuachia?

C. Kwa mwanya kuzibwa, nini kinatakiwa kikue katika mkazo wetu?—**Wagalatia 6:14a**

Jinsi gani tunaweza tukajilinda na kutokuvunjika kama meli kwa dhambi. Jinsi gani tunaweza kukua katika imani yetu, ili kwamba tuwe na uhusiano hai nyeti na Yesu Kristo?

Kama bado kuna dakika 15 zilizobaki kumalizia yafuatayo, yafanye darasani. Kama mda haupo, watayafanya kma "UTEKELEZAJI WA AZIMIO" wa somo.
Wapange wanafunzi na kisha waombe kufanya yafuatayo.

Mwelezee mtu mwingine ulichojifunza kuhusu ukuaji katika utakatifu na waelezee jinsi unavyoweza kutumia makamilisho ya Kristo katika maisha yako ya kila siku. Toa mfano wa mabadiliko maalumu katika maisha yako kama muumini kama matokeo ya kuongezeka kwa kuelewa kwako kwa utakaso.

# TABIA YA KIROHO – Azimio la Mafunzo 4

## **Uwezo wa Injili Inayobadilisha:** Uhuru Kutoka Utumwa wa Dhambi

Kuelewa uwezo wa injili inayobadilisha, lazima tutambue hali na mtazamo katika maisha ya mwanadamu. **Kwanza, hali ya maisha bila Kristo ni hiyo ya kutumikishwa na dhambi.** Katika hali hii ya kupotea , tu watumwa kwenye dhambi na hatuwezi kuwa huru kutokana na kusongwa kwa "mwili" (**Rum. 3:11-12; Rum . 6:16-18) Pili, mtazamo wa Mungu kwenye maisha ya muumini ni kwamba kifo cha kujitoa cha Yesu kinafunika dhambi zetu na hatuko tena kwenye hali ya "utumwa wa dhambi" lakini watakatifu."** Tumefunguliwa kutoka katika adhabu ya dhambi na kutoka katika nguvu ya dhambi. Tunaishi katika uhuru wa kweli kumpenda Yeye. Asili ya dhambi imekufa na hatuishi tena chini ya ukandamizaji wake, tumeungana na Kristo. (**2 Kor. 5:17-20**). **Tatu, "uzoefu wetu wa maisha" hauwakilishi kikamilifu ukweli huu halisi wa Mungu wa hali iliyotolewa ndani Yake.** Ni lazima tutambue dhambi zetu za kila siku na kuziungama, kuunganisha mawazo yetu na akili ya Mungu. Asili ya dhambi siyo bwana wetu, lakini kawaida inakazana kupata nguvu dhidi yetu. (**1 Yn. 1:9; Rum. 7:19; 8:9-13).**

Chagua wajumbe wawili jasiri wa darasa. Walete mbele ya darasa. Mmoja atashika wajibu wa mtu fulani katika hali ya kwanza na mwingine atashika wajibu wa mtu fulani katika hali ya pili na ya tatu.
.

Ngoja tuseme kwamba **__________**(jina) liko kwenye hali ya kwanza. Ngoja tufikirie asili ya hali hii.

**HALI YA KWANZA—Mwenye Dhambi Asiyeamini (Rum. 6:3-14; Rum. 8:5-8)**

1. **Bila tumaini**
2. **Kuzaliwa mara ya pili**
3. **Chini ya utumwa wa dhambi**
4. **kupotoka**
5. **Mwenye dhambi**
6. **Adui wa Mungu**
7. **Katika mwili**
8. **Asiyepatanishwa na Mungu**
9. **Chini ya adhabu ya dhambi**
10. **Kutengwa na Mungu**
11. **Chini ya sheria**

**I. Neema ya Mungu na mazoea ya Dhambi**

Kama neema ya Mungu kweli imejaa tele kupita dhambi zetu zote na tumehesabiwa haki kwa imani mbali na utii wetu, tuendelee kutenda dhambi? Kama neema ya Mungu imetolewa kwa hao ambao hata hawaistahili lakini wanaipokea kwa sababu ya imani yao ndani ya Yesu Kristo, ni kawaida kuuliza swali hili. Tuendelee kutenda dhambi na kutarajia neema ya Mungu kuzifunika? **(Gal 5:13, Rum. 6:1-2).**

**II. Tumebatizwa katika Kifo Chake – Na kufufuliwa katika Ufufuko wake**

1. Jinsi gani tulikufa? **(Rum. 6:3-5)**
2. Nini kimetokea kwa sababu ya kifo chetu na Kristo? (**Rum. 6:6-10)**
3. Nini kinatakiwa kiwe akilini mwetu kuhusiana na dhambi? (**Rum. 6:11)**

Ngoja tuseme kwamba __________(jina) ni hali ya pili. Ngoja tufikirie asili ya hali hii.

**HALI YA PILI-- Watakatifu – Ukweli halisi kama Mungu Anavyouona.**

1. **Kupatanishwa na Mungu**
2. **Kuungana na Kristo**
3. **Kusamehewa dhambi zote**
4. **Kufa kwa dhambi**
5. **Kutawaliwa na Roho Mtakatifu**
6. **Utu upya wa ndani**
7. **Uhuru kutoka utawala wa asili wa dhambi**
8. **Kufufuliwa kutoka kwa wafu**
9. **Siyo wenye dambi lakini watakatifu**
10. **Chini ya Neema**
11. **Tu hai na Kristo**
12. **Safi na wasio na mawaa**
13. **Wenye haki**
14. **Akili inakuwa kwa kile Roho anachotaka**
15. **Kuwa na maisha na amani**

Ngoja tuseme kwamba __________(jina) iko kwenye hali ya tatu. Ngoja tufikirie asili ya hali hii.

**HALI YA TATU -- Watakatifu – Uzoefu na maisha yanayodhaniwa kuwa ya kiutu**

Kila moja ya hali zilizoorodheshwa hapo juu ni ukweli halisi lakini uzoefu wetu na mtazamo ni pamoja na:

1. **Dhambi na lazima kutubu**
2. **Dhambi inakazana kupata nguvu**
3. **Kuonyesha matunda ya Roho**
4. **Roho Mtakatifu anathibitishia**
5. **Kusamehewa dhambi zote**
6. **Mtoto na mrithi wa Mungu**
7. **Onyesha Matunda ya Roho Mtakatifu**
8. **Uhuru kutoka kutawaliwa na asili ya dhambi**
9. **Siyo wenye dhambi lakini watakatifu**
10. **Akili inawekwa kwa kile Roho anachotaka**

**(1 Yohana 1:9; Gal. 5:22,23; Yakobo 1:13-14, 17-18; Rum 8:5, 16-17)**

**III. Nguvu ya kutofanya dhambi na nguvu ya kukutana na maisha katika Kristo:**

Ni nini mtu katika hali ya tatu anatakiwa kufanya?
Ni nini mistari hii yote inatuambia kuhusu maisha yetu mapya katika Kristo?

A. Elewa Asili Mpya (**Rum 6:6)**
B. Ishi katika Roho (**Rum 8:5-7; Gal. 5:16)**
C. Jilinganishe mwenyewe kama mtoto wa Mungu **(Rum. 8:16-17)**
D. Rejeza akili yako **(Rum. 12:2; 2 Kor. 10:5)**
E. Ujue ukweli (Y**ohana 8:32; Col. 1:5-6)**

1. Kwa nini kuna tofauti kati ya hali yetu ya kweli kama Mungu anavyotuona na kwa njia tunazojisikia na kutenda kwa nyakati?
2. Hii inamaanisha kwamba kutenda dhambi ni sawa kwetu?
3. Jinsi gani tunaweza kuleta kujisikia kwetu na kutenda karibu na ukweli wetu wa kiroho?
4. Jinsi gani unaruhusu hisia zako badala ya imani yako katika neno la Mungu kugusa namna unavyoyatazama maisha yako katika Kristo?
5. Tunapokuwa tunashindana dhidi ya dhambi, ambako kunaleta nguvu zaidi katika maisha yako: Kujaribu zaidi au kuamini zaidi?
6. Jinsi gani "hesabu" (pia imetafsiriwa "dhania" na "fikiria" katika **Warumi 6:11** imani inayoendana?
7. Nini kimetokea kwenye asili yako ya udhambi kufuatana na barua ya Paulo kwa Warumi?
8. Jinsi gani unaweza kuishi kwa Roho?

Liambie darasa. “Kuleta kitabu au daftari dogo kwenye kipindi kijacho kuandikia kumbu kumbu”

# TABIA YA KIROHO –Azimio la Mafunzo 5

## Kutunza Kitabu cha Kumbu Kumbu

**I. Kwa nini Kitambu cha Kumbu Kumbu?**

A. Ukumbusho wa Upendo wa Mungu na utegemezi tunapokutana na mahangaiko na kukatishwa tamaa
Jinsi gani kitabu cha kumbu kumbu ni sawa na ukumbusho wa Yoshua? **(Yos. 4:1-9)**

B. Kinasaidia kuanzisha uwajibikaji katika ukuaji kiroho na huduma.

C. Kinalazimisha kutafakari maisha yetu na kurekebisha vipao mbele vyetu.

D. Kinatusaidia kukua katika imani kwa kuona jinsi ufahamu wetu kwa Mungu ulivyokua.

E. Kinatusaidia kuona jinsi Mungu anavyojibu maombi.

F. Zana katika kuendelea kwa huduma zetu. .

**II. Mda wa Kila Siku na Mungu**

Waka pamoja na haya katika kitabu cha kumbu kumbu zako za kila siku

**Fungu la leo:** Nukuru kifungu cha Biblia unachosoma wakati wa sala yako.

**Utambuzi binafsi**: Soma fungu la Biblia, chukua mda kufikiri na omba juu yake. Nukuru ufahamu wowote Roho Mtakatifu anaokupatia kuhusu fungu. Nini fungu linasema? Ni nini unachunguza? Jinsi gani unaweza kutumia fungu hili kwenye maisha yako mwenyewe leo?

**Ahadi za kudai:** Kuna ahadi zozote katika fungu hili? Zinukuru na mshukuru Mungu kwa ukweli huu.

**Amri za Kutii**: Fungu hili linanukuru amri yoyote unayohitaji kutii?

**Maombi:** Orodhesha hitaji lolote la maombezi ambayo una mzigo nayo maalumu na vile vile kwa majibu ya maombezi yaliyopita uwe maalumu iwezekanavyo. Hii itakusaidia kumuona Mungu akifanya kazi kupitia maombi yako.

**III. Kuandika kumbu kumbu kila siku**

Kuweka kumbu kumbu kila siku kunakusaidia kumulika maendeleo ya huduma ya upandaji wako kanisa.

**Utekelezaji wa Azimio**: Nukuru kazi yoyote uliyofanya kwenye Utekelezaji wako wa azimio. Ordhesha shughuli zilizokamilika kwa utekelezaji wa azimio na kazi inayoendelea.

**Mawasiliano:** Orodhesha mawasiliano yako ya kiuinjilisti kwa siku hiyo. Nukuru matokeo ya mda wenu pamoja. Umeshirikisha ushuhuda wako? Jinsi gani wameitikia? Wako wazi au hawako wazi kwenye injili?

**Mikutano**: Andika kuhusu kikundi kiini chochote, mikutano ya majumbani au kazi maalumu. Lini na wapi mkutano ulifanyika? Nini mlichofanya (Kujifunza Biblia, kikundi cha maombi, kuonyesha mkanda wa Yesu kwa marafiki)? Ni watu wangapi walihudhuria? Ni wangapi ni wahudhuriaji wa kawaida? Wageni? Kuna yeyote aliyetoa maisha kwa Kristo? Nukuru tatizo lolote au juzu maalumu linalohitaji uangalizi zaidi.

**Kutafakari:** Chukua mda kufikiri kuhusu siku. Kuna chochote kilicho nje yako? Umejifunza au kuchunguza chochote kuhusu maisha yako binafsi au huduma unayotaka kunukuru? Kutafakari huku ni notisi za binafsi unazoandika kuhusu maisha binafsi. **Huhitaji kuzishirikisha kwa yeyote.** Zinakusaidia kuweka siku yako katika mtazamo na kunukuru chochote Roho Mtakatifu anachokufundisha

Kwa mda uliobaki, waelekeze wanafunzi ifuatavyo: “kwa kutumia daftari dogo walililoleta, fikiria katika na andika kumbu kumbu zako za kiroho kwa leo.” MKUFUNZI, unaweza ukahitaji kuwa na karatasi tupu kwa hao waliosahau kuleta dafutari lao.

### Utekelezaji wa Azimio

Katika mzunguko wote wa upandaji kanisa, tunza kitabu cha kumbu kumbu au cha kutafakari na maendeleo ya huduma. Unaweza ukataka kuanzisha vichwa hapo juu kama ambavyo utatumia kupangilia kitabu chako cha kumbu kumbu za kila siku. Jiandae kuonyesha kitabu hiki kwa mshauri au mkufunzi.

# MAOMBI—Azimio la Mafunzo 1, 2

## Kongamano la Maombi: Kuombea Uamsho

### I. Jinsi ya Kupanga na Kuongoza Kongamano la Maombi

Kongamano la maombi linakazia katika mawazo mawili ya kibiblia:
Maombi yanayoelekezwa kwa ndani

Maombi yanayoelekezwa kwa nje

A. **Kisa:** Kongamano la maombi linatakiwa lipangiliwe kuzunguka kisa

**B. Mambo ya kufanya:** Kutoa maandiko yanayounga mkono kisa.
**C. Kusherehekea:** Kumtukuza Mungu
**D. Kutubu na maandalizi:** Maombi ya kimya kimya ya kutubu
**E. Maombi ya Kikundi Kidogo**

uwe na washiriki kutoka katika makundi madogo ya watu 2-6 na ombea kuhusu kichwa cha maombi kadiri kinavyoendana na kimtaa, kimkoa, kitaifa na ngazi ya kitaifa. Baada ya mda uliopangwa kwa kikundi kidogo kuomba, ongoza katika maombi kwa harakati za maombi yanayokua katika jiji lako au mji au kimtaa.

**F. Utoaji:** Taarifa na nyenzo kama vile ramani na orodha.
**G. Kusifu na Kuabudu**

II. **Kongamano la maombi**

Mkufunzi anatakiwa aongoze darasa lote kwenye kongamano la maombi kwenye kisa cha "Maombi" kwa kutumia zana hapo chini:

A. Maombi ya Kusihi na Kutafakari: (Mkufunzi anaongoza sehemu ya kongamano)
**Katika kongamano hili, tutasisitizia mifumo ya maombi ambayo Yesu alisisitiza kwenye** Maombi ya **kielelezo**: **Mathayo 6:9-13**

"Hivi, kisha, ndivyo unavyotakiwa kuomba:
" baba yetu uliye mbinguni
Jina lako litukuzwe, — maombi ya Kusihi na Kutafakari
10 ufalme wako uje, — maombi ya Ushirika
Mapenzi yako yatimizwe
Duniani kama ilivyo mbinguni — maombi ya kujiachilia
11Tupe mkate wetu wa kila siku. — Maombi ya haja
12Tusamehe deni zetu, — maombi ya Kutubu
Kama tunavyowasamehe waliotukosea.
13Na usitutie majaribuni — maombi ya kufunguliwa kutoka kwa Mwovu.

Soma na kwa maombi tafakari kwenye mistari hii ya sifa.
**Waefeso. 1:6; 1 Petro 4:11; Zaburi 8:1; Zaburi 71:19**

Kwa kuwa huu siyo mda wa kujifunza Biblia, usichukue mda kujadili mistari kwenye maeneo tofauti tofauti ya kongamano la maombi. Liongoze kundi kwenye mda mfupi wa maombi ambao wajumbe wa kundi wanataja tabia, heshima, au jina la Mungu na kumtukuza.

B. Maombi kwa ajili ya Ushirika na Mungu (Mjumbe wa darasa anajitolea kuongoza kundi katika kipindi hiki cha kongamano.)

**Yohana 15:7-10; Yakobo 4:4-8**

C. Maombi ya Kujitoa (Mjumbe wa pili wa darasa anajitolea kuongoza kundi katika kipindi hiki cha kongamano.)

Soma na kimaombi tafakari juu ya mistari ifuatayo: Y**ohana 14:23-24; Warumi 6:12-13; Warumi 8:5**

D. Maombi ya Kusihi (mjumbe wa tatu wa darasa anaongoza kipindi hiki cha kongamano.)

**Wafilipi. 4:6-7; Yohana 15:5-7; Yohana 14:12-13**

E. Maombi ya toba na ukombozi (Mshiriki wa nne anaongoza kundi kwa maombi haya ya pole pole ya toba.)

**2 Kor. 7:10; Isaya 59:2; Zaburi 66:18-19**

Fanya darasa lijadili kila kipindi cha kongamano la maombi. Kisha waombe darasa kujadili maswali haya.

1. Nini kilichoonekana kufanya kazi vema?
2. Nini hakikufanya kazi vema?
3. Kulikuwa na sehemu yoyote ya kongamano iliyokuwa imepooza, kana ni hivyo kwa nini?
4. Nini kilionekana kuwa mtindo bora au njia ya kuongoza kongamano?

# MAOMBI – Azimio la Mafunzo 3

## Jinsi ya Kuwezesha maombi: Jinsi ya Kuhamasisha Maombi Kwa Kupanda kwako Kanisa

(Panga somo hili kwa kipindi cha masaa mawili)

**I. Maombi—** Kipengele Muhimu cha Uinjilisti na Upandaji Kanisa

**Rum. 10:1: Efe. 6:18; Efe. 6:19-20; Col. 4:2-4; 2 The. 3:1-3**

**II. Jinsi ya Kupanua Maombi Pamoja na Uinjilisti na Upandaji Kanisa**

Ni njia zipi za vitendo ambapo unaweza kuwahusisha waumini katika uombaji wa harakati zako za upandaji kanisa?

**A. Kwenye Vikundi Kiini**

1. Nini kikundi kiini kinatakiwa kikazie maombi yake?

B. **Maombi ya Utatu** (waumini watatu wanaomba pamoja)

1. Ni nini maombi ya utatu yanakazia maombi yake?

C. **Maombi ya Kutembea**

Jadili maombi ya kutembea. Unafikiri njia hii inafaa ? Ni ya ufanisi?

Mchanganuo 1:

Ujirani uliojulikana kuwa na idadi kubwa ya familia zenye matatizo ulikuwa umelengwa kupandwa kanisa. Matatizo ya kijamii kama vile kukosa ajira, kuvunjika kwa familia, madawa ya kulevya na ujambazi vilikuwa sugu. Mwanzoni mwa juhudi za upandaji kanisa, maombi ya kutembea yalikuwa yamepangwa katika kila mtaa kwenye ujirani huo. Walivyotembea na kuomba, walinukuru utambuzi wote Roho Mtakatifu aliowaonyesha. Waombaji wengine wengi walifuatia maombi hayo ya kwanza. Baadhi ya maombi ya kutembea yakafanyika kuzunguka shule, mengine katika na karibu na soko, mengine kwenye mzunguko wa ujirani. Na wengine walifanya kwenye misitu inayoangaliana na ujirani. Katika misitu hiyo, iliyojulikana kama sehemu ambayo madawa yalikuwa yakitolewa na wenye nayo, alama za wachawi ziligunduliwa kwenye miti. Kikundi cha maombi ya kutembea walitumia muda kuombea nguvu hizo za uovu. Katikati ya miaka mitatu tangu ujirani ulipolengwa upandaji kanisa, matatizo ya kijamii yakawa yamekwisha, ujambazi ukapungua kwa asilimia 40 na kanisa la watu 70-80 likawa limepandwa. Kuna mguso wa kiroho sasa wa kutia changamoto nguvu ya uovu wa uvamizi, na Mungu anafanya kazi katika maisha ya wengi (DAWN Europa Mwongozo wa Maombi, August 1994, Uk 13)

Ni nini utakachofanya kwa swala hili?
Ni kitu gani kikubwa kilichopatikana kwa aina hii ya maombi ya kutembea?
Nini kinaweza kuwa changamoto kubwa?

Mchanganuo 2:

Mpanda kanisa na familia yake walihamia katika nyumba za kupanga katika mji ambapo walikuwa na haja kuona kanisa limeanzishwa. Jioni sana moja, familia yote ilitembea kuzunguka nyumba nzima

waliyopanga. Walisimama mbele ya kila mlango na kila mmoja akaombea watu walioko kwenye nyumba hiyo. Kijana mdogo aliomba kwamba kila mtu katika nyumba hiyo amwombe Yesu kuingia moyoni mwake. Msichana mmoja akaomba kwamba mahitaji ya fedha yatimizwe, msichana mwingine akaomba kwa ajili ya mahusiano mazuri katika familia. Mama yao akaomba kwa ajili ya afya ya jamaa katika familia hizo na baba akaomba kwa ajili ya baraka za Mungu kwa wote walio katika nyumba. Baada ya maombi ya kutembea, mpanda kanisa na familia yake waliona watu 14 katika nyumba hiyo wakienda kwa Yesu na kanisa dogo likaanza.

Ni nini utakachofanya kwa swala hili?
Ni kitu gani kikubwa kilichopatikana kwa aina hii ya maombi ya kutembea?
Nini kinaweza kuwa changamoto kubwa?

**D. Timu ya Kusaidia Maombi**

1. Una timu ya kusaidia maombi? Ni kwa jinsi gani inafanya vizuri kwako? Nini unachoomba timu yako kuombea?
2. Ni kwa njia zipi unaweza kufanya timu ya kusaidia maombi kutaarifiwa maombezi yanayotakiwa na majibu kwa maombi?
3. Ni aina gani ya taarifa unazojisikia zingefaa kushirikisha timu ya maombi na ni aina gani taarifa zinaweza zisifae kushirikisha?
4. Ni mawazo mengine ya kusaidia maombi kwa huduma yako ya upandaji kanisa?

**III. Utafiti: Kukusanya Taarifa Kwa Ajili ya Maombi**

Ni aina gani ya taarifa zinaweza kukusanywa katika utafiti ambazo zinaweza zikawa za msaada zaidi kwa kuombea mtu binafsi au jumuia?

Habari kama vile makanisa katika eneo, mafumbo, makundi ya kishetani yaliyopo, ukuaji wa kanisa, na umoja wa waumini vinaweza kutumika kwa maombi yenu? Elezea?

### Utekelezaji wa Azimio

Kama hujafanya hivyo tayari, **anzisha timu yako ya kusaidia maombi.** Waombe angalau waumini wengine watatu kuomba kila wiki kwa ajili ya huduma yako. Jinsi gani utawafanya kutaarifiwa juu ya maombezi na majibu ya maombi?

**Fanya angalau maombi ya kutembea mara moja katika eneo lako lengwa na timu yako ya upandaji kanisa au wengine** wenye mzigo wa kuona eneo hilo limefikiwa kwa ajili ya Kristo. Jadili uzoefu huu na mshauri wako au mkufunzi.

# NJIA ZA KUJIFUNZA BIBLIA – Azimio la Mafunzo 1

## Utangulizi kwenye Kujifunza Biblia kwa Kufata neno: Kuruhusu Biblia Kutufundisha

**I. Kufata dhidi ya Kupunguza (2Tim. 2:15)**

**A. Njia ya Kupunguza**

1. Hoja ya Upunguzaji
   Tunaanza na kinachojulikana na wazo linalokubalika na kupunguza suluhu.
2. Njia ya Biblia ya Kufata
   Katika vifungu kumi vingine vya Agano Jipya, hamira inamaanisha dhambi. Tunaweza kupunguza kwamba inaweza ikamaanisha dhambi **Mat. 13:33**. Soma fungu. Je hamira inamaanisha dhambi hapa?
3. "Njia" ya Kawaida
   Walimu wa Biblia mara nyingi wanajua wanachotaka kusema, na kwa kifupi huja kwenye Biblia kutafuta mstari unaoonekana kuunga kuelewa kwao. Kwa nini hili lianzishe hatari ya kuelewa vibaya maana ya kweli ya fungu?

**B. Njia ya Kufata**

1. Hoja ya Kufata
   Tunauchunguza ukweli kwa karibu ili kujaribu kuelewa nini ukweli unamaanisha.

2. Njia ya Kujifunza Biblia kwa Kufata
Kwa uangalifu tunaichunza aya kupata kuelewa.
3. Njia Bora

**II. Hatua za Kujifunza kwa Kufata**

A. Uchunguzi – Inasemaje?
B. Ufafanuzi – Ina maana gani?
C. **Matumizi –** Nini natakiwa kufanya?
Soma Y**ohana 1:1-2** na jadili maswali haya matatu. .

**III. Kujenga Piramidi Imara**

A. Kuwahisha Utaratibu – Usiharakishe kwa kuanza na usomaji wa haraka na kudhania kuwa unajua inachomaanisha. Usifanye matumizi yake ya haraka na kuleta maswali.
B. Msingi Imara– anza kwa uchunguzi mkamilifu (kwa kuvunja dhahabu katika vipanda vidogo vidogo). Tunachuja yaliyomo kwenye fungu kuona maana yake ya kweli. Tunafanya matumizi ya yanayofaa.

Maswali ya kutafakari, marudio na matumizi

1. Ni nini tofauti ya msingi kati ya Upunguzaji na Ufataji?
2. kwa nini njia ya kujifunza kwa kufata ni njia ya juu ya kujifunza Biblia, ikilinganishwa na njia ya kupunguza?
3. Ni nini hatari ya njia ya "kawaida" kweye kujifunza Biblia na kuhubiri?
4. Ni maswali yapi unayoweza kujiuliza mwenyewe kuhusu kifungu cha Biblia ili kukazia kwenye uchunguzi juu yake?
5. Ni maswali yapi unayoweza kujiuliza mwenyewe kuhusu kifungu ili kukazia kwenye maana yake?
6. Ni maswali yapi unayoweza kujiuliza mwenyewe kuhusu kifungu cha Biblia ili kukazania kwenye matumizi yake?

## Utekelezaji wa Azimio

Utakapojifunza Biblia tena, andika muda uliotumia katika uchunguzi, ufafanuzi, na matumizi. Kufuatana na mida hii, tathimini kama unatumia njia ya kujifunza kwa kufuata neno, njia ya kujifunza kutumia mawazo au njia nyingine katikati ya hizo.

Katika kutayarisha somo litakalofuata juu ya uchunguzi, chukua mfano wa kifungu kidogo cha maandishi ya kujifunza (isiwe zaidi ya aya au vingine). Tumia angalau masaa mawili kwa maombi ukichunguza kifungu na kumuuliza Mungu kufungua masikio yako kwa vitu ambavyo hujaviona. Andika uchunguzi wako. Ni nini umejifunza?

# NJIA ZA KUJIFUNZA BIBLIA – Azimio la Mafunzo 2

## Kulichunguza Neno la Mungu

**I. Uchunguzi – Nini Soma Linasema?**

A. **Jiandae kwa Uchunguzi**
Ni nini nafasi ya Roho Mtakatifu (**1 Kor 2:14**)?
Ni nini nafasi ya maombi (**Efe. 1:18**)?
Ni nini nafasi ya utayari wa kutii (**Yakobo 1:22-25**)?
Ni nini nafasi ya kujichunguza mwenyewe kwa mwanga wa fungu lililosomwa (**2 Kor. 13:5**)?
Ni nini nafasi ya utayari wa kujifunza (**Matendo 17:11**)?
**B. Chukua Mda wa Kutosha**
C. **Angalia kwenye Mandhali**
Kuangalia kwenye mandhali kuna maana kuangalia yafuatayo:

1. Ni nini mistari inayofata inachozungumza?
2. Ni nini kisa cha fungu?

3. Ni nini kisa cha ukurasa?
4. Ni nini kusudi la kisa cha fungu?

**D. Chunguza Mfumo**

i. Maneno ya Ufunguo
ii. Ulinganifu na Utofauti
iii. Mwendelezo wa wazo
iv. Vitenzi
v. Viunganishi
vi. Mifano
vii. Aina ya maandishi

**E. Uliza Maswali: Nani? Nini?, Wapi ?, Lini?, Jinsi gani?, na Kwa Nini?**

Kikufata fanya mafunzo ya Yeremia 1 kwa kutumia zana na kanuni hapo juu ya uchunguzi. Kwanza, Soma fungu pamoja. Kisha jadili maswali kwenye topiki hii, "MFANO WA UCHUNGUZI."

(Endelea na majadiliano ya mchanganuo wa uchunguzi mpaka dakika 10 kabla ya mwisho wa saa. Kisha, jadili matokeo ya majadiliano kama darasa.

| Kama inawezekana, tengeneza kopi ya "Mfano wa Uchunguzi" kwa wajumbe wa darasa. |
|---|

**Mfano wa Uchunguzi**

A. Nani?

Ni kwa nani sehemu hii ya Maandiko inatolewa (Mstari 1)

Ni mtu yupi ametajwa katika fungu hili (mstari 1-2)?

Ni wafalme gani wametajwa katika mstari huu 2-3?

Ni watu gani Mungu anaowaarifu kuleta ghasia kwenye nchi (v.15)?

Mistari 18-19 inaorodhesha upinzani mkuu wa Yeremia. Watu hawa watakuwa akina nani?

(Mengine?)

B. Nini?

Ni tukio gani maalumu limenukuriwa mwanzoni mwa msatri wa 2?

Inawezekana kupunguza kilichokuwa wajibu wa Yeremia kutoka mstari wa 2?

Kama ni hivyo, nini ulikuwa wajibu?

Kufuatana na mstari wa 2, ni tukio gani lilitokea mwishoni mwa utawala wa Sedekia?

Nini kilimtokea Yeremia katika mstari wa 3?

Nini ilikuwa "neno la Bwana" lililomjia (mstari 5)

Ni matendo yapi manne yaliyotolewa kwa Mungu na yeye Mwenyewe katika mstari wa 5?

Katika mstari wa 5, Nini ilikuwa uwe wajibu wa Yeremia?

Nini kiilikuwa kiwango cha wajibu wa Yeremia? Alikuwa tu ni kwa taifa la Waisraeli, au kwa upana zaidi?

Nini yalikuwa majibu ya Yeremia katika mstari wa 6?

Ni nini majibu ya Mungu kwa Yeremia katika mstari wa 7-8?

Ni nini masharti mawili Mungu anayompa Yeremia katika mstari wa 7-8?

Nini uchaguzi alio nao Yeremia kutokana na mstari wa 7?

Ni hisia zipi za Yeremia ambazo Mungu anazizungumzia katika sehemu ya kwanza ya mstari wa 8?

Ni sababu mbili zipi zinazotolewa kwa Yeremia ya kwamba asiogope (mstari wa 8)

Mungu anamfanyia nini Yeremia katika mstari wa 9?

Mstari wa 10 unaelezea kazi ya Yeremia. Asili ya kazi hiyo ilikuwa nini?

Ni maendeleo yapi yaliyogunduliwa katika mstari wa 10?

Ni vitu viwili vipi ambavyo Mungu alimwonyesha Yeremia katika mstari wa 11-16?

Mstari wa 12 unaelezea nini kuhusu kile anachokifanya Mungu?

Kutokana na mstari wa 14 -16, Kitu gani kilikuwa karibu kuwapata watu wa Mungu?

Ni sababu gani maalumu ambayo inamfanya Mungu kuleta hukumu juu ya watu wake(mstari wa 16)?
Ni maelekezo yapi Mungu anampa Yeremia katika mstari wa 17?
Ni amri zipi zimerudiwa kutoka mwanzo?
Ni ahadi gani mpya katika (mstari wa 17)?
Watu watafanya nini kwa Yeremia katika mstari 18 (mstari wa 19)
Ni ahadi gani Mungu anampa Yeremia kwa ajili ya vita vilivyo mbeleni (mstari wa 19)?
(Mengine)?

C. Wapi?
Mpangilio wa fungu hili uko wapi kulingana na mstari wa 1?
Ni wapi hili linapatikana?
Ni wapi watu walioelezwa katika mstari wa 15 wanakotoka?
(Mengine)?

D. Lini?
Ni kipindi gani cha muda ulioelezewa katika yaliyomo kwa ujumla katika kitabu hiki?
Katika mstari wa 5, lini Mungu alijua (kumchagua) Yeremia?
Katika mstari wa 5, lini Mungu alimtenga Yeremia kwa ajili ya huduma?
Tukio katika mstari wa 18 lilitokea lini?
(Mengine)?

E. Kwa nini?
Kwa nini Mungu "analinda" katika mstari wa 12?
Kwa nini Mungu anatangaza hukumu juu ya watu wake (mstari 16)?
(Mengine)?

F. Jinsi Gani?
.Jinsi gani Yeremia ameelezewa katika mstari wa 1?
Jinsi gani baba yake Hilikia ameelezewa?
Jinsi gani Yeremia anamzungumzia Mungu katika mstari wa 6?
Jinsi gani Yeremia anaitikia neno la Mungu katika mstari wa 6?
Jinsi gani Mungu anamwelezea Yeremia katika mstari wa 18?

## Utekelezaji wa Azimio

Kama hukuwa na mda wa kutosha kukamilisha uchunguzi wa Yeremia 1, fanya hivyo kabla ya somo linalofata. Ona kama unaweza kuuliza maswali mengine yanayofaa ya baadhi ya vifungu. Yatunze maswali haya na majibu kwa kuyatumia katika somo linalofata.

# NJIA ZA KUJIFUNZA BIBLIA – Azimio la Mafunzo 3

### Warsha ya Uchunguzi

Ni muhimu kulirudisha kundi pamoja kwa mda wa dakika 15-wa kulinganisha matokeo. Hili linatakiwa lionyeshe kwamba kuna uwezekano mwingi wa maswali ambayo kawaidia yanaweza kumponyoka mtu

binafsi, au hata kundi dogo. Pia inawekea mkazo wa kufaa wa kujifunza maandiko pamoja kwenye kundi badala ya mtu mmoja "kuhubiri" anachoona kwenye somo. Gawanyika katika makundi ya watu 3-4. Chukua dakika 35 kusoma fungu, anzisha maswali ya **uchunguzi,** na andika majibu.

> Uwe na karatasi na penseli za ziada zikiwepo kwa kundi kutumia. Vile vile, utahitaji ubao wa kubandikia, ubao wa choki, au kitu kingine kinachoendana kuandikia maswali na majibu wakati kundi lilipokutana pamoja mwishoni mwa kipindi. Toa nakala ya zana hapo chini kama inawezekana?

**HATUA**

Tumia hatua zifuatazo ambazo zilikuwa zimewekewa alama katika somo 2 kwa Matendo 17:1-10a:
Omba kwa ajili ya kupewa mwanga.

Soma fungu mara kadhaa.

Chunguza mandhali na andika uchunguzi wako.

Chunguza muundo na andika unachoona.

Uliza kila mchanganyiko wa maswali sita ya ufunguo unayoweza kufikiria, na andika majibu unayopata. Siyo kila swali litahusika na fungu hili, lakini nukuru yale yanayoendana na kwenye fungu.

Chagua maswali yaliyo bora kwa kila sehemu kwa kutumia kama ungekuwa unakwenda kufundisha fungu.

MANDHALI: Kisa cha kichwa cha habari cha mistari inayozunguka fungu lililojifunzwa.

| | | |
|---|---|---|
| Mistari inayoendelea – | Fungu/sehemu - | Kitabu (Matendo) – |
| Mistari inayofata – | Ukurasa (17) - | Agano Jipya – |

**MUUNDO:** Muundo wa fungu linaendana na fasihi na aina ya lugha.

| | | |
|---|---|---|
| Maneno ya Ufunguo – | Vitenzi - | Aina ya lugha - |
| Mlinganisho au Utofauti – | Viunganishi – | |
| Mwendelezo wa mawazo - | Mifano– | |

**MASWALI YA UFUNGUO:** Uliza na jibu maswali yote kati ya sita mchanganyiko yanayowezekana
Nani? Nini ? wapi? Lini? Jinsi gani? Kwa nini?

# NJIA ZA KUJIFUNZA BIBLIA—Azimio la Mafunzo 4

## Kufafanua Neno la Mungu: Ina Maana Gani?

**I. Ufafanuzi – Hatua ya Pili ya Kujifunza Biblia kwa Kufata Neno**
**II. Utaratibu wa Matumizi**
- **A. Chuja katika Uchunguzi Ukweli Kupata Yale ya Ufunguo**
- **B. Onyesha Wazo Kuu la Mwandishi**
- C. **Onyesha Mtiririko wa mMawazo katika Fungu**

**III. Sheria za Msingi za Ufafanuzi**
- A. kanuni ya Jumla ya Ufafanuzi Kibiblia.
  1. Biblia ni mamlaka ya Neno la Mungu.
  2. Biblia inajifafanua yenyewe, ikionyesha tabia ya Mungu.
  3. Imani inayookoa na Roho Mtakatifu ni muhimu kuelewa maandiko.
  4. Unatakiwa kufafanua historia, matendo, tabia, uzoefu wa binafsi etc.,kwa mwanga wa maandiko na siyo maandiko kwa mwanga wa vitu hivi.
  5. Kusudi la msingi la Biblia siyo kukuza ufahamu wetu, lakini kubadilisha maisha yetu.
  6. Kila mkristo ana haki, jukumu, na nafasi ya kuchunguza na kufafanua neno la Mungu kwa msaada wa Roho Mtakatifu.
- B. Kanuni za Kibiblia za Ufafanuzi Kifasihi, Kihistoria, na Kitheolojia

1. Unatakiwa ufafanue maneno kufuatana na maana yake kwenye mandhali ya mwandishi kihistoria na kiutamaduni. Fikiria ambavyo wasikiaji wa kwanza wangekuwa wameelewa na kufanya kwenye ujumbe.
2. Ni muhimu kuelewa fasihi ya fungu kabla ya kujaribu kuelewa ukweli wa kitheolojia ambao linafundisha.
3. Lugha ya kitendawili kawaida ina wazo kuu moja. Usijaribu kusoma vitu vingi kwa aina hiyo ya fungu. (Tazama Ziada 2A "Lugha ya Biblia" kwa maelezo ya aina tofauti za lugha ya kimethali).
4. Hutakiwi kuwa wazi kwenye somo kuliko maandiko yalivyo wazi. Usiongeze kufikiri kwako mwenyewe au mapokeo ya kanisa kwa kile Biblia inachosema, kwa kuwa wewe au wengine wanaweza kuamini mawazo hayo kuwa ya kimaandiko halisi.

C. Makosa ya Kawaida ya Kuepuka Kwenye Ufafanuzi

Kuruka kutoka kwenye ubao wa sipiringi kutoka fungu hadi topiki nyingine unayotaka kujadili.

Fumbo-kutojali maana wazi ya maandiko na kujaribu kutafuta maana iliyofichika. Kutojali Ufunuo Unaoendelea- na kusahau asili inayoendelea ya maandiko

Tumia "Usaidizi,"Lakini Utumie kwa Uangalifu

Rejea nyuma kwenye uchunguzi wako kwenye Yeremia 1, na **fanyia kazi utaratibu wa tafsiri kadiri mda unavyoruhusu. Fata kanuni iliyoonyeshwa hapo chini.**

Toa nakala kama inawezekana.

## Mfano wa Ufafanuzi

**Baadhi ya Maswali yenye "Maana"**

Unapokuwa unafanyia kazi maelezo hapo juu, inaweza kuwa msaada kufikiria maswali yafuatayo juu ya maana ya somo. Pengine utaweza kufikiria maswali mengine mazuri au bora. Haya yametolewa kukunzisha kwenye utaratibu.

Mstari wa 5

Ina maana gani kwamba Bwana "alimjua" Yeremia?

"Kutengwa" ina maana gani

Ni nini baadhi ya mtazamo wa maelezo "…kabla hujazaliwa nalikutenga…?"

Mstari wa 6

Kwa nini Yeremia anaweza kujifikiria mwenyewe kama "mtoto?"

Kwa nini unadhani Yeremia alijibu kwa njia aliyotumia?

Mstari wa 7

Ni jinsi gani unaweza kutofautisha tabia ya wito kutoka kwa Mungu na ule unaouona katika mstari huu?

Jibu lako linasema nini juu ya Mungu na tabia yake katika swali linalofuata?

*Mstari wa 8*

Ni nini neno la Bwana linasema juu ya kuitika kwa watu kwenye huduma ya Yeremia ya mbeleni

Ni mvuto gani uliokuwepo kwa Yeremia kukutana na upinzani?

*Mastari wa 9*

Ni jinsi gani Bwana "aliweka" maneno yake ndani ya Yeremia?

*Mstari wa 10*

Nini unafikiri kifungu kidogo "kung'oa na kubomoa, kuharibu na kuangamiza, kujenga na kupanda" kinamaanisha?

Ni nini unaweza kudhani tabia ya Yeremia inayoweza kumwezesha kufuata katika mpango wa Mungu?

*Mstari wa 12*

Ni kanuni gani unayopata katika mstari huu inayohusu kuhusika kwa Mungu katika huduma ya hao aliowaita?

*Mstari wa 16***.**

Ni nini mstari huu unaonyesha juu ya tabia ya Mungu, hata unapokuja wakati wa kuhukumu watu wake mwenyewe?

Mungu alifanya haki kwa kile alichopanga kufanya kwa watu wake? Kwa nini?

*Mstari wa 17*

Nini ingeweza kuwa sehemu ya "kuwa tayari" kwa Yeremia?

Kwa nini unadhani Bwana alirudia alichokuwa ameshasema nyuma (mstari 8)?

*Mstari wa 18*

Ni nini maana na umuhimu wa mstari wa kifungu kidogo "mji wenye boma, nguzo ya chuma, na kuta za shaba?"

Kwa nini watu wa mstari wa 18 kuwa wapinzani kwa Yeremia na ujumbe wake?

Ni jinsi gani Mungu anajenga boma na kuandaa watu wake leo kusimama kwa ajili yake?

*Mstari wa 19*

Mistari hii inaonyesha nini juu ya tabia ya Mungu na kujitoa kwa watu anaowaita?

Kanuni ya Kibiblia

Kutoka katika kujifunza kwangu la Yeremia 1, ninakuta kanuni ifuatayo ya kibiblia isiyopitwa na mda (iandike):

## Utekelezaji wa Azimio

Malizia maswali yoyote yaliyobaki katika somo hili ambayo bado hujamaliza. Anza kufanyia kazi utaratibu wa ufafanuzi kwa kutumia Matendo 17:1-10.

# NJIA ZA KUJIFUNZA BIBLIA – Azimio la Mafunzo 5

## Warsha ya Ufafanuzi

Mkufunzi, tumia maelekezo yaliyotolewa kwa Njia za Kujifunza Biblia Azimio la 3 kuendesha "Warsha ya ufafanuzi" kwa kutumia Matendo 17:1-10a. wanafunzi watatumia notisi zao kutoka somo lililopita kama kiongozi kwenye warsha.

A. Chuja Uchunguzi Kupata Ukweli wa Ufunguo

Ninapoangalia uchunguzi wangu katika Matendo 17:1-10a, inaonekana kwangu uchunguzi muhimu zaidi ni (Orodhesha):

Mandhali ya fungu:

Wasikilizaji wa kwanza:

Hali ya mwanzo:

Ukweli mwingine na uchunguzi:

B. Eleza Wazo Kuu

Kichwa cha fungu ni:

Vitu ambavyo Luka anasema kuhusu kichwa hiki:

Ufupisho wa maelezo ya wazo kuu, ukionyesha mawazo mawili hapo juu, ni:

C. Elezea Mtiririko wa Mawazo

Luka anaanzisha wazo kuu la fungu kwa:

D. "Yana Maana Gani" maswali

Unapokuwa unafanyia kazi fungu hili kama kundi, andika hapo chini maswali ya ufunguo uliyouliza kuhusu maana ya fungu ambayo yalikusaidia kuelewa vema mistari ina maana gani.

[Zungushia maswali mawili ya msaada zaidi ambayo ungetumia kama ungekuwa unaongoza mafunzo ya kundi ya kifungu hiki.]

E. Eleza Kanuni ya Kibiblia

Kanuni isiyoisha mda ya fungu hili:

# NJIA ZA KUJIFUNZA BIBLIA – Azimio la Mafunzo 6

## **Kutumia Neno la Mungu:** Nini Ninatakiwa Nifanye?

**I. Matumizi – Hatua ya Tatu ya Njia ya Kufata (tii-Mat. 28:20, Yakobo 2:17)**

**Matumizi ni pamoja na kuuliza, "Ni nini katika maisha kinafanana na hali iliyoelezewa katika fungu?**

**II. Utaratibu wa matumizi**

**A. Matumizi ya topiki**

| | | |
|---|---|---|
| **1. Imani** | **4. Dhambi** | 7. **Muhusika** |
| **2. Tabia** | **5. Changamoto** | |
| **3. Matendo** | **6. Ahadi** | |

Jadili "Maswali ya Jumla" na "Maswali Maalumu" kama kiongozi katika kutumia Yeremia 1kwenye maisha yenu na huduma. Jadili matokeo ya majadiliano ya makundi haya kama darasa.

**Maswali ya Jumla**

Hendricks anaorodhesha idadi ya maswali ya matumizi ya kusaidia ambayo yanaweza kuulizwa na fungu lolote la maandiko haya:

Kuna mfano kwangu wa kufata?
Kuna dhambi ya kuepuka?
Kuna ahadi ya kudai?
Kuna maombi ya kufata?
Kuna amri ya kutii?
Kuna sharti la kutimiza?
Kuna mstari wa kukariri?
Kuna kosa la kuwekea alama?
Kuna chamngamoto ya kukutana?

Toa nakala kama inawezekana,

**Maswali Maalumu**

Maswali haya moja kwa moja yanaendana na kile unachotakiwa kufanya kama matokeo ya ujumbe. Kuna idadi isiyoisha ya maswali haya maalumu, kwa kuwa yako tofauti kwa kila fungu. Unazuiliwa na ubunifu wako tu. Kitu cha muhimu ni kufungua moyo wako kwa Bwana, na muruhusu akuonyeshe anachotaka kiwe tofauti katika maisha yako.

Baadhi ya maswali ya mfano yameorodheshwa chini. Jisikie huru kuongeza unapokuwa unafanyia kazi fungu.

Mstari wa 5

Ni nini mafundisho ya mstari huu unavyosema binafsi kwako kuhusu uhusiano wako binafsi na Mungu muumbaji?

Ni nini mstari huu unasema binafsi kwako kuhusu wito wako kwenye huduma?

Kama huna hisia wazi za wito, ni nini mstari huu unasema kwako?

Ni nini mstari huu unasema kwako binafsi kuhusu mapenzi ya Mungu kwenye maisha yako?

Unajua mapenzi ya Mungu ni nini katika maisha yako kwa wakati huu?

Ni mguso gani mstari huu ulio nao kuhusiana bna imani yako katika wenyezi wa Mungu?

Unakubaliana? Unapokea wazo hili bila kusubili?

Mstari wa 6

Unajilinganisha na kusita kwa Yeremia kukubali changamoto ya Mungu?

Ni nini kimekuwa “udhuru”?

Bado unatoa udhuru? Unahitaji kufanya nini juu yake?

Mstari wa 7

Unaafikiaje binafsi juu ya majibu ya Mungu kwa Yeremia?

Unafikiriaje binafsi juu ya kukosekana kwa uwazi wa “kunyumbuka” kwa upande wa Yeremia kukataa wito wa Mungu?

Kunaonekana kutokuwa na nafasi kwa Yeremia kufanya uamuzi wake mwenyewe. Unajisikiaje binafsi juu ya kutokuwa na uchaguzi wa hakika katika hali ya kuitwa na Mungu? Ungekuwa na uchaguzi?

Mstari huu unaleta shida kwa upande wa uhuru wa mwanadamu wa kuchagua na Utukufu wa Mungu?

Kama hili linaleta matatizo, utaitikiaje?

Mstari wa 8

Mstari huu unamaanisha nini kwako binafsi?

Utatumiaje hili binafsi katika hali ya maisha na huduma yako?

Mstari wa 9

Unaweza kuelezea mazingira ambayo Mungu “amekutana” nawe binafsi

Mstari wa 10

Ni nini mistari hii inasema kwako binafsi juu ya hatima ya lengo la Mungu kwenye huduma yako?

Unaweza kuona usawa kati ya kazi ya Yeremia na yako kama mpanda kanisa?

Kulikuwa na vipingamizi ambavyo Yeremia ilimbidi kukabiliana navyo ili kufikia lengo la kujenga na kupanda upya. Nini baadhi ya vipingamizi unavyokutana navyo unapofikia kuelekea kwenye kusudio sawa la kujenga ufalme wa Mungu kwa kujenga makanisa mapya?

Unajisikiaje juu ya matazamio ya kuwa katika nafasi ambayo unaweza kwenda kinyume na mapokeo na viongozi ambao wanaweza kupinga wazo lako la upandaji kanisa.?

Ni jinsi gani utashughulika na vipingamizi na hao ambao wanawezekana wakakupinga?

Mstari wa 12

Ni kwa jinsi gani unaona kanuni ya mstari huu ikileta maana kwako binafsi?

Mstari huu unafanya nini kwenye ujasiri wako kama mpanda kanisa?

Mstari wa 16

Unashughulikaje na swala la “miungu mingine” katika maisha yako mwenyewe?

Ni nini unahitaji kufanya kuhakikisha kuwa utii wako ni kwa Mungu tu na siyo kwa “miungu” kama vile mali, utaifa, n.k.?

Mstari wa 17

Unapimaje utayari wako katika hatua hii kuweza kusimama kwa ajili ya Mungu dhidi ya upinzani wote?

Unahitaji kufanya nini binafsi kujitayarisha katika misukosuko yote?

Ni eneo gani katika maisha yako linahitaji kusaidiwa kiroho?

*Mstari wa 18*
Mungu alimuimarisha Yeremia. Ni jinsi gani Mungu amekuimarisha kusimama kwa ajili yake.

Ni nini Mungu amekupatia kuwa nawe katika misukosuko yote?

Ni jinsi gani hili linakufanya kujisikia juu ya Mungu na msaada wake kwako na katika huduma?

Jinsi gani hii inakufanya kujisikia kuhusu Mungu na utoaji wake kwako na huduma yako?

Ufupisho:

Matumizi ninayoona kwa maisha yangu na huduma katika Yeremia 1 ni:

### Utekelezaji wa Azimio

Kama hukuwa na mda wa kutosha kukamilisha somo hili kama kundi, fanya hivyo kabla ya warsha ijayo ili kwamba uwe na kufahamu kanuni.

# NJIA ZA KUJIFUNZA BIBLIA – Azimio la Mafunzo 7

## Warsha ya Matumizi

Fata maelekezo hayo hayo yaliyotolewa kwa azimio la 3 kwa "Warsha Hii ya Matumizi."

**A. Kumbuka Kanuni ya Kibiblia**

Iandike tena kanuni ya kibiblia ambayo ulitoa kutoka Matendo 17:1-10a kutoka somo la 5:

**B. Linganisha Mandhali**

Ili kwa matumizi yako kuwa ya kufaa, mandhali yako yanatakiwa yawe sambamba na mandhali ya mwanzo ya kibiblia.

1. Kwa kifupi elezea mandhali ya mwanzo ya kibiblia ya Matendo 17:1-10a:
2. Kwa kifupi elezea mandhali yako ya sasa (wewe ni nani, nini unachofanya, n.k.):
3. Andika maelezo mafupi ya angalau kwa njia moja ambayo mandhali yako ni sawa na yale katika Matendo 17 (Tambua: Hili litatofautiana kwa namna fulani kwa kila mtu kwenye kundi, lakini pia kutakuwa na kufanana ambako unatakiwa kuweza kusaidiana mmoja kwa mwingine ).

**C. Fikiria Kuhusu Masomo ya Matumizi**

Soma fungu lote na ona kama moja ya topiki zifuatazo zinaonekana kufaa kwa hali yako. Kama ni hivyo, nukuru jinsi inavyoendana. Pengine kuna topiki nyingine zaidi zinazofaa. Kama ni hivyo, zinukuru hapo chini.

| | | |
|---|---|---|
| Imani | Dhambi | Muhusika |
| Tabia | Changamoto | (mengine) |
| Matendo | Ahadi | (mengine) |

**D. Maswali ya Jumla**

Uliza maswali ya jumla yaliyoorodheshwa hapo chini. Soma majibu yako kwa lolote linalofaa.

Kuna mfano kwangu wa kufata?
Kuna dhambi ya kuepuka?
Kuna ahadi ya kudai?
Kuna maombi ya kurudia?
Kuna amri ya kutii?
Kuna sharti la kutimiza
Kuna mstari wa kukariri?
Kuna kosa la kuwekea alama?
Kuna changamoto ya kukutana nayo?

**E. Uliza Maswali Maalumu**

Sasa unapofanyia kazi fungu hili pamoja, fikiria maswali maalumu kwa kila mstari ambao unakazia "Nini Ninatakiwa Nifanye?" andika maswali hayo, na majibu.

[Zungushia maswali bora mawili ambayo ungeweza kutumia katika kuongoza kundi la kujifunza kwa kufata la somo hili.]

Ufupisho:

Mtakapokutana tena, jadili na linganisha matumizi mnayoona katika fungu. Mwisho, linganisha maswali ya 'matumizi' ambayo kila kundi limechagua, na chagua mawili ambayo yatakuwa ya msaada zaidi kama mngekuwa mlikuwa mnaongoza mafunzo ya kujifunza kwa kufuata neno ya fungu.

**Utekelezaji wa Azimio**

Umeendelea mbele sasa katika hatua ya uchunguzi, ufafanuzi, na matumizi. Kabla ya semina ijayo, utatakiwa kuanza kwa ufupi njia ya kujifunza Biblia kwa kufuata neno kwa kutumia kanuni uliyojifunza. Utakuwa na dakika 20 za kutoa mafunzo haya ya Biblia wakati wa warsha katika semina hiyo. Semina ijayo itajadili kanuni za kuongoza kujifunza kwa kufuata neno.

Katika hatua hii, kazi yako ni kujifunza fungu kwa kutumia njia ya kujifunza kwa kufuata neno, na kutayarisha uchunguzi mwingi, ufafanuzi, na matumizi na maswali ya matumizi iwezekanavyo. Unatakiwa kuonyesha maana ya fungu, na matumizi wakati wa muda huu wa maandalizi. Kisha, kutoka katika maswali yako yote, chagua maswali 5-6 ya uchunguzi, 2-3 maswali ya ufafanuzi, na 1-2 maswali ya matumizi ambayo yatafaa kuongoza wafunzwa wengine kugundua na kutumia mafundisho ya fungu.

Unaweza kuchagua fungu moja kati ya yaliyoorodheshwa chini kwa mafunzo yako. Tafadhali linganisha uchaguzi wako na wafunzwa wengine ili kwamba kila mmoja asifanye fungu lilelile. Kama mfano kwa ajili yako, Ziada 7A ni mfano wa kujifunza Biblia kwa kufuata neno katika kuanzisha kanisa huko Efeso katika Matendo 19:1-10. Mafunzo yako yanatakiwa kuwa na muundo unaofanana, lakini hata hivyo utakuwa na maswali tofauti, wazo kuu, na matumizi.

**Vifungu vya mfano kutoka ambamo utachagua:**

**Matendo 13:4-12**
**(Pafo)**
**Matendo 13:13-52**
**(Antiokia)**
**Matendo 14:1-7**
**(Ikonio)**

**Matendo 14:8-20**
**(Listra na Derbe)**
**Matendo 16:11-40**
**(Filipi)**
**Matendo 17:10-15**
**(Beroya)**

**Matendo 17:16-34**
**(Athen)**
**Matendo 18:1-17**
**(Korintho)**

# UINJILISTI –Azimio la Mafunzo 1

## Utangulizi Kwenye uinjilisti: Kwa Jinsi Mungu Alivyopenda Ulimwengu

Somo halifuati Kozi ya Omega. Badala, linaweka msisitizo kwenye kujifunza jinsi y kutoa injili kwa kutumia Evangecube. Kama huwezi kupata Evangecubes kwa kila mmoja wa wanafunzi wako wapanda kanisa, tumia nyenzo kwenye Kozi ya Omega.

**I. Asili ya Uinjilisti**

- **A. Utaratibu**
  Ina maana gani kufata mfano wa paulo katika maombi katika **Efe. 6:19-20, Col. 4:2-6?**
- **B. Kuanzisha Mazungumzo kuhusu Evangecube**
- **C. Kuonyesha Evangecube**
  - a. Mtiririko 1 – Mungu ni pendo**. (1 Yohana 4:8,16**) Mtu ametengwa na Mungu kwa dhambi. **(Rum. 3:23)**
  - b. Mtiririko 2 – Kristo alikufa msalabani. **(Rum. 5:8, Yohana 3:16)**
  - c. Mtiririko 3 – Kristo alizikwa kaburini. (**1Kor. 15:3**)
  - d. Mtiririko 4 – Mungu alimfufua Yesu siku ya tatu (**1 Cor. 15:4)**
  - e. Mtiririko 5 – Yesu ndiyo daraja letu pekee kwa Mungu. **(Yohana 14:6)**
  - **f.** Mtiririko 6 – lazima tupokee zawadi ya bure ya uzima wa milele kwa imani, (**Efe. 2:8,9)**

**Maombi ya imani: (tulia palipoonyeshwa kwa /)**
**"Mungu, asante kwa kunipenda. / Ninakiri kwamba nimekutenda dhambi. /Ninaamini kwamba Mwanao, Yesu, / alikufa msalabani / kulipia dhambi zangu / na kwamba ulimfufua Yesu kutoka kwa wafu. / Na sasa naweka imani yangu kwa Yesu pekee / kunisamehe/ na kuniokoa kutoka dhambini**

**mwangu. / Ninakili kwamba Yesu ni Bwana! / asante kwa zawadi yako ya uzima wa milele. / Ninaomb kwa jina la Yesu, / Amina."**

| |
|---|
| Gawanya darasa katika jozi na fanya kila mjumbe katika jozi kutoa Evangecube kwa mjumbe anayefata. Jozi zinatakiwa kujadili uzoefu. |

**Kufuasa: "Kama muumini katika Kristo unatakiwa—kuomba kila mara (Flp 4:6-7), kutana na waumini wengine (Ebr 10:25), kujifunza Biblia (1Pet 2:2), kuwaambia wengine injili (Marko 16:15), kumpenda Mungu na wengine kwa moyo wako wote (Mat. 22:36-40.**

## Utekelezaji wa Azimio

**Nenda mlango kwa mlango kwenye eneo lengwa kwa kanisa lako mpya na kutoa injili kwa angalau wasio waumini watano kwa kutumia Evangecube.**

# UINJILIST – Azimio la mafunzo 2 & 3

**Kuanzisha Ushuhuda wako Binafsi:** Hiki ndicho Mungu alichonifanyia!

KIPINDI 2

**I. ASILI YA Ushuhuda**
- A. Tumeitwa kuwa Washuhudiaji **(Matendo 1:8)**
- B. Tumeitwa Kutoa Ushuhuda (**Matendo 10:42)**

**II. Thamani ya Ushuhuda**
- A. Kushinda upinzani kwenye injili (Ushuhuda binafsi **Matendo 26:12-18)**
- B. Kumshinda Shetani katika vita vya kiroho **(Uf. 12:10-12)**

**III. Mifano ya Shuhuda**
- A. Mwanamke kisimani (**Yohana 4:28-29)**
- B. Mtu aliyezaliwa kipofu (**Yohana 9:13-34)**
- C. Mazungumzo ya Paulo (**Matendo 9 22, 26)**
- D. Ushuhuda wa Paulo kuhusu tukio la Yerusalemu (**Matendo 24:10-21)**

**IV. Maandalizi ya Ushuhuda: Vitu vya Ufunguo**
- Maisha yako kabla hujakutana na Kristo yalikuwaje?
- Jinsi gani umekuja kumjua Kristo?
- Jinsi gani kumjua Kristo kumebadili maisha yako?

KIPINDI 3

**IV. Kushirikisha ushuhuda Binafsi**

Ushuhuda unatakiwa uwe **kamili, wazi, injli, na mfupi.**

| |
|---|
| Gawanyika katika makundi ya watatu. Kundi linatakiwa lifanye marudio ya ukamilifu, uwazi, injli na ufupisho. Kisha, kila mtu anatakiwa kushirikisha ushuhuda wake binafsi kwa wengine kwenye kundi. Darasa lote linatakiwa lilinganishe matokeo na, mda unavyoruhusu, washiriki wachache wanaweza kushirikisha ushuhuda kwenye darasa. (inaweza ikachukua dakika 60) |

## Utekelezaji wa Azimio

Shirikisha ushuhuda wako wakristo wengine angalau watatu watakaoweza kuona kama uko wazi katika kuwakilisha kwako.

Uwe tayari kushirikisha tena ushuhuda wako wakati wa mafunzo yajayo au wakati wa semina hii

Kwa maombi weka mpango ambao utaletea kushirikisha ushuhuda wako kwa watu wawili wasio wakristo au watu unaowasiliana nao katikati ya wiki mbili. Mwombe Mungu kuandaa "muda wa kimungu" kwa ajili yako kushirikisha ushuhuda wako (pengine bila maonyo ya kuendelea) katikati ya wiki nne zijazo.

# Omega Mwongozo wa Pili Azimio la Mafunzo

# MAONO YA KUM—Azimio ka Mafunzo 5

## Misingi ya Kibiblia ya Kueneza Upandaji Kanisa

### Kuijaza Dunia kwa Ufahamu wa Utukufu wa Mungu

**I. Kueneza katika Agano la kale**

1. Na nini ilikuwa dunia yote ienezwe katika mistari hii ya Agano la Kale? Zab**. 72:19, Isa. 11:9, Isa. 66:18**. Hili linahusika leo? Ukweli wake unadhihirika zaidi leo au unadhihirika kidogo?

**II. Huduma ya Yesu**

1. Ni nini **Mat. 4:23 na Luka 10:1** inatuambia kueneza kwa Yesu Galilaya? Kwa nini kukazia Galilaya kuliko kwenye taifa lote la Israeli? Hili linatuelekeza leo?
2. Katika mfano wake wa mbegu ya haradali (**Mat 13:31-32),** Yesu anatuambia kwamba kutoka kwenye mwanzo mdogo ufalme wa Mungu utakua kuwa Mkubwa. Katika mfano wa Hamira (**Mat. 13:33**), donge dogo la hamira linabadilisha donge la mkando kuukuza kama ufalme wa Mungu unavyokua. Je hili linachangia chochote kwetu kuhusu mapenzi ya Mungu na mpango kwa injili na kwa kanisa?

**III. Misingi ya Kibiblia kwa Kueneza Upandaji Kanisa**

| |
|---|
| DARASA KUBWA KULIKO 9 TUMIA KUNDI DOGO LA MAJADILIANO KWA MASWALI CHINI |

1. Ni nini **Efe 3:10** inatuambia ni **chombo** cha kueneza injili?
2. Ni nini **Matendo 1:8** na **Mat. 28:18-20** inachosema ni amri ya Yesu ya kuenezea injili
3. Jinsi gani inawezekana Ibrahimu kuwa mfano kwetu leo? **(Mwa. 12:1-3)**
4. Kulikuwa na **kueneza** upandaji kanisa na Paulo kupita Samaria? (**Matendo 19:9-10**)
5. Ni nini mistari hii inatuambia Mungu atafanya na jinsi atakavyolifanya? **(Ebr 2:14, Mat 16:18, Yohana 20:21, Matendo 13:1-3, 19:9-10)**

| |
|---|
| TUMIA VIKUNDI VIDOGO VYA MAJADILIANO KWA MASWALI HAYA, MDA UKIRUHUSU |

Inawezekana kuutimiza Utume Mkuu kwenye eneo maalumu bila upandaji makanisa?

Kanisa lako limevutwa na kusidi la kuzidisha na uenezaji?

Una mpango wa kupanda makanisa miongoni mwa wa mataifa mengine katika nchi yako?

Ni makanisa mangapi eneo lako linahitaji kuweza 'kuenezwa?'

Unaamini Mungu anataka kuongeza taifa lako kwenye ukurasa katika historia? Kama ni hivyo, jinsi gani?

| |
|---|
| Liambie darasa, "Leta matokeo ya Utekelezaji wa Azimio kwa Mwongozo wa Kwanza maono ya KUM somo la 4 kipindi kijacho." |

# MAONO YA KUM—Azimio la Mafunzo 6

### **Warsha ya Utafiti:** Kutoa matokeo ya Utafiti wa Eneo Lengwa

Somo hili linatokana na utekelezaji wa azimio wa Mwongozo wa Kwanza Maono ya KUM somo la 4. wanafunzi wapanda kanisa wanatakiwa walete matokeo ya utekelezaji huu wa azimio kwenye kipindi hiki. Waruhusu wafunzwa wote kutoa waliyopata kwenye agizo la utafiti wao kutoka kwenye Mwongozo wa Kwanza (maono ya KUM Ziada 4A, "Kuelewa Eneo Lako Lengwa"). Kama wana michoro, ramani, vibao vya matangazo, n.k. yaweke wazi haya ili kwamba yaweze kuonwa wakati wa mapumziko na mda huru. Kama kuna ripoti zaidi ya nne za kutolewa mda wa saa hii, unaweza kutaka kufanya kazi katika vikundi vidogo. Vinginevyo, unaweza kuchagua ripoti chache kusikilizwa na kila mmoja na kuzizungumzia.

Kila mfunzwa au timu ya wafunzwa wanatakiwa kuchukua dakika 10-15 kutoa waliyopata wakitumia mipaka ifuatayo:

**Sehemu ya Kwanza—Takwimu za Kawaida Zilizokusanywa (dakika 5-7):**

Elezea eneo lako lengwa. Weka kwa ufupi ulichojifunza katika hatua ya 2 na 3 kwenye Maono ya KUM Ziada 4A "Kuelewa Eneo Lako Unalolenga."

Jinsi gani ulivyokusanya taarifa zako (ukaguzi, mahojiano ya kawaida, uchunguzi, kuweka ramani, utafiti kwenye makitaba, n.k.)?

Jadili matatizo yoyote makubwa au ugumu uliokutwa na jinsi ulivyoshindwa. Ni nini ungefanya tofauti mda ujao?

**Sehemu ya Pili—Mchanganuo wa Utafiti (Kuweka ramani Kiroho) Takwimu (dakika 5-8):**

Ukumbusho wa utoaji unatakiwa kuelekezwa kwenye matokeo yaliyopatikana. Mkijibu maswali ya ufunguo yaliyoorodheshwa hapo chini inaweza kusaidia.

Ni taarifa zipi zilikuwa za kufurahisha zaidi ulizojifunza kuhusu eneo lako unalolenga na watu wanaoishi hapo?

Kulikuwa na taarifa zozote zilizokushitua?

Ni vitu gani maalumu ulivyojifunza ambavyo vitakusaidia kuonyesha mkakati wako kwa upandaji kanisa katika eneo lako unalolenga?

Ni ukweli gani mmoja kwa upandaji kanisa uliohakikisha kwamba ulikwisha kuujua kuhusu shamba la mavuno?

Ni utafiti gani mpya ambao ni muhimu sana kwa upandaji kanisa ulioofanya kuhusu shamba la mavuno ambao mwanzoni hukuujua?

Ni nafasi zipi ulizopata kama mlango wazi kwa injili?

Ni vikwazo gani ulivyopata na jinsi gani vinaweza kushindwa?

Ni utafiti gani zaidi unahitaji kufanyika ili kuanzisha uinjilisti mpana na mkakati wa upandaji kanisa kwa eneo lako unalolenga?

# MAONO YA KUM—Azimio la Mafunzo 7

### Kuhamasisha Rasilimali Kupitia Utafiti (Kuweka Ramani Kiroho)

Katika kufundisha somo hili, jaribu kutoa mifamo maalumu ya wapi kushirikisha utafiti kumepelekea katika kuhamasisha watu, maombi au rasilimali za juhudi za upandaji kanisa. Pia, jaribu kutoa mfano wa taarifa ambazo zimeshirikishwa isivyopasa zilivyopelekea mtokeo mabaya. Wasaidie wafunzwa kuona jinsi ambavyo hili lingekuwa limezuiliwa na nini wanahitaji kujifunza kutokana na makosa yao.

**I. Wito kwenye Utendaji**

Kufuatana na utafiti wako jibu swali, "Ni nini Mungu anataka kwa eneo langu lengwa? na "Jinsi gani kila mwanaume, mwanamke na mtoto katika eneo hili ataona na kusikia injili kwa namna inayoendana nao?"

Linganisha watu katika eneo lako unalolenga na hao walioelezewa katika **Mat. 9:35-38.** Jinsi gani unaweza kuelezea hali ya watu wanaoishi katika eneo lako unalolenga? Ni nini hali yao ya kiroho? Kuna kanisa lolote miongoni mwa watu hawa? Ni asilimia ngapi ya watu wanaohudhuria kanisani au wanaojilinganisha wenyewe kama wafuasi wa Kristo? Wako wazi kwenye injili? Ni makundi gani mengine ya watu wanaofanya kazi miongoni mwao? Ni makanisa mangapi yanahitaji kupandwa katika eneo lako unalolenga ili kwamba kila mtu anapata nafasi ya kusikia na kuona injili kwa njia ambayo inaendana nao na hali yao?

Ni nini hasa Mungu anakuitia na timu yako kufanya kuwafikia watu katika eneo lako lengwa?

Jinsi gani utajitolea mwenyewe kwenye maombi kwa watu katika eneo lako unalolenga?

Ni rasilimali zipi (watu, makanisa na huduma) vinaweza kuhamasishwa kusaidia kuwafikia watu wa eneo lako unalolenga?

Ni wajibu upi wewe na timu yako mtashika katika kuwaandaa wengine kuomba na kufanya kazi nanyi katika kuwafikia watu wa eneo hili linalolengwa kwa injili?

**II. Mipaka katika Kushirikisha Taarifa**

Ni kwa nani unatakiwa utoe matokeo ya utafiti wako?

Ni malengo yapi ya kushirikisha utafiti wako yatapelekea mengine?

**III. Onyesha Jinsi ya Kuhamasiha Nguvu ya Mavuno**

Utafiti ni zaidi ya kukusanya taarifa tu. Ni utaratibu wa kusisimua wengine kufata matakwa ya Mungu na makusudi. Kwa jinsi hiyo, taarifa zinazoshirikishwa isivyopaswa zinaweza kusababisha aibu na kusikia haya, kutakakopelekea hasira, kujilinda na mkao wa kutaka kutobadilika. Taarifa yako ya utafiti inaweza kuwa chombo chenye nguvu ambacho Mungu anaweza kutumia kuwapa wengine mzigo kwenye mahitaji ya eneo lako unalolenga na haja ya kuona watu wanaoishi katika eneo hilo wakigeuka kuwa wafuasi wa Yesu Kristo.

Ni mkakati upi utaanzisha kwa kuhamasisha nguvu ya mavuno?

Jinsi gani matokeo ya utafiti wako yanaweza kunufaisha juhudi zako za upandaji kanisa?

Jinsi gani kushirikisha utafiti wako kunagusa uhusiano wako na viongozi wa kikiristo bayana au kinyume?

## UTEKELEZAJI WA AZIMIO

Na timu yako ya upandaji kanisa, chunguza tena taarifa zako za utafiti na andika kile Mungu anachokuonyesha kwa upandaji wako wa kanisa. Shirikisha wito huu kwenye utendaji na mkufunzi wako au mshauri au watu wengine wanaofaa.

Andika harakati za kuhamasisha kushauri wengine kukusaidia katika juhudi za upandaji kanisa. Weka na wale utakaowashirikisha matokeo ya utafiti wako, nini utakachowashirikisha, jinsi gani unadhani watashiriki kwenye kazi yako (maombi, utoaji, kujiunga na timu yako, n.k.). Shirikisha mkakati huu kwa mkufunzi au mshauri.

Weka mkakati wako wa kuhamasisha na shirikisha matokeo na mkufunzi au mshauri au katika kipindi kingine cha mafunzo.

# KANISA—Azimio la Mafunzo 5

## **Asili ya Kanisa:** Kanisa ni kimbe Hai

**I. Maana na Matumizi ya Neno "kanisa"**

**A. Matumizi ya Neno Ekklesia (Kanisa) kwenye Agano Jipya**

Ni nini maana ya neno, kanisa, inavyomaanisha katika mistari hii? (**Col. 4:5, Matendo 15:4,22,30; 1 Tim 5:17, Ebr 10:25)**

Ni tofauti gani za kijografia katika matumizi ya kanisa katika mistari hii? (**Gal. 1:22, Matendo 9:31)**

Jinsi gani neno, kanisa linavyotumika leo?

**II. Dhana ya Uongo ya kanisa: Kanisa Siyo Hekalu**

Kwa nini Kielelezo cha Hekalu la Agano la Kale siyo kielelezo kinachotoshereza kwa kuelewa kanisa la Agano Jipya ? (**1 Kor. 6:19, Matendo 17:24)**

**III. Methali Zinazoelezea Kanisa Kama Kiumbe Hai**

Ni familia **(1Tim 3:14-16; Efe 3:15; 2The 3:15, 1Pet 2:17).**
Ni mwili (**1Kor. 12:12-27**).
Ni kundi **(Matendo 20:28-29).**
Ni watu **(1Pet 2:9-10).**
Ni bibi arusi (Ufu **21:2**).
Ni jengo (hekalu hai) **(Efe 2:20-22).**
Ni ukuhani (**Uf 1:5-6).**
Ni tawi (**Yn 15:1-16).**

Ni nini kila moja ya methali hizi inatuambia kuhusu asili ya kanisa?
Nini inaweza kuwa tatizo kuona kanisa kama mwili na ukuhani lakini siyo kama familia na kundi?

**IV. Upandaji Kanisa Hai**

Jinsi gani ukweli kwamba kanisa ni kiumbe hai kunagusa njia yetu ya upandaji kanisa la mtaa?

A. **Wajumbe wa Kanisa** la Mtaa Wanatakiwa Wawe **Waumini**

Ni nini lazima mtu afanye kuwa sehemu ya kanisa la Yesu Kristo (Mwili wa Kristo)? Jibu lako lizingatie kwenye maandiko.
Ni nini mtu lazima afanye ili kuwa sehemu ya kanisa la mtaa?
Ni kwa njia zipi uzoefu wako unaonyesha mafundisho ya Agano Jipya kuhusu asili ya kanisa?
Inatosha kwa mtu kuwa hai kwenye mashirika ya makanisa makubwa na kutokwenda kanisani? Kwa nini?

B. Kwa nini ni kwamba **jengo halitakiwi** kuwa **kitu cha msingi cha kufikiria?**
**C.** Unakubaliana na hao wanaosema kwamba **mahusiano ni funguo?**
D. Unakubaliana kwamba kanisa la mtaa lazima **lirithi kwenye utamaduni?**
E. Ni **mifumo ipi ya utaratibu** muhimu kwa kanisa? **(Matendo 20:7; Matendo 14:23, 1 Kor 5:1-5; 2 Kor 8:1-5)**
**F. Vikundi kiini** vinatakiwa kuchukua wajibu**. (Matendo 2:42-46)**

# KANISA-Azimio la Mafunzo 6

## Kazi ya Ushirika ya kanisa: Nini Kinatokea Mnapokuja Pamoja

**I. Ushirika Dhidi ya Majukumu Binafsi ya Kanisa**

**Kazi za ushirika za kanisa la mtaa zinatakiwa pia zitumike kwenye vikundi vidogo vya waumini.**
Ni kazi zipi za lazima ambazo "kanisa" lazima lizifanye?
Ni waumini wangapi wanahitajika kufanya kazi kazi ya ushirika wa kanisa
Jinsi gani tunatimiza amri ya **Waebrania 10:25** kama kanisa la mtaa halipo?

**II. Kazi ya Ushirika ya Kanisa**

**A.** Je **kuabudu** kunawekwa kwa kanisa kubwa au kundi la watu sita au nane wanaweza kufanya ibada ya ushirikiano?

**B. Maagizo**

1. Je ubtizo ni agizo la Agano Jipya? Ni nini mistari hii inatuambia kuhusu ubatizo: Lini unafanyika **(Mdo 8:36; Mdo 16:33),** na nani **(1Kor 1:14-17**)?
   a. Ubatizo ni dalili ya Nini? (**Matendo 2:41**) Jibu: Kujitambulisha kwa mtu kwa Kristo
   b. Ubatizo ni dalili ya nini tena? Jibu: mapatano kati ya mtu na Mungu (**Rum 11:27, 2 Kor 3:6, Ebr 12:24)**
2. Meza ya Bwana **(1 Kor. 11:23-34)** Ni nini kusudi lake na nani anatakiwa aitumie?

**C.** Huduma ya **Neno (1 Tim. 4:13)**

**D.** Kujengana mmoja kwa mwingine **Ni nini mistari ifuatayo inasema kuhusu kujengana?**
kupendana (Y**n 13:34; 15:12,17)**

kujitoa kwa mmoja kwa mwingine (**Rum 12:10)**
kukubaliana mmoja kwa mwingine (**Rum 15:7)**
Kuelekezana mmoja kwa mwingine (**Rum 15:14)**

**E.** Ni kazi gani **Yohana 15:26-27** inatuambia kuifanya? Jibu: Uinjilisti

**F.** **Utoaji ( Flp. 4:19) –** Ni kwa nani kundi dogo litoe sadaka

**III. Lini Wakati wa Kufanya Kazi ya Ushirika**

Fanya zoezi la darasa kwa kutumia mchoro hapo chini. Weka meza kwenye ubao au ubao wa kuonyeshea

Tambua kama unakubaliana na kazi zilizoorodheshwa.
Ongeza kazi zingine zozote unazofikiri kuwa muhimu lakini zinazokosekana.
Weka alama "ndiyo" au "hapana" kati kati na kulia kwenye safu kuonyesha kama au la unafikiri haya yanahitajika na vikundi vidogo, kanisa la mtaa, au yote. Jadili hoja yako.

**Mchoro: Kazi ya Ushirikiano**

| **Kazi ya Kibiblia** | **Kikundi Kidogo** | **Kanisa la Mtaa** |
|---|---|---|
| Uinjilisti wa Kirafiki | | |
| Utoaji kwa wapanda Kanisa | | |
| Ufuasishaji | | |
| Ibada ya Ushirika | | |
| Kuhubiri | | |
| Ushuhuda wa Mtu Binafsi | | |
| Ubatizo | | |
| Meza ya Bwana | | |
| Utoaji kwa Masikini | | |
| Uimbaji wa Kundi | | |
| Utunzaji wa Viongozi wa kanisa | | |

Maswali kwa majadiliano mengine (kundi dogo kama darasa ni kubwa):

Ni nini kazi ya ushirika ya kanisa?

Jinsi gani kazi ya ushirika inaendana na kundi dogo la waumini?

Ni nini kazi ya kuhubiri katika mkusanyiko wa ushirika? Ni nini kazi ya kujifunza Biblia kwa kundi?

Nini unachoelewa kuwa maana kuu ya ubatizo wa maji?

Kwa nini utoaji ni kazi ya ushirika ya kanisa?

## Utekelezaji wa Azimio

Pamoja na wajumbe wa timu yako ya upandaji kanisa, amua lini mtaanza kuendesha kusanyiko la ushirika. Ni mfumo upi makusanyiko haya yatachukua?

# KANISA—Azimio la Mafunzo 7

## **Kuanzisha Maelezo ya Kusudi la kanisa:** Kwa nini Kanisa Lako Liwepo?

Hii ni warsha. Washiriki wanatakiwa kuandika maelezo yao wenyewe ya kusudi la kanisa na kuyashirikisha kwa washirki waliobaki.

Katika Mwongozo wa Kwanza juu ya Somo la kanisa la 4, umeanzisha tafsiri ya kanisa la mtaa. Inajibu swali la "Nini" Maelezo ya kusudi yanajibu swali la "Kwa nini" – Kwa nini kanisa maalumu lipo? Andika inachokuambia kila mstari kuhusu swali la "Kwa nini"

| | | |
|---|---|---|
| **Mat 16:18** | **Matendo 2:42-47** | **Col 3:12-17** |
| **Mat 28:18-20** | **Efe. 3:10-11** | **Ebr 10:22-25** |
| **Matendo 1:6-8** | **Efe 4:11-16** | **1 Pet 2:1-5,9,12** |

**III. Andika maelezo ya kusudi**

Jiulize mwenyewe maswali yafuatayo:

**Kwa nini kanisa uliloitiwa lipo?**

**Ni nini itakuwa upekee wake na sehemu maalumu katika kazi ya ufalme wa Mungu?**

**Kama muwakilishi wa Mungu mahali panapolengwa, uko pale kufanya nini?**

Andika sababu 10 kwa nini watu wanatakiwa kuhudhuria kanisa lako mpya.

Mfano #1: Kanisa la Habari njema lipo kumwabudu Bwana, kuwaadilisha waumini na kutangaza injili kwa waliopotea huko katika kijiji cha Smith.

Mfano #2: Kanisa la Ushirika wa Injili lipo kutangaza injili katika mji wa Grant, kata ya Brown, taifa letu na ulimwengu.

Mfano #3: Kanisa la Ufufuko liko kuhudumu kwa familia kwenye mji wa Riverbendi.

Maswali ya kutafakari, marudio na matumizi

Tafsiri yako ya kanisa na ya maelezo ya kusudi la kanisa yanafuatana na uzoefu wako binafsi katika kanisa, au kwenye maandiko?

Maelezo yako ya kusudi la kanisa yanapatana na kusudi la kibiblia la kanisa lililojadiliwa katika "Somo la Kanisa la 2?" Kama siyo, nini kinakosekana?

Kwa nini maelezo yaliyoandikwa ya kusudi la kanisa ni muhimu?

Jinsi gani kanisa lako linakwenda kuwa tofauti kutoka makanisa mwengine?

## Utekelezaji wa Azimio

Ruduia hatua hii ya kufanaya na kuandika maelezo ya kusudi la kanisa na viongozi wa kanisa lako lililopandwa. Haya yanaweza yakawa yaliyotunzwa hivi karibuni, viongozi wanaoibuka, au wengine ambao unashirikiana nao kupanda kanisa. Kama hili ni kanisa binti, haya yanaweza kutoka kwenye kanisa mama; viongozi ambao wanajihusisha zaidi katika hatua ya kuzalisha makanisa binti mapya.

# KANISA—Azimio la Mafunzo 8

Falsafa ya Huduma ya Upandaji wa Kanisa: Jinsi Gani Kanisa Litahudumu Kwa Ulimwengu Uliopotea

**I.** Ni nini **Falsafa ya Huduma ya Upandaji kanisa?**

Jibu: **Kuelewe kwetu kwa "jinsi tunavyofanya vitu" au mkakati wetu wa kufanya huduma.**

**II. Hitaji** Kwa falsafa ya Huduma ya Upandaji Kanisa

A. Biblia inafundisha hitaji kwa **kupanga kwa kufikiri** (**Mithali 14:15: Mithali 15:22)**

Yesu alikuwa na mawazo juu ya jinsi ambavyo angeweza kufanya vitu? **Mat 16:21-23, Mk 1:45, Yn 6:5**

Paulo alikuwa na mawazo juu ya ambavyo angefanya vitu? **Rum 15:20, 1 Kor 2:1-2**

B. Falsafa ya huduma ya upanfdaji kanisa ni ya **kivitendo Efe 2:10**

C. Falsafa ya huduma ya upandaji kanisa inakazia kutenda kwetu

D. Falsafa ya huduma ya upandaji kanisa inatakiwa iwe maalumu – Inafikiria:

Uwezo na udhaifu wa mpanda kanisa

Kutumia timu ya upandaji kanisa inapowezekana

Ni ya kipekee kwa kanisa mpya

**III. Yaliyomo** kwenye falsafa yenye ufanisi ya huduma ya upandaji kanisa

A. Inajenga kwenye tafsiri na kusudi
B.Mandhali ni maalumu: Ni nini mandhali ya kanisa lako?
C. Kama inakazia watu: Ni watu gani kanisa lako linahudumu?
D. Inatumika **kama chombo cha kutathiminia**

Fata maelekezo hayo hayo yaliyotolewa kwa azimio la 3 kwa “Warsha Hii ya Matumizi.”

## Utekelezaji wa Azimio

Tumia zana hapo chini kumfanya kila mshiriki kuanzisha falsafa wazi ya huduma ya upandaji kanisa. Kama inawezekana, wape wanafunzi wapanda kanisa nakala ya yafuatayo kwenye lugha zao. Vinginevyo, andika maswali yote ubaoni .

**KUANZISHA FALSAFA YA HUDUMA YA UPANDAJI KANISA**

Ili kuanzisha falsafa wazi ya huduma ya upandaji kanisa, unahitaji kufikiria yafuatayo: Unatakiwa uwe na kuelewa wazi wa kile Mungu alichoitia kanisa kuwa na kufanya (Maelezo ya Kusudi) na anacholiitia kanisa lako mpya kuwa na kufanya. Ni nini Mungu anakutaka kukamilisha kwa miaka mingine ijayo 3-5 kama kanisa mpya?
Unatakiwa uwe na ufahamu wa watazamaji walengwa. Ni watu gani unatafuta kuwafikia?

Ni nini baadhi ya miundo inayowezekana unayoweza kutumia kuanzisha kanisa lako mpya (ibada ya kuabudu, vikundi kiini, shule ya Biblia, maombi ya utatu ya kufikia nje, n.k.)?

Ni nini vipawa, uwezo, na udhaifu wako mwenyewe na timu yako?

I. Maswali ya Kufikiria katika kuanzisha falsafa ya Huduma

Jibu maswali yafuatayo pamoja na wengine katika timu yako ya upandaji kanisa

A. Ni maneno yapi matatu utapenda kuelezea kanisa mpya unalopanda?
B. Ni akina nani wamo katika jumuia unayotaka kufikia? Ni aina gani ya watu watakuwa sehemu ya kanisa lako?
C. Ni nini kitalifanya kanisa hili kuwa tofauti?
D. Ni kitu gani kinaweza kuwa cha kuvutia zaidi kwa kanisa lako?
E. Ni nini ambacho kanisa lako litasihi kwa watu kwenye mji/kijiji unachotafuta kufikia?
F. Ni kwa nani kanisa lako litakuwa na kusihi kwingi?
G. Ni kwa nani ungependa kanisa lako kusihi?
H. Ni vipindi gani na shughuli zinaweza kuwa za ufanisi kwa kanisa? Jinsi gani utapima mafanikio haya?

II. Utofauti wa Kipekee Kuhusu Kanisa Lako

Ni nini cha kipekee au tofauti juu ya jinsi kanisa lako linavyofanya linachofanya (litakachofanya) katika maeneo yafuatayo—kuabudu, mafundisho ya maandiko, uinjilisti, ushirika, uongozi, kazi za vijana na watoto, mahusiano ya jumuia, huduma za kijamii, misheni, elimu, fedha, rasilimali, majengo na mengineyo.

III. Mtindo wa Huduma

Katika aya moja au mbili, eleza mtindo wa huduma unayowazia kwa ajili ya kanisa lako. Ni nini itakuwa kanisa lako la pekee “hadhi?”

IV. Thamani

Ni vitu gani vinalithamanisha kanisa lako? Ni mvuto gani utaelekeza juhudi za huduma yako katika miezi iyayo na miaka? Orodhesha angalau thamani 10 sasa.

V. Eleza Falsafa ya Huduma Yako

Katika aya mbili, jaribu kuandika maelezo ya falsafa ya huduma yako ambayo yatakuwa na vipengele kutoka katika karatasi hii ya mazoezi. Unaweza kubuni maneno machache ya kukumbukwa ambayo yanatwaa falsafa ya huduma yako ?

Falsafa Yangu ya Huduma ya Upandaji Kanisa
Kivumishi cha Kanisa Langu

VI. Jadili na linganisha maelezo yako na wengine

Kumbuka kwamba hakuna hali mbili zinazofanana, na kwa hiyo hakuna falsafa mbili ambazo zitafanana, jadili na linganisha maelezo yako na waliofundishwa na wengine. Kisha jadili na viongozi wa kanisa na wajumbe wa timu yako ya upandaji kanisa. Fanya marudio ya maelezo hayo mara kwa mara, na yatumie wakati wa utaratibu wa upandaji kanisa kutathimini kama unafanya kitu sahihi au la na katika njia sahihi.

# TABIA YA KIROHO—Azimio la Mafunzo 6

I. **Kuishi Kama watoto Badala ya Mayatima:** Wagalatia 4:1-7

**Maisha Kama Yatima**

Unakubaliana kuwa tabia hizi tatu ni za kawaida miongoni mwa mayatima?

A. Mayatima wamejawa na hofu na kutokuwa salama kukubwa
B. Mayatima wanaishi wakiwa na kipimo kisicho cha kawaida cha kujijali
C. Mayatima wanabeba hisia kuu za upweke

**II. Wakristo Wanaofikiri na Kutenda Kama Mayatima**

Maelezo haya ya yatima yanavuma kama chochote kinachofanana na maisha yako? Ni kwa njia zipi unafanya kama yatima wa kiroho? Ni jinsi gani tunaitikia kwenye magumu yetu? Nini tunachofikiri? Hatuwi na mashaka na kuogopa? Wakati mwingine hatufikiri kuwa mambo yanakwenda vibaya kwa sababu Mungu na kujali kwake kwingi ametusahau?

Soma **Wagalatia 4:1-7**. Jinsi gani uhusiano wetu na Mungu umeelezewa kwenye fungu hili? Ni nini muonekano wa uwana wetu?

**III. Uwana Wetu na Mungu**

Ni nini Y**ohana 14:18** anamaanisha maisha yako pamoja na Kristo?

Katika mithali ya **Gal. 4:1-7**, Ina maana gani kuwa mwana?

Kwa kufikiria Mungu ni nani, Ina maana gani kwamba tu wana wa Mungu?

**Kabla hatujawa watoto wa Mungu, ni nini Warumi 2:14-15 inasema dhamili zetu zinachofanya kwetu? Ni nini Warumi 8:1 inatuambia ni hali yetu katika Kristo? Ni nini Warumi 8:15-17 inatuambia ni uhusiano wetu na Baba?**

Ni nini Mungu ametupatia nafasi ya uwana?

Mungu siyo hakimu tena kwetu lakini sasa ni Baba yetu anayetupenda

**IV. Jinsi Tunavyoshindwa Kuelewa Uwana Wetu**

**<u>Kwa nini sisi, wavulana na wasichana tuliorithiwa, mara nyingi tunajikuta wenyewe kama mayatima? Kwa nini tunajisikia upweke kabisa, waliojawa hofu, na wanaojijali?</u>**

**A. Kufanya Injili kuonekana kutokuwa muhimu kupitia kiburi chetu**

Jinsi gani umefanya dhambi zako kuonekana kutokuwa muhimu?
Jinsi gani kuelewa uwana kunatusaidia kuwa wakweli kuhusu dhambi zetu?

**B. Kufanya injili kuonekana kutokuwa muhimu kupitia kutokuamini**

Jinsi gani umefanya injili kuonekana kutokuwa muhimu kupitia kutokuamini?
Mungu anawahukumu watoto wake kama anavyofanya kwa hao wasiomjua?

## Utekelezaji wa Azimio

"Agizo la ulimi":

Kwa siku mbila zijazo, usiongee upuuzi, usiseme vibaya juu ya mtu, usilalamike, usijitetee mwenyewe mtu anapokuambia vibaya, na usijivune kwa ajili ya mafanikio yako. Sema mazuri tu kwa ajili ya wengine, mshukuru Mungu kwa kila jambo, kiri kwa uaminifu unapokuwa na makosa, na ujivune tu kwa ajili ya udhaifu wako.

Zoezi la ulimi litakusaidia kuona matokea ya nguvu ambayo dhambi bado inayo katika maisha yetu na mahitaji yetu yanayoendelea ya neema ya Mungu. Baada ya zoezi hili utakuwa na shukurani ya ndani ya jinsi Mungu alivyokufanya mwana na siyo kwa ajili ya utii wako, lakini kwa ajili ya ukombozi wa Yesu kwa ajili yako. Hili ni zoezi la maisha yote, lakini kwa uangalifu timiza hili kwa siku mbili zijazo.

# TABIA YA KIROHO—Azimio la Mafunzo 7

## Kujifunza Kuwa Wana

**I. Moyo uliolemezwa dhidi ya Moyo Uliowekwa Huru**

A. Moyo mzito unasababishwa na uzito wa hatia zetu na hisia za kutokufaa. **(Zaburi 51:3)**
Moyo wa yatima wa kiroho unakuwaje? Uelezee.

B. **Warumi 8:31-35** – Katika fungu hili, kuna maswali sita. Ni nini majibu ya maswali haya yote sita? **Rum 8:39**

C. **Gal 5:1; Mt 11:30** Mistari hii inatia faraja? Kwa mfano sisi kama waumini tunatakiwa tupitie maisha kwa hatia na hofu au kukataliwa na Baba, maisha yatakuwaje? Unajisikia kamwe kulemezwa kwa hitaji la kujihakikisha mwenyewe? Umejisikia kamwe kana kwamba ulikuwa ukijaribu kumridhisha hakimu mkari?

**II. Moyo wa Kujisikia dhidi ya Moyo wa Ushirika na Baba**

Jinsi gani mwana anamuona Baba?
Jinsi gani **Yohana 6:6** inaonyesha kwamba Mungu anajaribu uhusiano wetu na yeye.
Kuitikia kwetu kwenye kujaribiwa kunaonyesha mtazamo wetu kwa Mungu. Umejawa na hofu au unajua Mungu ni wa upendo na Baba mwaminifu? Umeongeza juhudi zako mara dufu—pengine hata kushuka chini sana kwa mwingine tu—ili kupata kutawala hali mbaya?
Ni kuitikia gani Mungu anataka kwetu?

**III. Moyo wa Ubinafsi dhidi ya Moyo Huru Kupenda Wengine**

Jinsi gani tunajua kuwa Mungu bado anatupenda?
Jinsi gani tunatenda tunapofikiri kuwa Baba yetu wa mbinguni hatujali kiukweli?
Hili limetokea katika maisha yako ambalo linadhihirisha hali yako na Baba? Mkao wako wa akili ya kiyatima unakuacha ukijisikia kutopendwa? Au unajisikia ni lazima ung'ang'anie sana kwenye kile Mungu alichokupatia kwa hofu ya kukipoteza. Unaweza kwa uhuru kutoa kwa wengine, kwa sababu unaamini kwamba Mungu amekupa bure na kwa wingi?

Toa suluhu kwa somo kwa kufanya zoezi katika Ziada 7A hapo chini. Unaweza kuwaambia wanafunzi wapanda kanisa, "Nitasoma orodha ya mashariti kwa mayatima na wana mara mbili. Gundua maeneo mawili unayohangaika zaidi. Unapokuwa unayasoma mara ya pili, andika idadi na maelezo ya mayatima na wana kwa maeneo haya matatu." (Kama wanafunzi wana Kozi yote ya Omega, wanaweza kusoma haya wenyewe.)

**Ziada 7A.** Fikiria mfano wa kila moja ya maeneo matatu ambapo umeona hangaiko hili. Kwa kila moja, jinsi gani unamtaka Mungu kukubadilisha? Kisha liweke hili kwenye maombi kwa baba yako wa mbinguni.

| YATIMA | | WANA |
|---|---|---|
| KUISHI KWA "KUJARIBU SANA."<br>YESU "MSAADA" WA MWILI<br>*Yoh 14:18 "Sitawaacha kama yatima"* | | KUISHI KWA IMANI.<br>KRISTO MAISHA YETU! Gal 2:20<br>*Rum 8:15 "Atupa roho ya uwana"* |
| Kujisikia upweke; kukosa maana ya ukaribu wa kila siku na Mungu; "uwazi wa kujifikilia binafsi." | 1. | Kuwa na uhakika unaokua kwamba Mungu ni mpendwa wangu baba wa mbinguni (1Yoh 4:16) |
| Kuwa na mahangaiko mengi juu ya "mahitaji wanayohisi;" marafiki, fedha, n.k.; "niko peke yangu na hakuna anayejali." | 2. | Kumtumaini baba na kuwa na ujasiri unaokua katika ulinzi wake; huru kutokana na wasiwasi. |
| Kuishi kwa mafanikio/msingi wa kushindwa; lazima "uonekane vizuri kwa gharama yoyote; inayotokana na –utendaji. | 3. | Kujifunza kuishi katika uhusiano wa -kujifahamu kwa kila siku na Mungu; bila hofu. |

| YATIMA | | WANA |
|---|---|---|
| KUISHI KWA "KUJARIBU SANA."<br>YESU "MSAADA" WA MWILI<br>*Yoh 14:18 "Sitawaacha kama yatima"* | | KUISHI KWA IMANI.<br>KRISTO MAISHA YETU! Gal 2:20<br>*Rum 8:15 "Atupa roho ya uwana"* |
| Kujisikia kulaumiwa, hatia na kutofaa mbele za Mungu na wengine. | 4. | Kujisikia unapendwa, umesamehewa na kukubaliwa kwa ujumla kwa sababu uzuri wa Kristo unanifunika. |
| Kuwa na "imani kidogo" hofu nyingi, hakuna uwezo wa kumtumaini Mungu. "Ninatakiwa kusawazisha." | 5. | Kutembea kwa kila siku kwa matumaini ndani ya mpango mtakatifu wa Mungu katika maisha yangu kama mpendwa, mwenye hekima na mipango bora. |
| Kulemewa kwa kufikiri wajibu usio na mwisho, kujaribu sana kuridhisha, kuteketezwa. | 6. | Maombi ni kitu cha kwanza kukimbilia; "Ninakwenda kumuuliza baba yangu kwanza!" Baba (papa), Baba! |
| Kumwasi Mungu na wengine; mara nyingi baridi kiroho na vigumu kuchochewa. | 7. | Uwezo wa kuwa mtiifu; moyo (aliyevunjika na majuto) laini (Zab 51:17). |
| Anayejitetea; asiyetaka kusikiliza; mugumu anaposhitakiwa kujitakia haki- binafsi (kutoa mashitaka yanayoonekana kweli) | 8. | Aliyewazi kwenye upinzani, kwa kuwa ninafahamu kuwa ninasimama katika ukamilifu wa Kristo, siyo wangu; ninaweza kuangalia nia zangu za ndani. |
| Lazima kila mara awe sawa, salama, kutunzwa, asiyekubali kushindwa; kujitetea; asiyestahimili upinzani; anayestahimili sifa tu. | 9. | Kuweza kuchukua tahadhari—hata kushindwa. Kwa kuwa haki iko ndani ya Kristo, sihitaji kitu kujigamba juu yake, kulinda au kujitetea. |
| Mwenye-ujasiri lakini aliyekata tamaa, aliyeshindwa na asiye na nguvu za Roho. | 10. | Ujasiri-wa Kristo na kutiwa moyo kwa sababu ya Roho anayefanya kazi ndani yangu. |
| "Nitawaonyesha—wewe tazama moshi wangu tu!" "Waliposhindwa wengine." (nguvu zitaweza). | 11. | "Nayaweza yote katika Kristo anitiaye nguvu. |

| YATIMA | | WANA |
|---|---|---|
| KUISHI KWA "KUJARIBU SANA."<br>YESU "MSAADA" WA MWILI<br>*Yoh 14:18 "Sitawaacha kama yatima"* | | KUISHI KWA IMANI.<br>KRISTO MAISHA YETU! Gal 2:20<br>*Rum 8:15 "Atupa roho ya uwana"* |
| Juhudi binafsi; kutegemea vipawa na uwezo kuingia katika maisha na huduma. | 12. | Kujiamini kidogo mwenyewe na zaidi katika Roho Mtakatifu (na ufahamu binafsi- wa kumtegemea kila siku). |
| Kulalamika na kutoshukuru Mungu na wengine; lazima uangushe wengine chini; kuonyesha uchungu, roho ya upinzani. | 13. | Kumtegemea Roho Mtakatifu kuongoza ulimi wake kuutumia katika kutukuza, kuadilisha, na kutoa shukurani na kutia moyo (Efe 4:29). |
| Mtaalamu wa kuonyesha makosa; mara nyingi asiyetosheka na kitu fulani. | 14. | Asiye kipofu kufanya vibaya lakini anyechagua kuzingatia kilicho kizuri na cha kupendeza (Plp 4:8). |
| Maneno ya upuuzi (kukiri dhambi za watu wengine); kutaka kuwapinga wengine kujisikia thabiti; mjasiri wa kuchambua udhaifu wa wengine; aliye na kipawa cha "utambuzi." | 15. | Kuwa huru kuungama makosa kwa wengine na anayependa kupima mafanikio yao; ambaye mara zote si lazima awe sawa; anatafuta mara nyingi kuwa nina makosa; mwenye utayari wa kukua. |

| YATIMA | | WANA |
|---|---|---|
| KUISHI KWA "KUJARIBU SANA."<br>YESU "MSAADA" WA MWILI<br>*Yoh 14:18 "Sitawaacha kama yatima"* | | KUISHI KWA IMANI.<br>KRISTO MAISHA YETU! Gal 2:20<br>*Rum 8:15 "Atupa roho ya uwana"* |
| Mara kwa mara anayejilinganisha na wengine, anayeongoza kwa kiburi au udhaifu (kutegemeana na jinsi gani wengine wanaona vizuri au vibaya). | 16. | Anayesimama kwa ujasiri katika Kristo; kufaa kwa binafsi-kunatoka katika damu ya Yesu kristo na utakatifu, siyo katika mhimili uliotengenezwa na mwanadamu. |
| Asiye na nguvu ya kushinda mwili; hakuna ushindi hasa wa moyo juu ya "dhambi ya mnyama" hata hivyo hana hisia ya "kuwa mwenye dhambi mkubwa." | 17. | Anayetulia ndani ya Yesu, na anayeona zaidi na zaidi ushindi dhidi ya mwili (Rum 8:1-9)., bado anayejiona kama "mwenye dhambi mkubwa." |
| Karibu asiye mwombaji, maombi ni "kimbilio la mwisho;" anaomba mara nyingi mbele za watu, mara chache akiwa peke yake. | 18. | Maombi ni sehemu ya maana katika siku, asiyefungwa na kawaida tu "mda wa ukimya;" Kuongea na baba ni furaha (1The 5:16-18). |
| Ahadi za Biblia za nguvu za kiroho na amani kuzidhihaki: "Nini kimetokea kwa amani yako yote?" (Gal 4:15). | 19. | Ahadi za Mungu za nguvu na furaha zinaanza kujieleza zenyewe (Rum 15:13). |
| Anahitaji kujigamba; lazima kila wakati kuonyesha yale aliyokamilisha kuogopa kwamba mtu mwingine anaweza kuyaona. | 20. | Anayejua kuwa Yesu ni kichwa cha mazungumzo yake; anayejigamba katika Bwana na katika udhaifu wake (2Kor 12:9-10). |
| Kujenga kwa kutokujitambua "kumbukumbu" ya kazi ambazo zinahitaji kuonekana na kujitetea. | 21. | Haki ya Kristo ndiyo pekee "kumbukumbu" zinazosimama kamilifu ndani yake (1Kor 1:28ff). |
| Kujijali-mwenyewe: "kama wangeweza kuona vitu jinsi ninavyotaka!" Kuhitaji sana kutawala hali na wengine. | 22. | Kuwa anayetawaliwa-na Kristo; kuhudumu katika nguvu za Roho Mtakatifu, siyo katika uwezo binafgsi "mwili uliokombolewa." |
| Kitu kingine kuliko Yesu kinaweza kutoshereza; "miungu" katika maisha (mali, cheo, haja) inatoa hisia ya kufaa na haki. | 23. | Kristo ni nyama na kinywaji; Mungu anatoshereza roho. "…na dunia haina ninachohitaji zaidi yako" (zab 73:25). |
| Hitaji dogo la kushirikisha injili (kwa kuwa ukristo wake ni wa ovyo) anaposhirikisha, anaonekana kuvutiwa na hisia ya wajibu na kazi na siyo upendo | 24. | Haja ya kuona waliopotea wanapata kumjua Yesu, kushirikisha injili wengine, *hata anapokuwa nje ya msukumo wa utaratibu wa kanisa.* "..upendo wa Kristo unatuteka" (2Kor 5:14). |

# Maombi—Azimio la Mafunzo 4

**Kongamano la Maombi:** Kuabudu na Kutafakari

Mda huu wa kongamano la maombi siyo mda wa kutoa maelezo lakini kuwaongoza wafunzwa kwenye kipindi cha maombi. Utahitaji kusoma Zaburi 95 kabla ya mda na kutambua mgawanyo uliotolewa katika somo.Mda wa maombi haya na kuabudu unatakiwa utoe nafasi kwa kila mfunzwa kutafakari kwenye yaliyomo katika semina na kwa unyenyekevu kutafuta mwelekezo wa Mungu wa kwa jinsi gani itabadilisha maisha yake na huduma.

Zaburi hii inatuongoza katika hatua tatu, kama zilivyoonyeshwa katika jedwali chini:

| Zaburi 95 | |
|---|---|
| 1. Mwimbie Bwana | vv. 1-5 |

| | |
|---|---|
| 2. Piga magoti mbele za Bwana | vv. 6-7 |
| 3. Msikilize Bwana | vv. 8-11 |

**I.** Mshereheke Bwana (Zaburi **95:1-5)**

Njono tumwimbie Bwana kwa furaha

- Imba nyimbo za furaha

Piga kelele kwenye milima ya wokovu wetu

- Soma kwa pamoja kwa sauti kubwa kutoka zaburi ya ukombozi: **Zaburi 18:1-3, 30-36**

Njoni mbele zake kwa shukurani

Muwe na mda wa kutoa ushuhuda, hasa kumshukuru Mungu kwa anachokifanya katika maombi ya utatu na maeneo mengine ya upandaji kanisa

Mwinue Bwana kwa mziki na wimbo

Muwe na mda mwingine wa kumwimbia Bwana sifa

Soma pamoja mstari wa 3-5 Zab 95; mshukuru kwa ukuu wake wa kutawala anga lote

II. Mwabudu Bwana (Zaburi 95: 6-7)

Inama chini...Piga Magoti Mbele za Bwana Muumbaji Wetu

Watie moyo wafunzwa kuomba katika roho ya utu. Kama wako huru kufanya hivyo, piga magoti.

Ni Mungu Wetu...Ni watu wa Malisho Yake

Mtambue kama mchungaji wako. Mtukuze kwa ulinzi juu yako

III. Sikia sauti Yake **(Zaburi 95: 8-11**)

Usifanye Moyo Wako Kuwa Mugumu

Ungama kila dhambi inayojulikana katika maisha yako. Soma 1Yohana 1:9.

Chukua mda kumsikiliza Bwana. Muulize kukuonyesha kama kuna maeneno ambayo unahitaji kuachilia mfumo wa zamani, tabia, au njia za upandaji kanisa ambazo hazionekani tena kuwa za kibiblia kutokana na mistari iliyosomwa katika semina hii. Bishana na Mungu juu ya kitu gani uendelee nacho na kitu gani unahitaji kubadilika katika maisha yako na huduma.

Soma Waebrania 3:7-19. Mstari wa 13 unasema kutiana moyo kila siku. Gawanyika katika jozi. Ombeaneni maombi ya kutiana moyo.

# UONGOZI—Azimio la Mafunzo 1

## Kanuni za Kibiblia za Uongozi

### I. Tafsiri ya Uongozi

SHUGHULI ZA BINAFSI: Chukua mda kutafsiri neno “uongozi” katika maneno machache iwezekanavyo. Shirikisha tafsiri yako kwa wengine.

"Uongozi ni mguso, uwezo wa mtu mmoja kuwagusa wengine” Uongozi wa Kiroho na Sanders Uk. 31).

" Uongozi ni nguvu ya utaratibu ambao mwanaume au mwanamke alipewa uwezo-na Mungu wa kutawala watu wa Mungu kwenye kusudi lake katika kundi hilo.” (Clinton, making of a Leader, 14; cf. p. 127).

Linganisha tafsiri yako ya uongozi na hiyo ya Sanders na Clinton.

Tafsir ya neno moja kwa uongozi inaweza kuwa hiyo ya uongozi wa "mguso."

Ni nini muonekano wa kutafsiri uongozi kama "mguso?" Ni nani viongozi katika kanisa lako au huduma wenye tafsiri hii kichwani?

**II. kanuni za Uongozi wa Kibiblia**

Ulimwengu wa biashara ya kidunia mara nyingi unajitwalia kwamba "viongozi hawawezi kuwaamini wasaidizi wao kufanya ambayo wangetakiwa kufanya, "na kwamba "kama unawaamini watu zaidi, watachulia faida kwako." Viongozi wa kidunia wanaweza kuendelea kuamini kwamba watu watafanya kile unachowataka kufanya wanapokuwa tu wanavutiwa na malipo au wakitishiwa kwa kuadhibiwa. Matokeo ya kudhaniwa huku, viongozi wa kidunia mara nyingi wanajitwalia madaraka kwa misingi hasa ya ama nafasi wanayoshikilia, ama kwa nguvu ya hadhi.

Ukifikiria uhusiano wa mabwana na watumwa katika siku za Paulo, Ni nini Efe 6:9 inatuambia kuhusu vitisho?

Jinsi gani umejisikia kuathiriwa na viongozi waliofanya kufuatana na mawazo hapo juu?

A. **Mamlaka ya Kuongoza Yanatoka kwa Mungu**-Ni nini mistari ifuatayo inatufundisha kuhusu mamlaka?

Mamlaka ya haki ya Mungu – serikali ya raia (**Ru m 13:1-7, 1Pet 2:13-17),** familia **(Efe 5:22-23, 6:1-4**), na kanisa (Ebr **13:17).**

Kielelezo cha Yesu (**Yn 8:28-29).**

Viongozi wa kikristo wanachaguliwa na Mungu (**Yn 15:16).**

B. Utumishi wa kinyenyekevu Unatakiwa Kuwa na Tabia ya Viongozi Wakristo

Ni nini msitari hii inatuambia ni kinyume na utumishi? Jibu: kiburi. Mungu anachukia kiburi (**Mit 6:16-17**). Kielelezo cha Yesu (Flp **2:1-8; Yn 13:15).**

C. Uongozi wa Kikristo unahitaji kuendelezwa kupitia **Mafunzo ya Uangalifu na Mazoezi**

Kielelezo 1.1 Tofauti za Kiulimwengu dhidi ya Uongozi wa Kikristo

| Uongozi wa Kidunia | Uongozi wa Kikristo |
|---|---|
| Ujasiri wa Binafsi | Ujasiri ndani ya Mungu |
| Kumwelewa mtu | Kumwelewa Mungu na mtu |
| Kufanya maamzi yake mwenyewe | Kutafuta kupata mapenzi ya Mungu |
| Tamaa ya madaraka | Mtumishi |
| Kuanzisha njia zake mwenyewe | Kutafuta na kufata njia za Mungu |
| Kufurahia kuwaamrisha wengine | Anayefurahia kumpendeza Mungu |
| Anayevutiwa na fikira zake mwenyewe | Anayevutiwa na upendo kwa Mungu na mtu |
| Anayejitegemea | Anayemtegemea-Mungu |

Watu wanapoongelea "kiongozi wa asili" je mara nyingi wanazingatia kwenye huo "uongozi wa kidunia" au "uongozi wa Kikristo?"

**D. BibliaInaelezea Utofauti wa Mitindo ya Uongozi**

**Waefeso 4:11-12** inaelezea wajibu kadhaa wa uongozi ambao ulikuwa umeonyeshwa kwenye Kanisa la Agano Jipya. Ingawa ni tofauti kutoka kwa kila mmoja, kila mmoja unafanya kazi "kuandaa watu wa Mungu kwa kazi ya huduma" au kwa maneno mengine, kuwaongoza kwenye huduma.

Kielelezo 1.2 Kazi za Uongozi wa Agano Jipya

| Wito | Fikira | Kazi |
|---|---|---|
| Mtume | Maono | Mwanzilishi |
| Nabii | Dhambi | Kuhubiri |
| Mwinjilisti | Wokovu | Kufikia watu nje |
| Mchungaji | Kulisha Neno | Kufikia watu wa ndani |
| Mwalimu | Ukweli | Kuelekeza |
| | | |

Weka orodha ya shughuli kwenye 'Mzunguko wa Upandaji Kanisa" (Mwongozo wa Kwanza, somo la maono la 3) ubaoni. Mfanye kila mjumbe pekee kuangalia kwa dakika kadhaa kwenye "Mzunguko wa Upandaji Kanisa." Kisha, kwenye vikundi vidogo (kama ni darasa kubwa), jadili mitindo ya uongozi ambayo ni ya lazima kwa kila ngazi ya mzunguko.

**E.** Kazi ya Msingi ya **Uongozi** wa Kanisa **ni Kuandaa**

Ni nini **Waefeso 4:11-12** kwenye jukumu la msingi la kiongozi wa kanisa?

Kelelezo 1.3 Viongozi Waelekevu na Wawezeshaji

| KIONGOZI MWELEKEZAJI | KIONGOZI MWEZESHAJI |
|---|---|
| Ana asili ya kazi: Kufanya kazi kufanyika" | Ana asili ya watu: Anafanya watu kuhusika" |
| Mtendaji | Mwakilishi |

| | |
|---|---|
| Lengo- “Kufanya kazi ya huduma” | Lengo- “Kuwaandaa wengine kuhudumu” |
| Anayefanyia mazoezi cheo | Mwandaaji, Mwezeshaji, Mfundishaji |

Je “Uongozi wa uelekezaji” au “uongozi wa uwezeshaji” unafaa zaidi wa Ukristo?

Jinsi gani watu wanakuwa viongozi katika utamaduni wako?

Kwa nini ni muhimu kwamba viongozi wote wawe wafuasi wazuri?

Kwa nini kuelewa kwamba “mamlaka ya kuongoza yanatoka kwa Mungu” kunabadilisha mtazamo wako kwenye uongozi wako?

Ni nafasi zipi zinachukuliwa kujinufaisha wakati muumini mpya mwenye uwezo wa uongozi kiasili anapopewa uongozi kanisani?

Ni upi kati ya mitindo ya uongozi iliyoonyeshwa katika kielelezo 1.2 ni ya kawaida zaidi kwako?

Ni kwa njia zipi dhana hizi za kibiblia za uongozi zinatofautiana na kanuni za kidunia za uongozi?

UONGOZI
*ZIADA*
IA

# Mchanganuo wa Uongozi

## KANUNI ZILIZOTUMIKA

**Karatasi ya Maswali ya Mazoezi: Jibu maswali yanayohusiana na mchanganuo wa utafiti chini**:

1. Yuri amekuwa akiongoza mradi wa kupanda kanisa huko Yekatarinburg. Misha na Marina wamekuwa wajumbe wa timu kwa miezi mitatu. Hivi karibuni Misha na Mrina wameanza kujisikia hali ya kuchanganyikiwa kutokana na huduma. Wana baadhi ya hisia nzuri za uinjilisti lakini hawajisikii uhuru hata wa kuweza kuelezea hisia zao. Kiongozi wao, Yuri, anaonekana kutokuwa tayari kuwasikiliza ushauri wao. Badala yake anawaambia wanachotakiwa kufanya na jinsi gani wafanye. Matokeo yake, Misha na Marina wanafikiria kuiacha huduma na kuanzisha ya kwao**. Jinsi gani unaweza kutathimini uongozi wa Yuri**

2. Gennadi profesa anayejulikana wa chuo kikuu aliyempata Kristo wakati jirani yake Nic alipompatia Biblia kusoma. Alianza kuwa anahudhuria kanisa na Nic alikuwa amevutiwa na mafunzo ya Biblia ya watu wazima wanaokutana kila jumatano usiku. Katika wiki chache za kwanza, mtu mmoja alishauri kwamba Gennadi, mwalimu mzuri, aongoze mafunzo. Uongozi wa Gennadi ulikuwa ukileta wageni wengi kwenye kikundi kwa kuwa anajulikana na hasa kwa ualimu wake mzuri pia. **Je Gennadi aongoze mfunzo ya kikundi**?

3. Slava anaongoza timu ya familia tatu katika kupanda kanisa huko Rostov. Slava anatoa mahubiri mazuri zaidi wakati wa ibada kila jumapili na anaongoza kikundi kiini katikati ya wiki, ambacho kimekua kwa karibu ya wajumbe waaminifu 20. Kila mmoja anapenda uwezo wa Slava wa kufundisha na kuhubiri neno la Mungu, vilevile na uwezo wake wa kupanga shughuli. Kwa jinsi hiyo, Slava anaanza kujisikia kuchoka kutokana na mzigo wa kazi. Slava anamuuliza mwanakikundi Anatoli kuanza kikundi kingine kidogo na wachache kutoka katika kikundi cha Slava. Lakini, kuna haja ndogo ambayo inamkatisha tamaa Anatoli. **Tathimini jinsi Slava alivyochulia kuhamisha madaraka kwa Anatoli**

4. Kanisa mpya katika eneo la Smolensk linakua kwa kiwango cha haraka. Wengi wanahesabia ukuaji huu kwa uongozi bora wa Victor na Luba walioutoa. Walianza kanisa baada ya Victor kutoka Moscow chuo kikuu. Wengi wa hao wanaohudhuria ni waumini wapya wasiokuwa na

uzoefu wa nyuma wa kanisa hata kidogo. Victor anafanya karibu mahubiri yote na Luba anapanga taratibu za madarasa ya jumapili. Kwa kuwa wamekua, Victor anaanza kutafuta viongozi wengine kutoka nje wa kumsaidia katika kazi za kanisa. Lakini hakuna hata mmoja anyeonekana kufaa kuongoza. Anajisikia angalau angepata vijana watatu ambao wanaweza kufundishwa kwa ajili ya uongozi wa kanisa. Victor alipata msaada wa kusomesha wawili wao kuingia chuo kikuu cha Moscow. Wanaondoka karibu mwezi wa nane kuanza kozi ya miaka 3. **Jinsi gani unaweza kutathimini njia hii ya maendeleo ya uongozi huu**

5. Boris anaisha katika mji mdogo wa kusini mwa Urusi ambao hauna makanisa ya kiinjili. Boris hivi karibuni amegundua waumini kadhaa katika kijiji chake wanaosafiri sehemu tofauti kuhudhuria kanisa-wengine umbali kama wa km 30. Chini ya uongozi wa Boris, waumini wamejipanga katika kanisa jipya. Waumini wanapokutana, wote wanahamasa ya kanisa jipya la mtaa na kila mmoja kwa shauku anashirikisha hisia juu ya jinsi kanisa linatakiwa kupangwa kutokana na uzoefu wao wa makanisa yao ya mwanzo. Lakini Boris anaweka wazi kwamba atakuwa mchungaji na kwamba watu wanatakiwa kusahahu juu ya mapokeo yoyote au walivyofanya katika makanisa waliyotoka, kwa sababu ni mkuu kama mchungaji wa kanisa hilo jipya. **Unafikiri ni nini itakuwa matokeo ya njia ya Boris?**

6. Keril amepanda makanisa matatu katika miji tofauti ya magharibi ya Urusi. Keril ni mpanda kanisa wa kawaida. Ana juhudi na mchangamfu, mwenye kipawa kama mwinjilisti. Anapiga gita na kuimba na anaweza kuburudisha umati kwa masaa. Anapenda kuanzisha vitu na kisha kuhamia kingine tena. Makanisa anayoanzisha yanaonekana kufanana na hadhi yake. Yanaonekana kuvutia mwanzoni lakini mara hufifia kitu kingine cha kuvutia kinapotokea. Keril anashikilia kauli kwamba hii ndiyo hadhi yake na kwamba hakuna kitu hasa anchoweza kufanya kuibadili. Anajua kuwa Mungu anamtumia bila kujali hilo. **Jinsi gani utatathimini uongozi wa Keril?**

7. Zhenya amekuwa anfanya kazi kwa juhudi katika kupanda kwake kanisa kwa miaka kadhaa. Kanisa linafanya vizuri sana. Limekua karibu kufikia 200 kwa miaka mitatu iliyopita. Mke wake na watoto wanne wakati mwingine wanamaliza siku kadhaa bila kumuona kwa sababu anaondoka asubuhi mapema na kurudi usiku sana. Zhenya hapendi kuishi hivi lakini watu wake ni wahitaji sana. Wengi wao ni wagonjwa na wanahitaji kutembelewa, jiko la mchuzi wa walala nje linahitaji kuangaliwa kwa karibu. Zhenya anajua kama akiacha kufanya yote anayoyafanya, huduma itayumba, watu hawataokoka na kanisa halitakua zaidi tena. **Unafikiri Zhenye ni kiongozi mzuri? Kwa nini na kwa nini siyo?**

# UONGOZI—Azimio la Mafunzo 2

## Sura ya Kiongozi

**I. Tunza Tabia Inayofanana na ya Yesu**

Ni nini baadhi ya vitu vya Tabia Inayofanana na ya Yesu?

**II. Fanya kazi Vema na Timu**

Una timu ya kufanya nayo kazi? Kwa nini na Kwa nini siyo?
Wewe au timu yako mna malengo ya huduma yenu?

**III. Endeleza kujaliwa Vipawa na Uwezo kwa Wengine**

Kama mkazo wetu ni kutumia vipawa vyetu, ni wito gani wa mtu tunaonekana kuukosa? (**2 Tim. 2:2)**

IV. Jua Jinsi ya Kugawa Majukumu

Kwa nini kiongozi agawe majukumu?
Ni kazi gani maalumu unayofanya ambayo unatakiwa uigawe kwa wengine?

**V. Weka Malengo, Maazimio na Makusudio na Fanya Kazi Kulekea Kwayo**

Jinsi gani kiongozi anaweza kuwafanya wengine kuhusika katika uwekaji malengo? **(Mit . 20:18, Lk. 14:31)**

Kutoka katika orodha ya tabia za kiongozi wa kikristo chini, ni tabia zipi mbili unaamini uko imara zaidi kwazo na zipi mbili ambazo uko dhaifu zaidi kwazo? Elezea.

**Kufanana na Yesu mwezeshaji, mfundishaji mgawaji, mpangaji, muonaji, mvumilivu, mwinjilisti**

**VI.** Jinsi gani **unaweza "Kubainisha Maono kwa namna Kwamba Yanavuta Wengine?"**

**VII. Uwe Mvumilivi na Shinda Vizuizi**

<u>Ina maana gani kuwa mtendaji na kwa nini mpanda kanisa anatakiwa kuwa na tabia hii ?</u>

**VIII. Ongoza katika Uinjilisti**

Ni nini ni muhimu zaidi ufundishaji wa viongozi au uinjilisti wenye juhudi?

Ni kati ya tabia ipi hapo juu (sehemu ya V) umejaliwa kama mpanda kanisa? Ni kwa njia zipi unapungukiwa?

| |
|---|
| Unaposoma habari katika Ziada 2A, uliza darasa kugundua tabia za Kiongozi. |

Ziada 2A Kiongozi

Kiongozi alikuwa angalau na kazi ya kufanya. Misheni yake ilikuwa kuubadilisha ulimwengu. Mabadiliko ambayo kiongozi huyo alipanda hayakuwa tu mapambo, au kitu cha mda tu. Yalihusu kwa ujumla falsafa mpya ya maisha yanayotokana na utamaduni mpya kuwafikia kila kabila na taifa. Kusema machache, kiongoizi alikuwa na kazi ngumu zaidi mbele yake. Viongozi wengine mashuhuri walijaribu vitu kwa ufahari kidogo na kushindwa. Kusema kwa kibinadamu, kiongozi alikuwa peke yake kwenye misheni hii. Hakuna mtu mwingine tena aliyekuwa amejitoa kwa hilo, hata mmoja kuielewa. Ni kwa jinsi gani angeweza kukamilisha kazi yake? Ni jinsi gani angeweza kufikisha ujumbe wake nje? Ni kwa jinsi gani angeweza kuwavutia wengine kuishi kufuatana na hiyo?

Uchunguzi wa njia za kiongozi una mengi ya kushangaza. Kiongozi hakufanya mengi kati ya ambayo pengine tunatarajia. Hakutafuta ofisi za uma au kukusanya jeshi. Hakufungua wizara yoyote, au kuendesha semina za kawaida kufundisha katika falsafa yake mpya; hakuwavuta mbali wafuasi wake kwa kipindi kilichopangwa cha kiakili. Hakukabidhi maandishi kwenye uchapishaji kuzalisha vitabu na magazeti yanazolenga mpango wake. Badala yake, kiongozi alianza kwa kujikusanya kikundi kidogo cha wafuasi (Mt 10:2-4). Badala ya kukazania umati, alitumia mda wa miaka mitatu maalumu kuwafundisha watu hawa kwa njia yake inayobadilisha katika maisha kwa tumaini kwamba wangemsaidia kubadilisha umati.

Na watu 12 tu, hii ilionekana kama mwanzo mdogo wa kukatisha tamaa. Hata hivyo, aliishi kwa imani yake na kuwapenda hawa 12 kana kwamba ilikuwa sehemu ya familia yake. Waliishi pamoja, kula, kupumzika, kufanya kazi na kujilaza bila kizuizi wala mpaka wowote. Katika yote haya, kiongozi anaweka fikira zake katika matendo kwa kuishi kwa kuyaonyesha kwa wafuasi wake. Walisafiri pamoja kutoka kijiji hadi kijiji mahali alipozungumza na wengine, kukutana na mahitaji ya aina zote. Kiongozi kawaida alihubiri kwa makutano makubwa (Mk 4:1). Mahubiri yake hayakuwa ya kufafanua; alitumia vielelezo vingi kutoka katika maisha kama walivyokuwa wanaishi katika nchi hiyo na mda huo. Angeweza mara nyingi kurudi na wanafunzi wake peke yake kijijini alipofanya mahubiri yake kuwa ya maana kwa undani ikifuatiwa na majadiliano (Mk 4:34).

Wafuasi walikuwa wamejitoa na kuonekana wenye bidii ya kujifunza, lakini walionyesha ahadi kidogo. Wengi wao walikuwa wanakijiji wa nyuma, wanaoweza kusoma kidogo,; mmoja amekuwa mkusanya kodi, cheo kilicho dharauliwa na watu wa kawaida; wachache walikuwa katika biashara ya uvuvi. Kwa zaidi walikuwa watu wa kawaida, siyo 'wapasuaji' aina ambayo miongoni mwao mtu asingetarajia mambo makubwa. Hakuna mmojawao aliyemiliki maelezo kama karisma inayohitajika na viongozi wa harakati . Na ingawa kiongozi alikuwa na ujumbe wa kiroho, hakuna mmoja wao aliyemchukua aliyekuwa kiongozi wa kidini. Bila kujali haya yote ya kutokuwa na sifa, hawa wafuasi wasiotarajiwa walikuwa ndio

aliochagua mwenyewe kusimama peke yao mstari wa mbele wa harakati kuu. Kiongozi alidhani kwamba sifa za watu hawa ingekuwa kwamba wamekuwa pamoja naye.

Kiongozi alikuwa na utu usio wa kawaida. Hakujali kwenye maneno ya uchungu yaliyokuwa wazi juu ya mji wake. Alikuwa ameridhika kujulikana kama kijana wa kwenye mji mdogo na mtoto wa selemala. Hakutafuta sifa wala heshima, lakini alitafuta kuwawezesha wengine na kukaa nje kwenye nuru yake nyeupe. Baadhi walidhani kwamba angeweza kuwa na matokeo makubwa kama uongozi wake ungekuwa zaidi wa kawaida, kama angelitumia mfumo uliokuwepo. Lakini kiongozi alikataa hadhi ya kawaida. Alikataa utawala wa moja kwa moja wa ufalme wa duniani hata ulipotolewa kwake (Mt 4:8-10). Badala ya kufanya kuelekea mageuzi ya mfumo uliokuwepo, kiongozi alijitahidi kuwasha harakati zote mpya.

Kwa kutazama yaliyopita, tunaweza kushangaa juu ya ujasiri wa kiongozi, Kufanya urafiki na wenye dhambi (Mk 2:15-17). Mahubiri yake na mafundisho yalikanyaga juu ya miguu ya wengi waliokuwa katika nafasi ya kusaidia chanzo. Kwa tofauti ya wachache, kiongozi hakuonyeha ujasiri kwa viongoizi wa kidini katika siku zake. Kiwango chake kilikuwa cha juu—alihitaji yote au hakuhitaji chochote kutoka kwa watakao kuwa wafuasi wake na wengi hawakuweza kujitoa (Mt 10:37-39).

Kiongozi alitathimini tamaduni na kawaida kulingana na matokeo ya kazi yao. Kwa mfano, kwa kiongozi, "anayefanya kazi nyingi" ingeweza kuwa mtego ambao ungewazuia watu kutokana na vitu muhimu halisi (Lk 10:41-42). Kuhusu sheria za kidini, kiongozi mara zote alikuwa mwenye heshima wakati pia akiwa mtendaji, bila kuzuiliwa na barua za sheria. Aliachilia kiwango cha hasira zake zote wakati alipoona hekalu linatumiwa kwa kazi ambayo haikukusudiwa. Kiongozi alikemea mapokeo na matambiko yaliyokuwa yamewalemea watu badala yake kuwapa uhuru wa ndani, Alikuwa na fikara za mabadiliko ya ndani kulingana na 'roho ya sheria' kuliko uthibitisho wa nje kutawala kwa kanuni na taratibu. (Mt 15:7-9).

Kiongozi aliwapenda watu kwa undani; misheni yake ilihusisha utumishi-kama huduma kwa watu wengine. Pengine hii ndiyo sababu watu wengi hawamkumbuki kwanza na kuendelea kama 'kiongozi,' Kutoelewa vema uongozi kama 'daraja' 'nafasi' au 'hadhi' kunawafanya wengi kutomfikiria mtu huyo kama kiongozi. Badala yake, anakumbukwa kama mtumishi, mwalimu, mponyaji, mshauri, au cheo chochote kinachoweka wazi kwamba mtu huyu alisaidia na kuwaelekeza watu. Utu wake wa siku hadi siku ilikuwa mara kwa mara kuvutwa na mahitaji ya wengine. Mara zote alichukua mda kuongea na watu wa kawaida, kutimiza mahitaji yao kwa kuwaponya au kuwaelekeza kuelekea uhuru wa ndani. Wakati umati mkubwa ulipomjia, aliitikia kwenye haja zao na mahitaji na kwa kujali kudogo ratiba za kawaida au mahitaji yake mwenyewe. Hakujali usumbufu wa watoto (Mt 19:13-15). Alishughulikia kineema namna zote za usumbufu usio wa kawaida, hata paa lilipobomolewa juu ya kichwa chake. Hakuweza kutekwa katika mgawanyo usio muhimu wa wanadamu. Ndivyo watu walivyokuwa muhimu sana kwake kwa hiyo alifupisha sheria kiuhusiano.

Hakuwa amependezwa sana kwa ufahamu, utajiri, au utii uliojifunga kwenye sheria, kama alivyokuwa kwa imani. Kwa hakika, kama ulitaka kumfurahisha kiongozi, kuiweza imani ilionekana kama njia nzuri ya kuweza hilo. Imani pengine kilikuwa ndio kipimo cha kupimia wengine. Aliendelea kusisitiza wengine kuamini na alikuwa karibu azimie kwa kuonyesha mlipuko wa nje wa kukumbatia alipopata watu wa imani. Wakati fukara wa jamii alipoonyesha imani ndani yake, hata katika njia ya usumbufu, kiongozi alimpokea (Lk 7:36-38). Ingawa yeye mwenyewe alikuwa na uwezo wa asili, katika hatua mabalimbali alieleza kuwa alikuwa hasa anazuiliwa na kukosa kwa imani kwa watu wengine.

Karibu na mwisho wa kazi yake na wafuasi , ilionekana kana kwamba kulikuwa na kushindwa kwingi. Wafuasi wake mara nyingi hawakuweza kuelewa alichofundisha. Watu wote kwa ujumla walikuwa wamechanganyikiwa juu ya alikuwa nani. Wafuasi wake walikuwa wamejitoa kwake alipokuwa wa watu wengi lakini hawakusimama naye alipowahitaji zaidi. Hata mmoja wa wafuasi aliyekuwa karibu alikataa kuwa alimjua kiongozi wakati muhimu sana (Mt 26:69-74). Mfuasi mwingine alimsaliti kwa ajili ya vipande vya fedha vya kwanza kuvipata, lakini mara baada tu akajinyonga. Hatimaye kuanzishwa kuligeuziwa kwa kiongozi. Alikamatwa, akajaribiwa, akahukumiwa na kuwekwa katika kifo kama adui wa watu. Zaidi kwa kuubadilisha ulimwengu.

Kulikuwa hakuna shaka kwamba wafuasi wake walishangazwa na kuvunjwa moyo kwa kuondoka kwa kiongozi kusikokuwa kwa kawaida na kwa ghafla. Hawakujisikia kuwa tayari kwa kiongozi kuondoka. Ilionekana kana kwamba ndiyo alikuwa anaanza. Alikuwa ameshakuwa na matokeo ya ajabu, lakini ulimwengu, wakiwa wamemkataa kiongozi, walikuwa mbali na kubadilishwa. Kwa sababu kazi ilikuwa haijamalizika, kiongozi, katika kuondoka kwake, aliwapa wafuasi wake maagizo kuendeleza kama alivyofanya (Mt 28:18=20). Alikuwa kwa kikamilifu amewaandaa ili kwamba kama watatumia walichojifunza kutoka kwake, wangeweza kuwa na matokeo (hata makubwa zaidi) ya yake.

Na kuongoza wafuasi hawa kulifanyika. Waliibuka kama watu wa imani kubwa na maono ya mabadiliko aliyotaka kiongozi. Kwa jitihada za ajabu na shauku waliendeleza misheni. Walipokuwa wakifanya hivyo walifanya kitu kimoja wazi—kiongozi hakuondoka hasa. Ilionekana hivyo kwa kitambo kidogo tu. Kwa hakika, uwepo wake wa kiroho ulikuwa ndio ufunguo wa mabadiliko aliyotaka. Yeye, kiongozi, alikuwa nao walipopanga kueneza ujumbe wake kwa kila kabila na taifa. Uwepo wake ulikuwa ndio ujumbe wao na mvuto wa Mungu!
Na kuongoza wafuasi hawa kulifanyika. Waliibuka kama watu wa imani kubwa na maono ya mabadiliko aliyotaka kiongozi. Kwa jitihada za ajabu na shauku waliendeleza misheni. Walipokuwa wakifanya hivyo walifanya kitu kimoja wazi—kiongozi hakuondoka hasa. Ilionekana hivyo kwa kitambo kidogo tu. Kwa hakika, uwepo wake wa kiroho ulikuwa ndio ufunguo wa mabadiliko aliyotaka. Yeye, kiongozi, alikuwa nao walipopanga kueneza ujumbe wake kwa kila kabila na taifa. Uwepo wake ulikuwa ndio ujumbe wao na mvuto wa Mungu!

Wafuasi hawa, kwa kuonyesha wenyewe kuwa wafuasi wazuri baada ya yote, hawakuacha umaana kutoka katika mfano ambao kiongozi alikuwa ameanzisha. Waliendeleza majadiliano yenye nguvu na watu wa kawaida katika sehemu za masoko, vile vile na majumbani). Wafuasi wake waliishi kulingana na ujmbe na kuwapenda wengine kwa undani, wakati wakiendelea kuwakusanya wafuasi wengine kufanya wanayofanya. Watu walipokubali ujmbe, ushirika wa mtaa ulishangilia uwepo wa kiongozi kuanzishwa. Kama kiongozi, wafuasi hawa na washirika wao wa mitaa walikuwa na matokeo ya ajabu kiasi kwamba serikali na dini zilitishika vibaya sana—mpaka kwenye hatua ya kufanya malipizi.
Siyo vizazi vingine baadaye, wafuasi waliendeleza zaidi njia ya"kutatanisha" ya kumfata kiongozi. Mara nyingine kwa kudhani "kufanya kama Waroma wanavyofanya' kuliko kufanya kama kiongozi alivyofanya, walitumia utawala wa mtindo wa kidunia unavyofanya. Harakati za hiari zisizo za kawaida zilizosisitiza uwepo wa kiongozi zilitoa njia kwa wizara na vipindi vigumu vya kawaida. Mashirika ya kuvutia, majengo makubwa, na vipindi vya 'ncha ya kukatia' vilikuwa badala ya sherehe za kawaida na kutangaza hisia za moyo ambazo ni utii upasao kwa kiongozi alioonyesha. Mwelekeo huu ulitoa usalama fulani na ulinzi, lakini uwepo wa kiongozi ulifunikwa na kile alichosimamia kiongozi kilikataliwa. Kwa kuanzisha na kuheshimu mifumo kwa gharama ya utendaji, matokeo halisi ya misheni yake ilipotea.

Mvuto wa kiongozi unaendelea. Hao wanaomfata kiongozi wameamriwa kufanya kazi kama alivyofanya. Kama maelezo ya azimio kwa kubadilisha ulimwengu kwa vipindi na wizara zinaonyesha ahadi kidogo kuliko ambavyo haijawahi kuwa, wafuasi wake wanatakiwa tena wakumbushwe njia ya pekee ya kiongozi. Hisia ya msingi ni rahisi kiajabu: kiongozi, anayeishi kufuatana na anachoamini, kwa undani akiwapenda wafuasi wake ambao anachangia nao njia ya maisha—huu ni uongozi kwa kiwango cha juu. Huyu ni kiongozi mkuu anayegusa maisha na kubadilisha ulimwengu.

# Vikundi Kiini—Azimio la Mafunzo 1

## Kazi na Faida za Vikundi Kiini

**I. Misingi ya Vikundi Kiini**

Kulikuwa na vikundi kama hivyo tunavyoviita vikundi kiini katika kanisa la Agano Jipya?
Ni vitu gani vinafanya vikundi kiini vya kikristo kuwa tofauti kutoka makundi mengine?
Ni tofauti gani ya msingi kati ya kikundi vidogo na kikundi kiini?

## II. kazi za Vikundi Kiini

Ni nini baadhi ya kazi za **ushirika wa** vikundi kiini vya Agano Jipya? **(Matendo 2:42, Ebr. 10:25, Matendo 20:7,11)**

**Ni baadhi ya kazi zipi zinazowezekana za vikundi kiini ambazo zinaweza kuzalisha** kutiwa moyo kwa wote, kushirikisha na urafiki katika **Kristo?**

**Ni baadhi ya kazi zipi za** kuabudu **katika vikundi kiini vya Agano Jipya? Mdo** 2:47, 1:14, 6:4, Col 4:2)

Ni baadhi ya shughuli zipi za vikundi kiini ambazo zinaweza kuzalisha **kumwinua Mungu?**

Ni baadhi ya kazi zipi za ufuasishaji za vikundi kiini vya Agano Jipya **? (Mdo 6:4, Col 4:17)**

Ni baadhi ya kazi zipi za vikundi kiini ambazo zinaweza kuzalisha **kusaidia, kufundisha na kushauri?**

Ni baadhi ya **kazi zipi za uinjilisti** za vikundi kiini vya Agano Jipya? **(Matendo 5:42, 4:20, 20:20)**

Ni baadhi ya kazi zipi zinazowezekana za vikundi kiini zinazoweza kuzalisha **kufikia nje** kwa habari njema ya Kristo?

**III. Faida za Vikundi Kiini**

Ni nini faida za vikundi kiini leo?

A. Ni nini faida zake kwa **uinjilisti** wetu?

B. Ni nini faida za vikundi kiini kwenye **uhusiano wetu na Mungu**?

Ni nini faida kwenye **ushirika wetu na mmoja kwa mwingine**?

Ni kwa jinsi gani ni ya ufanisi huduma ya "mmoja kwa mwingine"iliyofanyika katika ibada ya kanisa la mapokeo ya jumapili asubuhi ? Itakuwa na matokeo gani kwa wakristo kama matakwa haya hayakutimizwa? Wakristo wapya watakua na kukomaa kama mahitaji haya hayakutimizwa?

C. **Faida kwenye Ufuasishaji**

Ni nini unafikiri ni faida za "Ufuasishaji wa Pamoja" miongoni mwa wajumbe wote wa kikundi kiini ufuasishaji wa "njia moja"?

D. Ni nini faida za vikundi kiini kwa **Maendeleo ya Viongozi?**

E. Faida kwenye **upandaji kanisa?**

1. **Kuna mipaka yoyote katika kanisa lako ambayo inaweza kuzuia asiyeamini ambaye hajawahi kamwe kuwa kanisani kutokuja katika moja ya ibada zako? Ni kwa jinsi gani vikundi kiini vinaweza kutumika kama "daraja" kwa wasioamini?**
2. Kwa ujumla, jinsi gani vikundi kiini vinaweza kutumika kama sehemu ya kueneza kwa ufanisi kwa mkakati wa upandaji kanisa?

## UTEKELEZAJI WA AZIMIO

Tafuta rafiki wa kikristo au mtu uliyekaribu naye ambaye hajui juu ya vikundi kiini. Elezea kwake faida za njia ya vikundi kiini kwenye huduma, na muulize akupe sababu kwa nini anakubaliana au kutokubaliana na wewe. Kama inawezekana, jadili majibu yake na wafunzwa wengine wanaojifunza nyenzo hii.

# Vikundi Kiini—Azimio la Mafunzo 2

## Kanuni za Uongozi wa Kikundi Kiini

**I. Wazo la Jumla la Uongozi**

Eleleza Maisha ya Kikristo—**Ni nini wajibu wa kueleleza uongozi wa Agano Jipya?** 1 The 1:6-7; 1 Kor. 11:1

**B. Endeleza Viongozi wapya**

Je kiongozi wa kikundi kiini agawe shughuli na majukumu kwa wajumbe wote wa kikundi kiini, na siyo tu kwa kiongozi mwanafunzi? Kwa nini na Kwa nini siyo?

Ni kwa mda gani baada ya kikundi kiini kuanza kiongozi wa kikundi kiini asubiri mpaka kuja

kuchagua kiongozi mwanafunzi? Ni aina ya shughuli gani kiongozi wa kikundi kiini anazofanya na mwanafunzi kumwanadaa kuongoza kikundi chake mwenyewe?

**C. Andaa na Toa Kwenye Huduma**

Vikundi kiini vinasaidia kuandaa viongozi kwa kutoa nafasi. Ni aina ya vitu gani kiongozi mwanafunzi anaweza kujifunza kutokana na majukumu yanayofanyika katika kikundi kiini? Toa mifano.

**II. Kuongoza Mkutano wa Kikundi Kiini**

Utaratibu wa mutamo "halisi"wa kikundi kiini:

- Ushirika na kushirikishana kati ya wajumbe wa kundi.
- Kuabudu kwa maombi, kumwimbia na kumtukuza Mungu.
- Kujadili na kujifunza Biblia.
- Kisha kundi linahamia kwenye mda wa kufikiri wapi wajumbe wanajadili shughuli za binafsi na za kundi kuwafikia marafiki, majirani, na pengine kundi kubwa kwa injili. Hii inaweza kuwa ni pamoja na mda wa maombi kwa watu binafsi ambao bado hawajakaribishwa kwenye kundi.

Ni aina gani ya maandalizi yanahitajika kwa kila moja ya sura hizi za mahitaji ya mkutano wa kikundi kiini:

A. Mahali
B. Ushirika
C. Kuabudu
D. Maombi
E. Majadiliano ya Biblia
F. Kufuasa
G. Uinjilisti

Kwa nini ni muhimu kwamba kila mjumbe mpya wa kundi akabidhiwe "mzazi" wa kiroho atakayemfuasa?

**III. Usimamizi wa Kikundi Kiini**

Kwa nini kiongozi wa kikundi kiini ajisumbue kuanzisha mpango kwa ajili ya kundi kwa ujumla na kwa kila moja ya mikutano? Kwa nini tu asiruhusu kundi kuhusika "kiasili" kwenye mwelekeo wowote linaotaka?

Ni baadhi ya sababu gani kiongozi wa kikundi kiini anaandaa azimio la malengo na makusudio? Jibu: Kwa ajili ya uwajibikaji na ukuaji

Kama darasa ni kubwa, gawanyika katika kundi la karibu watano. Mkabidhi mjumbe mmoja wa kundi kusimama katika nafasi ya kiongozi wa kikundi kiini. Na mwingine ashike wajibu wa mwanafunzi. Waliobaki washike wajibu wa wajumbe wa kikundi kiini. Kundi linatakiwa kutumia "Nitabahatisha Hujui" mchezo huu wa ushirika wa kundi. Soma maelekezo yanayopatikana chini kwenye darasa. Kisha tumia baadhi ya maswali ya majadiliano, "Ni nini ulikuwa wakati wa furaha katika maisha yako? Kikundi kiini kisha kinatakiwa kuhusika kwenye mda wa maombi. Kundi linatakiwa kutathimini na kujadili mkutano wa kikundi kiini. Kama darasa ni dogo, unaweza kufanya darasa zima kufanya hili.

Nitabahatisha Hujui Hili

Kila mtu kwenye kundi anaandika kwenye karatasi tupu kitu fulani ambacho anadhani hakuna yeyote kwenye kundi anayejua kuhusu yeye mwenyewe. Kipande cha karasi kinakunjwa, na kuchanganywa vema, na kuwekewa namba kwa mfuatano. Kisha mtu anayechaguliwa anazisoma, akitaja namba kwanza. Kila mjumbe wa kundi anaanza kukusanya orodha ya watu ambaop anajisikia kana kwamba wanaoana vema na idadi ya kila muhusika. Baada ya muhusika wa mwisho kusomwa, mtu mwenye zinazooana zaidi anashinda.

VIKUNDI KIINI ZIADA

2A

# Vikundi Kiini Vivunja Barafu

"Vivunja barafu" vinachekesha, njia zisizotisha za kuwajua watu zaidi. Hizi zinatumika mara nyingi wakati wa mda wa ushirika wa kikundi kiini kipya. Baadhi ya nukuru:

Kivunja barafu lazima kifae kwa ajili ya kikundi kiini. Ni ya kitoto zaidi, watu hawatajisikia kuridhika. Kama inatisha zaidi, watu watarudi nyuma.

Weka wazi kwamba kila mmoja anatarajiwa kushiriki.

Baadhi ya vivunja barafu vinaweza kutumika mara nyingi.

Uwe na hali ya kuwafahamu watu ambao wanaonekana kutoridhika na mchezo au shughuli.

Vivunja barafu vinageuka kuwa vifupi na umuhimu mdogo wakati kikundi kinaposongamana kwa nguvu kwa kipindi cha mzunguko wa maisha ya kikundi kiini. Unaweza kutumia nusu ya mda kwenye vivunja barafu wakati wa mikutano miwili ya kwanza, lakini unahitaji tu kutumia dakika 10 au 15 baada ya miezi michache.

**Maswali ya Kufungulia**

Ulipokuwa kati ya umri wa miaka 7-12….

1. Uliishi wapi? Ulikuwa na dada na kaka wangapi?
2. Ni aina gani ya usafiri familia yako walitumia?
3. Ni mtu gani ulijisikia kuwa karibu sana naye?
4. Ni lini Mungu alikuwa wazi zaidi kwako kuliko maneno?

**Mimi ni Nani?**

Andika majina ya wanaojulikana/ au wahusika katika Biblia kwenye karatasi. Zigundishe kwenye mgongo wa kila mmoja. Mtu hawezi kusoma karatasi yake. Watakwenda nyuma ya chumba wakiuliza swali moja baada ya mda juu ya wao ni nani mpaka watakapohisi wao ni nani.

**Nitabahatisha Wewe Hujui Hili**

Kila mtu kwenye kikundi anaandika kwenye kipande wazi cha karatasi kitu fulani anachodhani kwamba hakuna mtu kwenye kikundi atakayejua juu yake. Vipande vya karatasi vinakunjwa, na kuchanganywa vizuri, na kuwekewa namba kwa kufuatana. Kisha mtu aliyechaguliwa anaanza kuzisoma, kwa kusema namba kwanza. Kila mjumbe wa kikundi anaanza kubuni orodha ya watu ambao anajisikia zaidi kwamba wanaoana na kila muhusika. Baada ya kidokezo cha mwisho kusomwa, mtu mwenye kuoanisha kwa usahihi anakuwa mshindi.

**Utangulizi**

Kila mtu katika kikundi anaambiwa kuwa wana dakika kadhaa za kufikiri swali na kuliuliza watu wengine kwenye kikundi. Baada ya kila mmoja kufikiria swali, wanatakiwa kuanza kuzichanganya na za wengine, wakiuliza maswali yao. Andika jina la kila mtu na jibu. Baada ya kama dakika 10, kikundi kinakwenda kwenye mzunguko na kueleza walichopata juu ya kila mtu. Kadiri swali linavyokuwa zuri, ndivyo utakavyopata majibu yenye ubunifu na ufahamu.

Aina Mbili za Ukweli na Uongo

Kila mtu aandike ukweli wa mambo mawili juu yake na uongo mmoja. Kila mmoja kisha anaamua ni kipande gani cha karatasi kiende na mtu gani, ni yapi maelezo yake yalikuwa uongo. Unaweza kuacha sehemu ya kwanza yaani (kila mtu anashikilia kipande chake cha karatasi na watu wanabuni tu ni maelezo yapi ni uongo). (siyo halali kama mtu fulani anachukua uongo karibu na ukweli).

**Kutoa Taarifa ya Hali ya Hewa**

Nenda katika mzunguko, anza na kiongozi, na eleza jinsi unavyojisikia kwa sasa kwa maana ya kutoa taarifa ya hali—kuwa na mawingu kidogo, jua, n.k. Washiriki wanaweza kuelezea kwa nini wamechagua aina hiyo ya hali ya hewa. Kiongozi anaweka mfano kwa undani.

**Kutembea kwa Tumaini**

Unda vikundi katika jozi. Mfunge kitambaa mtu mmoja usoni katika kila jozi. Kila mtu ambaye hakufungwa kitambaa usoni anamwongoza aliyefungwa kitambaa usoni kuzunguka kwenye ujirani wa sehemu ya mkutano kwa ujumla. Jaribu kutoa tofauti nyingi za uzoefu—zichukue mpaka kwenye ngazi fulani, nenda nje na ndani, wasaidie kugusa vitu mbalimbali (majani, sakafu, uchafu) lakini usiseme kitu baada ya kuwa mmeanza kutembea. Unaweza bila kuongea kuwakilisha kila ujumbe. Baada ya kama dakika tano badilisha sehemu. Baada ya dakika zingine tano kikundi kinakutana tena. Shirikisha ni aina gani ya hisia ulizokuwa nazo ulipokuwa umefungwa na ulipokuwa ukigusa vitu, n.k. Umejisikiaje juu mtu mwingine? Ilikuwaje kutokuwa na udhibiti wa yaliyokuwa yakitokea? Umejifunza nini juu yako mwenyewe? Hii inahusianaje na uhusiano wako na Mungu? Na wengine?

**Mchezo wa senti**

Kama una watu wapya katika mkutano wako wakati mwingine, Unaweza kutunza mchezo wa senti kichwani kwa ajili ya kivunja barafu. Mpe kila mmoja senti kumi. Kila mtu lazima aandike jina la kitu kimoja juu yake mwenyewe ambacho kinatofautiana na cha kila mtu mwingine. (Kwa mfano, mjumbe jasiri wa kikundi anaweza kusema, “Nimepanda vilele vya mkuki.”) Msemaji anaweka senti katikati. Kama mchezaji mwingine pia amepanda kilele cha mkuki, anaweza kuweka senti pia. Mtu wa kwanza kumaliza senti zake zote anashinda.

**Kutegua Kwa Timu**

Kwa shughuli hii unahitaji timu mbili na vyumba viwili. Gawanya kikundi katika timu mbili. Timu A inafikiri juu ya aina ya mwendo au shughuli kwa ajili ya kuigizwa na timu B (mf. Kunywa chai asubuhi) bila kutumia maneno yoyote. Timu A inamwambia mtu mmoja tu (tutamwita “Laura”) kutoka timu B shughuli ni nini, na Laura haruhusiwi kumwambia mtu mwingine yeyote katika timu yake. Timu B inasubiri katika chumba cha kwanza, wakati Laura akichukua mtu mwingine kutoka kwenye timu yake (Tutamwita “Michael”) kwenye chumba cha pili. Katika chumba cha pili, timu A inaangalia wakati Laura anaigiza shughuli kwa ajili ya Michael (kumbuka, hakuna maneno!) Kisha Laura anarudi kwenye chumba cha kwanza na kumpeleka mwingine mmoja kutoka timu B. Kisha Michael anaigiza shghuli kwa mtu mwingine, na Michael anarudi kwenye chumba cha kwanza na kumpeleka mwingine kutoka kwenye timu yake. Utaratibu huu unarudiwa, mpaka mtu wa mwisho kutoka timu B anaangalia shughuli. Mtu wa mwisho kwa hiyo lazima abuni shughuli ni nini. Kisha timu zinabadilishana wajibu na timu B inafikiri juu ya shughuli kwa ajili ya timu A kuigiza.

**Majibu na Waandishi**

Kwenye vipande vya karatasi, andika maswali yanayotisha au yasiyotisha ambayo yanaweza kudhihirisha kitu fulani juu ya mtu (mf. Ni nini mali unayopenda zaidi? Ni nini ungependa kufanya ambacho huwezi kufanya kwa sasa? Ni yapi mapumziko yako ya maana? Watu wanatakiwa kujibu kila moja, au angalau matatu, lakini waelekeze wasiweke majina yao kwenye karatasi. Kisha kiongozi anakusanya karatasi na kusoma majibu yake, na kila mmoja anajaribu kubuni nani ametoa majibu hayo.

**Majirani Zangu Wote**

Kila mmoja anaanza kukaa kwenye viti vilivyoandaliwa katika mduara, kasoro mtu mmoja ambaye anaanza kusimama katikati. Mtu wa katikati anahitaji kutafuta baadhi ya "majirani." Kufanya hili anahitaji kufanya maelezo ya kweli juu yake mwenyewe, ambayo pengine yatakuwa kweli juu ya majiarani zake (Mf. "Majirani zangu wote wanapiga kinanda"). Kila mtu ambaye atasema maelezo haya kiukweli lazima asimame na kutafuta kiti kipya. Hawezi kurudi kwenye kiti alipokuwa amekaa. Mtu wa katikati pia anatafuta kiti. Kwa hiyo kila wakati kutakuwa na mtu atakayekuwa katikati bila kiti. Lazima atoe maelezo ya kweli na kutafuta baadhi ya "majirani" ambao kwao maelezo hayo pia ni kweli.

**Majadiliano ya Kikundi**

Chini kuna maswali machache ambayo yanaweza kutumika wakati wa mda wa kushirikiana. Tambua kuwa baadhi ya maswali haya yanafaa kwa vikundi vichache, na baadhi ya maswali ni vizuri yakiwekwa kwenye vikundi ambavyo wajumbe wameshajuana kidogo. Kawaida, swali moja tu litatumika katika kila mkutano wa kikundi kiini.

1. Ni wakati gani ulikuwa wa furaha katika maisha yako?
2. Unaweza kutuambia nini kuhusu tarehe yako ya kwanza?
3. Ni nini majuto makubwa kuhusu maisha yako?
4. Ni kitu gani kilikuwa kigumu katika vitu ambavyo umewahi kufanya?
5. Ni sifa gani kubwa ambayo umewahi kupata?
6. Ni nani rafiki yako sana wa hapa duniani? Mwelezee
7. Ni chumba kipi katika nyumba yako unachopenda zaidi?
8. Ni kitu gani kimoja unataka kukitimiza wiki ijayo?
9. Ni wapi ulijisikia uvuguvugu na usalama ulipokuwa mtoto?
10. Kama ulikuwa na mashine ya mda ambayo ingefanya kazi mara moja tu, ni hatua gani ya mbeleni au katika historia ungetembelea?
11. Ni lini mara ya mwisho umefanya kitu kwa mara ya kwanza?
12. Wakati wa chakula marafiki zako wanaaza kukuumbua kawaida ya kirafiki. Unafanya nini?
13. Kama ungeweza kunywa vidonge ambavyo vitakuwezesha kuishi mpaka kufikia miaka 1000, unaweza kunywa? Kwa nini?
14. Unapofanya kitu fulani kiupumbafu, ni kwa kiasi gani inakuudhi kuona watu wengine wamejua na kucheka?
15. Ungependa kujua tarehe kamili ya kifo chako?
16. Kama ungeweza kubadilisha mambo mawili ya jinsi ulivyolelewa, yangekuwa ni yapi, kama umetoka katika familia iliyoachika, ni kwa jinsi gani imekuathiri?
17. Ni yupi ndugu yako unayempenda zaidi? Kwa nini?
18. Ni kumbukumbu gani ya mda uliotumia, kama mtoto, na baba yako? Na mama yako?
19. Ni nani Mungu alimtumia kukuweka katika hatua ambayo ulijua kwamba ulimuhitaji Yesu?
20. Kama ungebadilisha sehemu na wahusika wa Biblia, Ni yupi ungechagua? Kwa nini?
21. Ni kitabu gani cha Biblia unachokipenda zaidi? Kwa nini?
22. Kama ungekwenda sehemu yoyote ulimwenguni, ni wapi ungekwenda?
23. Fikiria nyumba yako iko inawaka moto na una mda tu wa kuchukua kitu kimoja (familia yako iko salama). Ni nini utachukua?
24. Ni kipindi gani katika TV unachopenda zaidi?
25. Ni nani amekuwa na mguso mkubwa katika maisha yako tangu tulipokaa kwa mara ya mwisho?
26. Ni kitu gani kizuri kimekutokea wiki hii iliyopita?
27. Fikiria mda ambao ulishindwa hivi karibuni?
28. Taja mtu fulani unayemtamani ambaye ameweza kushinda vipingamizi vikubwa kufikia alipo sasa?
29. Ni kitu gani unathamini zaidi katika uhusiano wa kibinadamu? Katika uhusiano wako na Kristo? Na wazazi wako?
30. Unafanyaje unapokuwa hukushukuriwa kwa kutoa mda wako kwa ajili ya mtu fulani?
31. Ni mda gani mzuri zaidi kwako katika siku?
32. (Bachela) Aina ya msichana /mvulana ninayetaka kuoa/kuolewa… (Wliooana) Nini kilinisababisha kuolewa au kuoa mwenzi wangu?
33. Ni nini kilikuwa cha kukatisha tamaa katika maisha yako?
34. Ni vipawa gani (mbali na kukata shauri kwako) ambavyo hutasahau?
35. Ni nini ilikuwa tukio muhimu katika maisha yako wiki hii iliyopita?





36. Kama ungechagua kwenda sehemu yoyote duniani kwa siku tatu, wapi ungekwenda na kwa nini?
37. Kama ungechagua kukutana na mtu yeyote ambaye amewahi kuishi katika nchi yako, angekuwa nani huyo, na kwa nini ungependa kukutana naye?
38. Kama ungechagua kuishi kokote ulimwenguni, ni wapi ungeishi, na kwa nini?
39. Ni kipawa gani (kiroho, kihisia, kiakili n.k.)unaamini unakileta kwenye mkutano huu? (kwa maneno mengine, Ni nini unadhani unaleta ambacho kinaweza kuchangia kwenye kutia moyo kwa wengine?
40. Ni uzoefu gani ulikuwa wa maana katika maisha yako ambao ulibadilisha utaratibu wa thamani yako kabisa kabisa?
41. Ni nini baadhi ya malengo yako kwa miaka ijayo?
42. Ni nani wazazi wako, ni nini wanafanya na nini ungependa kubadilisha juu yao?
43. Kama ingekuwa kwamba uchague cheo chako tena, ungefanya nini?
44. Kama unakuwa kiongozi wa nchi yoyote ulimwenguni ingekuwa ipi na kwa nini?
45. Ni nini ulikuwa uzoefu wako mzuri na mbaya zaidi wa wiki yako?
46. Kama ungechukua safari ya bure ya wiki-mbili kwenda sehemu yoyote ulimwenguni, ingekuwa wapi na kwa nini?
47. Kama ingekuwa kwamba uongee na mtu yeyote anayeishi sasa, angekuwa nani na kwa nini?
48. Mpe kila mmoja kipande cha karatasi na waambie kuchora picha ya kazi zao au chochote wanachofanya kila siku. Elezea michoro yako.
49. Kwa nini una furaha kuwa katika kikundi kiini hiki jioni ya leo?
50. Ni nini baadhi ya hatua imara na dhaifu katika uhusiano wako na mtoto wako mkubwa au wazazi wako-mashemeji au mme wako?
51. Mjulishe kila mmoja kwamba wamepewa dola milliono moja. Ruhusu kila mmoja kusema ni jinsi gani angetumia kipato chake kipya.
52. Una jina la utani na kama ndiyo ni lipi? Ni majina gani ya utani uliyonayo kwa ajili ya mme wako na watoto?
53. Kuna kipindi cha wakati ambacho ungependa kuwa ungeishi humo? Kama ndiyo kwa nini?
54. Kikundi kiini kimekuwa msaada kwako? Tumia mda kukiongelea na kushukuriana.
55. Kiambie kikundi kiini vitu vitatu ambavyo unashukuru juu ya familia yako na njia tatu ambazo unakuta ugumu juu yake katika nyakati.
56. Ni kitu gani kimoja ungependa kuona kinatokea mda huo katika familia yako? katika kanisa lako? Katika kikundi kiini chako? Katika ulimwengu?
57. Ni rafiki gani wa karibu uliyenaye kwa kipindi hiki katika maisha yako?
58. Umekuwa na maombi yaliyojibiwa hivi karibuni? Shirikisha historia.
59. Ni nini kazi yako? Ni nini unachoofurahia juu yake?
60. Ni nani amekuwa msukumo mkubwa katika maisha yako ya kikristo na kwa nini?
61. Ni kitabu gani, senema, video umeona/kusoma ambavyo ungevishauri kwa wengine? Kwa nini?
62. Ni nini unadhani kinamfurahisha Mungu kuliko vitu vyote katika maisha yako?
63. Ni kitu gani cha kutia moyo kimesemwa kwako wiki hii?
64. Ni tendo gani la kutia moyo umefanya kwa mwingine wiki hii?
65. Ni nini kilikufanya kuhudhuria kanisa hili?
66. Ni nini bado unapenda kukamilisha katika maisha yako?
67. Ni nini uzoefu wako unaotia aibu zaidi?
68. Ni kwa lipi unashukurani?
69. Ni tukio gani la kukumbukwa katika maisha yako na kwa nini?
70. Shirikisha andiko lenye kuleta maana kwako na kwa nini linamaanisha hivyo?
71. Ni jinsi gani wewe na mwenzi wako mlikutana na nini kiliwafanya muanze kwenda nje pamoja au ni mtu wa aina gani ungependa kuwa naye kama mwenzi wako?
72. Maisha yako yangekuwaje kama ungejua kuwa Yesu angerudi katika kipindi cha wiki moja?
73. Ni mtu yupi wa kuvutia zaidi umekutana naye?
74. Ni siku zipi za kupumzika unazopenda zaidi?
75. Shirikisha uzoefu wa kiroho ambao umewahi kuwa nao.
76. Ni nini kinakuudhi juu ya mwenzi wako au rafiki?
77. Ni jinsi gani unavyopumzika?
78. Ni aina gani ya mziki/wimbo unaopenda zaidi n.k.?
79. Ni nini kimetokea kwako wiki hii ambacho ungependa kuwaambia kikundi chote?
80. Ni lini mara ya mwisho ulipokasirika hasa?

81. Kama usingeshindwa, ungependa kufanya nini?
82. Kama ungeishi tena maisha yako ni nini ungebadilisha?
83. Ni nini unataka kiandikwe kwenye jiwe lako la kaburi?
84. Ni nini unataka kisemwe kwenye msiba wako?
85. Ni nini hutaki kisemwe kwenye msiba wako?
86. Kama ungekwenda kuishi kwenye mwezi na kuweza kubeba kitu kimoja tu, ni nini kingekuwa?
87. Ni nini ungefanya kama ungeliona (1) Mtu akiwa ameibiwa (2)Mtu anayezama (3)Nyumba inayoungua moto?
88. Ni kitu gani kimoja kilianzisha taabu katika maisha yako wiki hii?
89. Ni nini kitu kimoja kinachokufanya kujisikia hatia?
90. Ni kitu gani kimoja ambacho hujui juu ya jinsia tofauti?
91. Kama ingekuwa kwamba uirudie wiki hii tena, ni kitu gani ungefanya tofauti?
92. Elezea kundi jingine dogo ambalo ulikuwa mjumbe nje ya kanisa lako. Kwa nini unadhani kundi lilifanyika (halikufanya)? Hauzuiliwi na makundi ya "dini". Wengi wetu tunakutana katika vikundi vidogo kazini.
93. Ni Biblia gani ya kukumbukwa uliyowahi kupata? (Mf. Katika ubatizo wako, ndoa, kukata shauri, n.k.) Tuambie kwa nini ina maana kwako.
94. Ni kitu gani kinachokuja akilini mara ya kwanza unapofikiri juu ya Mungu?
95. Ni swali gani kubwa ulilonalo juu ya uhusiano wako na Mungu?
96. Ni katika misukosuko ipi unajisikia upweke zaidi? Upweke kidogo? Kwa nini?
97. Ni katika eneo gani la maisha yako ni vigumu kumutumaini Mungu? Watu wengine? Wewe mwenyewe?
98. Kwa nini unaamka asubuhi? Kusudi ni kutafuta nini nguvu ya mvuto iko katika maisha ya mtu huyo. Ni sawali rahisi lakini linachukua mawazo hasa kulijibu kwa uaminifu.
99. Ni lini ilikuwa mara ya mwisho ulipokubari umekosa? Kwa nini ni vigumu kufanya hivyo?
100. Nini uliyojifunza hivi karibuni kutoka kwa muumini?

**VIKUNDI KIINI**
***ZIADA***
**2B**

# Mfano wa Shughuli Katika Mkutano wa Kikundi Kiini

Ifuatayo ni mfano wa shughuli kwa kila moja ya sehemu nne za mkutano wa kikundi kiini. Mda ulioorodheshwa kwa kila kazi ni makadilio:

| Ushirika | Kuabudu | Kuadilishana | Uinjilisti |
|---|---|---|---|
| Mtu kwa mtu | Mtu kwa Mungu | Mungu kwa mtu | Mwili wa Kristo kwa ulimwengu |
| "Kwa ndani" | "Kwa juu" | "Kwa chini" | "Kwa nje" |
| Dakika 20 | Dakika 20 | Dakika 30 | Dakika 20 |
|  |  |  |  |
| • Furahia shughuli za kufurahisha pamoja<br>• Kula chakula pamoja<br>• Pata kujuana zaidi<br>• Kutiana moyo<br>• Shirikishana furaha<br>• Shirikishana matatizo<br>• Ombeaneni | • Imba nyimbo za sifa<br>• Mshukuru Mungu kwa ukuu wake<br>• Mshukuru Mungu kwa yote aliyofanya<br>• Omba kwa sauti au kimya kimya<br>• Soma vifungu vya kuabudu (kwa mfano, Zaburi).<br>• Soma mithali za kikristo | • Jifunze vifungu vya maandiko kama kikundi<br>• Tumia ukweli wa kibiblia katika hali za kila siku<br>• Husika katika huduma na kikundi<br>• Gundua na tumia vipawa vya kiroho<br>• Kariri mistari ya Biblia | • Unda “maombi ya utatu” na waombee marafiki wasiookoka<br>• Wakaribishe wasioamini kwenye kikundi<br>• Kama kikundi, timiza mahitaji ya watu wanaowazunguka<br>• Anzisha urafiki na wasioamini<br>• Shirikisha habari njema za Kristo kwa watu wengine |

# Vikundi Kiini—Azimio la mafunzo 3

## Kuanzisha Kikundi Kiini

**I. Jiandae kwa Ajili ya Kikundi Kiini –**Kwa nini kila moja ya yafuatayo kuwa muhimu?

**A. Unda Timu ya maombi (Efe 6:19, 1 The 5:25)**
**B. Unda Timu ya Uinjilisti (Luka 10:1)**
**C. Tafiti Eneo Lako Lengwa**

**II. Fanya Mawasiliano**

Ni nani watazamaji wako wanaolengwa?
Jinsi gani unaweza kuunda mahusiano na wao?

**III. Tafuta Mahali**

Nini panaweza kuwa mahali pa kawaida kwa kikundi kiini chako kukutana?

**IV. Andaa kwa Ajili ya Mkutano wa Kwanza**

Ni baadhi ya matatizo gani ya kipekee unayoweza kuwa nayo unapokuwa unafanya "uvumbuzi" wa upandaji kanisa kwenye eneo lisilo na ushuhuda wa kikristo?

Ni nini kinaweza kufanyika kushinda vipingamizi hivi?

Ni nini unachoweza kusema kwa muumini ambaye ni sehemu ya kikundi kiini chako lakini aliye mwoga kufungua nyumba yake kwa wageni ambao hajawajua?

Kama mda unaruhusu, fanya Utekelezaji wa Azimio wakati wa kipindi hiki. Liombe darasa kuandika vitu vya kwenye Ziada 3A unapokuwa unavisoma. Mwende kwenye makundi madogo na jadili maazimio ya wajumbe wa kundi.

## Utekelezaji wa Azimio

- Ngoja tuseme kwamba utakuwa na mkutano wa kikundi kiini chako katika mda wa wiki moja. Tumia ziada 3A, "Karatasi ya Kufanyia Mpango, mkutano wa kikundi kiini," kufanya mpango wa mkutano huu wa kwanza. Ingia kwa undani zaidi iwezekanavyo. Kuna vipengele vingine vya mkutano ambavyo utaviweka kwenye mpango pia? Unapomaliza, shirikisha mpango wako kwa mmoja wa wafunzwa na muombe autathimini. Na wewe utathimini mpango wake pia.
- Kama hujamaliza utafiti wa eneo lako unalolenga, unahitaji kufanya hili sasa. Baada ya kufanya utafiti wa eneo lako unalolenga, tumia kanuni na hatua za vitendo katika somo kuanzisha mpango wa kuanza kikundi kiini kipya. Weka na majina ya timu ya uongozi, majina ya wanaowaombea, jinsi utakavyofanya mawasiliano, ni hitaji gani dhahiri kikundi kiini chako kitajaribu kulitimiza, lini na wapi kundi litakutana, na kitu gani kingine unadhani kinatakiwa kuwa sehemu ya mpango. Baada ya kukamilisha mpango huu, Mpatie mkufunzi wako au msimamizi aufanyie marudio.

ZIADA 3A - KARATASI YA KUPANGIA—Mkutano wa Kikundi Kiini

Tarehe na mda wa mkutano: ____________________

Eneo na Mkarimu: ____________________

**Ushirika**

Vinywaji: ____________________

Shughuli, Mchezo: ____________________

**Kuabudu**

Kiongozi wa wimbo: ____________________

**Maombi**

Shughuli za maombi: ____________________

**Majadiliano ya Biblia**

Kiongozi wa majadiliano: ____________________
Kifungu cha maandiko: ____________________

**Makusudio ya huduma**

Mda wa kushirikishana: ____________________

Shughuli za kikundi: ____________________

Shughuli za mtu binafsi: ______________________________

Vifaa vingine vya kupangia: ______________________________

Vitu vya Kufikiria Juu Yake:

- Ni yupi kiongozi wako mwanafunzi?
- Ni nani anafuasa kila mjumbe wa kikundi chako? (Ni nani unayemfuasa?)
- Ni nini unachofanya kumsaidia kiongozi mwanafunzi kuendeleza ujuzi wa uongozi? Ni jinsi gani unavyogawa huduma kwake? Ni jinsi gani unavyokuwa kielelezo cha huduma kwake?
- Unamuombea kila mjumbe katika kikundi kiini chako?

Kwa ajili ya majadiliano ya kikundi

1. Ni sura ipi ya upangaji ilikuwa rahisi zadi kwako? Kwa nini?
2. Ni sura ipi ilikuwa ngumu zaidi? Kwa nini?
3. Nini unachoweza kufanya kama hutaona yeyote kuwa kiongozi wa nyimbo?
4. Ni sura gani ya mkutano wa kikundi kiini unaweza kutarajia kwenda vema? Elezea.
5. Ni sura gani unayoweza kutarajia kwenda vibaya zaidi? Elezea.

KIKUNDI KIINI
*ZIADA*
3A

# Karatasi ya Kupangia

## MKUTANO WA KIKUNDI KIINI

Tarehe na mda wa mkutano: ______________________________

Eneo na Mkarimu: ______________________________

**Ushirika**

Vinywaji: ______________________________

Shughuli, Mchezo: ______________________________

**Kuabudu**

Kiongozi wa wimbo: ______________________________

**Maombi**

Shughuli za maombi: ______________________________

**Majadiliano ya Biblia**

Kiongozi wa majadiliano: ______________________________
Kifungu cha maandiko: ______________________________

**Makusudio ya huduma**

Mda wa kushirikishana: ______________________________

Shughuli za kikundi: ______________________________________________

Shughuli za mtu binafsi: ___________________________________________

Vifaa vingine vya kupangia: ________________________________________

**Ya kufikiria:**
Ni yupi kiongozi wako mwanafunzi?

Ni nani anafuasa kila mjumbe wa kikundi chako? (Ni nani unayemfuasa?)

Ni nini unachofanya kumsaidia kiongozi mwanafunzi kuendeleza ujuzi wa uongozi? Ni jinsi gani unavyogawa huduma kwake? Ni jinsi gani unavyokuwa kielelezo cha huduma kwake?

Unamuombea kila mjumbe katika kikundi kiini chako?

# Vikundi Kiini—Azimio la Mafunzo 4

## Uinjilisti wa Kikundi Kiini

**I. Aina Mbili za wasioamini**

- **A. Aina ya A ya Wasioamini: hao Walio na Nia**
- B. **Aina B ya wasioamini: hao wasiotaka Kujua (Efe 2:17)**

**II. Kuelewa Oikos-wa nyumbani**.

Zoezi: Ukitengeneza Orodha ya Oikos Yako ya mahusiano Soma na Elekeza mazoezi Yafuatayo.

Kwenye kipande cha karatasi, chukua dakika chache kuandika majina ya watu ambao unazungumza nao au unaongea nao mara kwa mara katika kipindi cha wiki au kwa mwezi. Andika jina moja kwa kila mstari. Fanya orodha yako isizidi watu 20 (kama kuna zaidi, chagua 20 ambao umekuwa na uhusiano nao wa karibu zaidi).

Sasa, chunguza majina yako katika orodha. Kwa kila mtu unayemjua kuwa ni muumini, weka alama ya msalaba mbele ya jina lake. Inayofata, fikiria juu ya watu ambao siyo waumini. Kwa watu wote wa “aina ya A” weka alama ya A mbele ya majina yao. Hawa ni watu unaodhani wana weza kuwa wazi kwa mambo ya kiroho, kwa kujifunza Biblia, au kujifunza zaidi juu ya kusudi la Mungu katika maisha yao.

Mwishoni, Agalia majina yaliyobaki. Kama hawa ni watu unaowajua kuwa hawana mpango na Mungu au mambo ya kiroho, ambao hawatapenda kuja kujifunza Biblia, na ambao hawamuoni Mungu kuhusiana katika njia yoyote katika maisha yao ya kila siku, weka B mbele ya majina yao. Hawa ni “aina B” ya wasioamini.

Tunza orodha hii, pengine ndani ya Biblia yako. watu wenye alama ya msalaba mbele ya majina yao ni waumini ambao pengine inawezekana wangekusaidia kuanza kikundi kiini kipya. Watu wenye alama ya A mbele ya majian yao ni hao ambao unaweza kuwa unawaombea na kuwaalika kwenye kikundi kiini chako. Watu wenye alama ya B mbele
ya majina yao ni watu ambao unaweza kuwa unawaombea juu ya kupata mda zaidi wa kuwa pamoja nao. Unaweza kushangazwa kuona jinsi wachache (kama wapo!) wasioamini wako kwenye Oikos yako bianafsi. Wakristo wenge wana uhusiano kidogo na wasioamini. Muumini mpya atakuwa na uhusiano zaidi na asiyeamini. Kwa jinsi hiyo, kadiri wakristo waanapoanza kushirikiana na wakristo wengine, wanagundua mara moja kwamba wanatumia mda kidogo au hakuna tena na marafiki zao wasio wakristo.

**III. Makundi ya kushirikisha—**watu wawili au watatu waliotumia mda na aina B ya wasioamini wanaowajua. Nini unachoweza kufanya na aina ya B ya wasioamini kwamba watakubali na kufurahia?

**IV. Utaratibu wa Uinjilisti wa Kikundi Kiini**

A. Uinjilisti wa Oikos—Ombea na alika aina ya A kwenye kikundi kiini chako.

Uinjilisti wa Kulenga—Vikundi kiini vilivyohusika katika uinjilisti wa Oikos kisha vinaweza kufikia nje kwa wageni.

Hii inaweza kuhusisha kuanzishwa kwa haja, mapendeleo au shughuli za vikundi. .

Ukubwa wa kundi na kuzidisha—ukubwa ni 15.Gawanyika kama inafikia ukubwa huu.

Maswali ya kutafakari, marudio na matumizi

Katika **Luka 5:32,** Yesu alisema, “sikuja kuwaita wenye haki, lakini wenye dhambi wafikie toba.” Ni mda kiasi gani Yesu alitumia na wenye “dhambi” wakati wa kipindi cha huduma yake duniani? Toa mifano miwili au mitatu ya watu Yesu aliokutana nao ambao wangedhaniwa kuwa aina A na aina B ya watu.

Ni aina gani ya shughuli unaweza kudhani kuwa unaweza kujengea uhusiano na aina B ya watu kutoka kwenye orodha yako binafsi ya Oikos? Ni wakristo gani wengine wanaweza kwenda na wewe unapofanya mahusiano haya?

Ni mda kiasi gani unadhani inachukua kujenga uhusiano wenye maana na watu wasioamini? Ni nini vipao mbele, kama kuna chochote, unachoweza kubadilisha katika maisha yako ili kuweza kutumia mda zaidi na wasioamini?

### Utekelezaji wa Azimio

Kama kikundi kiini chako, kinaanzisha mkakati wa kuwafikia nje kwa kutumia uhusiano unaojengwa wa kila mjumbe. Kama wengine katika kikundi chako hawajafanya orodha ya uhusiano kwenye Oikos yao, wafanye hivyo kwenye mkutano ujao. Wanakikundi waamue ni yupi kweye aina A wa kuombea na kuwasilana naye, na watu gani wa aina B wa kuombea na kuanza kutumia mda pamoja nao. Kiongozi wa kikundi kiini lazima atunze orodha ya majina haya, ili kwamba kikundi kiweze kujiwajibisha kuwafikia.

# Vikundi Kiini—Azimio la Mafunzo 5

Kuonyesha Mfano wa Kikundi Kiini

Somo hili linahitaji mpango na maandalizi ili kuwa lenye faida. Mkufunzi lazima afikiri mbele kabla ya mda ni shughuli ipi atapenda kufanya na kundi la wafunzwa, na kupanga kufuatana. Kama aina yoyote ya mda wa mafunzo ya Biblia itakuwa sehemu ya shughuli za ndani ya darasa, mfunzwa anatakiwa apewe siku moja au mbili kabla ya somo hilo ili kujiandaa.

Kuna aina nne za kimsingi za shughuli za kuchagua kutoka, na zinahusiana na sehemu nne halisa za mkutano wa kikundi kiini: ushirika, kuabudu, kuadilishana, na uinjilisti. Labda kuwe na zaidi ya saa moja ya kutumia katika somo hili, inahofisha kwamba mkufunzi atakuwa na mda wa kutosha kufanyia mazoezi sehemu zote nne. Uwezekano mkubwa wa mtiririko wa matukio ni kwa wakufunzi kuchagua shughuli moja au mbili za kufanyia majaribio. Uchaguzi huu utakuwa upande wa idadi, aina, uzoefu na maswali.

Mifano na mapendekezo yaliyotolewa katika somo hili ni maelekezo ya utaratibu. Kama mkufunzi anafahamu sehemu fulani zenye matatizo au maswali yanayohusiana na mandhali maalumu, anatakiwa kwa njia zozote kurekebisha shughuli za somo hili kujibu matatizo hayo au maswali.

Kama kundi la wafunzwa ni kubwa, wanatakiwa wagawanywe katika makundi madogo ya wasiozidi watu 8-10 kwa zoezi la darasani. Mkufunzi anatakiwa amwagize “kiongozi” wa kikundi kiini kwa kila makundi yanayofanya kazi. Kutegemeana na shughuli, mkufunzi anaweza kutaka kuwa na watu kadhaa kushikilia nafasi ya uongozi wakati wa mda wa zoezi hili.

Weka kichwani kwamba lengo kwa ujumla la somo hili ni kutoa majaribio, uzoefu wa kutenda katika shughuli mbalimbali za maisha ya kikundi kiini na huduma. Inatakiwa pia iwe ya kufurahisha!

**Maeneo Manne ya Mkutano wa Kikundi Kiini**

A. **Ushirika—**Mtu kwa mtu-Kwa ndani
B. **Kuabudu—**Mtu kwa Mungu-Kwa juu
C. **Kuadilisha—**Mungu kwa Mtu- Kwa chini: ufuasishaji, mafunzo ya Biblia kwa kufata neno, mafundisho ya kimamlaka.
D. **Uinjilisti—**Mwili wa Kristo kwa ulimwengui-Kwa nje: Ushuhudua wa binafsi, maazimio ya mbeleni ya huduma, kundi la kushirikisha.

**Tathimini shughuli za kikundi kiini:** Nini ilikuwa uwezo wao na udhaifu? Jinsi gani "kiongozi" wa kikundi kiini alichukulia matatizo tofauti au maswali? Nini kingeweza kufanyika tofauti?

Maswali ya kutafakari, marudio na matumizi

Kwa nini ni muhimu kupanga kwa ajili ya kila sehemu ya mkutano wa kikundi kiini?

Ni kwa njia zipi viongozi wa "vikundi kiini" kwenye zoezi hili wamekuwa na ugumu na majukumu waliyoshika? Kutakuwa na ugumu huo huo kwenye mkutano wako halisi wa kikundi kiini?

# Vikundi Kiini—Azimio la Mafunzo 6

## Falsafa ya Huduma ya Kikundi Kiini

**I. Falsafa ya Kikundi Kiini**

A. Viini Vinamaisha ya Mzunguko

| AwamuP | Kudumu | Maelelezo |
|---|---|---|
| **Mazoezi ya kazi** | Wiki 1-4 | Watu wanajifunza kuhusu kila mmoja ngazi ndogo ya kushirikishana. |
| **Mpito** | Wiki 5-10 | Wajumbe wanajua, kukubali na kuaminiana. |
| **Jumuia** | Wiki 11-15 | Hatua ya kujitoa inayokua, uwazi, na mazingira. |
| **Utendaji** | Wiki 16-35 | Mapana ya kundi kuingiliana na kutumia ukweli wa kibiblia. |
| **Kuzidisha** | Wiki 36-40 | Viongozi wanafunzi wanaanzisha makundi mapya—mzunguko wa kuzidisha. |

B. Viini Vinafanya Kazi Kuelekea Lengo Moja

C. Viini ni sehemu Muhimu ya Mkakati wa Kueneza Upandaji Kanisa

**II. Kielelezo cha Huduma ya Kikundi Kiini**

A. Kielezo 1: Vikundi Kiini **ambavyo vinaanzisha makanisa ya mapokeo kwa viini**

B. Kielezo 2: kanisa lililopo **linaanza kutumia Vikundi Kiini**

C. Kielezo 3: Kikuindi kiini ambacho **kinaanzisha kanisa la kikundi kiini**

D. Kielezo 4: Vikundi Kiini kadhaa v**inakua, kuzidi,** "Kulisha" Makanisa ya Mtaa Yaliyopo.

Zoezi la Kikundi kidogo: Baada ya kusoma kila mchanganuo, vikundi vidogo vijadili (1) Ni kielezo gani muonekano unatokana nacho (kama kuna chochote), na (2) faida na hasara za muonekeno huu kama mkakati wa upandaji kanisa.

Mchanganuo 1

Mpanda kanisa anahamia kwenye mji ambao hauna kanisa na kuweza kuanzisha vikundi kiini kadhaa vipya. Vikundi kiini vina mafanikio makubwa, na kuanza kukua na kuongezeka vyenyewe. Watu katika viini wanajisikia ukaribu wa mmoja kwa mwingine, na kuamua kuwa wataanza kanisa moja kutoka kwenye vikundi. Kila kikundi kiini kipya kilichoanzishwa kitaendelea kuwa sehemu ya kanisa hili moja kubwa.

Mchanganuo 2

Wapanda kanisa kadhaa wanaanza kuanzisha vikundi kiini. Kundi lina maono ya kufanya uinjilisti na kuongezeka, lakini halitaki kuanzisha makanisa mapya. Badala yake, wanaelekeza waumini wapya katika moja ya makanisa yaliyopo katika mji. Baadhi ya vikundi vina wajumbe ambao wanaendelea kukutana katika vikundi, vilevile na kuhudhuria makanisa ya mtaa ya madhehebu mengine.

Mchanganuo 3

Miaka michache iliyopita huduma kutoka magharibi ilileta wamishenari ambao walianzisha baadhi ya vikundi vodogo vya kujitegemea kutoka kwenye makanisa ya mtaa yaliyopo. Makundi haya yanakutana mara moja kwa wiki na kufanya mafunzo ya Biblia kwa kufata neno.

.

Mchanganuo 4

Kanisa la kiinjili lina vikundi vidogo vingi ambavyo vinakutana kujifunza Biblia. Watu walewale wameshawahi kukutana katika vikundi hivi miaka kadhaa iliyopita, na vikundi havikukua. Vikundi kadhaa vina watu wanaoisha

karibu, lakini wanaoishi mbali kutoka kanisani. Vikundi hivi vinaamua kuwa vingependa kuanzisha kanisa mpya karibu na wanapoishi.

Mchanganuo 5

Mpanda kanisa anahamia kwenye mji mpya na anaanza kufanya uinjilisti. Watu ni wapokeaji, na mara ameanza vikundi kadhaa vidogo, ambavyo kila kimoja kina maono ya kuinjilisha na kuzidisha. Vikundi vinakutana jumapili kwa ajili ya mda wa kuabudu na mafundisho, na jumatano jioni wanaalika marafiki wasio-amini kwa mda wa burudani na kushirikiana. Hakuna mpango wa kujenga jengo la kanisa, na mara moja kila baada ya wiki sita kikundi kinakodi ukumbi kwa ajili ya jioni ya ibada ya pamoja na mafundisho.

**Kujenga mkakati wa kikundi kiini: Vitu Muhimu**

1. Gundua lengo lako la huduma kwa ujumla. Unaanzisha harakati za kueneza upandaji kanisa? Kanisa moja? Makanisa ya kutosha kuujaza ujirani, mji au eneo la kijografia?
2. Jinsi gani viini vinahitaji **kufanya kazi kikujitegemea na kwa pamoja** ili kuona lengo limekamilishwa?
3. Ni nini **eneo linalolengwa**, na ni watu gani ni walengwa? Utafiti unatakiwa ufanyike?
4. Ni nini ni **aina ya uinjilisti** kikundi kiini kinaweza kutumia ambao unafaa kwenye eneo lengwa/watu?
5. Ni nani ni **ni viongozi wa ufunguo katika eneo lengwa**?
6. Ni **aina gani kikundi kiini kinaeleza** (hapo juu) unayohitaji ili kukamilisha malengo yako?

Maswali ya Kutafakari, marudio na matumizi

Kikundi kiini chako kitakuwa katika moja ya awamu ya mzunguko wa maisha (mazoezi ya kazi, mpito, jumuia, vitendoa au kuzidisha). Kwa nini hili linamaanisha unapokuwa unapanga kwa ajili ya shughuli za mkutano wako? Kwa nini hli linamaanisha kutoka katika mtazamo wa mkakati wa jumla wa kikundi kiini?

Kwa nini vikundi kiini ni sehemu muhimu ya mkakati wa kueneza upandaji kanisa?

Ni vielezo gani kutoka kwenye sehemu ya "Vielezo vya Huduma ya Kikundi Kiini" vingeweza kufanya kazi vema kwenye eneo lako lengwa?

## Utekelezaji wa Azimio

Katika sentensi kadhaa, andika tafafsiri ya vikundi kiini kwa kifupi lakini yenye mambo mengi. Mpatie hii mkufunzi.

Kulingana na unachojua juu ya eneo lako unalolenga na malengo uliyoweka kwa ajili ya eneo hilo, andika msingi wa mkakati wa jinsi unavyoweza kutumia vikundi kiini ili kuyatimiza malengo hayo. Weka pamoja na vigezo kutoka kwenye “Fikira za mkakati wa kikundi kiini” sehemu katika mpango wako. Shirikisha mpango wako na mfunzwa mwingine, na kila mmoja wenu atathimini mpango wa mwingine. Kwa kusudi la somo hili, mpango wako unatakiwa usiwe zaidi ya uefu wa vifungu vichache

# Njia za Kujifunza Biblia—Azimio la Mafunzo 8

### Njia Tofauti Tofauti za Kutumia Mafunzo ya Biblia Kwa Kufata Neno

**I.** Marudio ya **kanuni za Mafunzo ya Biblia kwa Kufata Neno**

A. Sababu ya Njia ya Kujifunza Kwa Kufata –Tulichojifunza katika Mwongozo wa Kwanza ni faida za kutumia njia ya kujifunza kwa kfuata?

B. Hatua za Njia ya Kujifunza kwa Kufata – Ni hatua zipi tatu za njia ya kujifunza kwa kufata?

C. Msisitizo wa Njia ya Kujifunza kwa Kufata- Ni baadhi ya kanuni gani muhimu za jumla za njia ya kujifunza kwa kufata? (Jibu ni pamoja na:)

Uliza Maswali Mengi Mazuri Kams Vile Nani? Nini? Wapi? Lini? Jinsi Gani? na Kwa Nini?
Angalia Wazo Kuu
Elewa Kusudi la Mwandishi
Ruhusu Ufunuo Unaoendelea

Elewa Mandhali
Eleza Kanuni za Kibiblia
Linganisha Mandhali ya Kibiblia na ya Sasa
Omba

**II. Kujifunza Habari za Maisha – maisha ya mtu kibiblia**

**A. Kwa Nini Kujifunza Habari za Maisha?**

Ni mifano gani ya kibiblia mbali na mmoja wa Musa katika **1 Kor 10:11** unaokuja akilini mwako?

**B. Jinsi ya Kufanya Mafunzo ya Habari za Maisha**

1. Jinsi gani unaweza kufanya uchunguzi kwenye mafunzo ya habari za maisha?
2. Jinsi gani unaweza kufanya ufafanuzi kwenye mafunzo ya habari za kimaisha unapokuwa na vifungu kadhaa?

**C. Maswali ya Matumizi**

Jinsi gani uzoefu wangu uko sawa na hili?
Nina uwezo kama huo? Udhaifu?
Kwa nini Mungu amemuhusisha mtu huyu kwenye maandiko?
Ni vitu gani maalumu Mungu anataka kunifundisha kupitia mafunzo ya maisha yake?

**III. Mafunzo ya Kitabu**

Kila injili imeandikwa kutoka kwenye mtazamo wa kipekee

Mathayo – Inamuonyesha Yesu Kama Masiya wa Wayahudi (ufalme)
Marko – Inamuonyesha Kristo kama mtumishi (mnyenyekevu)
Luka – Inamuonyesha Kristo Kama Mwana wa Mtu (Binadamu)
Yohana– Inamuonyesha Kristo kama Mwana wa Mungu (Uungu)

**A. Kwa nini** tunatakiwa **Kufanya Mafunzo ya Kitabu?**

**B. Jinsi gani ya Kufanya Mafunzo ya Kitabu?**

1. Soma Kitabu Mara Kadhaa
2. Ni vitu gani vimehusishwa kwenye 'Mpangilio' wa Kitabu

**Jibu: Mwandishi**
Wapokeaji
Tarehe
Mtindo wa Maandishi

3. Nini kimehusishwa kwenye "Yaliyomo Kitabuni"

Jibu: a. Kisa cha Kitabu
b. Mwendelezo wa Kisa

4. Weka Mchoro wa Maendeleo ya Kisa cha kitabu

Kwenye muhimili wa kwanza wa mchoro (jedwali), safu inaweza kuwa pamoja na kurasa, sehemu, huduma kwa, watu mashuhuri, matukio maalumu, na kanuni. Vichwa vya mihimili mingine (safu ya kwanza) inaweza ikawa ni pamoja na makundi ya mistari iliyokamilishwa.

5. Tumia Kisa cha Kitabu kwenye Hali yako

Ni nini katika maisha yangu kinafanana na hali ya kwenye kitabu?
Ni nini katika maisha yangu kinafanana na mwandishi wa kitabu?
Jinsi gani ningekuwa nimeshughulikia hali hii?
Ni nini hasa kimezungumzia kwenye moyo wangu niliposoma kitabu?

## IV. Mafunzo ya Kisa: Kuichunguza topiki

A. Kwa nini Kujifunza Juu ya Kisa?
B. Jinsi ya Kufanya mafunzo ya Kisa

Hatua za Kujifunza:
Tafuta Mistari Inayoendana
Ipange mistari katika utaratibu
Jifunze na fupisha kila mstari katika mandhali
Fupisha mafundisho juu ya kisa
Tumia ukweli **(Yakobo 1:22-25).**

## Utekelezaji wa Azimio

Fanyia kazi  mafunzo ya historia ya maisha kwenye maisha ya Barnabas katika Ziada 8A. Fikiria kwenye nafasi yake katika utaratibu wa upandaji kanisa katika Matendo. Ni matumizi yapi unayoona kwa ajili ya maisha yako mwenyewe na huduma?
Chukua mda kutumia njia ya kujifunza kwa kufata neno na kwa kujifunza kisa. Chukua kitabu kidogo au kisa kinachowezekana kwa ajili ya jaribio lako la kwanza. Tathimini ufanisi wa njia hii katika kukusaidia kugundua vitu ambavyo hujawahi kuviona katika neno.

**ZIADA 8A:  JIFUNZE MAISHA YA BARNABAS**

Soma kila mstari au kifungu kidogo kwenye orodha ifuatayo, na andika uchunguzi wako na ufafanuzi kwa kila moja. Kisha liweke kwa kifupi fungu dogo.

**A.  Matendo 4:36,37**

1. Uchunguzi:
2. Ufafanuzi/Ufupisho: (Endelea kufanya uchunguzi na ufafanuzi wa mistari katika B-J.)

B.  **Matendo 11:19-24, C. Matendo 11:25-26, D. Matendo 11:27-30, E. Matendo 12:25, F. Matendo 13:1-13;42-43, G. Matendo 14:1-23, H. Matendo 15:2-4, 12, 22, 25, 35-39, I.  Wakolosai 4:10, J. Wagalatia 2:11-13**

Kuweka kwa kifupi mafundisho

Na sasa kwamba umeangalia kwenye vifungu pekee, ni wakati wa kuangalia katika matokeo na kuweka kwa kifupi nini Biblia inafundisha kuhusu  Barnabas.  Unapofanya hivyo, Fikiria maswali yafuatayo:

Ni nini historia ya nyuma aliyokuwa nayo Barnabas?

Kwa nini unafikiri kwamba mitume  walimpa Yusufu jina la utani  "Barnabas?"

Ni udhihirisho gani unaona kutoka katika mafungu haya mafupi kwamba Barnabas alikuwa mtia moyo?

Ni nini umuhimu wa utaratibu ambao Paulo na Barnabas (au Barnabas na Paulo umetajwa)

Jinsi gani Barnabas aliitikia kwenye mabadiliko kwenye uongozi kwa Paulo?

Jinsi gani aliitikia kwenye migogoro? **(Matendo 15:1-4 na Matendo 15:36-40)**

Kwa nini unafikiri aliitikia kama alivyofanya katika  **Gal 2:11-13**?

Na sasa andika maelezo kuweka kwa kifupi ulichojifunza kuhusu maisha ya Barnabas. Hakikisha kuwa inakuwa pamoja na mawazo yote ya ufunguo uliyoona katika kila moja ya vifungu vidogo.

**KUJIFUNZA BIBLIA**
***ZIADA***
**8A**

# Kujifunza Juu ya Maisha ya Barnabas

Tumia njia ya kujifunza Biblia kwa kufata neno unapofanyia kazi mafunzo ya historia ya maisha ya Barnabas. Unapokuwa na maswali juu ya utaratibu, rejea nyuma kwenye wazo namba 11. "Mafunzo ya Historia ya Maisha" ya njia za kujifunza Biblia somo la 8: "Njia Tofauti za Kutumia Kufanya Mafunzo ya Biblia kwa Kufata Neno."

**1. KUJIFUNZA VIFUNGU VINAVYOENDANA**

Mistari ambapo Barnabas ametajwa kwa jina imeorodheshwa  kwa ajili yako. Soma kila mstari au kifungu katika orodha ifuatayo, na andika uchunguzi wako. Kisha weka fungu kwa kifupi. La kwanza limefanywa kwa ajili yako.

A. Matendo 4:36,37
   1. *Uchunguzi:*

Alikuwa mlawi

Alitoka Kipro

Jina lake alilopewa ni Yusufu

Mitume walimpatia jina la “Barnabas”

Mwana wa kutia moyo

Aliuza ardhi yake kusaidia kufadhili kazi ya kanisa

Alitoa zawadi yake kwa utii (“chini ya miguu ya mitume”)

2. *Ufafanuzi/Ufupisho:*
Barnaba alikuwa ‘mtia moyo’ kwa asili yake—hata kwa kiasi cha kutoa mali yake kutia moyo na kuwezesha waumini wengine.
B. Matendo 11:19-24
1. *Uchunguzi*
2. *Ufafanuzii/ufupisho*

A. Matendo 11:25-26
1. *Uchunguzi*
2. *Ufafanuzi/Ufupisho*

B. Matendo 11:27-30
1. *Uchunguzi*
2. *Ufafanuzi/Ufupisho*

E. Matendo 12:25
1. *Uchunguzi*
2. *Ufafanuzii/Ufupisho*

F. Matendo 13:1-13; 42-43
1. *Uchunguzi*
2. *Ufafanuzi/Ufupisho*

G. Matendo
1. *Uchunguzi*
2. *Ufafanuzi/Ufupisho*

A. Matendo 15:2-4, 12, 22, 25, 35-39
1. *Uchunguzi*
2. *Ufafanuzii/Ufupisho*

B. Wakolosai 4:10
1. *Uchunguzi*
2. *Ufafanuzi/Ufupisho*

C. Wagalatia
1. *Uchunguzi*
2. *Ufafanuzi/Ufupisho*

**11. FUPISHA MAFUNDISHO**

Sasa umeshaangalia katika vifungu vya pekee, ni muda wa kuangalia katika matokeo na kuweka kwa kifupi kile Biblia inachofundisha juu ya Barnabas. Unapofanya hivyo, tafakari maswali haya:
Barnabas alikuwaje nyuma?

Kwa nini unafikiri kwamba mitume walimpatia Yusufu jina la utani la”Barnabas?”

Ni uthibitisho gani unauona kutoka katika vifungu hivi kwamba Barnabas alikuwa mfariji?

Ni nini maana ya agizo ambalo Paulo na Barnabas (au Barnabas na Paulo) wametaja?

Ni jinsi gani Barnabas alipokea badilikoa la uongozi kwa Paulo?

Ni jinsi gani alifanya wakati wa migogoro? (Mdo 15:1-4 na Mdo 15:36-40)

Kwa nini unafikiri kuwa aliitikia kama alivyofanya katika Wagalatia 2:11-13?

Sasa andika maelezo kufupisha ulichojifunza juu ya maisha ya Barnabas. Hakikisha yanakuwa na aina zote za mawazo uliyoyaona katika kila kifungu:

**111. AMUA NINI CHA KUFANYA JUU YAKE**
Kujifunza maandiko kuna thamani kidogo mpaka tunapoamua jinsi gani tunahitaji kuyatumia katika maisha yetu. Fikiri katika mafundisho ya maisha ya Barnabas unapoangalia maswali yafuatayo:

Umewahi kuwa na "akina Barinabas" katika maisha yako? Walikuwa akina nani na jinsi gani walivyokutia moyo?

Unamfahamu mkristo yeyote anayehitaji kutiwa moyo? Ufanye nini ili kumtia moyo?

Katika Mdo 9:26ff na 11:26-26, Barnabas alihatarisha sifa yake njema kwa kuwatia moyo wengine. Uko tayari kufanya sawa naye kwa ajili ya injili?

Barnabas alihamia pembeni na kumuruhusu Paulo kujitwalia nafasi ya kwanza katika uongozi. Uko tayari kuwafundisha viongozi wapya na kuwaruhusu kujitwalia uongozi hata kama ni lazima uchukue nafasi ya juu?

Ni somo gani hasa Bwana amekuwa akikufundisha ulipojifunza maisha ya Barnabas?

Kwa maombi fikiri jinsi gani Mungu angekufanya uishi tofauti kwa matokeo ya mafundisho haya. Katika nafasi chini, andika unachokusudia kufanya juu yake, na kisha muulize Mungu kukusaidia kwa uaminifu ukamilishe hilo.

# Nja za Kujifunza Biblia—Azimio la Mafunzo 9

## **Kuongoza Njia ya kujifunza Biblia Kwa Kufata Neno:** Kuongoza Wengine Kwenye Ugunduzi

**I. Tabia za Kundi la Kujifunza Biblia kwa Kufata Neno -**
**Kundi la kujifunza biblia kwa kufata neno ni kundi dogo la watu wanaokutana pamoja kwa kusudi la kujifunza Biblia. Jinsi gani Kundi la kujifunza Biblia kwa kufata neno lilivyo tofauti na mahubiri?**

Majibu: A. Muhubiri anaweza kuonwa kama mamlaka—kundi la kujifunza maandiko ndilo lenye mamlaka

B.Mafunzo ya kundi ya Biblia yanasisitiza lengo la ugunduzi

C. Kiongozi ni mwezeshaji

**II. Maandalizi ya Mafunzo** – Ni vitu gani kiongozi anaweza kufanya kuandaa mafunzo?

Jibu:

A. Jifunze fungu mwenyewe
B. Andika kusudi la kujifunza
C. Andaa maswali kwenye fungu ambayo yanafunika Sehemu zote hizi tatu za Njia ya Kutumia Neno
D. Fanya marudio ya maswali kuonyesha: uwazi, kueleweka, hitaji kutafiti fungu, maliza uchunguzi vema, maswali ya utekelezaji yanapelekea kwenye utendaji.
E. Andaa MaswaIi ya Kiutangulizi Kuwafanya Wajumbe Kuwa na Shauku Kuhusu kujifunza Biblia

**III. Kuongoza Mafunzo** – Ni baadhi ya yapi ya ufunguo ya kufikiria ili kuendesha mafunzo?

Majibu:

A. Mafunzo Yanatakiwa Yaanze kwa Maombi na Kumaliziwa kwa Maombi
B. Kiongozi Anatakiwa kuwa Tayari Kujifunza Kutoka kwenye Kundi
C. Kiongozi Anatakiwa asijibu Maswali yake Mwenyewe au maswali yanayoweza Kuibuka Kutoka Katika Kundi
D. Usiogopeshwe na Ukimya
E. Kiongozi Hatakiwa wakati Wote Kuridhishwa na Jibu la Kwanza Lililotolewa
F. Swali Ambalo halikujibiwa na Kundi Linaweza Kuachwa Bila Kujibiwa
G. Jibu Lisilo Sahihi au Jibu Sehemu Linatakiwa Lisahihishwe Kwa Maandiko na/au Kundi, Na Siyo Kiongozi
H. Tunza majadiliano Kwenye Kisa Kikuu cha Fungu
I. Usisahau Kuuliza Maswali ya Utekelezaji

J. Linda Kushiriki kwa Hao Wanaoongea Sana na Wanaozungumza Kidogo Sana
K. Mwishoni Mwa Mafunzo, Kiongozi Anaweza Kufupisha Kile Ambacho Kundi Limejifunza na Kuonyeshwa.

- Kwa nini ugunduzi ni muhimu kwa ukuaji wa kikristo? Kwa nini kuhubiri peke yake hakutoshi?
- Nini kitakuwemo katika maswali mazuri ya majadiliano?

## Utekelezaji wa Azimio

Kwenye somo linalofata (10,11), utawaoongoza baadhi ya wafunzwa kwenye mafunzo hayo kwa kutumia kanuni za somo hili. Chukua mda kufanya marudio mafunzo hayo, na fikiria jinsi utakavyoongoza majadiliano. Mshauri wako au mkufunzi anaweza kukusaidia katika maandalizi ya Mat. 20:17-28 or Luka 15:1-7.

MAFUNZO YA BIBLIA *ZIADA*

9A

# Mafunzo ya Biblia Kwa Kufata Neno Mathayo 20:17-28

*Tambua: Mafunzo haya yametolewa kama mtindo wa mafunzo ya Biblia kwa kufata neno. Ni muhimu kabisa, kama ni lazima kabisa , yanaweza kutumika kwa Warsha katika Somo la 10, 11. Kwa jinsi hiyo, inashauriwa sana kwamba hii inatumika tu kama mwongozo, na kwamba unafanya mafunzo yako mwenyewe katika moja ya kifungu kilichoagizwa katika Mwongozo wa kwanza.*

**UTANGULIZI**

Somo la uongozi katika kozi hii ya upandaji kanisa litakuwa linaangalia katika huduma ya Yesu kama kielelezo kwa uongozi. Kuna aina nyingi za 'uongozi' ulimwenguni, lakini Yesu alitoa tofauti kubwa ya kuelewa nini inamanisha kuwaongoza wengine. Kama tunavyoona katika Mathayo 20:17-28, hata wafuasi wake walikuwa na wakati mgumu wa kukabili matokeo ya aina hii mpya ya uongozi wa kikristo. Tunataka kujibu swali la: Nini maana ya uongozi wa kikristo?

**1. KUOMBA**

Anza mafunzo kwa kumwomba Mungu kuondoa vipingamizi vingine kutoka akilini mwako, na kukuruhusu kukazia juu ya kujifunza ukweli wa kifungu ili kwamba uwe kiongozi mkristo mzuri.

**11. SOMA MATHAYO 20:17-28**

Soma fungu kwa uangalifu na kwa kufikiri. Mtu mmoja anaweza kusoma lote, au unaweza kugawanya usomaji miongoni mwa wanakikundi

**111. UCHUNGUZI**

Kazi yetu ya kwanza ni kugundua kile Biblia inachosema. Angalia kwa karibu kwenye kifungu kisha jibu maswali yafuatayo"

*Kutoka kwenye mandhali ya (Mt 19:27-20:16)*

Ni kwa njia ipi inawezekana mafundisho ya Mathayo na Yohana yamechochea haja ya kutawala katika ufalme?

Ni nini kiini kikuu cha mfano wa Mathayo 20:1-15, Kama ilivyofupishwa na Yesu katika mstari wa 16?

Kutoka kwenye kifungu (Mt 20:17-28)

Ni wapi Yesu na wanafunzi walipokuwa wanakwenda, na nini kilikuwa kinakwenda kutokea pale?

Ni upendeleo gani mrs Zebedayo anaomwuliza Yesu?

Ni jinsi gani wanafunzi wengine walivyofanya kwenye ombi lake, na kwa nini?

Ni nani anaamua nani anakaa wapi kwenye ufalme, na nini kipimo cha mpangilio huu?

Ni kwa jinsi gani vipimo, hivi vinatofautiana kutoka kwenye utaratibu wa kidunia (mataifa)?

**1V. UFAFANUZI**

Na sasa tuko tayari kuangalia maana ya kifungu hiki. Fikiria kwa uangalifu juu ya maswali yafuatayo unaporejea nyuma kwenye uchunguzi wako:

Ni kwa jinsi gani unaweza kufupisha nia ya Mrs. Zebedayo na wanafunzi walipokwenda Yerusalemu? Ni nini walitarajia kuwa kingekuwa pale (fikiria juu ya maana ya ("mkono wa kulia na mkono wa kushoto"). Ni nini hii inadokeza juu ya sababu zao za kumfuata Yesu?

Ni nini Yesu alimaanisha kwa "kikombe?" (Tambua: tuna faida ya matokeo yake! ) Ni nini kilihusisha katika maisha ya Yesu na kwa jinsi gani baadaye kilitimizwa katika maisha ya mitume? Ni aina maalumu ya huduma, matendo, nia, au kitu kingine?

Ni SAWA kwangu kuwa na haja ya kuheshimiwa katika ufalme wa Mungu? Ilikuwa ni tatizo kwamba wanafunzi walitaka kuheshimiwa , au kwamba walitaka waheshimiwe sasa badala ya wakati Yesu atakaporudi?

Weka kwa kifupi katika sentensi au katika kiini kikuu cha mistari hii. Lielezee katika misingi ya kibiblia kama inawezekana. Liandike katika nafasi hapo chini.
Kanuni ya kifungu:

**V. MATUMIZI**

Sasa unahitaji kufikiri jinsi kanuni hii inavyoweza kutumika katika maisha yako na huduma yako leo. Fikiria kwa uangalifu juu ya maswali haya:

Ni nini mvuto wangu wa kumtumikia Kristo kama mpanda kanisa? Ni nini ninachotumaini kupata, na lini?

Kama haja yangu ni kumpendeza Kristo, ni jinsi gani uongozi wangu utofautiane na huo wa wengine wanaonizunguka? Ni nini hasa ninatakiwa kuwa nafanya ili kuongoza kama mtumishi na kutoa maisha yangu kwa hao Yesu aliowanunua?

**UFUPISHO**

Kama ulivyofanya kazi katika kifungu hiki, unatakiwa uwe umejibu maswali, "Ni nini maana ya uongozi wa kikristo?" Umefikiria pia kwamba hiyo ingekuwa na maana gani kwako mwenyewe katika maisha yako na huduma. Na sasa ni wakati wa kuanza kuomba kwa Mungu msaada wa kuishi maisha ya aina hiyo. Hasa kumuuliza kusaidia maeneo hayo ambayo sasa unaona kwamba una udhaifu au nia mbaya.

# Njia za Kujifunza Biblia—Azimio la Mafunzo 10,11

## Warsha Juu ya Kuongoza Mafunzo ya Biblia kwa Kufata Neno

(Panga somo hili kwa kipindi cha masaa mawili)

Kipindi hiki cha masaa mawili chote kimetolewa kuwaruhusu wafunzwa kufanya mazoezi ya kuongoza mafunzo ya Biblia kwa kufata neno, na kufanyia tathimini wanapofanya hivyo. Kazi yako kama mkufunzi ni kupanga makundi, na kisha kuyazungukia kati yao kusikiliza mawakilisho, na kuhakikisha wafunzwa wanafanya kazi ya haki na kamilifu na kufanyia kazi yote yaliyoorodheshwa baada ya kila moja. Watie moyo wafunzwa kuwa waaminifu, lakini wazi. Waulize wafunzwa kuandika orodha hapo chini na tathimini wengine kwa kujibu ndiyo au Hapana.

Orodha: Jina la Mfunzwa ____________________

| Maswali ya Kutathimini | Tathimini |
|---|---|
| 1. Mafunzo yamefata njia ya kujifunza kwa kufata neno—uchunguzi, ufafanuzi, na matumizi? | Ndiyo Hapana |
| 2. Maswali yalikuwa wazi na ya kueleweka? | Ndiyo Hapana |
| 3.Maswali yamekusaidia kuelewa fungu zaidi? | Ndiyo Hapana |
| 4. Kiongozi ameruhusu kikundi kujibu maswali, badala ya kujibu mwenyewe? | Ndiyo Hapana |
| 5. Kiongozi amechochea maswali yaliyoulizwa tena kwenye kikundi? | Ndiyo Hapana |
| 6. Kiongozi amerudia kusoma maswali yaliyo magumu kueleweka? | Ndiyo Hapana |
| 7. Kiongozi ameweza kuwasaidia wajumbe wote kuhusika katika majadiliano? | Ndiyo Hapana |
| 8. Kiongozi ameweza kufanya mtu yeyote asitawale majadiliano? | Ndiyo Hapana |
| 9. Kiongozi amefupisha mambo ambayo kikundi kimegundua kwenye mafunzo? | Ndiyo Hapana |
| 10. Kiongozi ameruhusu kikundi na maandiko kusahihisha jibu lolote lisilo sahihi? | Ndiyo Hapana |

| | |
|---|---|
| 11. Kiongozi ameweza kukamilisha mafunzo yote katika mda uliotolewa? | Ndiyo Hapana |
| 12. Kiongozi ameanza na kumaliza mafunzo kwa maombi? | Ndiyo Hapana |

Jinsi gani mafunzo haya yalikuwa tofauti kuliko mafunzo ya Biblia uliyohudhuria nyuma?

Njia hii ilikusaidia binafsi kujifunza? Unafikiri inaweza kuwa ya ufanisi kwa hao unaofundisha au kuongoza? Kwa nini na Kwa nini siyo?

**Utekelezaji wa Azimio**
Ni juu yako sasa kuchukua zana ulizonazo sasa, pamoja na tathimini kwa wafunzwa wengine wa uwezo wako wa kuongoza mafunzo, na yatumie kufanikisha ukuaji wako wa kiroho mwenyewe, na huduma yako.

# Uinjilisti—Azimio la Mafunzo 4

## Uinjilisti na Upandaji kanisa: Kukimbia mbio zote

**I. Hitaji la Njia Mpya –** Kwa nini njia mpya kwenye uinjilisti inahitajika?
**II. Mbio za Mashindano:** Jinsi gani uinjilisti na ufuasishaji ni kama mbio za mashindano?
**III. Kanuni kwenye Uinjilisti**

A. Tumia **Mitandao ya Kawaida**: Ni mitandao ipi ya mahusiano Yesu aliyotumia katika kuwaita wafuasi wake? **(Yohana 1:40-41, 4:28-30, Luka 8:38-39)**

B. Kwa Nini **Waumini Wapya Washuhudie Mara Moja?**
Kwa nini waumni wapya ndio wainjilisti wafanisi?
Majibu:
1. Imani yao ni "Moto moto."
2. Waumini wapya wanakuwa bado na marafiki wasio wakristo wanaoweza kuona mabadiliko

C. **Nenda kwa “walinda Mlango"** Nani ni walinda mlango? Kwa nini kuwaendea?
Jibu: Hao walio na mvuto mkubwa wanaweza kusogea kuelekea kwa Kristo pole pole zaidi, lakini mguso wao wa mda mrefu kwa injili unaweza kuwa mkubwa.
Kutoka katika maandiko haya, taja baadhi ya mifano ya "walinda mlango" **(Matendo 16:11-15, 17:1-9, 18:7)**

D. **Fikiria Mipaka ya Kiutamaduni** – Je watu wanavuka mipaka ya kiutamaduni? Kwa nini ni hivyo?
Jinsi gani unaweza kuweka kanisa kuwafaa watu unaojaribu kuwafikia? (**1 Kor 9:20-23)**

**E.** Tafuta ‘Kianzio cha kawaida’ **Ni nini baadhi ya shughuli ambazo ni za kawaida kwa waumini na wasio waumini?**

| |
|---|
| Kwenye darasa zaidi, tumia Ziada 4A kama zoezi. Soma kila hali na liulize darasa kuitathimini kwa misingi ya (kiasi cha mawasiliano ya mtu binafsi aliyonayo, (2) kutimiza hitaji lililopo la aliyepotea, (3) kutumia mitandao ya kawaida ya mawasiliano, (4) kukazania kwa watu wanaopokea, na (5)kutoa ufuatiliaji wa ufuasishaji: |

**Ziada 4A—Kutathimini Mkakati wa Uinjilisti**

Mkakati 1: Daudi na Lidia wanaishi katika mji wa watu 100, 000 pasipo na makanisa ya kiinjili. Wakiwa na haja ya kupanda kanisa, wanaanzisha mfunzo ya Biblia ya kiuinjilisti nyumbani kwao. Baada ya mwaka mmoja watu 15 wanahudhuria kwa uaminifu na wanavyoona 9 kati yao ni waumini. Wanatambua kuwa kwa watu 15 kikundi kinakuwa kikubwa kuweza kujisikia kila mmoja anahusika, wanaanzisha kikundi kingine kinachokutana katika usiku mwingine katika nyumba ya familia nyingine. Daudi anatumaini kwamba watakapokuwa na watu wa kutosha katika makundi haya, watakodi ukumbi na kuanza kuabudu kila jumapili kama kanisa.

Mkakati 2: Musa ana mpango mkubwa wa kupanda kanisa katika mji mkubwa. Musa amemaliza chuo cha Biblia hivi karibuni. Wakati akiwa chuoni Musa alifanya mawasiliano na kikundi moto moto cha kimisheni kilichojitoa kumsaidia katika mradi huo. Kwa pamoja, Musa na Wamarekani wanapanga kuanzisha mambo mwezi wa sita wakati wanafunzi 20 wa chuo cha Kiamerika watakapokuja kusaidia katika uinjilisti. Mpango ni kwa wiki watakayokuwa na wamarekani wakazane sana. Ukumbi utakodishwa na mkutano wa wazi pamoja na mziki, shuhuda, na kuwakilisha injili vitafanyika kila jioni. Wakati wa mchana Mmarekani

na Mrusi wataungana na mkarimani kuzungukia mji wote, wakitoa vijitabu vya maandishi na kwenda mlango kwa mlango kutangaza mkutano wa jioni. Musa anatarajia kuwa matokeo ya uinjilisti wa wiki hiyo watu wa kutosha watakuwa wameokoka tayari kufungua kanisa lake mara moja.

# Uinjilisti—Azimio la Mafunzo 5

**Vizuizi kwenye Uinjlisti wa Ufanisi:** Madaraja Badala ya Vizuizi

Chunguza **madaraja** yafuatayo **ya uinjilisti wa ufanisi.** Jinsi gani Yesu alishinda vizuizi vifuatavyo na mwanamke kisimani katika **Yohana 4?** (Mnaweza kutaka kujadili swali hili kwenye vikundi vidogo.)
**Vizuizi vya Nje: A. Vizuizi vya Kiutamaduni, B. Vizuizi vya Lugha, C. Vizuizi vya Kidini, D. Vizuizi vya Kiroho**
**Vizuizi vya Ndani: A. mapokeo, B. Kuhukumu, C. Hofu, Na D. Thamani**

Nini tunachoweza kufanya kupunguza kuchanganyikiwa na kuchanganywa wanakojisikia wasioamini wanapotembelea ushirika wetu au majumbani?

Ni aina ya vitu gani vinakufanya kutojisikia vizuri au ugumu katika hali isiyo ya kujulikana?

Ni vizuizi gani binafsi umekutana navyo ulipofikilia kufikia nje kwa injili? Umevishinda? Kama ndiyo, ni kwa njia zipi umevishinda?

Ni makundi yapi ni waathirika kihistoria kwa hukumu katika utamaduni wako? Ni nini Bwana angekuruhusu kufanya kugusia hiyo hukumu?

Ni mabadiliko yapi ya vitendo unayoweza kufanya kwa wiki zijazo kushinda vizuizi na kukuza uinjilisti wakowa ndani?

# Uinjilisti—Azimio la Mafunzo 6,7

## Utaratibu wa Kukata Shauri: Kuwasaidia watu Kusogea Kuelekea Imani Ndani ya Kristo

| |
|---|
| Kabla ya kuanza maelekezo yako, wafanye wafunzwa kurudia baadhi ya masomo waliyojifunza kwenye mafunzo yao ya mifano ya udongo katika Mathayo 13:3-9,18-23. |

**I. Kutathimini Watu Walipo Katika Kuelewa Kwao kwa Injili**

**Aina ya A ya wasioamini** wanaonyesha nia kwa Mungu kwa kiasi fulani, Biblia, na wako wazi na welekezo wa Mungu katika maisha yao. **Aina ya B ya wasioamini** ni hao wasio na haja ya Biblia, ambao hawatakwenda kanisani, pengine hata wasioamini katika Mungu, na wanaweza kiuwazi kuwa wapinzani au hata wakatili kwenye ujumbe wa injili.

Baadhi ya aina ya B ya wasioamini wanaweza hata wasiwe kwenye mchoro bado hapo chini, wakati wengine watakuwa tu kwenye moja ya ngazi kwenye hatua ya "mavuno". Aina ya A ya wasioamini, kwa jinsi hiyo, wanaweza kuwa katika moja yoyote ya ngazi kwenye hatua kabla ya "uvunaji."

Fikiria watu unaowaombea, ukitumia nao mda, na kuwashuhudia. Wapi unapoweza kuwaweka katika mchoro huu?

**Kielelezo 6.3 Hatua Kuelekea Kwenye Imani**

| HATUA ZA KUITIKIA |
|---|

Unapokuwa mzoefu wa mchoro huu, jiulize mwenyewe maswali yafuatayo :

| | |
|---|---|
| MAANDALIZI | **-12 KWENDA NJIA YAKE**<br><br>**-11 UFAHAMU WA KUWEPO KWA MJUMBE**<br><br>**-10 NIA YA MOYO MWEUPE KWA MJUMBE**<br><br>**-9 UFAHAMU WA TOFAUTI KATIKA MAISHA YA MJUMBE**<br><br>**-8 MWANZO WA KUFAHAMU KUHUSIANA KWA BIBLIA NA MAISHA** |
| KUPANDA | **-7 NIA YA MOYO MWEUPE KUHUSU BIBLIA**<br>**-6 UFAHAMU WA MISINGI YA INJILI**<br>**-5 KUELEWA MAANA YA INJILI NA MATOKE YAKE**<br>**-4 NIA YA MOYO MWEUPE KWENYE INJILI** |
| UVUNAJI | **-3 UTAMBUZI WA HITAJI LA MTU**<br><br>**-2 UAMZI WA KUTENDA**<br><br>**-1 KUTUBU NA IMANI**<br><br>**0 KIUMBE KIPYA NDANI YA YESU!** |
| UKUSANYIKAJI | **+1 HAKIKISHO LA IMANI NA UIMARISHAJI**<br>**+2 KUSHIRIKISHA KATIKA UANGALIZI WA JUMUIA YA WAKRISTO**<br>**+3 UKUZAJI! UHAMASISHAJI KUKOMAA KATIKA KUFANANA NA YESU**<br>**+4 KWENDA! UHAMASISHAJI "KUISHI KWA USHUHUDA" KWA WENGINE** |

Ni wapi watu ninaofanya nao kazi wanapofaa katika mchoro huu?

Ni katika hatua gani vifaa na zana zilizopo kwa ajili ya uinjilisti zinapoweza kutumika zaidi?

Ni katika hatua zipi kuna ukosefu wa hali ya juu wa vifaa vya kutumia kwa watu ninaofanya nao kazi?

**III. Kuelewa Hatua Nne za Shughuli Zinazohusiana na Kuwaleta watu kwa Kristo**

**Kielelezo 6.4 Awamu Nne za Shughuli Zinazohusiana na kuwaleta Watu Kwa Kristo**

| Shughuli | Uandaaji | Upandaji | Uvunaji | Ukusanyaji |
|---|---|---|---|---|
| **Maelezo** | Inazungumza kwenye moyo kupitia uhusiano wa kujaliana | Inazungumza kwenye akili kupitia maamzi na mawasiliano | Inazungumza kwenye utayari, ikihitaji majibu ya imani kwenye majadiliano | Inazungumza kwa mtu kamili kuhusu ukuaji binafsi ndani ya Kristo |
| **Msisitizo** | Kuwepo kwa Mjumbe | Kutangaza ukweli wa injili | Kushawishika kwenye uamzi | Kuhusika na kushiriki katika ushirika wa mtaa |
| **Mifano ya Kibiblia** | Yohana 3 & Yohana 4 | Yohana 4 na Matendo 8 | Yohana 4 na Matendo 16 | Matendo 2:40-47 na Matendo 8 |
| **Hatua Kuelekea Kwenye Imani** | -12 mpaka -8 | -7 mpaka -4 | -3 mpaka 0 | +1 mpaka +4 |

**IV. Kuonyesha Mkakati wa Kiuinjilisti**

Yafuatayo ni maelezo jinsi unavyoweza kuonyesha mkakati wako wa uinjilisti kutokana na habari ulizojifunza hapo juu

**A. Mahitaji ya Msingi**—Kimwili, ulinzi, upendo/kupendwa, mafanikio/kuhesabia, kujitosheleza/kujitambulisha

Maria ni mwanamke kijana kutoka kwenye familia ambayo wazazi wameachana. Mtoto pekee, alikataliwa na baba yake. Mama yake alikuwa na kazi nyingi kuweza kutoshereza familia na kuwa na mda kidogo sana wa kukaa na binti yake. Yeye na mama yake waliishi kwenye mji mbali na familia yao pana. Sasa kama mtu mzima anajisikia kutopendwa. Unachunguza hitaji lake la kupendwa/upendo. (Tazama Utawala wa Maslow wa Mahitaji Kielelezo 6.1).

**B. Upokeaji wa Injili**

Katika hatua zake kwenye imani (angalia Kielelezo 6.3), Maria yuko kwenye -12. Maria hakuwa na dini alipokuwa analelewa, hakuwa na mawasiliano na wakristo. Alikuwa na wazo lisilofahamika vizuri kwamba kanisa linadai kuwa sehemu inayomfaa, ingawa hajui chochote kuhusu madai ya Yesu Kristo. Jinsi gani hii inaweza kugusa uinjilistim wako?

**C. Tathimini ya Mkakati Wako wa Kiuinjilisti**

Maria hayuko tayari katika kupanda mbegu. Kwako wewe kumpatia vijitabu vya injili au pengine Biblia isingefaa kuwa ya ufanisi. Anachohitaji ni kuonyeshwa upendo wa Kristo kwa uvugu vugu, kukubali anga, hatua ya maandalizi katika kielelezo 6.4. Unaamua kumualika kwenye kikundi kidogo ambapo kuna kujaliana kwa aina nyingi kwa mmoja kwa mwingine. Kisha unaweza kumhusisha katika mafunzo ya kiuinjilisti.

Unapouangalia mkakati wako wa kuwafikia watu hao ambao Mungu ameshaweka kwenye moyo wako, unaweza pia ukaanza kuomba kwa ajili ya kuwafikia watu ambao, kama wamefikiwa kwa injili, wanaweza kuwa mkakati katika kufikia eneo lako unalolenga kwa injili.

Unakusudia kumkabili kila mtu ukitumia njia ile ile ya kiuinjilisti au zana? Jinsi gani unaweza kukuza utendaji wa kazi nyingi?

Unajua namna watu unaotaka kuwafikia wanavyofikiri ambako kunaweza kuwa tofauti na wewe?

Unajua utamaduni wao? Una tatizo katika kutoa maandalizi ambayo wanaweza kuridhika nayo?

Unamjua yeyote ambaye amekuwa mkataaji kwenye injili lakini sasa yuko kwenye misuko suko ambayo inaweza kumfanya kuwa mpokeaji?

**Ufupisho**

Uinjilisti wa Ufanisi Unahusisha…

- kuchukua hatua za mwanzoni, kwenye nguvu na upendo wa Roho Mtakatifu, kumsaidia mtu kusogea hatua moja karibia katika utaratibu wa uamzi kidogo kwa Kristo,
- kuwepo kutia moyo na kuwaelekeza katika kujua jinsi ya kufanya uamzi huo,
- kuwaombea kufikia sehemu ya toba kamili na imani katika Kristo na kukutana na wokovu katika Kristo kwa njia ya imani peke yake, na
- kuwaleta kikamilifu kwenye ushirika na huduma ya kanisa la mtaa.

## Yesu kama kielezo chetu

Kwa kila moja ya vifungu vifuatavyo, jibu maswali yafuatayo: **Yohana 3:1-21, Yaohana 4:5-26, Yohana 9:5-7, 35-39, Marko 10:17-22**
Ni kwa nani Yesu anazungumzia?
Ni nini tunachojua juu ya mtu huyu kutoka kwenye fungu hili?
Jinsi gani mazungumzo yalianza?
Ni katika mstari gani mwelekeo wa majadiliano yalibadilika?
Nini Yesu alichotaka?
Nini Kristo anachotoa?
Jinsi gani mtu binafsi anavyoitikia?

# Maazimio ya Mafunzo ya Omega Mwongozo wa Tatu

# Maono ya Kum – Azimio la Mafunzo 8

**Kuendelea kwa Kwanza**: Harakati za Upandaji kanisa katika Matendo

**I. Kuzaliwa kwa kanisa la Agano Jipya– Matendo 2:42-47**
Kanisa la kwanza la Israeli lilikuwa kama nini? Ni nini unachotamani zaidi kuhusu kanisa hili?

**II. Mateso katika Matendo 8:1; 11:19-26**
Jinsi gani mateso yaligusa kuenea kwa injili? Mateso yamepelekea upanukaji wa kanisa katika kizazi cha hivi karibuni?

**III. Safari ya Paulo ya Kimishenari**

**A.** safari ya Kwanza (Mdo 13-14) – Kupanuka kwenda Kipro na Galatia – Wapi Paulo na Barnabas walikwenda kwenye safari ya kwanza ya kimishenari (**Matendo 13:4, 13-14; 14:1, 6-7**)? Nini walichofanya **(Matendo 13:32-33, 42-49, 14:21-22)?**

**B.** Safari ya Pili **(Matendo 15:36-18:22) –** Kupanuka kwenda Masedonia na Akia – Wapi Paulo alipokwenda kwenye safari yake ya pili ya kimishenari na nini walichofanya **(Matendo 15:36, 15:41-16:2-5, 9-12; 17:1-4; 18:1-11,20-22)?**

C. Safari ya tatu **(Matendo 18:23-21:15)** – Kupanuka kwenda katika jimbo la Asia – Wapi Paulo alipokwenda katika safari ya tatu ya kimishenari na nini walichofanya **(Matendo 18:23; 19:17-22; 20:1-2,17-22)?**

Elezea mabadiliko katika msisitizo kati ya safari ya kwanza na ya tatu ya Paulo.

**IV. Baraza la Yerusalemu (Matendo 15)**
Kwa nini baraza la Yerusalemu lilikuwa muhimu hivyo?

V. Kanuni Nyuma ya Shughuli za Kimkakati za Kimishenari

**A. Kujitoa** kwenye uongozi wa Roho Mtakatifu

Je Roho Mtakatifu anazungumza wazi zaidi kwako wakati unafanya huduma au wakati unasubiri uelekezi?

**B.** Kusogea kwa Haraka **– Nini kinatakiwa kituelekeze kwa jinsi gani kwa haraka tunasogea katika kupanda makanisa mapya?**

C. **Kuwezesha wengine** katika huduma – Ni somo gani tunatakiwa tujifunze kutoka kwenye mda wa ziada Paulo aliotumia Korintho na Efeso

D. **Kuhubiri kwa watu Wanaoitikia** – Paulo aliwapata Mataifa wazuri waliokuwa wakimuogopa Mungu kwenye Sinagogi kuwa waitikiaji. Ni akina nani katika eneo lako wanaonekana zaidi kuwa waitikiaji kwenye injili?

E. Kufanya Kazi Kutokea Kwenye **Msingi wa Kimkakati** kwa Harakati za Kieneo
Jinsi gani **Matendo 19:10** inashauri kwetu njia ya kuufikia mkoa?

1. **Nini ilikuwa tabia za watu, jiji, na mkoa ambako Paulo alipanda makanisa?**
2. Ni maswali yapi ya utafiti Paulo anaweza kuwa aliulizwa alipochagua sehemu za kufanyia kazi?
3. Ni matukio yapi ya ufunguo ambayo yalipelekea kwenye harakati kuu za upandaji kanisa za karne ya kwanza?

# Maono ya KUM—Azimio la Mafunzo 9

## Asili ya Harakati za Upandaji Kanisa

**Mwamba Mugumu wa KUM ni Neno la Mungu.**

I. **Mapana ya Kimsingi** kwa Harakati za Upandaji Kanisa
Kwa nini kila moja ya chimbuko la misingi hii kwa upandaji kanisa—maono, kanisa na uongozi?

**II.** Matofali sita ya kujengea ya **Kueneza Harakati za Upandaji Kanisa**

A. Maombi**:** Kutangaza Utegemezi kwa Mungu
Harakati za maombi ni sehemu ya azimio lako la upandaji kanisa?

B. Utafiti (**Kuweka Ramani Kiroho):** Kuona picha Kubwa
Ni nini makusudi ya kuweka ramani kiroho kwa mkoa wako au mji?
Una azimio la kimkoa la kupanda makanisa katika miji inayozunguka?

**C. Kuhamasisha Rasilimali**
**Kwa nini ni lazima rasilimali za binadamu kwa ajili ya harakati za KUM zitoke katika nchi yenyewe?**
**Jinsi gani tunavyofanya kazi na mwili wa Kristo uliopo kabla ya upandaji kanisa?**

D. Kufundisha/kushauri: **Kuwaandaa wengine katika huduma**

| |
|---|
| Katika vikundi vidogo (kwa darasa la zaidi ya 9), jadili yafuatayo: |

Fikiria njia mbili za kawaida za kufunza viongozi. Zitathimini kwa misingi ya kanuni nne:

1. **Mafunzo Yanatakiwa Yakazie Kwenye Uongozi**

Mafunzo ambayo viongozi wanapokea yanatakiwa yawawezesha kuwaandaa wengine kwa ajili ya harakati zinzozalisha makanisa na kueneza injili kwenye eneo lote. Tambua katika Matendo 20:15-38 kwamba Paulo anawakumbusha viongozi wa efeso jinsi alivyofanya kazi nao wakati akiwafundisha uongozi. Kutoka Efeso, Paulo aliwaandaa waumini kuendesha harakati za kiroho ambazo zilifunika eneo lote.

Kitabu cha Matendo kinaonyesha Paulo akielezea jinsi alivyowafundisha viongozi na kumwambia Timotheo jinsi ya kuwachagua. Timotheo ya kwanza 3:1ff inaonyesha vitu vya lazima kwa mmoja kuwa kiongozi. Kwa mfano, tabia inachukua kipao mbele dhidi ya upendeleo (2Tim 3:2-10). Mafunzo ya uhusiano ya Paulo na Timotheo yalikuwa ya Baba na Mwana (2Tim 2:1).

2. **Mafunzo Yawe Yanayozaliana**

Harakati za uandaji kanisa zinahitaji mafunzo yanayoweza kuongezeka (i.e. yanayoweza kufundishwa tena kwa wengine). Mafunzo ya Paulo yaliendelea kwa vizazi vine. Yalianza na Paulo akipitisha mafunzo kutoka moyoni mwake (2Tim 2:2). Kisha Timotheo aliwafundisha watu waliokuwa "wakiweza

kuwafundisha wengine pia." Mafunzo na mafundisho tunayoyatoa tunapokuwa tunasaidia watu kukua ndani ya Kristo na kuandaa viongozi wapya yanapaswa yafanyike ili kwamba waweze kuyazalisha.

Mafunzo lazima yahusishe yote maneno ya mifano.

**3. Mafunzo Yanatakiwa Yapatikane**

Ni kazi ya makanisa ya mtaa kuwafunza wafanya kazi kukamilisha Utume Mkuu. Wakati, makanisa ya mtaa yanachukulia bila mzaha majukumu yao ya kufundisha wafanya kazi, kisha mafunzo yanapatikana kwa watu wengi.

**4. Mafunzo Yanatakiwa Yakue Kutokea Kwenye Msingi wa Kimkakati**

Wakati wa safari ya tatu ya Paulo ya kimishenari, alitumia karibu mda wake mwingi Efeso (Mdo 19:9-10). Alichagua mkakati wa kufanya kazi kuanzia kwenye msingi wa kimkakati kuwafundisha viongozi ambao wangeweza kulifikia eneo lote. Kutoka kwenye kipindi cha mafunzo ya Paulo, viongozi hawa walikwenda nje na kufikia jimbo la Asia kwa neno la Bwana.

Uinjilisti: **Shamba ni Nyeupe**

Ni wapi katika mkoa wako kufanya kazi kwa Mungu kunaonekana?

**Kutupa Maono**

Makanisa katika eneo hili yamekamata maono kwa ajili ya KUM?

Ni nini maono yako mwenyewe?

III. Matokeo: Harakati za Upandaji Kanisa

**Ni kwa umri gani na ukubwa kanisa liwe wakati linaanza kupanga kuanza kupanda kanisa mpya?**

Ni ipi kati ya vitu hapo juu vya harakati za upandaji kanisa vipo katika mkoa wako?

# Kanisa – Azimio la Mafunzo 9,10

## **Kanisa na Vipawa vya Kiroho:** Uwezeshaji wa Mungu Kwenye Huduma

(Panga somo hili kwa kipindi cha masaa mawili)

I. Kwa nini **Tunahitaji Vipawa Vya Kiroho ? (2 Kor. 10:3-4, Matendo 1:4-5, Efe. 4:12)**

II. **Vipawa vya Viongozi:** Vimetolewa na Yesu **Kuandaa Mwili**. **(Efe. 4:11-16)**

Jinsi gani vipawa vya uongozi vinatofautiana na vya ofisi?

**III.** Uwezo: **Vimetolewa na Roho Mtakatifu Kuuimarisha Mwili**

**A. Tafsiri**

- Kila muumini ana angalau kimoja (1Kor 12:7; 1Pet 4:10)
- Vinatolewa kwa kutaka kwa Roho badala ya kuhitaji kwetu wenyewe (1Kor 12:11)
- Vipo kwa ajili ya faida ya wote badala ya faida ya mmoja (1Kor 12:7; 12-27 Rum 12:4-5)
- Kipawa (vipawa) tulivyonavyo ni kazi ya Roho (1Kor 12:4).

**B. Vopawa vya Kiroho na Mwili wa Kristo**

1. Jinsi gani vipawa vinaendana na umuhimu wa kila mjumbe?
2. Ni nini Kazi ya watu "Waliojaliwa" kanisani?
3. Ni nini **1 Pet. 4:10-11** inachotuambia kuhusu vipawa katika kuhudumu neema ya Mungu?

Baadhi ya vipawa vinaheshimiwa zaidi na wajumbe hao hao wa kanisa kuliko wengine. Tutamani vipawa vinavyotamaniwa? Kwa nini na Kwa nini siyo?

**C. Kudhihirika kwa Kipawa (V) cha Mtu**

Kamwe Mungu anaonyesha neema yake kwa kufanya kazi kinguvu kupitia mtu kwenye eneo mbali na hilo ambalo mtu amejaliwa?

Jinsi gani tunajua kwamba tuna kipawa?

**D. Maelezo ya Vipawa vya Kiroho (Rum. 12:6-8, 1 Kor. 12:4-31;14:1-5)**

**IV. Vipingamizi vya Kugundua Vipawa vya Kiroho**

A. sababu za mtu – Ni sababu zipi kwamba waumini hawagundui vipawa vyao na kuvitumia?

**B. Matatizo ya Kichama**

Ni kwa baadhi ya njia zipi makanisa yanatenda ambako kunarudisha nyuma ugunduzi na matumizi ya vipawa?

**V. Kuhamasisha Kanisa kufuatana na Kujaliwa Vipawa**

A. Jinsi Gani Kanisa Linaweza Kusaidia Wengine Kugundua na Kutumia Vipawa Vyao?

**1 Tim. 3:6** inaonya kushika ofisi kwa waumini wapya. Ni nini hatari katika hili?

Baadhi ya ofisi ni za hatari kuliko zingine?

**VI. Vipawa vya Kiroho na Upandaji Kanisa**

Ni vipawa vipi ni muhimu zaidi kwa mpanda kanisa? Kwa nini?

## Utekelezaji wa Azimio

- Tafsiri hitaji ambalo unaamini Mungu anataka kundi lako litimize. Orodhesha nafasi za huduma ambazo Mungu ameonyesha kwenye kikundi.
- Uwe na mda wa kujitoa kwa Bwana ukimuuliza kukuwezesha na kutoa vipawa vinavyohitajika kutimiza mahitaji mliyonayo. Usikazanie kwenye vipawa isipokuwa kwa mtoaji wa vipawa.
- Ruhusu kila mtu kuanza kutimiza mahitaji wanayojisikia kuwa tayari kuyatimiza. Tia mkazo na msisitizo kwenye kutimiza mahitaji badala ya kwenye kipawa.
- Wafundishe watu kulingana na kipawa cha huduma wanachojisikia kuwa tayari kutumia katika kutimiza mahitaji.
- Ruhusu wengine kutathimini na kushauri kwa uthibitisho wa vipawa ulivyokuwa ukitumia.

# Kanisa—Azimio la mafunzo 11

## Nguvu ya Kijamii ya Kanisa: Jinsi Gani Utamaduni Wetu Unaathiri Kanisa

| |
|---|
| Mkufunzi: Uwe mwangalifu ili kwamba usishambulie imani au wanayofanya waumini wenzake. |

**I. Kanuni za Kibiblia**

**A. Kutunza Uwiano.** Ni nini swala la kuwianisha kiutamaduni **Matendo 14:11-18 na 1 Kor. 9:19-23?**

Ni nini baadhi ya dalili za kiutamaduni katika nchi yako au eneo? Vilitoka wapi? Vimetokana na historia, dini, siasa, tabia ya nchi, aina ya maisha au kitu kingine?
Jinsi gani muumini atofautishe kati ya kitu fulani ambacho ni dhambi na kitu fulani ambacho kinapingana na utamaduni wake wa kidini?

**B. Mfumo na kazi – Jinsi gani tunaweza kurithi mifumo ya kanisa letu kwenye utamaduni bila kuangukia dhambini?**

**II. kanisa la Agano Jipya na Utamaduni**

A. Kanisa la Yerusalemu – wapi wakati mwingine walipoomba (**Matendo 2:46, 3:1)?** Wapi walipokutana kwa ajili ya kuabudu na meza ya Bwana **(Matendo 2:46)?** Ni watu gani wawili aliotumia Mungu kusogeza kanisa kupita Yerusalemu? Ni ofisi gani zilianzishwa kuhudumia kanisa (**Matendo 6:1-7)?**

B. Kanisa Miongoni Mwa Mataifa—Ni kwa njia zipi kanisa lilibadilika wakati wa karne ya kwanza—katika njia ambazo watu walifikiwa (**Matendo 8:1),** katika tabia kuelekea kwa mataifa (iliyoonyeshwa katika halmashauri ya Yerusalemu (**Matendo 15:1-21**), na katika ofisi za kanisa (**1 Tim 3:1-11, Tit. 1:5)?**

**III. Kutoka Agano Jipya Mpaka Sasa**

A. Maendeleo ya Kanisa la Kifalme – Constantine aliufanya ukristo kuwa kanisa la Kifalme. Mabadiliko kama vile msisitizo juu ya mifumo na kufahamika kwa kidini kulikohudumu kurudisha nyuma imani.

Kanisa katika nchi yako limeguswa zaidi na mateso ya kiserikali au kwa kukumbatia serikali, kustawisha na kudhoofisha kanisa, la ama ni kweli?

**B. Mgawanyiko wa Magharibi-Mashariki**

Imani ya Waothodox ilipotoshwa kwa uzuri na utajiri. Ni nini kinalishawishi kanisa katika utamaduni wako?

C. Matengenezo ya Protestanti – Kwa wanamageuzi kama Martin Luther, mfumo ulikuwa na maana kidogo kuliko kazi. Mabishano yametokea katika makanisa katika nchi yako juu ya mifumo? Juu ya kazi?

IV. **Utamaduni wa Wakati Huo na Kanisa**

A. Tunakataa kubadilisha mifumo utamaduni unapobadilika, tukipoteza nafasi nyingi kwa ajili ya uinjilisti?

B. Tunawatarajia wasioamini kujigeuza kwenye utamaduni wa kanisa letu?

Jinsi gani tunaweza kutofautisha mfumo kutoka kwenye kazi tunapofikiria miguso ya kiutamaduni?

Baadhi ya yaliyofanyika katika Kanisa la Agano Jipya (Kama vile kanisa la Yerusalemu) kwa utamaduni wao tu na mda, na siyo kwa utamaduni wako na nchi? Kama ndiyo, ni nini baadhi ya mifano?

Kuna mifumo yoyote katika kanisa lako ambayo inaweza kuwa kizuizi kwenye upandaji kanisa mpya?

# Tabia ya Kiroho – Azimio la Mafunzo 8,9

## **Sheria na Injili:** Maisha katika Roho

(panga somo hili kwa kipindi cha masaa mawili)

Hili ni somo la masaa mawili, mengi ya mawazo katika somo hili yanatoka katika Warumi 7:1-13, Wagalatia 3:1-5 na 3:19-26. Katika kufanya maandilizi ya kufundisha kipindi hiki, uwe na uhakika wa kushukuru vifungu hivi.

**I. Kusudi la Mungu kwenye Sheria**

A. Jinsi gani sheria inaonyesha utakatifu wa Mungu (**Kutoka 21:15-17, 22:20)?**

B. Ni nini sheria inaonyesha kuhusu sisi (**Rum. 7:7)?** Jib: Dhambi zetu.

C. Ni nini sheria inatuonyesha kwamba tunahitaji (**Gal. 3:24**)? Jib: Sheria inatuonyesha hitaji letu kwa Kristo.

1. Jinsi gani zana katika somo hili juu ya sheria linaendana na --ya EvangeCube?
2. Katika hali yake ya anguko, mtu amepotoka (bila mfumo wowote wa utakatifu). Kwa sababu ya upendo wa Mungu na utakatifu, utakaso wa dhambi unahitajika kwa ajili ya msamaha. Jinsi gani Mungu ametoa kwenye utakaso huu kwa mtu?
3. Kama Mungu hangekuwa mzuri kabisa na mtakatifu, nini kingekuwa matokeo kwenye thamani yetu ya maisha duniani?
4. Ni nini kusudi la sheria katika maisha ya mkristo?

**II. Upungufu wa Sheria**-Ni upungufu gani wa sheria umeonyeshwa kwenye mistari ifuatayo?

**A. sheria haishughuliki na Moyo, lakini utakatifu kimsingi ni swala la moyo** (Mat. 22:37-38).

B. Sheria inazaa hatia na inaweza kuwalemeza watu chini **(Gal. 3:10).**

C. sheria inazaa kiburi **(Rum 2:23).**

III. Kuishi kwa sheria -- kuhalalisha

Katika vikundi vidogo, jadili maswali haya.

1. Mkristo kamwe anakua kwa kufanya vema awezavyo kwa uwezo wake mwenyewe kutii sheria kuwasaidia wengine, kuhudhuria kanisa, au kuomba mara kwa mara? Elezea jibu lako.
2. Nini kinatokea kwetu tunapojaribu kupata upendeleo wa Mungu kwa kufanya aina ya vitu hivi
3. Jinsi gani hatia na kiburi vinaendana? Jinsi gani vinaepukwa?

**IV. Roho Anatuweka Huru Mbali na Sheria**

1. Ni nini tofauti kati ya Yesu kukamilisha sheria na kuitangua?
2. Kwa nini ni kwamba sheria haituhukumu tena?

3. Jinsi gani imani katika injili ya kifo cha Kristo kwetu inatuwezesha kuishi katika upya wa Roho?

**V. Maisha katika Roho na Imani katika Injili**

Ukuaji wa Binafsi katika Roho. Ni nini Yesu anachosema lazima tufanye kufanya kazi anazohitaji Mungu (**Yohana 6:28-29)?** Je haki inatokana na sheria au Roho **(Rum. 8:1-4)?**

**Roho Anatuongoza katika Huduma. Bado Mungu anawaitia watu kwenye huduma kama alivyomfanya Paulo** (Flp 3:14)?

1. Jadili ambacho **Efe. 1:13; Gal. 4:6 and Rum. 8:14** inatuambia kuhusu nguvu inayofungua ya injli na ukaaji wa Roho Mtakatifu.
2. Njia ya kujua kama tunatembea katika Roho ni kutambua jinsi tunavyoitikia kwenye dhambi zetu? Toa mifano ya jinsi watu wanavyoitikia kwenye dhambi na jadili nini hii inatuambia kuhusu maisha yao.
3. Tunapotafuta badiliko (kwa ajili ya uzuri) katika maisha ya hao tunaowahudumu, kuna maswali matatu muhimu ambayo lazima tujiulize wenyewe. Jibu maswali haya matatu:
   - A. Ni nini LENGO la huduma kwa wengine?
   - B. Ni MTINDO UPI WA HUDUMA nitakaotumia kufikia lengo hili – uhalalishaji au Roho?
   - **C.** Jinsi gani binafsi NIELELEZE badiliko ninalobadilika? **(1 Pet 5:3)**

Je mahubiri yako na ushauri kwa wengine kawaida unakazia juu ya sheria, kwa sababu unafikiri kwamba inawaimarisha kubadilika?

Kwa nini sheria haina nguvu kuzalisha utakatifu ndani yetu?

Jinsi gani imani katika injili inatuwezesha kuishi katika upya wa Roho?

Ni nini kuhalisha? Unafikiri kwamba ni kukataliwa kwa uwezo wa injili na kuweka tumaini katika sheria? Kwa nini na Kwa nini siyo?

# Tabia ya Kiroho—Azimio la mafunzo 10

## Toba Kama Njia ya Maisha

**Kisa: Mit**. 6:23, Zaburi 51

I. Tabia za Toba ya Kweli

Ni nini Toba ya Kweli?

- **A. Tambua Dhambi Yako** – Ni nini tabia ya Daudi katika Zab**. 51:3** siyo kama hiyo ya **Zab. 32:3?**
- B. Fahamu "**Udhambi wa Dhambi**" –Unafikiri **Zab. 51:4** inadhihirisha kufahamu udhambi wake? Kwa nini?
- C. **Uvunjike Moyo** Juu ya Dhambi – Ni nini **Zab. 51:17** inachotuambia kuhusu kuvunjika?
- D. Hatari **ya kutojali na kitubio** (kitubio ni pamoja na kuomboleza mda mrefu, kujiadhibu, kujaribu kujitakasa, na njia nyingine za kujaribu kumfanya Mungu kukubali) – Unakubali kuwa kitubio ni kushindwa kukubali kwa unyenyekevu hitaji letu la kweli la neema ya Mungu?
  1. Umewahi kutekwa na dhambi inayojirudia lakini hukuitambua kama dhambi?
  2. Ni nini kilitokea kilichokufanya kuifahamu?
  3. Tunajua kuwa hasira inaweza wakati wote isiwe dhambi **(Efe. 4:26)**. Mchungaji mara alisema kwamba mara kwa mara anapatwa na hasira na kuendelea kuomba kwa ajili ya kujilinda. Anatakiwa aombe kwa ajili ya kujilinda au kwa ajili ya hasira?
  4. Umewahi kufikia sehemu ya kuvunjika na kutubu mbele za Mungu? Ilifatiwa na hisia kuu za upendo na furaha?
  5. Tunatakiwa tutafute njia za kuteseka ambazo zitalipia dhambi zetu?

**II. Toba ya Kweli Kama Njia ya Maisha**

- A. Baba anasubiri kutusamehe – (**Rum 8:1)** Unakubaliana kwamba Mungu anataka kusamehe?
- B. Toba ni kukubali kwa ukweli wa tatizo letu hasa – Nini kinaleta dhambi kwenye ufahamu wako?
- C. Mungu amejitoa kufanya kazi ndani yetu– Nini unachosema kwa Mungu unapotambua ukweli wa **Zab. 139:23-24**? Je Mungu anatuthibitishia dhambi leo kama Daudi alivyomuomba kufanya? Elezea.

**III. Baraka za Toba ya Kweli**

Ni nini baraka za toba ya kweli zilizogundulika katika **Zaburi 51:1, 2:8-12**?

Katika makundi madogo, jadili maswali yafuatayo.

1. Baadhi wanaamini kwamba tunamtarajia Mungu kutusahau tu kama baba zetu wa kidunia walikuwa wenye upendo na wenye kutusamehe. Unakubaliana? Unamfikiria Mungu kama hakimu mkari au mwenye rehema, Baba mtoaji?
2. Unafikiri waumini wako kwenye hatari ya kuchukua mtazamo sawa kama wasio waumini kuelekea dhambi?
3. Je kufundisha neema na uhuru kunatia moyo maisha ya purukushani ya kikristo? Kwa nini?

# Maombi—Azimio la Mafunzo 5

## Maombi na Kufunga

I. Asili Muhimu ya Maombi

Anajua mambo yote. Mungu pia anaweza yote: anaweza kufanya mambo yote. Kwa nini kisha tunatakiwa tuombe? Kama kitu fulani ni mapenzi ya Mungu, hawezi tu kufanya? Je maombi yanamuhusisha Mungu katika namna kwamba kama hatuombi, hilo kwa namna fulani inamzuia Mungu mwenye nguvu zote kutokufanya kazi?

A. **Mifano ya Agano la Kale—Ni nini mistari hii inatuambia kuhusu maombi? (**Kutoka 3:7, 32:7-14, 2 Nya. 7)

B. Mifano ya Agano Jipya – Ni nini mistari hii inatuambia juu ya maombi? (**Yakobo 5:13-18, Luka 6:12-16, Mat 6:5-8, 7:7-12**

Kutoka katika mifano hii, unafikiri kwamba Mungu wakati mwingine anaahirisha kazi yake mpaka watu Wake wanapokuwa wameomba?

Mungu anachagua kujiunga mwenyewe na kazi Yake kwenye maombi yetu?

Unafikiri ni kwa nini anafanya hili?

Inamaanisha nini kwamba "Mungu anasubiri watu kuomba?"

Ni nini ulichojifunza kuhusu asili ya maombi? Toa mifano.

II. Jukumu la Kufunga

Unaweza kufikiria mstari wa maandiko ambao tumeamriwa kufunga?

A. **Mafundisho ya Kristo – Ni nini Yesu alisisitizia katika mistari hii** (Mat 4:2, 6:16-17)?

B. Mifano ya Kanisa la Kwanza–Nini waliyofanya kanisa la kwanza **(Matendo 13:1-3,14:23)?**

C. **Aasili na Kufunga**

Katika makundi madogo, jadili maswali yafuatayo:

1. **Ni nini Marko 2:18-19 inamaanisha kwako kuhusiana na endapo au la hutakiwi kufunga?**
2. **Nini unachofikiri kuwa asili muhimu ya kufunga?**
3. **Ni vitu gani unafikiri unatakiwa kuepuka unapofunga?**

### Utekelezaji wa Azimio

### Soma Mathayo 6:16-18.

Elezea jinsi "unafiki" ulivyoonekana walipofunga. Kwa nini walifanya hilo?

Elezea jinsi mtu anavyotakiwa aonekane anapofunga

Jinsi gani tunaweza kutunza ufungaji wetu kutokuwa kawaida za dini?

Panga na kutana na malezi ya kiroho ya kufunga. Chini kuna njia kidogo ambazo baadhi ya wakristo wanafanya hili.

Unaweza kuamua kufata moja ya hizi, lakini mfumo ni juu yako.

Acha badhi ya vyakula na kunywa kwa mda maalumu

Acha vyakula vyote lakini kunywa maji ya matunda na baadhi ya vinywaji kwa mda maalumu.

Acha baadhi ya vyakula lakini si vyakula vyote.Tenga siku moja kwa juma /mwezi ambayo utafunga.

Fanya orodha ya vitu maalumu ambavyo utaombea wakati unafunga.

Andika katika kitabu chako cha kumbukumbu za kiroho ulivyoona wakati wa kufunga kwako. Ulijisikiaje? Nini ulichojifunza juu yako? Juu ya Mungu?

# Maombi—Azimio la Mafunzo 6,7

## Kongamano la Maombi

(Panga somo hili kuwa la kipindi cha masaa mawili)

Waongoze wafunzwa katika kuomba kwa maombi ya Paulo katika Wakolosai 1:3-14, ukitunza mda wa mafunzo kwa kifupi ili kwamba mda mwingi utumike katika kuomba.
Inashauriwa kwamba wafunzwa wawaombee wafunzwa wapanda kanisa wengine katika nchi zingine wanaopitia katika mafundisho ya aina moja.

**I. Mshukuru Baba – Wakolosai 1:3-5**

A. Mshukuru Baba kwa watakatifu.
B. Mshukuru baba kwa upendo, imani, tumaini na injili.

Baada ya kujadili sehemu hapo juu darasani, waulize darasa kuunda makundi na kutoa shukurani kwa baba katika maombi ya kundi (dakika 10)

**II. Omba kwa ajili ya injli kusikika ulimwenguni kote? Wakolosao 1:6-7**

A. Omba kwa ajili ya matunda katika maisha ya watu uliowashuhudia, katika makanisa yaliyopandwa na wengine, katika huduma za wamishenari unaowajua, na kwamba Mungu ataita watumishi zaidi waaminifu kuchukua injili mpaka miisho ya dunia.

Baada ya kujadiliana sehemu ya II darasani, waulize darasa kuunda makundi na kuomba kwa ajili ya injili kusikiwa ulimwenguni kote. Unaweza ukawaomba wajumbe wa darasa kutafuta watu wapya wa kuombea (dakika 29)

III. Omba kwamba Mungu atakujaza kwa ufahamu wa mapenzi yake. Wakolosai **1:9-11**

A. Katika karatasi yako, orodhesha sababu ambazo Paulo aliomba kwamba waweze kujazwa kwa ufahamu wa mapenzi ya Mungu katika hekima yote ya kiroho na kuelewa. Nini yalikuwa matokeo yaliyodhamiriwa. Kwa mfano, "Kwamba waumini waweze kuishi maisha yaliyojawa na Bwana.
B. Kwa kutumia orodha hii, ombea mambo haya kwa wanafunzi wenzio wapanda kanisa katika mafunzo haya.

Toa mda kwa wajumbe wa darasa kufanya zoezi kipekee. (Dakika 20)

IV. Toa shukurani kwa Baba. **Wakolosa**i **1:12-14**

A. Mshukuru Baba kukuleta katika ufalme wake, kwamba huishi tena chini ya kifungo cha Shetani, kwamba umekombolewa, kwamba dhambi zako zimesamehewa, na kwamba unamwita "Aba" yaani Baba."

Baada ya kujadili sehemu ya IV darasani, waulize darasa kuunda makundi na kutoa shukurani na heshima kwa Baba. Unaweza kuwaomba wajumbe wa darasa kutafuta watu wapya wa kuombea (Dakika 20)

# Uongozi – Azimio la Mafunzo 3

## Mzunguko wa Uongozi

**I. Mifano ya Yesu**

**Katika makundi madogo, jadili mafundisho na tabia ya Yesu kwa kila mmoja wa hao alioongoza: wale 3, wale 12, wale 70 na umati. Jadili jinsi alivyoeleleza uongozi wa ufanisi. Ni kweli kwamba**

**alikuwa kiongozi mkuu wa nyakati zote? Mlinganishe Yesu kama kiongozi na viongozi wengine wakuu (Dakika 20).**

**II. Mzunguko wa Upandaji Kanisa wa Uongozi**

Katika mzunguko wa upandaji kanisa ni watu gani wapanda kanisa wanaowaongoza? Ni yupi anatakiwa atumie mda mwingi naye? Kwa nini? Anatakiwa afanye kazi na watu hawa wote au wale tu wanaoonekana kufikia wakati huo kuwa maarufu zaidi? Wengine wanakua ili kwamba waweze kuwa viongozi wanafunzi kama kiongozi mwanafunzi wa wakati huo ametolewa kwenye huduma? Kama anatoa mda wake mwingi kwa viongozi waliopo, nani atahudumu kwa wengine ili kwamba wasiachwe? **(Efe 4:11-12)**

**III. Mzunguko Wako wa Uongozi**

Wachukue darasa katika mazoezi yafuatayo:

Ni akina nani ni watu unaowaongoza katika mzunguko wako mwenyewe wa uongozi? Ni kazi zipi kwa sasa hazitoshelezwi? Andika majina yao na wanachofanya.

- Kama huna timu ya upandaji kanisa ya 'kawaida', pengine una moja 'isiyo ya kawaida'. Kuna kundi dogo la waliojitoa unaofanya nao kazi kwa karibu mkiwa na lengo la upandaji kanisa mpya? Wanafanya kama timu yako, hata kama siyo 'kiofisi.' Lakini unapowaongoza ukitumia kanuni katika nyenzo hii, unaweza ukataka kujadili uwezekano wa kuunda timu iliyoshikamana hivi karibuni.
- Wakati mwingine unatakiwa uanze kazi mwenyewe, kama vile katika eneo mpya pasipokuwa hata mmoja anayeamini. Kama hii ni hali yako, unaweza kufaa kwenye mzunguko wa nje, lakini unatakiwa kuanza kupanga sasa jinsi utakavyofundisha waumini wapya na kuwasogeza kwenye hatua mapema iwezekanavyo. Hali yako ni mbali kutoka halisi, na inatia mashaka kwamba utafanikiwa sana katika upandaji kanisa mpya labda kama unaweza kuanza kutafuta watu kwa ajili ya mzunguko wa ndani.
- Kama una mashaka kuwa watu wangekuwa kwenye mzunguko wa 'juu', andika majina yao ambayo yanatengwa na mistari mingine. Hii itakukumbusha kutumia mda wa maana kuwatathimini watu hawa, na kuanzisha shughuli za kujifunzia kuona kama kweli ni waminifu.
- Usiwe na wasiwasi kuwa na watu wengi kwenye mzunguko wa ndani. Yesu aliweza kukazia wafuasi watatu tu—Petro, Yakobo na Yohana. Usiwe na mahangaiko kama huwezi kukamilisha zaidi kuliko Bwana. Kuwa na mwanafunzi kiongozi ni bora kuliko kutokuwa na hata mmoja. Na ni vizuri zaidi kuwa na mmoja tu na kumfundisha, kuliko kufundisha kadhaa kidhaifu.
- Kama huwezi ukafikiria hata mmoja ambaye anaweza kuwa katika mzunguko wa ndani, unatakiwa kuanza bila mzaha, maalumu, kwa mkazo kuomba kwamba Mungu atatoa viongozi kutoka ndani ya kanisa mpya.

Na sasa kwamba umejaza mzunguko wako, fikiria jinsi unavyotumia mda wako na nguvu. Kama una watu katika kila ngazi, unatakiwa uwe unakazania mda wako karibu na katikati. Unafanya hivyo? Ni mda gani mwingine zaidi unaotumia na hao walio kwenye mzunguko wa ndani kuliko wa nje? Ni aina gani ya shughuli unayofanya nao? Unaendeleza uongozi kwa uangalifu na ujuzi wa huduma kwao?

Kwa kudhani kwamba unatumia mda wa kutosha na viongozi mashuhuri, mzunguko wa nje umeachwa? Hutakuwa na mda wa kutosha na nguvu kuwahudumia peke yako na bado uwaendeleze viongozi. Ni lazima kwamba unajifunza kugawa huduma kwa hao wanaofanya kazi nawe. Unatakiwa kuwa mwandaaji na mtu wa chanzo kwa hao wanaofanya huduma hiyo. Jinsi gani unafanya katika hilo?

**Utekelezaji wa Azimio**

Tumia kielelezo chako 3.3 kilichomalizika kuanzisha mpango kuwasaidia hao katika kila mzunguko kuendelea kama viongozi. Kisha kiujuzi tathimini mpango wako kuona kama inawezekana kwako kuuweka. Utakuwa na mda wa kutosha kutumia mzunguko wa 'ndani'? Kiasi gani? Mwingine atahudumia kwenye mzunguko wa 'nje'? nani? Lini? Jinsi gani? Fanya marekebisho yoyote yanayohitajika kwenye mpango wako, na kisha ujadili na mshauri wako. Kisha fanya.

# Uongozi – Azimio la Mafunzo 4

## **Utangulizi Kwenye Kazi ya Timu:** Kufanya kazi na Wengine

**I. Ni nini kazi ya Timu?**

Fanya darasa kujibu swali hili.

Kuna tabia kadhaa za kawaida kwa yote kufanya kazi kwa kawaida na kusiko kwa kawaida kwa timu:

- Maono ya huduma (lengo) yanaonyeshwa na kundi.
- Kundi linafanya maamzi.
- Matatizo yanamilikiwa na kundi.
- Wajumbe wa kundi wanawajibika kwa pamoja kwa mmoja kwa mwingine.
- Kila mjumbe anatumia uwezo wake kuchangia kwenye mafanikio ya ukamilishaji wa kazi.
- Mmojawapo anatambulika kama 'kiongozi'
- Kundi linakamilisha zaidi kuliko mtu pekee ambavyo angefanya peke yake

**II. Misingi ya Kiblia kwa Kazi ya Timu**

A. Unakubaliana na maelezo haya, "Tuliumbwa Kuwa Pamoja?" **(Wim. 4:9-12)**

B. Viongozi Wanatakiwa Wasifanye Kazi Peke Yao –Nini kilimtokea Musa baada ya kufanya kazi peke yake kwa mda? (**Kut. 17:4, Hes 11:10-14)** Kwa nini?

**C.** Kufanya Kazi Pamoja Ilikuwa Kipande cha Kawaida kwa Huduma ya Agano Jipya? Tambua Mifano **Lk 10:1, Matendo 10:23, 13:2, 14:23, 15:36-41)**

Jadili swali hapo chini katika makundi (Dakika 20)

**1.** Ni nini unachofikiri kuwa kidhihirisdho cha kibiblia kizuri kwa matumizi ya kufanya kazi kwa timu? (Wiml. 4:9-12; Kut. 17:4; Hes. 11:10-17; Kut. 18:17-26; Luka 10:1; Matendo 10:23; 13:2; 15:41)

**III. Tabia za Kufanya Kazi kwa Timu kwa Ufanisi**

**A. Maono ya Pamoja na Kuielewa Kazi—**Mifano(1) Timu yetu ipo kupanda kanisa hai, linalozaliana katika___________. (2) Tunafanya kazi pamoja kuwezesha kuzaliwa na maendeleo ya harakati za kueneza upandaji kanisa katika____________.

1. Andika lengo lenye maana ambalo timu yako ya upandaji kanisa linaweza kuanzisha.

B. Mda uliotumika pamoja kwa maombi na upangaji

C. Mahusiano Yenye tabia ya Upendo

D. Majukumu wazi na Yanayotofautiana

Kwa mfano, kundi linalopanda kanisa mpya pamoja linaweza kuhitaji watu wanaowajibika kwa yafuatayo:

- Uinjlisti
- Ufuasishaji
- Kuabudu
- Hazina/Majengo
- Kuwafanya wajumbe wapya kitu komoja
- Huduma ya Kikundi Kiini
- Mafunzo ya Huduma
- Kutunza Wagonjwa
- Ukarimu

Tambua majukumu mawili unayojisikia kuyaweza zaidi kuyafanya. Hii ina maana gani kwa misingi ya kufanya kazi na wengine? Ni jukumu lipi unalifikiria kuwa muhimu zaidi katika kuanzisha kanisa mpya? Kuna jukumu lolote lisilo muhimu?

E. Mawasiliano ya kiukweli na kiuwazi kati ya wajumbe

**Maswali ya kutafakari, marudio na matumizi**

- Ni faida gani zipo kwa wapanda kanisa kufanya kazi pamoja na wengine, badala ya kufanya peke yako? Ni nini Baadhi ya hasara za njia hii?
- Kazi ya timu inahitaji maoni ya pamoja. Ni mambo gani matatu unaweza kufanya kama kiongozi kusaidia hao wanafanya kazi na wewe kuunda na kukumbuka maoni ya pamoja?
- Wakati mwingine mikutano inaonekana kama kitu cha "kutia uvivu" na "kupoteza mda." Ni aina gani ya mikutano inaweza kuwa ya kupoteza mda, na ni mikutano ipi inaweza kuwa ya faida kwenye kundi linalofanya kazi pamoja kupanda kanisa?

**Utekelezaji wa Azimio**

Orodhesha kazi nne za ufunguo zitakazokamilishwa katika kazi yako ya upandaji kanisa. Fikiria kwa nani unaweza kukabidhi majukumu kwa kila kazi, kulingana na vipawa walivyonavyo na uwezo wa waumini

wengine ambao wanaweza kuwa wako tayari kusaidia. Kisha amua jinsi unavyoweza kuandaa na kumfundisha mtu kwa kazi hiyo. Kisha zifanye.

# Uongozi – Azimio la Mafunzo 5

## Maendeleo ya Timu

**I. Kuunda Timu Yako –** Ni nini unachofikiria ni tabia muhimu zaidi za watu watakaofanya kazi nawe katika upandaji kanisa?

A. Kujitolea kwenye Lengo la Upandaji Kanisa
B. Tabia ya Kimungu
C. Makubaliano ya Kkukuza Uwezo Kupitia Majukumu wazi

Jadili yafuatayo katika makundi madogo (Dakika 15)

1. Watathimini wajumbe (au wajumbe mashuhuri) wa timu zako kwa misingi ya kila maeneo matatu yaliyohusika hapo juu "Kuunda Timu Yako".
2. Ni yapi kati ya maeneo haya matatu unayofikira kuwa muhimu zaidi?
3. Kwa nini kujisumbua na maeneo haya matatu wakati kuna kazi inayohitajika kufanyika (Yaani kupanda kanisa mpya)?

**II. Kuongoza Timu Yako**

A. Endeleza **Uhusiano** wa Wajumbe Wako wa Timu **na Mungu**. Jinsi gani unaweza kulifanya hili vema?
B. Endeleza **Uhusiano** wa wajumbe wa Timu yako **na Mmoa kwa Mwingine'** – Hili linahitaji nini?

- Kuwasaidia wajumbe wa timu kujua vishawishi vyao..
- Kuwasaidia wajumbe wa timu kujua uwezo wao wa mahusiano na udhaifu.
- Kuwasaidia wajumbe wa timu kuendeleza tabia bayana kwenye tofauti zao.
- Kugundua maeneo yenye wasiwasi wa kimahusiano.

**C.** Endeleza **Maono** ya wajumbe wa Timu yako' **kwa Ajili ya Huduma**—Wasiliana mara kwa mara na kwa shauku
D. Endeleza **Ujuzi wa Huduma** wa Wajumbe Wako– Kwa maombi andaa moyo wako na akili. Angalia nyakati za kufundishika na nafasi (Mit **25:11)**

Jadili yafuatayo katika makundi madogo:

1. Elezea ambacho wewe binafsi unaamini kuwa jukumu la kiongozi na majukumu ya wajumbe katika kazi ya upandaji kanisa.
2. Katika hali ya undani, maeneo manne hapo juu ya maendeleo yanaweza kutokea kwa mfululizo au mengine yanahitaji kuja mapema?

**III. Kuielewa Timu** Yako

Kama inawezekana, wape wanafunzi mchoro 5.2 ukurasa 85 wa Kozi ya Omega

Ainisha ni hali gani unafikiria timu yako imo: **Timu ambayo Haijakomaa (kiongozi kujijali), Timu changa (watu wanaojijali), Timu inayojifunza (kujali utaratibu, Timu inayokomaa (Kujali makusudi?.**

Sasa, tathimini timu yako kwa misingi ya uwezo wake katika kila moja ya maeneo yafuatayo ya **kiutendaji: uongozi, kusudi la pamoja, mahusiano, majukumu yaliyowekwa maalumu, utaratimbu unaonyumbulika, mawasiliano, na mapana ya maisha kiroho.**

1. Nini kinaweza kutokea kwenye timu inayokomaa kwenye baadhi ya maeneo na kubakia kutokomaa kwenye maeneo mengine?
2. Nini kinaweza kutokea kwenye timu inayokomaa kwenye baadhi ya maeneo na kubakia kutokomaa kwenye maeneo mengine?

**Utekelezaji wa Azimio**

- Kwa kutumia mchoro katika jedwali 5.2, "Hatua nne za maendeleo ya timu." Onyesha ni katika hatua ipi timu yako kwa sasa ilipo kwenye maeneo yaliyoorodheshwa. Katika kipande cha karatasi kinachojitegemea, tengeneza orodha ya kila eneo (uongozi, kusudi, mahusiano, n.k.) na andika wapi timu yako ilipo kwenye (hatua 1, 2, 3, au 4).

- Angalia kwenye mchoro kuona nini zitakuwa baadhi ya tabia za timu ambazo zimeendelezwa zaidi katika kila moja ya maeneo haya. Kwa kila eneo lililoorodheshwa kwenye karatasi yako, andika angalau matatu yanayoonekana, vitu vinayopimika ambavyo unaweza kufanya ili kuisaidia timu yako kuendelea na kukomaa katika eneo hili.
- Anza kuweka mawazo yako, na baada ya miezi miwili, utazame upya mchoro huu na rudia zoezi hili. Ni katika maeneo gani timu yako imekua? Ni katika maeneo gani imeendele kuwa karibu sawa? Ni njia gani zingine unaweza kujaribu kusaidia timu yako kuendelea kukua na kuendelea kukomaa katika maeneo haya ya "kutojongea"? Fanya marudio ya mawazo yako na ufahamu pamoja na mshauri wako.

# Vikundi Kiini—Azimio la Mafunzo 7

## Nguvu ya Majadiliano ya Kikundi Kiini

Ingawa kusudi la somo hili ni kumwandaa kiongozi wa kikundi kiini kuongoza mda mzuri wa majadiliano, majadiliano yenyewe siyo lengo la mwisho kwenye kikundi kiini. Mda wa majadiliano yenye maana kati ya wajumbe wa kikundi yanatia moyo ushirikiano, yanaimarisha mahusiano, na kutoa njia ya kujifunza na kutumia ukweli wa kibiblia. Kwa kujifunza jinsi ya kuongoza majadiliano vizuri na kuepuka mataizo ya mawasiliano, kiongozi wa kikundi kiini ataweza kujenga uaminifu na kujitoa kati ya wajumbe wa kikundi na kukivutia kikundi kutimiza makusudi yake.

**I. Kuongoza Majadiliano katika Kikundi Kiini**
Kutoka katika Uzoefu wako ni nini baadhi ya vitu ambavyo kiongozi wa kundi dogo anatakiwa kufanya? Majibu yanaweza kuwa pamoja na:

A. Kusikiliza
B. Kuuliza
C. Kuchanganua
D. Kuhakikisha
E. Kuzidisha
F. Kuongoza Upya
G. Kufupisha
H. Kuthibitisha (tambua na shukuru mchango wa kila mtu)

**II. Endeleza Maswali mazuri** (Tazama 7A chini)

A. Maswali ya Ushirika
B. Maswali ya Biblia ya Kujadiliana

**III. Matatizo ya Majadiliano**

A. Aina ya Matatizo ya Majadiliano

Katika makundi madogo, jadili asili ya matatizo haya manane hapo chini na kila namna ya kuchukulia kila moja (Dakika 20)

1. Mmoja anazungumza sana/Mmoja hazungumzi kabisa
2. Muongeaji amekuwa kwa ujumla zaidi au Asiyeeleweka vizuri
3. Majadiliano yamekwenda nje ya jambo linalozungumziwa
4. Kuna swali ambalo kiongozi na kikundi hawakuweza kulijibu
5. Wajumbe wawili au mmoja wanaingia kwenye mabishano
6. Mtu fulani wakati wote anachekesha
7. Mtu fulani pengine hazingatii, au anashughulika na kitu kingine tu
8. Wajumbe wawili kila mara wanakuwa na mazungumzo ya "siri" kati yao

**B. Zoezi: Kuchukulia Matatizo ya Majadiliano**
Wagawanye wafunzwa kwenye makundi mawili, kikundi A na kikundi B. Kikundi A kinachagua mtu mmoja kutoka kwenye kikundi chao "kuongoza" kikundi B. Wakati wanachagua, kikundi B kisiri kinachukua wasiozidi watu 3-4 kuigiza moja ya jukumu lililoorodheshwa hapo chini. Kwa mda wa karibu dakika tano, kikundi B kinatakiwa kujadili jambo litakalozungumziwa "Jukumu la Kanisa katika Kukuza Jamii" (au jambo lolote wanalotaka). Kikundi A kinachunguza.

“Tatizo” watu katika kikundi B wanatakiwa waigize majukumu yao kiulinganifu, na kiongozi kutoka kikundi A anatakiwa ajaribu kutatua matatizo yanapotokea. Kumbuka, watu wa “kawaida” wanatakiwa pia wachangie kwenye mazungumzo, na siyo tu “matatizo” ya watu! Mwishoni mwa dakika tano, kikundi A kinaweza kubuni mtu gani amecheza nafasi zipi. Makundi yote yanatakiwa yatathimini jinsi kiongozi alivyojaribu kuchukulia matatizo yaliyotokea.
Kikundi B sasa kinachagua mtu wa kuongoza kikundi A, wakati kikundi A kisiri kinachagua watu 3-4 kuigiza tatizo la nafasi, n.k. Shughuli zinaendelea kadiri mda unavyoruhusu.

**Nafasi ya Tatizo:**

- Mtu mwenye aibu asiyeongea
- “Mweny matani” ambaye mara zote anakuwa kichekesho
- Msemaji anayeongea mda wote
- Mtu mwenye shughuli ambaye amezingwa na kufanya kitu kingine tofauti
- Marafiki wawili wanaoendesha mazungumzo yao ya faragha
- Marafiki wawili wanaofikia katika mabishano yaliyochemka
- Mtu ambaye kila mara anapenda kuzungumzia kitu kingine tofauti
- Mtu ambaye mara zote haeleweki sana na hayuko wazi
- Mtu anayetoa mahubiri badara ya jibu fupi kwenye swali jepesi

- Maswali ya kutafakari, marudio na matumizi
- Ni ujuzi gani wa mawasiliano unaofikiria kuwa muhimu zaidi kwa kiongozi wa kikundi kiini? Kwa nini?
- Ni aina gani za maswali ya majadiliano yangefaa kwa kikundi kipya, au kwa mtu mpya aliyekuja kwenye kikundi kilichopo? Ni aina gani ya maswali yanaweza yasifae katika hali hizi?
- Wakati wa zoezi la “kushughulikia matatizo”, ni kwa njia zipi “kiongozi’ ameshughulika na matatizo vizuri? Ni kwa njia zipi “kiongozi” ametatua matatizo vibaya zaidi?

**AZIMIO LA UTEKELEZAJI**

- Tumia mda fulani ukiandaa maswali ya mfano ya kutumia kwenye kikundi kiini kipya. Ni nini ungefanya kusaidia wajumbe wapya kuweza kujuana?
- Inayofata, Andaa baadhi ya maswali ambayo ungetumia kusaidia kikundi kukua kwa undani kwenye mahusiano yao. Ni jambo gani la kuzungumzia au maeneo ya maisha unayoweza kuzungumzia?
- Mwishoni, andaa maswali ambayo yanaweza kutia moyo kikundi kufikia nje kwa watu walio kwenye mzunguko wao wa mahusiano ya Oikos. Nini ungeweza kuuliza ambacho kingeweza kuwatia moyo kujenga mahusiano na kushirikisha Kristo?

## 7A –Vikundi Kiini: Mfano wa maswali ya Majadiliano

Maswali yaliandaliwa kwa ajili ya kutumia wakati wa mda wa mkutano wa ushirika wa kikundi kiini. Kama huwezi kutoa nakala ya maswali haya kwa wajumbe wa darasa, toa nakala moja kupitishwa na kunakiliwa.

**MAHUSIANO AINA NNE:**

**1. UHUSIANO KWA MUNGU**

1. Ni lini mara ya kwanza ulipokuwa macho kwamba Mungu anakupenda?
2. Ni mvuto gani ulio nao wenye nguvu kwa Mungu?
3. Ni nini unafikiri ni kitu kimoja Mungu anajaribu kukuambia?
4. Ni kitu gani kimoja ungetaka zaidi Mungu kukusikia ukisema kwake?
5. Ni swali gani peke yake ungetaka zaidi Mungu kulijibu kwa ajili yako?
6. Elezea mtu unayemjua kwamba anamjua Mungu kiundani wa mahusiano.

**11. UHUSIANO WA MWENYEWE**

1. Chora shungi au mkono wa koti kama unavyokuelezea vizuri, na uelezee kwenye kikundi
2. Nini ambacho ungefanya kama ungejua kuwa usingeshindwa
3. Ni nini unapenda kufanya zaidi miaka mitano ijayo kama kusingekuwa vizuizi?
4. Ni mtu yupi anafurahisha zaidi ambaye umewahi kukutana naye? Ni nini ulipenda juu yake?
5. Ni nini ulichokamilisha kinachotoshereza zaidi? Katika maisha yako ya mwanzoni? Katika miaka ya hivi karibuni?
6. Shirikisha mawazo yako makuu matatu
7. Ni nini ukumbusho wako wa kufurahisha zaidi (katika hatua tofaut tofauti)?
8. Elezea tukio lenye maana zaidi katika maisha yako
9. Elezea tabia za "mtu mashuhuri" kwenye kikundi.
10. Nani, mbali na wazazi wako, amekuwa wa kuigwa katika maisha yako?
11. Ni kipawa gani kingeweza kukubariki zaidi?
12. Ni nani unataka idhini yake zaidi?
13. Ni katika uwepo wa nani unafarijika zaidi? Kwa nini?
14. Kama ungekuwa na ulichotaka hasa katika maisha, Nini ungekuwa nacho?
15. Kwa kifupi orodhesha shabaha-ndefu na fupi ya malengo yako.
16. Elezea kichochezi zaidi, mtu mbunifu uliyewahi kukutana naye.
17. Ni nini watu watasema juu yako baada ya kuwa umekufa?
18. Orodhesha baadhi ya ubunifu, njia zinazosaidia kuianza siku na kuimaliza.
19. Ni katika nini unatumainia zaidi?
20. Ni nani amebadili maisha yako zaidi?
21. Ni vitabu gani bora zaidi umewahi kusoma (tofauti na Biblia)?
22. Jinsi gani unapenda kutumia mda wako wa ziada?
23. Ni nini kinakufanya zaidi kujisikia kupendezwa?
24. Ni nini kinakufanya kuwa na mashaka zaidi, kuwa na wasiwasi, au kuogopa?

**111. MAHUSIANO NA WENGINE**

1. Elezea mtu anayemaanisha zaidi kwako, na sema kwa nini.
2. Ni mtu gani wa kwanza aliyekuelewa zaidi?
3. Ni mtu wa aina gani unajikuta mwenyewe ukimwamini zaidi?
4. Ni nini kinamfanya mtu kuwa msikilizaji mzuri?
5. Uko aina ya mtu ambaye wengine wanaweka matumaini yao kwake? Kwa nini?
6. Unajisikiaje kundi hili limekusikiliza (kiushirikiano na kipekee)?
7. Nini kinafanya ndoa nzuri?

**1V. UHUSIANO KWA ULIMWENGU**

1. Ni nini ungetaka zaidi kujulikana na ulimwengu unaokuzunguka?
2. Ni nini kinahitajika zaidi kwenye jamii yetu?
3. Elezea unavyojisikia juu ya kutokuwa na usawa kwenye jamii yetu. Ni nini kinakufanya kusikitika zaidi?
4. Ni kitu gani muhimu unachoweza kufanya juu ya huko kutokuwa na usawa?
5. Ni nini hitaji dhahiri zaidi kwenye jamii?
6. Nini utafanya kubadili kanisa lako, jumuia yako, au kazi yako kwa ajili ya uzuri?

# Vikundi Kiini—Azimio la Mafunzo 8

## Kuwatunza Watu kwenye Kikundi Kiini

**I. Kujenga Mahusiano**

A. **Kupendana (1 Yohana 4:19,21) –** Jinsi gani Mungu anaonyesha upendo kwetu na jinsi gani tunaweza kuonyesha upendo kwa wengine?

B. **Kuombeana** (**Yakobo 5:16) –** Una orodha ya watu unaowaombea mara moja moja?

C. **Tumia mda pamoja (Ebr 10:25)** Kwa nini kutumia mda pamoja ni muhimu hivyo?

**II. Tambua mahitaji ya Watu**

Mfano: Natalie amekuwa akihudhuria kikundi kiini chake kwa miezi. Anawapenda watu kwenye kikundi, ingawa hakujua mmoja wao vizuri sana, alifurahia kwenda kwenye mikutano mara moja kwa wiki. Mme wa Natalie, ambaye hakuja kwenye kikundi, hivi karibuni amepoteza kazi yake. Pesa zao zilikuwa zinakwisha, na Natalie alikuwa amehofu sana juu ya nini watafanya kama familia. Alitaka kusema kitu kwenye kikundi, lakini alikuwa anajisikia vibaya na hakutaka kuwasumbua kwa matatizo yake. Mara baada ya hilo, aliacha kuwa anakuja kwenye mikutano ya kikundi, na wajumbe wakati mwingine walishangaa kwa mshangao, "Chochote ambacho kimemtokea?"

Tumia maswali yafuatayo katika majadiliano ya swala la natalie.

Nini kibaya katika hali hii? Jib: Tatizo halisi ni kukosekana kwa uhusiano mwema katika kundi lake.

Je Natalie alihisi upendo wa kikundi kiini chake? Nini inaweza kuwa baadhi ya sababu kwa hili?

Unafikiri kwamba kuna yeyote katika kikundi aliyemtembelea Natalie? Kwa nini unafikiri hivyo? Kiongozi wa kikundi kiini amtembelee Natalie sasa au amechelewa sana?

Jinsi gani hali hii inaweza kuepukwa kwa watu wenye woga?

**II. Kama kiongozi wa kundi, jinsi gani unaweza kuwa macho kwa baadhi ya vimuli ambavyo vinaashiria matatizo au hitaji?**

Jinsi gani unaweza "kuangalia" matatizo ya watu na mahitaji?

**III. Tunza mahitaji katika Kikundi Kiini Chako**

A. Itikia kwenye Mahitaji -- Kujilinganisha **(1 Cor 12:26),** maombi ya kundi **(Yakobo 1:5),** Biblia **(2 Tim 3:16-17),** kutunza **(Rom 12:13),** swala la dhambi (**Gal. 6:1). Nini tunachotakiwa kufanya kuitikia kwenye mahitaji?**

**B. Zoezi:** **Soma kila swala kwenye darasa na jadili swali.**

Ifuatayo ni mionekano ya matukio kadhaa ya baadhi ya hali unazoweza kukutana nazo kwenye kikundi kiini chako. Darasani, jadili kila hali na shauri njia ambazo kikundi kiini kinaweza kusaidia. Kunaweza kukawa hakuna jibu "sahihi" au "si sahihi" kwenye hali hizi.Wazo kuu ni kwamba upendo unajionyesha wenyewe katika matendo – watu tofauti wanaweza wanarudishia tofauti

- Eunice: Unapokea simu kutoka kwa Eunice asubuhi baada ya mkutano wako wa hivi karibuni. Anakwambia kwamba hatahudhuria mkutano tena, lakini haeleweki sana sababu ni kwa nini. Unapolifikiria, unakumbuka kwamba Katarina alizungumza kidogo wakati wa ushirika au wakati wa majadiliano, na kuondoka bila kuongea na mtu yeyote baada ya mkutano kumalizika. Utafanya nini?

- Katya: Wakati wa moja ya mikutano, wajumbe wa kikundi wamekuwa wakishirikisha maombezi binafsi. Inapokuwa zamu ya Katya, anaangalia kwenye sakafu na kusema polepole kila kitu ni sawa, asante. Wakati wa mda wa kuomba, huna uhakika, lakini unahisi kuwa analia. Utafanya nini?

- Andrew na Maria: Andrew na Maria: Watu waliooana, Andrew na Maria, wamekuwa wakija kwenye kikundi chako karibu mwaka mzima. Wakati wa mda huo, mahudhurio yao yamekuwa ya hapa na pale, iwezekanavyo. Hivi karibuni, wakati wa mda wa mkutano, ni wazi kwa kikundi kwamba kuna hali dhahiri ya kuhangaika kati yao. Unahisi pengine wana tatizo kwenye ndoa yao, lakini hujisikii kwamba unawafahamu vizuri vya kutosha kuweza kuwauliza juu yake. Utafanya nini?

- Michael: Hivi karibuni, mmoja wa wajumbe wa kikundi alimkaribisha mmoja wa wafanya kazi wenzake anayeitwa Michael kwenye kikundi. Wakati wa mda wa majadiliano, anauliza maswali mengi na kutaka kujifunza zaidi juu ya Yesu. Kwa jinsi hiyo, Michaeli ana hadhi ya kutotulia, na wakati wote anawachokonoa watu (ionekanavyo bila kulifahamu hilo). Uwepo wake umefarakanisha kile ambacho kilikuwa kikifurahiwa sana mda wa mkutano. Kwa mda wa wiki kadhaa sasa, hajahudhuria mkutano, na kuwa mkweli, wengi wa wajumbe wamepata nafuu kwamba hayuko hapo tena. Utafanya nini?

Maswali ya kutafakari, marudio na matumizi

- (**1The 2:8**) Kwa nini "kushirikisha maisha yetu" ilikuwa sehemu muhimu ya huduma ya Paulo?
- Kikundi kiini kinatakiwa kiwe chepesi kusaidia katika mahitaji kifedha? Kwa nini na Kwa nini siyo?

**UTEKELEZAJI WA AZIMIO**

- Andika njia mbili au tatu ambazo kikundi kiini chako kinaweza kukua kwenye upendo wao wa mmoja kwa mwingine. Andika shughuli kadhaa ambazo kikundi kiini chako kinaweza kufanya kuombeana zaidi.
- Andika mawazo mawili ya njia ambazo kikundi kiini chako kinaweza kutumia mda pamoja nje ya mkutano wa kawaida. Panga kufanya hili wakati mwingine wakati wa miezi mitatu ijayo.
- Watie moyo wajumbe wa kikundi kiini chako kushirikisha mahitaji, masikitiko na matatizo na kikundi, na angalia njia ambazo kikundi kinaweza kusaidia.

# Vikundi Kiini—Azimio la Mafunzo 9

## Kuwafunza Viongozi wapya wa Kikundi Kiini

**I. Chagua Kiongozi Mwanafunzi**

A. **Umuhimu wa Viongozi wanafunzi**—Muhimu kwenye Kuzaliana—Wataongoza vikundi kiini vipya.

B. **Utaratibu wa Kuchagua Kiongozi Mwanafunzi—(2 Tim 2:2)**
Welekevu unaohitajika: tabia, uzoefu, na ujuzi. Tabia ndiyo inayohitajika tu mtu kuanza.
Dalili za tabia **(1 Tim 3:2-12)**
Kikundi kiini kinatakiwa kutumia mda wa kutosha katika maombi kabla ya kuchagua.

Chagua mapema vya kutosha kuwa na mda wa kufundisha na uzoefu lakini usiharakishe uchaguzi.

Zoezi:

**(1 Tim 3:1)** Uongozi utachaguliwa kwa mtu "anayeandaa moyo wake" juu yake na "yuko tayari" na "anayetamani kuhudumu". Ukomavu kiroho ni hitaji la kwanza kwa uongozi, lakini kiongozi mwanafunzi lazima pia kiukweli awe anataka kumtumikia Bwana.

Darasani, jadili hali zifuatazo:

1. *Mtirirko wa Matukio*: Michael hivi karibuni ameanza kikundi kiini kwenye ujirani wake. Lengo lake ni kuanzisha vikundi kiini vya kutosha vinavyozaliana ili kwamba makanisa kadhaa mapya yaweze kupandwa katika mji wake. Amewaalika marafiki kadhaa na wanafamilia, na kundi limekutana kwa miezi kadhaa tayari. Kila mmoja katika kikundi ni muumini mpya, na hakuna anyeonekana kukomaa vya kutosha kuwa kiongozi mwanafunzi. Michael ameliombea hilo, lakini hana uhakika afanye nini. Anaweza kuchagua muumini mpya kuwa kiongozi wake mwanafunzi? Ungeshauri nini?

2. *Mtiririko wa matukio*: Petro ameanza kikundi kiini kwa msaada wa waumini wengine wawili. Watu wengine hawa wamekuwa wakristo wa miaka kadhaa, lakini hakuna mmoja kati yao aliye na uzoefu wa huduma. Petro anafikiri angesubiri kwa mda mrefu kabla ya kuchagua mmoja wao kuwa kiongozi wake mwanafunzi, ili kwamba wawe na nafasi ya kutosha kumwangalia anapoongoza kikundi kiini. Unafikiria nini juu ya namna hii? Nini ungeshauri?

3. *Mtiririko wa Matukio*: Eugene ameanzisha kikundi kiini kwenye jumuia na watu wengi wasio wafanaya kazi. Kundi linajaribu kuwasaidia watu kwenye jumuia kutafuata kazi, vile vile na kuwatambulisha kwenye Biblia. Eugene aliwauliza wachache waliokuja kuwakaribisha marafiki wengine waliokuwa nje ya kazi. Mwitikio ulikuwa wa kushangaza, na kikundi kilikua kufikia watu 15 kwa mwezi mmoja. Eugene anajua kwamba kundi linatakiwa liongezeke linapokuwa limefikia watu 15, lakini hili ni wazi haliwezi kutokea kwa kuwa hakuna mmoja wa wajumbe ambaye anaamini. Ana wasiwasi kwamba kundi litaendelea kukua,

na hajui la kufanya. Ni ushauri gani unaweza kumpa? Unafikiria nini juu ya mkakati wake? Kuna kitu kingine ungekuwa umefanya tofauti?

**II. Mwandae Mwanafunzi Wako kwa Uongozi**

**Muhusishe Mwanafunzi wako katika Kila Sura ya Huduma Pamoja Nawe**

**Mtathimini Mwanafunzi Wako**

**Muombee na Omba na Mwanafunzi Wako**

Jadili maswali yafuatayo katika makundi madogo (Dakika 15).

Nini unachoweza kufanya kumwandaa mwanafunzi wako kwa huduma yake?

Jinsi gani unaweza kupata taarifa zinazohitajika kumtathimini mwanafunzi?

Nini unatakiwa uhusishe katika maombi yako kwa mwanafunzi wako?

**III. Mtoe Mwanafunzi Wako kwenye Huduma**

- **A. Mpatie Maono Mwanafunzi Wako**
- **B. Teua Huduma kwa Mwanafunzi Wako**
- **C. Mwachilie Mwanafunzi Wako Kuanzisha Kikundi Kiini Kipya**
- D**. Anza Utaratibu wa Mwanafunzi Tena**

Jadili maswali yafuatayo katika makundi madogo (Dakika 15).

Ni baadhi ya vitu gani unavyoweza kuhusisha kwenye maono unayowasilisha kwa mwanafunzi?

Jinsi gani unafanya uamuzi kugawa majukumu fulani kwa mwanafunzi?

Kwa nini wakati mwingine ni vigumu kwa kiongozi wa kikundi kiini kugawa?

Ni baadhi ya vitu gani unatakiwa kujadili pamoja na mwanafunzi wakati unapokuwa mda wa kumwachilia kuanzisha kikundi kiini kipya?

## Utekezaji wa Azimio

Kama bado hujachagua mwanafunzi kutoka kundini mwako mwa kikundi kiini, liombee na kisha lifanye. Kama hakuna anayeonekana kuwa na sifa chagua mtu fulani wa kufuasa na kumwendeleza kwenye uongozi.

Muhusishe mwanafunzi wako kwenye huduma pamoja nawe, na kwa juhudi teua huduma zaidi na zaidi kwake.

Kutoka mda mpaka mda, mtathimini mwanafunzi wako, na muulize mwanafunzi wako kukutathimini kulingana na huduma yako na kikundi. Muombee kiongozi wako mwanafunzi.

# Uinjilisti—Azimio la Mafunzo 8

## **Uinjilisti wa Kimahusiano:** "Hakuna Mtu Aliye na Upendo Mkuu. . ."

I. Fanya Urafiki na Wasio Wakristo

A. Mifano Mitatu: Somo Moja –(Luka 15)

B. Ni Masomo Gani Tunaweza Kujifunza Kutoka katika Mifano

- Nani Yesu alimzungumzia kwenye mfano huu kulingana na mstari 1 na 2?
- Nini kinasababisha kufurahia huku mbinguni kulingana na mstari wa 9 na 10?
- Nini ni muhimu zaidi kwa Mungu—kundi la watu tisini la waumini wanaomwabudu yeye kwa uaminifu—au toba ya mtu mmoja mwenye dhambi (v. 9,10)?
- Je malalamiko ya kaka mkubwa yalihakikishwa (Ms 29-30)? yaIioana na moyo wa Baba?
- Nini kilimfikirisha Yesu zaidi: hakikisho la kidini au wokovu wa waliopotea?
- Unaweza kujichukulia mwenyewe kwenye mfano wa mwana mpotevu? Tabia ipi unayofanana nayo zaidi? Tabia gani unataka kuwa?
- Ni nini tabia ya kunena katika makanisa yetu kwenye kuwafikia waliopotea? Makanisa yetu yanafanana na Baba au na kaka mkubwa zaidi? Uko tayari kuchukua msimamo tofauti, kama ni muhimu kufanya urafiki na kuwafikia waliopotea.
- Ni aina gani ya juhudi zitakuwa za lazima kuwafikia watu unapoishi.

Jinsi gani naweza kuanzisha mawasiliano na wasio Wakristo nilio karibu nao katika jumuia?

Jinsi gani naweza kuanzisha mahusiano na Wasio Wakristo katika jumuia yangu?

Katika makundi madogo, jibu maswali yafuatayo: (Dakika 15)

**Jinsi gani tunaoanisha Luka 15 na mistari ifuatayo** 2 Kor. 6:14; 1 Yn 2:15; 1 Kor. 15:33?
Ni nini mistari hii inatuambia kuhusu "Kumfata Kristo Kiurafiki": **Rum 5:6-8; Yn 15:13; Marko 10:45?**

**II. Kuhesabu gharama**

A. Ni nini gharama ya Kufanya Urafiki na Wasio wakristo?
B. Ni nini faida za Kufanya Urafiki na Wasio Wakristo?

**IV. Uzoefu wa Maisha Kuhusiana na Uinjilisti wa Kirafiki**

Tumia mda unaobaki wa somo mkishirikishana vielelezo na mifano ya binafsi juu ya umuhimu wa mahusiano katika uinjlisti kutoka katika maisha yako mwenyewe.

**Utekelezaji wa Azimio**

Omba kwa ajili ya muguso wa asili kwa wasio-wakristo. Ni kwa njia zipi unaweza kuanza uhusiano na wasio-wakristo katika jumuia yako? Omba kwa ajili ya ujasiri kutembea katika milango anayofungua. Omba kwa ajili ya ufahamu wa kuwaona.
Nitahesabu gharama na kuonyesha imani kufanya urafiki na watano wasio-wakristo kwenye jumuia yangu mwezi huu hatimaye kuwaleta kwa Kristo?
Ishike siku! Kuwa rafiki na wapate hao marafiki kwa Kristo! Washirikishe katika mafunzo yako ya Biblia, ushirika na huduma ya kufikia nje. Wafanye kuwa sehemu ya timu!

# Kufuasa—Azimio la mafunzo 1

## Utangulizi Katika Kufuasa

Somo la kufuasa kwenye mwongozo waTatu na Nne linaendana pamoja. Imeshauriwa kwamba mkufunzi mmoja aongoze njia yote ya somo la kufuasa. Kama anahitajika mkufunzi zaidi ya mmoja, wakufunzi lazima wawe na ulinganifu wa karibu. Karibia na kuanza mzunguko wa kufundisha wakufunzi wanatakiwa wasome mwendo wote (masomo yote sita, pamoja na utekelezaji wa azimio) kupata uelevu wa njia ya kipekee kwenye yaliyomo.

**I.** Msingi wa Kibiblia wa Ufuasishaji (**Mat 28:18-20**) Agizo ni nini? Jib: Ubatizo unaoendelea. Mafundisho. Nini ni ahadi?

**II. Tafsiri ya** Mwanafunzi na Kufuasa

Nani ni mwanafunzi? Jib: Mwanafunzi anaweza kutafsiriwa kama mmoja ambaye ameweka imani yake katika Kristo na, kupitia ubatizo, amejitambulisha mwenyewe kama mfuasi wa Kristo na mjumbe wa kanisa la Kristo.

Nini maana ya kufuasa? Jib: Kufuasa kunaweza kutafsiriwa kama utaratibu ambapo kanisa, kutegemeana na mamlaka na uwepo wa Kristo, linachukua hatua…

- Kuwaongoza watu kwenye imani na kujitoa kwa Kristo,
- kuwashirikisha kwa Kristo na jumuia yake ya agano, kanisa, kupitia ubatizo
- kuwaongoza kwenye maisha ya utii kwenye mapenzi yote ya Kristo

**III. Wito wa Mungu Kufanya Wanafunzi**

A. **Kuwandaa Bibi Arusi wa Kristo—(Efe 1:23; 5:25-27)** Jinsi gani kanisa ni sehemu ya mpango wa milele?
B. **Kumfanya Bibi Arusi Kufaa kwa Bwana Arusi—**Ni vitu gani tunaweza kufanya kwa sasa?

- Tunawaandaa watu kukua katika umoja na Mungu na mmoja kwa mwingine? Tunawaongoza kuishi maisha yanayodhihirisha upendo huo wa kimungu ambao unaonyesha muungano huu?
- Tunawaandaa watu kukua kwa undani katika imani zao na matumaini katika Kristo?

- Tunawaandaa wanafunzi wetu kuhudumu kwa ufanisi kwa wengine, kuwajenga wengine kwa Kristo?
- Tunawaandaa watu kuwa mabalozi wa Yesu, kuwaita wengine kuwa sehemu ya jumuia takatifu ya Mungu na kwa hivyo kupanua Bibi arusi wa Kristo?

**IV. Jinsi gani Kufuasa Kunachangia Kwenye Upandaji Kanisa?**
**V. Kuanza na Mwisho Akilini**
Ni nini lengo lako la kufuasa? Ni nini hali ya watu wako? Jinsi gani unaweza kuwasaidia watu wako kukua kutoka walipo kwa sasa kuelekea kwenye lengo lako la kufuasa?

- Nini kisicho sawa kwa uinjilisti usio na ufuasishaji?
- Nini tofauti ambayo huduma ya kufuasa kwa ufanisi inafanya kwenye kanisa jipya?...katika kuanzisha harakati za upandaji kanisa?
- Inawezekana kupanda kanisa bila msisitizo mzuri wa kufuasa? Kwa nini na kwa nini siyo?
- Ni katika mandhali gani tofauti/ taratibu kanisa linaweza kufanya kazi kuelekea kufuasa?

**Utekelezaji wa Azimio**
Elezea nini aina za malengo ya kufanya wafuasi kanisa lako kwa sasa liliyonayo.
Orodhesha malengo ya kufanya wanafunzi unayodhani unatakiwa kuwa nayo.

# Kufuasa—Azimio la Mafunzo 2

## **Jukumu Lako Katika Ufuasishaji:** Funguo kwa Ufuasishaji Wenye Mafanikio

I. Kukua Kiroho
- **A. Endeleza Utambuzi wa Kiroho**
- **B. Jifunze Nini Kinazalisha Ukomavu wa Kiroho**
- C. **Endeleza Mguso wa Kiroho**

Jadili maswali yafuatayo katika makundi madogo: (dakika 15)

1. Inamaanisha nini kwa utambuzi wa kiroho?
2. Ni nini cha muhimu kwa mpanda kanisa kuwa na utambuzi wa kiroho?
3. Jinsi gani tunapata utambuzi wa kiroho?
4. jinsi gani utambuzi kiroho unagusa tabia zetu au haja?
5. Ni nini kinahitajika kwetu kujua jinsi ya kusaidia wengine kukua kiroho?
6. Nini tunatakiwa tufanye ili kuweza kugusa wengine?

**II. Kuonyesha Upendo Unaofanana na wa Kristo kwa Wanafunzi**
Ina Maana Gani Kuwapenda Wanafunzi Wako? **(Ebr 1:24-25, Flp 4:1, 1 The 2:17-18)**
Jinsi Gani Upendo Huu Unavyodhihirika Wenyewe Katika Maisha Yako? (**1 Kor 13:4-7)**
Nini Baadhi ya Ushauri wa Vitendo wa Kuonyesha Upendo kwa Wanafunzi? **(Rum 12:10-21, Flp 2:1-8)**

Jadili maswali yafuatayo katika makundi madogo: (Dakika 15)

1. Jinsi gani upendo unaonyeshwa kwa muumini mwingine?
2. Ni nini uhusiano wa kuwa wamoja au “mmoja kuwa ndani ya moyo wa mmoja?”
3. Kwa kutumia **1 Kor 13**, jadili jinsi upendo kwa wengine unavyoonyeshwa?

III. Kazania Juu ya Mahitaji Halisi ya Kiroho ya Watu, na siyo Vipindi
- **A. Fanya Mambo Kuwa Rahisi**
- **B. Wawezeshe Kutunza Sawa Sawa Vipao Mbele Vyao**
- **C. Uwe Mvumilivu**

**IV. Nipo kwa Ajili ya Kuzaliana na Kuzidisha—**Ni msaada aina gani wanahitaji ili kuweza kuzaliana na kuzidisha?
**V. Mara kwa Mara Tathimini Huduma Yako Kuwa Tayari Kufanya Mabadiliko Yanayohitajika**
**VI. Jifunze, Jifunze, Jifunze!**

Tathimini njia yako kwenye huduma na jadili tathimini na kundi. Tumia maswali yafuatayo:

1. Ninatunza mkazo kwenye upendo, imani na uwazi katika maisha yangu mwenyewe?
2. Ninawasaidia wengine kutunza mkazo huu?
3. Ninaanzisha vipao mbele na kuvitunza?
4. Ni mvumilivu kwa wengine walio komaa kidogo katika imani?
5. Ninatoa msaada kwa wengine?
6. Niko tayari kutathimini huduma yangu na kufanya mabadiliko yanayohitajika?
7. Nina rasilimali katika kufanya wanafunzi kushirikisha wengine? Taja baadhi unayoweza kushauri kwa wengine kwenye kundi.

## Utekelezaji wa Azimio

Soma **1Wakorintho 13:1-7** na tafakari juu ya tabia za Upendo wa Kikristo katika Ziada 2A. Chagua hali maalumu tatu mpaka tano ambazo unahitaji kutumia tabia za upendo. Katika kitabu cha kumbukumbu zako andika jinsi ulivyotumia tabia hizi na matokeo yake.

Unganisha orodha ya nyenzo zilizopo katika lugha yako au lugha inayolengwa ya watu unaotafuta kuwafikia katika kupanda kwako kanisa.

# Kufuasa—Azimio la Mafunzo 3

## Jua Lengo Lako, Jua Watu Wako

**I. Elewa Lengo Lako la Kufuasa**

Upambanuzi wa Kukomaa Kiroho—Imani, Tumaini na Upendo

Upambanuzi wa Mafanikio Katika Huduma

Katika mwanga wa hatima ya kusudi la Mungu, ina maana gani kuwa mkomavu kiroho?

Ina maana gani kuwa mfanisi katika huduma?

Kutoka katika mistari ifuatayo, jadili nini ufunguo kwenye utii kwa Kristo: **Mat. 22:36-40; Yohana 14:21; Rum. 13:8-10; Gal. 5:6**

Kutoka **Efe. 4:15-16 na Mat. 20:28**, nini ufunguo kwenye huduma yenye ufanisi.

**II. Elewa Hali ya Kiroho Iliyopo ya Watu Wako**

Kazania juu ya Maswala ya Moyo, na Siyo Tabia ya Nje

Tathimini Ukomavu Katika Upendo, Imani na Tumaini

Tathimini Ufanisi Katika Huduma ya Wengine

Chagua mmoja wa wanafunzi wako wa kutathimini ukomavu kwa misingi ya upendo, imani na tumaini. Mtathimini mwanafunzi huyo kwa kutumia maswali hapo chini. Baada ya kuwa umemaliza tathimini, jiunde katika makundi na jadili tathimini. Kama hujaanza kufanyia kazi yeyote, tumia tathimini hii kwako mwenyewe. Usimulinganishe mtu huyo ni nani kwa wengine kwenye kundi. Katika majadiliano ya kundi, fikiria maswali haya: (Dakika 20)

- **Jinsi ya Kutathimini Ukomavu katika Upendo**

**a) Upendo kwa Mungu**

Wanamtamani Mungu kuliko vitu vingine vyote au mahusiano? Ni namba moja ya kipaombele katika maisha yao? Kama siyo, nini kimechukua nafasi yake katika mioyo yao? Nini wanatamani kuliko yeye?

Wanamfurahia Mungu kuliko vyote? Wanamfurahia kuliko vingene? Kama siyo, nini wanachofuarahia zaidi yake? Nini kimechukua nafasi yake katika mioyo yao?

Wana moyo mmoja, roho na akili na Mungu? Kama siyo, nini kimechukua nafasi yake katika mioyo yao? Kwa nani au nini mioyo yao na akili imeelekea? Na nani au nini wanachojilinganisha? Nani uthamani wao unamuonyesha? Uaminifu wao umegawanyika?

Jinsi gani wanatembea katika upendo huu kwa kuendelea? Wakati gani wanaanguka, jinsi gani wanafanya haraka kutubu na kuanza kutembea na Mungu tena?

Wanadhirisha upendo wowote (usiofaa) kwenye ulimwengu huu? Lazima tufahamu uzito wa swala hili. Kwa hakika ni swala la kiibada ya miungu. Upendo kwa ulimwengu na upendo kwa Mungu havipatani

**b) Upendo kwa Wengine**

Wanatamani kuwa na ushirika wa kweli na waumini wengine na kutumia mda pamoja nao?
Wanawafurahia waumini wengine? Wanafurahishwa na waumini wengine?
Wana moyo mmoja na akili na kaka na dada zao katika Kristo? Wanaonyesha kwa njia za vitendo umoja wao na upendo?
Wanapenda familia zao? Wanahudumia famila zao kila mara kwa upendo, wakiimarisha umoja wao kama familia na kujenga kila mjumbe kwa Kristo?
Wana moyo kwa waliopotea? Wanaonyesha kila mara upendo kwa waliopotea?

**2. Jinsi ya Kutathimini Ukomavu katika Imani**

a) Wanaelewa imani ni nini?
b) Wanaelewa neema ya Mungu?
c) Imani yao imejengwa imara kwenye maandiko? Wanaelewa vya kutosha ukweli wakati wa kibiblia
d) Wana mvuto wa ndani kwamba Mungu anawapenda kuhusu ukweli huu?
e) Wana mvuto wa ndani kwamba Mungu anawapenda na amewakubali kikamilifu katika Kristo?
f) Wanaishi kwa imani, wakitegemea neema ya Mungu katika kila eneo la maisha yao?

**3. Jinsi ya Kutathimini Ukomavi katika Tumaini**

Mioyo yao imeelekezwa kwa kristo na wito wake kwao? Hivi ndivyo hasa wanavyoishi kwa ajili?
Wanaelewa ahadi za Mungu kwao? Wanamtumaini Mungu kuwa mwaminifu kwenye ahadi zake?
Wana shawishika kuwa Mungu anasababisha mambo yote kufanyika kwa ajili ya mazuri kwao, kuwaandaa kwenye mwisho alio nao kwa ajili yao?

**C. Tathimini Ufanisi Kwenye Huduma ya Wengine**

Ni wafanisi kwa kutumia vipawa vyovyote walivyonavyo na uwezo Mungu aliowapa kuwajenga wengine katika upendo, imani na tumaini?
Wanawatia moyo na kuwawezesha watu kukua katika umoja na Mungu na mmoja kwa mwingine?
Wanawawezesha wengine kuishi maisha ambayo yanadhihirisha upendo huo wa kimungu ambao unawasilisha muungano huu.?
Wanawapa ndugu msaada wa vitendo wanaohitaji ili kushinda ugumu wa kiroho katika maisha yao?
Wanawakilisha Injili kwa ufanisi kwa waliopotea?
Wanawaoongoza waliopotea kwa ufanisi kwa Kristo na kuwashirikisha kwenye mwili wa Kristo?
Wametiwa moyo na kuwezesha wakristo wengine kwa ufanisi kuwasilisha injili kwa waliopotea kwa maneno na matendo?

---

1. Ni eneo lipi la tathimini lilikuwa gumu zaidi?
2. Zilikuwa ni aina gani za taarifa au ufahamu ambao ulitumia katika tathimini?
3. Unahisi kwamba una msingi mzuri kwa tathimini hizi?

**III. Mipaka ya Kivitendo kwa Kufuasa**

Tumia mda mara moja moja nao. Rum 12:10-21, Flp 2:1-8 na 1Kor 13:4-7.
Tumia mda wako pamoja nao.
Shirikisha mahangaiko yako.
Omba pamoja.
Jifunze pamoja.
Uwe mbunifu.
Upatikane
Tafuta mapendekezo na msaada kutoka kwa wakristo wenginme.

Kabla ya somo lijalo, tunza kumbu kumbu za mda uliotumia kwa kila moja ya “mipaka ya kivitendo kwa kufuasa.”

# Kufuasa—Azimio la Mafunzo 4

## Kuwasadia Wanafunzi Kukua Kiroho

Kulingana na uzoefu wako mwenyewe, jaza Ziada 4A kabla ya darasa na tayarisha ubao wa kuonyeshea yaliyomo kwenye darasa (lazima isijulikane). Jaribu kulipa darasa wazo zuri la ni nini wanachojaribu kufanya na karatasi hizi za mazoezi. Baada ya utangulizi mfupi, tumia majibu yako mwenyewe kwenye Ziada 4A kuelezea jinsi "ukuaji kiroho unaohitaji tathimini" unavyoweza kufanyika.

I. Tambua Sababu ya Kawaida ya Mahangaiko ya Kiroho

Kila mpanda kanisa mwanafunzi peke yake atamalizia fomu hapo chini kutathimini mtu fulani kwenye kikundi kiini chake. Kama hawana mtu wa kutathimini, wanatakiwa wajitathimini wenyewe. Pasipo na kujilinganisha na yeyote kwa mwanafunzi mwingine ambaye ameshatathiminiwa.

Ziada 4A **Mzani wa kupimia: 1-siyo tatizo, 5-a tatizo kubwa**

_____________________________________________ (Jina la mtu)

| | Siyo tatizo | | | | Tatizo kubwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | **1** | **2** | **3** | **4** | **5** |
| 1. Anashindwa kuelewa baadhi ya funguo za ukweli wa kibiblia | **1** | **2** | **3** | **4** | **5** |
| 2. Kutojua kufanya linalotakiwa | **1** | **2** | **3** | **4** | **5** |
| 3. Kutokuwa na hakika kwa jinsi ya kuhusika katika huduma kwa wengine | **1** | **2** | **3** | **4** | **5** |
| 4. Anajua baadhi ya ukweli maalumu lakini haukubali kabisa | **1** | **2** | **3** | **4** | **5** |
| 5. Kwa kifupi anasahau au rahisi kukatishwa | **1** | **2** | **3** | **4** | **5** |
| 6. Anaruhusu upendo wa ulimwengu kumshinda au anakuwa mtumwa wa dhambi | **1** | **2** | **3** | **4** | **5** |
| 7. Anaogopa | **1** | **2** | **3** | **4** | **5** |
| 8. Wamekatishwa tamaa kwa Mungu au wakristo wengine na sasa wana hasira nao. | **1** | **2** | **3** | **4** | **5** |
| 9. Wanakosa mvuto | **1** | **2** | **3** | **4** | **5** |
| 10. Mengine | **1** | **2** | **3** | **4** | **5** |

II. Onyesha Msaada Waumini Wanaohitaji Kushinda Vipingamizi vya Kiroho

Wanafunzi wanarudi kwenye kundi lile lile kujadili maswali yafuatayo:

Ni aina ya msaada gani watu lazima wapate ili kushinda vipingamizi hivi? Ni aina gani ya usaidizi lazima wawe nao ili kuendelea kuishi maisha ya upendo, imani na tumaini? Nini wanatakiwa kuwa nacho ili kuhudumu kwa wengine kiufanisi?

Katika majadiliano ya mwanzoni, ni shughuli gani za msaada hapo chini zilionekana kuwa za kutumika zaidi.

(Dakika 15 )

- Kuonya, kutia moyo, kusaidiana mmoja kwa mwingine (1The 5:14),
- Kusahihisha na kuonya (2Tim 4:2),
- Kukanusha (Tit 1:9),
- Kuondoana kutoka kwenye dhambi (Yak 5:19-20),
- Kusema ukweli katika upendo (Efe 4:15),
- Kushauriana (Col. 3:16),
- kutiana moyo na kujengana (1The 5:11),
- kusisimuana na kupenda matendo mema (Ebr 10:24),
- kuimarisha wanyonge (Ebr 12:12),
- kufarijiana na kuhojiana (1The 2:11-12),
- kurejezana. Kubebeana mizigo (Gal 6:1-2),
- kuchukuliana (Efe 4:2),
- kusameheana (Col 3:13),
- kuombeana (Efe 6:18, Yak 5:16, 1Jn 5:16),
- Kuungamiana dhambi (Yak 5:16),
- kuhudumiana (Gal 5:13),
- kukubaliana (Rum 15:7),
- kuheshimiana (Rum 12:10),
- kutendeana mema (Gal 6:10).

- Ni nini baadhi ya sababu za kawaida katika kushindwa kiroho kwa waumini wapya?
- Kwa nini wanashindwa kuhudumia wengine kwa ufanisi?
- Nini ukweli muhimu zaidi wanaoshindwa kuelewa au kuamini?
- Ni vitu gani muhimu zaidi wanavyoshindwa kufanya au wasivyojua jinsi ya kuvifanya?
- Ni aina gani ya msaada ni wa muhimu zaidi kwa waumini wapya katika mwanga wa vizuizi vyao zaidi vya kawaida?

**Utekelezaji wa Azimio**

- Soma na tafakari Ziada 4A, "Kukua Kiroho Kunahitaji Tathimini." Malizia fomu ya tathimini na jibu majibu mwenyewe na angalau kwa mmoja wa wanafunzi wako.

# Kufuasa –Azimio la Mafunzo 5

## Mifumo ya Kufuasia

Uwe na hakika wafunzwa wanaelewa agizo la "utekelezaji wa azimio" lao. Lazima waje na mipango yao ya kufuasa kwenye mafunzo ya Mwongozo wa Nne. Maliza kabla ya mda nakara yako ya Ziada 5A, "Azimio la Kufuasa" kama kwa waumini wapya "halisi". Uandae ili kuonyeshwa kwenye kibao kama mfano kwa darasa.
Wafunzwa washirikishe walichopata kuwa cha ufanisi kutoka kwenye ufuasishaji wao wenyewe na uzoefu wa kufuasa. Waalike wafunzwa kufanya kama hivyo
Waulize darasa zima kutathimini kila moja ya mifumo ya ufuasishaji chini kwa misingi ya faida zake na upungufu.

**I. Mfumo 1: Ukuaji wa Binafsi—**Mwanafunzi anafanya kazi mwenyewe katika kujifunza, maombi, ushuhudiaji, n.k.

**Faida**:

- Kiasi kikubwa cha ufahamu na uzoefu vinaweza kupatikana rahisi.
- Usomaji unaweza kulenga kwenye hitaji maalumu la mtu.
- Viongozi wanawekwa huru kutoa mda wao na nguvu kwenye mahitaji ya huduma nyingine

- Mwanafunzi anaweza kujifunza kwa mda wake na kuchukua mda wa kutafakari na matumizi.

**Vizuizi:**

- Mpaka ujaribiwe katika baadhi ya njia, hakuna njia ya kujua ni kiasi gani kimeeleweka au kupatikana.
- Hakuna nafasi ya kumchunguza mwanafunzi anapokuwa anajihusisha katika huduma ili kwamba uweze kumpa ushauri unaosaidia.
- Misaada mingine ya kiroho bado inahitajika.
- Njia isiyo ya binafsi inayoelekeza ubinafsi na siyo kwa jumuia.

**II. Mfumo 2: Ufuasishaji wa Mmoja kwa Mmoja**—kiongozi au mshauri, anakutana na watu tofauti tofauti kipekee.
**Faida:** Wakata shauri wengi wapya watakua wakati usikivu pekee unatolewa kwao.

- Kuna kiwango cha juu cha nafasi kumpa mtu msaada anaohitaji.
- Kufundisha na kufunza kunaweza kulengwa kwenye mahitaji maalumu ya mtu pekee.
- Kuna kiwango cha juu cha matokeo, kutambua ni kiasi gani kimeeleweka na kupatikana.
- Kuna kiwango cha juu cha kumsaidia kuweka anayojifunza kwenye vitendo na kumsaidia kuweza kuhusika kwenye huduma kwa wengine.
- Kiongozi anaweza kufahamu kirahisi na kuwafundisha hao walio na umuhimu wa kufanya huduma ya mmoja kwa mwingine na wengine.
- Huu ni muundo wa ajabu kwa kufundishia ujuzi.

**Vizuizi:**

- Mtu mmoja hawezi kutimiza mahitaji yote ya kiroho ya mtu binafsi. Kwa jinsi hiyo, hii inaweza kuhesabika na mikutano kadhaa tofauti ya mmoja kwa mwingine.
- Kiongozi anaweza kuwa na huduma ya mmoja kwa mwingine na watu wachache tu. Ongezeko la washauri wapya inakuwa ni lazima.

**III. Mfumo 3: Huduma ya Kikundi Kidogo**—vikundi kiini, vikundi vidogo vya shule ya jumapili, vikundi vidogo vya kujifunza Biblia, n.k. Kila kiongozi wa kikundi anatakiwa kuwa na msaidizi ambaye amefunzwa kuwa kiongozi wa kikundi. Msaidizi huyu atajifunza kwa "kuchunguza" na "kufanya" chini ya usimamizi.
**Faida:**

- Viongozi wenye ujuzi kidogo wanaweza kutumiwa kuongoza kundi.
- Kila mmoja anaweza kuhusika. Mawasiliano ni maelekezo-mengi. Kila mmoja ana nafasi ya kutumia na kuendeleza vipawa vyake vya huduma.
- Hao walio na vipawa vya kufundisha au vipawa vingine vya uongozi wanaweza kufahamika kirahisi na kuendelezwa. Hii inafanya kuongezeka kwa huduma kirahisi.
- Kuna nafasi kubwa ya matokeo, kutambua ni kiasi gani kimeeleweka na kupatikana.
- Ni rahisi kukazia mafunzo na mafundisho kwenye hitaji halisi la wajumbe wa kikundi.
- Kuna nafasi kubwa zaidi ya kuelewa undani wa mahitaji ya kiroho ya watu kwenye kikundi na kutoa aina ya msaada wanaohitaji. Kuna nafasi kubwa ya kuwasaidia kuweka wanachosikia kwenye vitendo

**Vizuizi:**

- Viongozi wengi wanahitajika kama idadi kubwa ya watu itahusika kwenye vikundi vidogo (Hii inaweza kuwekwa kando kama kundi dogo limetumika kama eneo la kufundishia viongozi wapya.)
- Watu wengi hawatashirikisha mahitaji yao ya kiroho ya ndani, hata mbele ya kundi dogo. Kama kundi limechanganyika (wanaume na wanawake), kunaweza hata kukawa na uwazi mdogo.

**IV. Mfumo 4: Huduma ya Kikundi Kiini—**Mahubiri wakati wa ibada ya kuabudu, shule ya jumapili, vikundi vikubwa vya kujifunza Biblia, semina, n.k.

**Faida:** Viongozi wachache wenye ujuzi/wafanyakazi wenzao wanahitajika kufundisha kundi kubwa la watu.

**Vizuizi:**

- Watu wachache mbali na mzungumzaji (wa) mkuu wana nafasi ya kutumia na kuendeleza vipawa vyao vya huduma.
- Njia hii haitumiki kuendeleza viongozi wa baadaye. Isipokuwa njia nyingine imepatikana kuendeleza viongozi, itakuwa vigumu kuongeza huduma kwenye harakati za upandaji kanisa.
- Kufanyika vema, kunahitaji mtu aliye na kipawa kama mwalimu/muhubiri. Mara nyingi ni vigumu kupata watu wa kutosha wenye sifa.
- Kiongozi mmoja hana vipawa vyote vinavyotakiwa kukidhi mahitaji yote ya kiroho ya kikundi.
- Kuna nafasi ndogo ya matokeo, kwa hiyo ni vigumu kuelewa kiasi gani kimeeleweka na kupatikana.
- Kuna nafasi ndogo ya kuelewa mahitaji ya ndani ya kiroho ya watu kwenye kikundi na kutoa aina ya msaada wanaohitaji. Kuna nafasi ndogo ya kuwasaidia kuweka katika matendo wanayosikiliza.
- Kuna mazoea ya wasikilizaji wengi kuwa wa kutendewa.
- Hakuna mmoja anayehudumu kwa kiongozi (v)
- Kama huu ni mfumo wa msingi wa huduma, kisha watu wengi hawatakomaa kiroho.

## III. Maswali ya kutafakarti, marudio na matumizi

- Katika mandhali yako, ni "mifumo" ipi mara nyingi makanisa yanatumia katika kufuasa watu wao?
- Ni jinsi gani mifumo hii imekuwa ya ufanisi kutumika kutoa kile wanafunzi wachanga wanachohitaji?
- Ni mahitaji yapi hayajatimizwa?
- Mifumo ipi unadhana inayoweza kufaa zaidi katika kutimiza mahitaji haya?
- Ni mifumo ipi unajisikia uhuru nayo zaidi kuitumia? Ni mifumo ipi unajisikia huna uhuru nayo kuitumia? Kwa nini?
- Ni mfumo upi unafikiri unaweza kuwa bora katika huduma yako ya upandaji kanisa? Kwa nini?
- Ni kipi kati ya vizuizi vya mfumo huu unachofikiria kuwa kipingamizi kikubwa kwako?
- Jinsi gani unaweza kushinda vizuizi hivi vema?

**Utekelezaji wa Azimio**

Kwa Kutumia ziada 5A, "Azimio la Kufuasa", tayarisha mpango wa kufuasa kipekee kwa kila mtu unayemfuasa katika huduma yako ya upandaji kanisa. Ni lazima ulete mpango wako uliomalizika kwenye somo lijalo la kufuasa, amblo litafanyika unapoanza mafunzo ya mwongozo wa Nne.

**Ziada 5A (**Ifanye kuwepo kwa wanafunzi ikiwezekana.)

Katika kujaza katarasi hizi za mazoezi, weka vigezo vifuatavyo akilini:

- Onyesha ni mfumo gani (kundi kubwa, kundi dogo, mmoja kwa mmoja, mtu pekee) unafaa zaidi kwa ukweli/mawazo/thibitisho au tabia/ujuzi unaotaka kufundisha.
- Onyesha utaratibu ambao ukweli na ujuzi unatakiwa ufundishwe. Mswala ambayo ni nyeti zaidi kwa uponaji wa kiroho wa kila mtu unatakiwa ushughulikiwe mapema, badala ya baadaye.
- Amua ni nyenzo ipi iliyopo ya ufuasishaji, kama kuna yoyote, unayotaka kutumia. Katika njia sawa, orodhesha nyenzo zitakazotakiwa kwa mafunzo ya mtu pekee.

**Karatasi ya Mazoezi 5A.1 – Ni nini Waumini Wapya Wanataka KUJUA na KUFANYA**

**Maelekezo:**

Orodhesha vitu hivyo ambavyo waumini wapya wanavihitaji zaidi kwa dharura KUVIJUA kuweza kufanikiwa kuishi maisha ya upendo, imani na tumaini na kwa ufanisi kuwahudumia wengine kwa kiwango cha ufahamu wa kuelewa kwenye uthibitisho wanaotakiwa kuwa nao.

Orodhesha vitu hivyo ambavyo waumini wapya wanavihitaji KUFANYA kufanikiwa kuishi maisha ya upendo, imani na tumaini na kwa ufanisi kuhudumia wengine. Vingi kati ya vitu hivi vinahusu tabia wanayotakiwa waendeleze. Vingi pia vitahusu ujuzi watakaohitaji kujifunza.

| | **Wanachohitaji KUJUA (ukweli au mawazo/uthibitisho)** | **Wanachohitaji KUFANYA (mazoea/ujuzi)** |
|---|---|---|
| **Kuishi maisha katika upendo na umoja na Mungu** | | |
| **Kuishi maisha katika upendo na umoja na familia zao na waumini wengine na kuwajenga katika Kristo** | | |
| **Kuishi maisha katika imani** | | |
| **Kuishi maisha ya tumaini** | | |
| **Kiufanisi kuhudumu kwa waliopotea** | | |

Kila safu katika karatasi ya mazoezi 5A.2 inawakilisha mwezi. Ongeza safu kutoa kwa ajili ya mwaka mzima. Unaweza kuandika somo moja katika muhula mmoja. Kwa mfano, katika mikutano yenu ya mmoja kwa mmoja katika mwezi wa kwanza unaweza kuorodhesha somo tofauti la kutimizwa kila juma, kama vile: mda binafsi na Bwana, jinsi ya kuomba na jinsi ya kushughulika na dhambi. Kwa upande mwingine, wakati wa mwezi wa sita, mnaweza kuamua kutumia mwezi mzima kwenye somo moja, kama vile, kuanzisha ushuhuda binafsi.

**Karatasi ya Mazoezi 5A.2 – Azimio la Kufuasa la Mtu Pekee**

__________________________________ Jina la Mtu

| Mwezi | Pekee | Mmoja kwa Mmoja | Vikundi Vidogo | Vikundi Vikubwa |
|---|---|---|---|---|
| 1 | | | | |
| 2 | | | | |

# Vita vya Kiroho – Azimio la Mafunzo 1

## Kuelewa Mtazamo wa Kidunia

**I. Mtazamo wa Kawaida wa Ulimwengu**

A. **Mtazamo wa Ulimwengu wa Kidunia**— Katika mtazamo wa ulimwengu wa kidunia, ulimwengu wa asili na anga la binadamu vinatawaliwa na "sheria za asili". Kama nguvu isiyo ya kawaida ipo haina uhusiano na mwanadamu.

B. **Mtazamo wa Ulimwengu wa Kizama**—Roho kutoka anga lisilo la kawaida inaisha katika vitu vya kawaida na watu na ina nguvu kutawala vitu Kulindwa na uponyaji vinaweza kutoka katika ustahili kwa roho.

C. **Mtazamo wa Ulimwengu wa Kimaumbile**—Nguvu zisizo za kawaida na za kawaida zinamwendesha mwanadamu asiye na nguvu.

- Ina maana gani kusema "mtazamo wa ulimwengu?"
- Ni nini matokeo ya mtazamo maalumu wa ulimwengu juu ya mtu anayeshikilia mtazamo huo?
- Jinsi gani mtu ambaye ndiyo amepoteza kazi na kipato cha familia yake anachukulia tukio hilo katika mtazamo wa ulimwengu wa kidunia? Mtazamo wa ulimwengu wa kizama? Mtazamo wa ulimwengu wa kimaumbile?
- Ni nini mitazamo iliyotapakaa kwa watu katika eneo lako?

**II. Mtazamo wa Ulimwengu wa Kibiblia**
**A. Asili Kupita ya Kawaida**
**1. Mungu Mwenyezi**, yupo nje ya mda, wa milele, anayejitoshereza, Muumba wa mbingu na dunia, hana wa kulingana wala mshindani, katika uwenyezi wake anatawala matukio yote ya historia. **Kristo** alikuja ulimwenguni na kuishi miongoni mwa wanadamu. Kristo alipaa kwenda mbinguni na kumtuma **Roho Mtakatifu** juu ya kanisa lake. Biblia inathibitisha kazi ya juhudi ya Roho Mtakatifu katika na kupitia maisha ya waumini. Anauthibitishia ulimwengu juu ya dhambi, utakatifu na hukumu **(Yohana 16:8-11**). Anawapa waumini maisha mapya **(Rum 8:11).** Anashuhudia kuwa tu wana wa Mungu (**Rum 8:16).** Roho Mtakatifu anatusaida kuomba (**Rum 8:26**) na anafundisha **(Yohana 14:26, 1 Yohana 2:27).**
2. **Roho Hai Zilizoumbwa (Shetani na Malaika)—(Col 1:16)** Mungu (katika Krsto) aliumba vitu vyote, mbinguni na duniani, vinavyoonekana na visivyoonekana. Malaika wanatenda katika ulimwengu wetu leo **(Ebr 13:2).** **(Uf 12:4)** Shetani alipoanguka alichukua moja ya tatu ya malaika (mapepo) pamoja naye. Wanatenda katika ulimwengu (**Yakobo 3:15, 1Tim 4:1**). Maandiko yanafundisha kwamba Mungu ni mshindi dhidi ya mapepo. Malaika wote wapo kutudhuru?
**B. Asili**
Mungu aliumba ulimwengu wa vitu. Baadhi wanasema kwamba ni muonekano tu (maumbile); baadhi wanatunza heshima ya kicho kwake (kizama); wengine wanashikilia kuwa ni kitu mtu lazima akishinde na kukitawala (kidunia).
Kufuatana na Biblia, uumbaji wa Mungu ulikuwa umekusudiwa kutangaza utukufu wa Mungu **(zaburi 19).** Je uumbaji wa Mungu unatangaza utukufu wake? Ni nini lengo la Shetani kwa uumbaji wa Mungu.
**C. Mwanadamu** Mtu aliumbwa nje ya ulimwengu wa kawaida lakini pia Mungu akampulizia pumzi ya uhai na kumuumba mtu kwa mfano wake. Na kwa hiyo mtu ni kiumbe aliyetengenezwa, ni yote vitu na kiroho. Sehemu ya maajabu ya mtu ni kwamba ana uhuru wa kuchagua, haendeshwi tu. Anaweza akachagua kumpenda Mungu, na anaweza kumkataa **(Yosh 24:15).** Ungelipenda Mungu asingelitoa uhuru wa kuchagua? Kwa nini?
III**. Mtazamo wa Ulimwengu na Upandaji Kanisa**
Bado Mungu anahangaika na shetani au shetani ameshashindwa **(1Yn 3:8, Col 2:15, Ebr2:14-15**). Kupitia injili kama ilivyotangazwa na kanisa, Mungu anazungumza kupatanisha mtu kwake mwenyewe. Ni nini Shetani anachotafuta kufanya kwa mtu (Uf **12:9, 1Pet:8, 1The 3:5, Uf 12:10**)?
Ni nini uwanja wa mapambano ya vita vya kiroho kati kati ya anga la mtu? **(2 Kor 10:3-5).** Tambua jinsi mtume Paulo anavyooanisha kati ya kuangusha ngome na mawazo mabaya na kuteka nyara kila wazo kwenye utii wa Kristo. Mwishoni, fikiria **Yohana 8:32**, Kadiri tunavyoujua ukweli na kuufanyia kazi,

ndivyo tutakavyokuwa washindi. Upandaji kanisa ni vita vya kiroho. Kuelewa mtazamo wa ulimwengu kiusahihi inawasaidia wapanda kanisa kutambua nini kinachotokea katika maisha yake na huduma.

- Ni kwa kiwango gani unaamini kwamba Mungu amehusika katika historia?
- Ni kwa kiwango gani Mungu amehusika katika maisha yetu ya kila siku?
- Ni kwa kiwango gani Shetani na malaika zake wanahusika katika matukio yanayotokea katika kazi zetu na huduma?
- Unaweza kutoa mfano wa tukio katika siku hizi ambapo ilionekana kwamba Shetani anaweza akawa ameshinda juu ya watu wa Mungu?
- Ni nini madhumuni ya Mungu katika uumbaji?
- Ni nini mtazamo wa kibiblia katika uwezo wa mtu kufanya maamzi kinyume na kuwajibika kwa maumbile?

**IV. Maswali ya kutafakari, marudio na matumizi**

- Kama ambavyo umeshawekwa kwenye ukweli wa somo hili, umeshajifananisha na unayofanya mwenyewe katika maisha yako ambayo hayalingani na mtazamo wa ulimwengu wa kibiblia? Vipi juu ya wanayoyafanya hao walio katika eneo lako unalolenga?
- Ni nini wanayofanya hao walio katika eneo lako lengwa ambayo hayaendani na mtazamo wa kibiblia wa ulimwengu?
- Jinsi gani kutokulingana huku katika maisha yako kunaathiri uhusiano wako na Mungu, na mwenzi wako, watoto wako au waliopotea?
- Kama mpanda kanisa anaugua sana, hii ina maana kwamba Shetani anamshambulia kwa magonjwa? Lini hili linaweza kuwa ni sababu?

**UTEKELEZAJI WA AZIMIO**

Kutana na muumini mwingine na elezea wazo kuu la somo hili. Shirikisha jinsi tabia yako inavyokwenda kubadilika kutokana na ukweli mpya uliojifunza.

Fikiria juu ya mtazamo wa ulimwengu wa watu walio katika eneo lako unalolenga. Ni katika njia zipi mtazamo wao wa ulimwengu ni sawa na mtazamo wa ulimwengu wa kibiblia? Ni kwa njia zipi ni tofauti? Ni jinsi gani hili litaathiri mkakati wako wa uinjilisti? Jinsi gani na nini utawafundisha waliokata shauri wapya ili kuleta mtazamo wao wa ulimwengu zaidi katika mstari wa mtazamo wa ulimwengu wa kibiblia?

# Vita vya Kiroho – Azimio la Mafunzo 2

## Nguvu Ya Vita vya Kiroho

**I. Anga la Mungu –** Ni nini mistari inatuambia kuhusu utatu?
**A. Mungu Baba: Col. 1:13; Yohana 17:11**
**B. Mungu Mwana: Mat. 1:23; 28:18-20; Plp. 2:6,7,10; Rum. 8:3,34; Col. 2:10**
**C. Mungu Roho Mtakatifu: Yohana 16:8-13; Rum 8:2,9,11,26-27; 2 Kor. 3:3; 1 Yohana 4:4**

**II. Anga la Mtu—wanaoamini na wasioamini—Zab 8:5-6; Rum. 3:23, 6:23; Efe. 2:1,12, 6:11;Yohana 15:19, 16:18-21**

**III. Anga la Roho hai-malaika/malaika wanaohudumu na Shetani/mapepo—Mat 6:10, Ebr 1:14, 1 Pet 5:8, Uf 12:9, Yohana 8:44, 1 Yohana 5:19, Mat 4:1**

**IV. Anga la Vita**

1. Kutoka katika maandiko haya, kati ya nani anayefanya mapambano ya kiroho? Y**ohana 17:14; Efe. 6:10-17; 2 Kor. 10:3-5**
2. Ni nini malaika/roho zinazohudumu zinachofanya kwa mtu? **Luka 10:17,18**
3. Nani ni Shetani? Y**ohana 8:44;16:11; 1Pet. 5:8**
4. Ni nini anachofanya Shetani? **Uf. 12:7-9, 2 The. 2:9, Ebr. 2:14**
5. Ni kati ya anga lipi unamopata furaha kuu katika mda wako wa maombi na katika maisha yako?

**Mimi ni Nani katika Kristo?**

Kama muumini katika Kristo, mimi

- siko chini ya hukumu **(Yohana 3:18, Ro 8:1)**
- ni kimbe kipya **(2Ko 5:17)**
- nimewekwa mbali na sheria ya dhambi na kifo **(Rum 8:2)**
- nimechaguliwa na Mungu (**Efe 1:4)**
- nimerithiwa na Mungu. Ni Baba yangu **(Efe 1:5)**
- ninakubaliwa na Mungu **(Efe 1:6)**
- nimekombolewa, nimenunuliwa, na kuthaminiwa na Mung **(Efe 1:7)**
- mrithi pamoja na Kristo (**Efe 1:11; Rum 8:17)**
- nimefungiwa na Roho Mtakatifu **(Efe 1:13)**
- kiroho ni hai **(Efe 2:1-7)**
- mpokeaji wa neema ya Mungu **(Efe 2:8)**
- muhudumu Wake **(Efe. 2:10)**
- nimeondolewa na Kristo kutoka nguvu za giza na kuwekwa katika ufalme wa Mwanae **(Col. 1:13)**
- hekalu la Mungu aliye hai **(2Kor 6:16)**
- mkamilifu ndani yake **(Col 2:10)**
- chumvi na nuru ulimwenguni (**Mt 5:13,14)** ninayeenda kuwa kama Kristo atakaporudi **(1Jn 3:1,2)**

# Vita vya Kiroho – Azimio la Mafunzo 3

## Mapambano ya Kiroho Wapanda Kanisa chini ya Mashambulizi

**I. Uwanja wa Mashambulizi ya Kishetani –** Ni nini viwanja vya mashambulizi ya kishetani?

**A.** Mashambulizi katika uwanja wa kimwili—**Mat 9:32-33, Lk 13:16, Mk 5:1-13, 1 Jn 2:15-16**
B. Mashambulizi katika uwanja wa vitu —**Mat 4:8**
C. Mashambulizi katika uwanja wa akili/hisia—**Mk 5:1-10**
D. Mashambulizi katika uwanja wa kiroho —**1 The 3:5**

**Katika makundi madogo, jadili maswali yafuatayo: (Dakika 15)**

1. Umeshashambuliwa katika maeneo ya kimwili na vitu katika mahitaji ya kiafya, haja, nguvu au umiliki? Kama ni hivyo, jadili mifano ya hili?
2. Je kuna njia wazi tunayoweza kutambua kati ya matatizo ya akili/hisia ambayo yanatokana na mashambulizi ya adui na hayo ambayo siyo?
3. Ni aina ya shughuli zipi za kimafumbo zilizo bayana zaidi katika eneo lako?

**II. Jinsi ya Kujua Kama Tatizo Linatoka katika Sababu za Kikawaida au ni Mashambulizi ya Shetani**

Kielelezo: "Nilikuwa peke yangu chumbani, nikiwa nimesinzia fofofo. Ghafla nilikuwa nimeamshwa bila sababu yoyote. Giza chumbani lilionekana la kukandamiza na nikajikuta moyo wangu unakwenda mbio, pumzi yangu ikitoka kwa shida na mwili wangu ukijawa na jasho. Nikahisi kuwa hili lilikuwa ni shambulizi la Shetani, nilikaa kitandani, nikawasha taa na kwa sauti kubwa nikaanza kumkiri Yesu kristo kama Bwana na kumuuliza ulinzi kutokana na roho wabaya wowote wanaojaribu kunidhuru. Nilipoomba, mkandamizo ukaondolewa na nikalala chini na kisha nikalala tena fofofo."

Mtu anayehusika na masimulizi haya alikuwa ameshambuliwa na Shetani na mara akaendelea na kurudisha mashambulizi. Unaweza kuhisi kuwa uko chini ya mashambulizi ya Shetani, Hapa kuna baadhi ya kanuni za kibiblia za kufikiria. Hazikuandikwa kwa utaratibu wowote.

- Zijaribu roho uone kama zinatoka kwa Mungu (**1Yoh 4:1-3)**
- Tafuta msaada kutoka kwa mtu katika mwili wa Kristo mwenye kipawa cha kutofautisha kati ya roho (**1Kor 12:10).**
- Majaribu yanaweza yakawa yanatoka kwa Bwana kutufanya kukomaa na wakamilifu (Yak 1:2-4)
- Majaribu yanatoka kwa mwovu; kama tunaruhusu haja zetu wenyewe mbaya kutusababisha kutoa nafasi , matoke yake ni dhambi **(Yak 1:13-14).**
- Shetani anashambulia kutufanya kutenda dhambi, lakini Mungu analeta mema (Mwa 50:19-20).
- Shetani anatuma vitu katika maisha yetu ambavyo Mungu anatumia kuonyesha nguvu zake katika udhaifu wetu **(2Kor 12:7-9).**

**III. Jinsi ya Kujilinda Mwenyewe Dhidi ya Mashambulizi ya Kishetani**

A. Teka Nyara kila Mawazo kwenye Akili ya Kristot (**2 Kor. 10:3-5)**
B. Rejeza Akili Yako (**Rum. 12:1-2)**
C. Vaa Siraha Zite za Mungu (**Efe. 6:10-18)**
D. Kubali kufunikwa kwa Damu ya Mwana Kondoo **(Uf. 12:11)**
E. Usiiachie Dhambi Kukutawala (**Rum. 6:12)**

Ni vitu gani maalumu unatakiwa kufanya kutumia kila moja ya njia hizi za kujilinda?

**IV. Mipaka katika Kushughulika na Kukandanizwa Kimapepo**

A. Omba na Tafuta Hekima Kutoka kwa Roho Mtakatifu
B. Fanya Kazi na Wengine
C. Angalia Kilichosababisha
D. Shughulikia Maswala ya Dhambi (Mat 12:43-45)
E. Ufunguzi – Jinsi gani tunaweza kusaidia wengine au kupata ufunguzi wenyewe?
F. Ufuatiliaji – Baada ya ufunguzi, nini kinaweza kufanyika kumsaidia mtu?

| |
|---|
| Katika makundi madogo, jadili kila moja ya mipaka hapo juu. Ni upi unaofikiri ni muhimu zaidi kwa maisha yako? (Dakika 20) |

**Utekelezaji wa Azimio**

Katika maisha yako na huduma kama mpanda kanisa, unakutana na chochote ambacho unaweza kufikiri kuwa ni mashambulizi ya moja kwa moja ya mwovu? Kama ni hivyo, Orodhesha njia kutoka katika mafunzo haya zinazoonyesha nini unatakiwa kufanya kusimama kinyume na mashambulizi haya. Mshirikishe hili mkristo aliyekomaa atakayeomba nawe

# Maazimio ya Mafunzo ya Omega Mwongozo wa Nne

# Kanisa – Azimio la Mafunzo 12

## **Nguvu za Makanisa Yanayoibuka:** Lini Linakuwa Kanisa

**I. Lini Kanisa ni Kanisa?**

A. Nani Anaamua Lini Kanisa ni Kanisa? Jib: matakwa ya kibiblia (kuwa kanisa machoni pa Mungu), matakwa ya kidhehebu (kuwa kanisa la kidhehebu), matakwa ya kisheria (kutambulika na serikali),

Ni baadhi ya njia zipi tofauti tofauti makundi/madhehebu yanaunda makanisa mapya?

B. Tafsiri ya Kanisa la Mtaa

Ni nini tafsiri ya kanisa lako la mtaa? (Tazama Mwongozo wa Kwanza Somo la Kanisa la 4)

C. Kutofautisha Kundi Kutoka Kwenye Kanisa

Ni matakwa yapi kusanyiko linatakiwa kutimiza kuwa kanisa?

1. Kuwa na waumini wenye imani ndani ya Kristo**-Maandiko hayaainishi idadi ya chini.**
2. Kukutana Pamoja Mara Moja Moja kwa Ajili ya Ushirika, Kuabudu, na Mafundisho (warumi 14:5-6)
   **Jengo siyo lazima lidhaniwe kuwa kanisa.**
3. Kufanya Maagizo- **Ni mistari ipi katika Matendo inayoonyesha kwamba ubatizo na meza ya Bwana vilifanywa na kanisa la kwanza? Jib: ubatizo-Matendo? Jib: 2:41, 8:12; Meza ya Bwana Mf. Matendo 2:42, 20:7.**
4. Kuwa na Uongozi wenye Sifa- Kama kanisa linaamini katika wingi wa wazee, wanatakiwa kuwa na angalau wawili. Kama wanaona mashemasi kuwa wa lazima, kisha lazima kuwe na wajumbe wenye sifa za kuhudumu.
5. **Lenye Kujiweza Kifedha**
   Je kundi lisiloweza kujisaidia linaweza kufikiriwa kama kanisa?

**(1 Tim. 5:17-18).** Kanisa la kwanza liliwasaidia kifedha wajane na masikini kwenye kusanyiko, walitume fedha kwenye makanisa mengine yenye mahitaji, na kusaidia wamishenari wapanda kanisa. Kundi la familia kumi linaweza kumsaidia kiongozi mmoja. Kama kiongozi aliyepo hahitaji mshahara mzima, visivyo tasilimu pia vinaweza kutumika.

**II. Kupangilia kama Kanisa**

**A.** Vipande vya kipengele cha Kanisa la Mtaa Hai-waumini, vikundi, mikutano ya ushirika

**B.** Kuongeza "Ibada ya Ushirika"

- Kabla kanisa halijaanza ibada ya ushirika, fikiria yafuatayo:
- Kuna msingi imara ulio na vikundi kiini kadhaa vinavyozidi vikiwa na jumla ya watu 30-40 wanaohudhuria?
- Kuna watu wa kiini waliofunzwa kama wainjilisti na wafuasishaji?
- Viongozi wa huduma wamefunzwa na wako tayari kuchukua majukumu mapya?
- Viongozi na wapanda kanisa wameungana kuhusu falsafa ya huduma ya kanisa?

C. **Kutunza Uinjilisti, Ufuasishaji na Vikundi Kiini**

Endelea kufanya uinjilisti, mkikutana katika kufuasa, na kuwa na vikundi kiini hata baada ya ibada ya ushirika kuanza.

1. Ni maswala yapi ya kati ya kufikiria kabla ya kanisa mpya kuanza kuabudu kwa ushirika kwa kawaida?
2. Ni nini baadhi ya vionyesho kwamba kundi liko tayari kuanza kuabudu kwa ushirika kunakoendelea?
3. Elezea utaratibu ambao kikundi kimoja au zaidi kinakuwa kanisa.
4. Kwa kudhania kuwa kanisa jipya limekuwa likianza kwa kutumia vikundi kiini, elezea nafasi ya kiini katika maisha ya kanisa jipya.

# Kanisa – Azimio la Mafunzo 13

## Tabia za makanisa Yanayokua:

Pata watu Wapya, watunze na Waweke Kazini

**I. Ni nini Kanisa Linalokua?** Jib: Linaweza kukua kiidadi, kiroho, na kijamii (chumvi)

**II. Jinsi gani ukuaji wa kanisa unatokea?**

Makanisa Yanayokua **Yanawavutia watu wapya**
Makanisa Yanayokua **Yanatunza Watu Wapya**
Makanisa Yanayoka **Yanawaandaa watu Wapya kwa Ali ya Maisha na Huduma (Efe 4:11-16)**

**III. Tabia Kumi na Mbili za Makanisa Yanayokua**

Waulize darasa kujadili kama wanakubaliana na orodha iliyoandikwa chini kama tabia za makanisa yanayokua:

A. Wanakwenda kwa Waliopotea
B. Wanatumia Vikundi Kiini
C. Wanashiriki katika Kazi za Kijamii na Wasioamini
D. Wanatunza Mtandao wa Kazi na Mahusiano
E. Wanabadilika ili Kuwapata Waliopotea **(1Kor 9:19-23)**
F. Wanajihusisha na Wahitaji
G. Wanahusisha Mara Moja Waumini Wapya
H. Wana Maisha Ya Mwili Unaotikisika
I. Wanawaandaa Wajumbe kwa Ajili ya Maisha (ukomavu)
J. Wanawaandaa Wajumbe kwa Ajili ya Huduma Kwenye Mwili
K. Wanawaandaa Wajumbe kwa Ajili ya Huduma kwa Waliopotea
L. Wanaandaa Wajumbe kwa Ajili ya Huduma kwenye Kusanyiko Mpya (kuzaliana)

**Ni nini maisha ya mwili unaotikisika? Jib**: Mfundishio wazi ya Biblia na kuhubiri, kupenda ushirika, kujitoa kwenye meza ya Bwana, maombi yanayobadilisha maisha na kushirikishana

**IV. Kutathimini na Kumulika Ukuaji wa Kanisa**—kuandika kumbukumbu za ufunguo kwa marudio ya idadi ya vikundi kiini, ubatizo, mahudhurio, n.k.

**Maswali ya kutafakari, marudio na matumizi**

- Kanisa lako linakua? Kwa namna gani? Kihesabu? Kiroho? Kijamii? Baadhi ya haya? Yote kati ya haya?
- Ninatimiza wajibu wangu kuwaandaa waumini kwa ajili ya huduma, au ninajaribu kufanya hili mwenyewe? Jinsi gani ninawaandaa? Inafanya kazi?
- Kwa nini asiyeamini atake kuja kanisani kwangu? Kwa nini muumini mpya atake kubakia? Ninaweza kufanya kanisa langu kuwa zaidi la kuwapokea?
- Nimeanzisha jengo la kanisa tayari? Vikundi kiini? kama siyo, ni nini ninachosubiri?

## Utekelezaji wa Azimio

A. Hudhuria kanisa jingine na jifikilie kuwa hauko muumini. Utaweza kurudi kwenye kanisa hilo? Kwa nini au kwa nini siyo? Jinsi gani inalingana na kanisa lako? Ni nini ulichojifunza kutokana na hili ambacho kitakusaidia kanisani kwako?

B. Fikiria juu ya makanisa katika eneo lako, ni lipi kati yake linakua, na lipi halikui. Linganisha tabia za kila moja kwenye hali katika somo. Ni tabia ipi inaonekana kuwa sababu kwenye ukuaji wake au kutokua? Unaweza kutafsiri baadhi ya tabia zingine zinazosaidia?

# Kanisa – Azimio la Mafunzo 14

## **Utawala wa kanisa na Ofisi za Kanisa:** Nani Anawajibika

**I. Kanisa ni Nini?**

**II. Aina za Utawala wa Serikali**

A. Utawala wa serikali

1. Episcopal—Mfumo wa Episcopal wa utawala ni pamoja na serikali ya kanisa inayosimamia kanisa la mtaa. Mamlaka yanafanyika kupitia askofu wa kanisa. Mamlaka yanatirirka kwenda chini kutoka maaskofu kwenda kwa makasisi kwenda kwa waangalizi na mwishowe kwa wajumbe wa kanisa. **(Mdo 14:23, Tit 1:5)**

2. Presbyterian—Mfumo wa utawala wa Presbyterian pia una mtindo wa serikali ya kanisa. Mamlaka yanawekwa daima kwa mawakala waliochaguliwa na watu, wanaotenda kwa manufaa

yao. Wazee hawa pamoja na mzee anayefundisha (mchungaji) wanaunda kipindi. Mzee anayefundisha na mwakilishi wa wazee watawala kutoka eneo la makanisa ya mtaa yanaunda kasisi, ambaye ana madaraka juu ya vipindi vya mtaa. Wawakilishi kutoka kwa makasisi kadhaa wanaunda sinodi, na wawakilishi kutoka katika kila sinodi wanaunda kusanyiko kwa ujumla, ambalo ndilo lenye mamlaka ya juu. **(Matendo 15)**

**B. Kutano**

Katika mfumo wa kutano, utawala na majukumu yanabakia kwa wajumbe wa kanisa hilo. Mamlaka hayo hatimaye yanatoka kwa Kristo peke yake, na siyo kutoka kwa mwili wa mwanadamu awaye yote au mtu pekee. Wajumbe peke yao wanafanya maamzi ya lazima kwenye mwili wao na kuchagua viongozi wao wenyewe. Katika kutenda hasa, wanaweza kuwaruhusu viongozi wao uhuru wa kufanya maamzi kwa kuwafikiria, lakini bado wanawajibika kwenye kusanyiko, ambao lazima ndio wapitishe maamuzi makuu **(Matendo 6:5)**

**III. Ofisi katika Kanisa**
**1 Timotheo 3, Tito1, Mdo 20:17,28 na 1Pet 5:1,2).**

**A. Sifa za Mwangalizi katika Timotheo 3:1-7**

8. Njia ya hapo juu
9. Kuwa na mke mmoja
10. Kujiweza Kuwa na kiasi
11. Anayeheshimika
12. Mkarimu
13. Anayejitoa kufundisha
14. Asiwe mlevi
15. Asiwe mwenye fujo, lakini mpole
16. Siyo mchokozi
17. Asiwe anapenda fedha
18. Anaongoza familia yake vizuri
19. Anayeona kwamba watoto wake wanamtii kwa heshima
20. Siye aliyekata shauri mpya
21. Awe na sifa njema kwa watu wa nje
22. Awe na sifa njema kwa watu wa nje.

**B. Sifa za Wazee/Waangalizi katika Tito 1:5-9**

23. Asiye na lawama
24. Mme wa mke mmoja
25. Watoto wanaamini na siyo wenye fujo na wasiotii
26. Asiyechukua zaidi
27. Siyo mwepesi wa kughafirika
28. Asiyejitoa kwenye ulevi
29. Siyo mwenye fujo
30. Asiyefanya kazi ya mapato yasiyo ya halali

| Katika vikundi vidogo, malizia mazoezi yafuatayo: (Dakika 15) |
|---|

Karibu na orodha ya sifa za Wazee/ Waangalizi, andika mstari hasa kutoka 1Timotheo 3:1-7 na Tito 1:5-9 ambao unaunga mkono kuwemo kwa kila sifa. Jadili umuhimu wake.

**C. Sifa za Mashemasi katika 1 Timotheo 3:8-13**

31. Kuheshimiwa
32. Mwaminifu
33. Asiyekunywa kupindukia
34. Siyo mchoyo wa fedha
35. Awe na dhamiri njema
36. Aliyejaribiwa
37. Awe na mke mmoja
38. Anayeangalia watoto wake na nyumba yake

| Katika vikundi vidogo, malizia mazoezi yafuatayo: (Dakika 15) |
|---|

Karibu na orodha ya sifa za Mashemasi ukurasa wa 4 8 wa Mwongozo wa Nne, andika mstari hasa kutoka 1Timotheo 3:8-37 ambao unaunga mkono kuwemo kwa kila sifa. Jadili umuhimu wake.

**IV. Majukumu na Nafasi za Viongozi wa Kanisa**

Katika makundi madogo, chunguza vifungu vifuatavyo na tambua majukumu ya wazee/wachungaji/waangalizi.

**2Tim 4:5, 1Tim 4:13, 2Tim 4:1-2, Tit 2:1,**

Ni nini heshima ya kuwa kiongozi wa kanisa?

Unapofikiria aina za serikali ya kanisa iliyoelezewa katika somo hili, ni nini baadhi ya vitu yakini ambavyo vingeweza kuchangia kwenye kuzidisha? Ni nini baadhi ya vitu vilivyo kinyume ambavyo vinaweza kurudisha nyuma kuzidisha kwa kanisa?

Unakubaliana na mausia ya Paulo ya kuwalipa wazee wanaofundisha? Ni mahali gani kanisa unalopanda litakapochukua juu ya hili?

### Utekelezaji wa Azimio

Ainisha wanaume (wawili) kwenye jengo lako la kanisa ambao unadhani wana umuhimu kuwa wazee. Anzisha mpango wa kufuasa na kuwajaribu kwenye hali ya tabia maalumu zinazohitajiwa kwa mzee.

# Tabia ya Kiroho – Azimio la Mafunzo 11

## Upendo Kama Msingi kwenye Huduma

**I. Kanisa kama kielezo kwa Mahusiano**

Jinsi gani injili ni tofauti kutoka kwenye dini?

**A. Injili inaokoa**

Ni kurasa zipi za maandiko zinazoonyesha kwamba injli inaokoa? Mf. Rum 1:16

**B. Injili inabadilisha**

Ni vifungu gani vinaonyesha kwamba injli inabadilisha maisha? Mf. Flp 3:21, Ebr 9:14

**C. Injili inatoa kielezo kwenye Mahusiano**

Ni kwa njia zipi injli inatoa kielezo cha mahusiano na wengine? **(Efe 4:23)**

**II. Upendo wa Mungu usio na sababu, na wa kujitoa**

**A. Amri Kuu—Mat 22:34-40**

**B. Amri Mpya—Yn 13-33-34, 15:12-13**

Unakuta aina hii ya upendo ukitiririka miongoni mwa waumini katika kanisa lako? Kama siyo, kwa nini ni hivyo?

Yesu anamaanisha nini anaposem Anatoa amri mpya - Yohana 13:34?

Tambua watu (wawili) katika kupanda kwako kanisa unaofikiri kuwa wana umaarufu wa kuwa wazee. Anzisha azimio la kuwafuasa na kuwajaribu katika mkondo wa tabia maalumu unaohitajika kwa mzee. Ni nini Yohana 15:12-13 inatuambia kuhusu aina hii mpya ya hadhi?

**III. Upendo wa Mungu Uliotumiwa kwenye Mahusiano**

**IV. Upendo Kama Msingi wa Huduma**

Soma mistari ifuatayo na sema ni uhusiano gani kila mmoja unamaanusha kwake: **1 Tim 3:5, 1 The 5:12-13, Matendo 20:28, Gal. 6:10, Mat. 22:36-40.**

Maswali ya kutafakari, MARUDIO na matumizi

39. Jinsi gani unaweza kueleza "jirani" kama ilivyotumika katika amri kuu (mpende jirani yako kama unavyojipenda)? Ni nini ingekuwa matokeo kama kanisa lako lote lingetii amri hii?
40. Yesu alimaanisha nini aliposema pendaneni "kama nilivyowapenda?"
41. Ni muhimu kwa viongozi kutii amri hii kuliko kwa wengine kanisani? Kwa nini na kwa nini siyo?
42. Jinsi gani unawapenda watu vyema?
43. Fikiria tofauti upendo inaofanya kwenye hali zifuatazo: familia/marafiki; waumini na wasioamini? Wajumbe wa kanisa/viongozi?
44. Jinsi gani imani yetu inayokua inavyogusa jinsi tunavyowapenda wengine?

### Utekelezaji wa Azimio

45. Muulize Mungu akuonyeshe baadhi ya waumini ambao utaonyesha aina ya upendo Yesu alioamuru. Andika majina yao na nini utafanya. Acha nafasi ya kuandika matokeo wakati hili linapokamilika

46. Muulize Mungu akuonyeshe baadhi ya "majirani" ambao unatakiwa kuwaonyesha upendo. Andika majina yao na nini utafanya kuonyesha upendo kwao. Acha nafasi ya kuandika matokeo hili linapokamilika.
47. Fikiria mtu ambaye uko karibu naye (mwenzi, mzazi, au mtoto). Jinsi gani unampenda mtu huyu? Ni kwa njia zipi ukosefu wako wa imani katika injili umeathiri jinsi ulivyowapenda? Ni dhambi ipi unahitaji kuitubu kwao? Fikiria njia thabiti unayotaka kumpenda mtu huyu kwa sababu ya imani yako iliyolejezwa kwenye injili.

# Tabia ya Kiroho – Azimio la Mafunzo 12

## Kuuelewa Moyo wa Baba

**I. Mifano Mitatu Kuhusu Vitu Vilivyopotea- Luka 15**

**A. Mandhali ya Luka 15**

Hapa tunaona Yesu akiwa amezungukwa na wakusanya kodi na wenye dhambi" wakiwa tayari kusikiliza mafundisho yake (Lk 15:1). Fikiria itakuwaje kwa Yesu kukaa akiwa anasimulia wakusanya kodi na "wenye dhambi." Hili lingefanyika wapi—nje? Kwenye uwanja wa nyumba kwenye aina ya nyumba za kimediteraniani? Kwenye dari? Ni aina gani ya watu wangekuwa kwenye kundi la waliokaa kumzunguka Yesu? Nini kingekuwa mezani? Kungekuwa na chakula? Ungesikia vicheko? Watu wanajaribu kumridhisha Yesu kwa masimulizi yao?

Baada ya kuwa na picha akilini mwako ya Yesu akiwa amekaa na wakusanya kodi na wenye dhambi, Sasa fikiria Mafarisayo na walimu wa sheria (Lk 15:2). Wapi wangekuwa wamesimama au kukaa? Kwa hakika siyo katika chumba kimoja na wakusanya kodi na wenye dhambi. Mafarisayo wasingeweza kuchanganyika na wenye dhambi. Pengine wangesimama nje gizani au kwenye matamvua ya umati umbali fulani –ili kutogusa mojawapo ya wenye dhambi. Ni nini Mafarisayo wananung'unikia?

Ruhusu mwenye hisia za kusikia mguso wa tukio hili, na mkazo kati ya Yesu, umati uliokusanyika na Mafarisayo. Ukiweka tukio hili akilini, soma mifano ambayo Yesu anasimulia mwishoni mwa ukurasa.

**B. Mifano**

Jinsi gani unaweza kufikiria mchungaji, mwanamke na baba walivyojisikia wakati walipopata vitu vyao vilivyokuwa havipo? Ni aina gani ya furaha unadhani ilitokea? Ni aina gani ya sherehe ungefanya kama ulikuwa umepoteza kitu fulani cha thamani kubwa na kisha kukipata tena?

Kuna tofauti moja kati ya mifano ya kwanza miwili (kondoo aliyepotea, sarafu iliyopotea) na wa mwisho (wa mwana aliyepotea). Siyo sawa na ya kwanza miwili, katika mfano wa mwana mpotevu, hakuna anayekwenda kumtafuta. Kwa nini ni hivyo? Watu wengi wanadhani kuwa sababu kwa hili ni kuonyesha kwamba mtu anatakiwa awajibike kwenye matendo yake mwenyewe na "kuja nyumbani" Hili linaweza kwa sehemu kuwa kweli, lakini siyo wazo alilokuwa akifanya Yesu hapa. Kuna sababu ya undani ambayo inatakiwa iwe wazi tunapoangalia kwa karibu kwenye fungu.

**II. Mfano wa Mwana Mpotevu**

**A. Baba**

**B. Kaka Mdogo**

**C. Kaka Mkubwa**

**D. Ufafanuzi**

**III. Matumizi—Tunapenda Kama Baba Anavyopenda?**

> Ruhusu mda kwa wanafunzi kuandika majibu yao wenyewe kwenye maswali hapo chini.

Hatari halisi kwa waumini ni kwamba ingawa wote tumeshawahi kuwa wapotevu na kurudi nyumbani, tuna mazoea yenye nguvu ya kuwa kama kaka mkubwa baada ya mda. Yesu anatutaka tutubu kama kijana mdogo alivyofanya na kuwa na upendo ambao baba alikuwa nao. Maswali yafuatayo yatakusaidia kuonyesha hali yako ya kweli (kama au la umekuwa kama kaka mkubwa kwenye mfano).

Ni nini tabia yangu kwa waliopotea? Ninawadharau? Ni mwenye kuhukumu? Ni mwenye huruma na mwenye kusamehe ? Fikiria nyakati ambazo umewahi kuwa karibu na watu “wasiopendeka”. Nini ulichofanya?

Ninawatafuta waliopotea kwa juhudi au kuwasubiri tu “waje?” Linganisha maneno ya Yesu katika Luka 19’10.

Nimeridhika “kula na wenye dhambi? Ninajari zaidi kile ambacho watu watasema juu yangu kuliko nilivyo kwa wenye dhambi?

“Ninakimbia kukutana na wenye dhambi” na kuwaonyesha huruma, au ninawakataa pamoja na dhambi zao? (Kwa mfano, nitafanya nini kama kahaba au mlevi wa madawa anapokuja kwenye ushirika wangu?)

Upendo wangu kwa baba ni kama ninavyowapenda hao anaowapenda? Wakati wenye dhambi wanapotubu, ninafurahi na kuwakubali kama makaka na madada?

Niko nanung’nika kwa ndani jinsi gani ninafanya kazi kwa juhudi na jinsi nisivyoshukuriwa badala ya kufurahia na kushangilia pamoja na Bwana?

### Utekelezaji wa Azimio

Soma Luka 15. Kisha soma tena na jibu maswali kwenye matumizi. Tumia mda katika maombi na muulize Mungu akupe moyo sawa wa huruma kwa watu alionao Mungu. Kama kuna vitu unavyohitaji kukiri kwake, fanya hivyo. Kama unahitaji kukiri kwa wengine au kufanya mpango wa hatua makini kuhusu kuhusiana na wengine kama Mungu anavyohusiana nawe, andika hili pamoja na jinsi gani utakavyolifanya.

# Tabia ya Kiroho – Azimio la Mafunzo 13

## Neema ni kwa Wanyenyekevu

**I. Utu --Ni nini maana ya Utu? (Rum 12:3, Flp 2:3-8)**

| |
|---|
| Unapokuwa unasoma vitu, kila mmoja atajikadiria kipekee kwenye maswali ya “Jaribio la Utu” na moja ya majibu yafuatayo: Kiuhakika (vema), kwa namna fulani, siyo kabisa (siyo vema). |

1. Jinsi gani unachukulia upinzani?
2. Watu wanaona rahisi kuja kwako? Unaingilika?
3. Mara kwa mara unajihusisha na mahangaiko ya madaraka na mabishano?
4. Unajikuta ukifikiri kuwa kila mmoja ana makosa isipokuwa wewe?
5. Je hasira inajibanza karibu na maisha yako?
6. Unaweza kufurahia unaposikia mafanikio ya wengine?
7. Wengine wanaweza kukudhania kama mtu mpinzani?
8. Unajikuta ukijitetea mwenyewe kwa wengine?
9. Ni msikilizaji mzuri, unayweza kukazania wengine badala tu majibu yako au ni nini kitu sahihi cha kufanya?
10. Kimakusudi unachukua sehemu ya chini? (Luke 14:7-11)
11. Ni mwenye rehema na mpole, au kuna ukingo mgumu kwenye utu wako?
12. Maombi ni harakati zako za kwanza kwa moyo wako?

**II. Mifano ya Unyenyekevu**

A. Yesu

Unyenyekevu wa Yesu ulitokana na utegemezi kamili kwa Baba. Anachofanya **Yohana 5:19-20** na **Yohana 14:10** ni wa Baba. Jinsi gani kisha tuishi maisha yetu? Jinsi gani kiukweli tunaweza kuishi hivi?

B. Paulo

Ni nini katika maisha yako ya sasa ni “Aina ya maisha ya Sauli?” (**Flp 3:4-11, 2 Kor 11:22-29**) Ni aina ipi “ya maisha ya Paulo?”(**1 Kor 15:9, 2 Kor 12:9-10**)

**III. Maombi yanaonyesha unyenyekevu kuelekea kwa Mungu**

Hii inamaanisha nini kwetu katika kujiunganisha kwa Mungu na mkazo wa kila siku?

**IV. Maisha ya Kikristo Yana Tabia ya Unyenyekevu**

Kama tunapita katika siku nzima kwa juhudi bila kupoa kujitoa mapenzi yetu kwenye ukuu wake, kupenda kutoa upendo, tumekuwa wanyenyekevu kwa swala hilo? Hii ina maana gani kuhusu jinsi tunavyotakiwa kuomba na jinsi tunavyotakiwa kuishi?

Jinsi gani mtu mnyenyekevu anavyoongoza kitofauti na mtu mwenye majigambo?

Soma **1 Petro 5:1-6**. Jadili kinachoweza kujifunzwa kuhusu uongozi wa unyenyekevu kutoka katika kila moja ya mistari hii

48. Kwa nini unadhani wakristo wengi, wakiwemo viongozi, wanahangaika na unyenyekevu?
49. Ni katika njia zipi unakuta kwamba ni vigumu kuwa mnyenyekevu?
50. Kwa nini Mungu anataoa neema kwa wanyenyekevu?
51. Ni tofauti gani unyenyekevu unafanya katika maisha ya mpanda kanisa?

**UTEKELEZAJI WA AZIMIO**

- Tafuta mtu wa kuwajibika kwake, mtu ambaye unaweza kushirikisha kwa ukweli na uaminifu.
- Muulize mshiriki wako wa kuwajibika kukusaidia kumulika vitu vilivyo kwenye mtihani wa unyenyekevu.
- Katika kumbukumbu zako za kiroho, andika mabadiliko unayoyaona yakitokea katika maisha yako.

# Maombi – Azimio la Mafunzo 8,9

## Kongamano la Maombi: Kuomba Kibiblia

**(Panga somo hili kwa kipindi cha masaa mawili)**

I. Injili kwa Watu Wote—**Ni kwa matukio mangapi maombi yametoa nguvu na mvuto wa kushuhudia katika Matendo?**

**A. Wanafunzi 120 katika Matendo 1:12-14**
**B. Kanisa la Yerusalemu katika Matendo 4:23-31**
**C. Petro juu ya dari katika Matendo 10:9-15**
**D. Paulo na Barnabas huko Antiokia katika Matendo 13:1-3**

### Kongamano la Maombi: Kuombea Ulimwengu

(Tumia muundo huu kama kiongozi cha kongamano la maombi kwa siku hizi)

**A. Omba kwa Ajili ya Mahitaji Binafsi na Matatizo**

Wakati mwingine tunatakiwa kuachilia mizigo yetu ili kwamba tuweze kuweka akili zetu vema kwa vitu ambavyo viko kwenye moyo wa Mungu kwa mataifa yetu, mikoa, jiji, miji, vijiji, na ujirani.

Gawanyika katika makundi ya watatU, kwa kifupi shirikisha mahitaji binafsi na tumia mda mkibadilishana kuombea kila mmoja.

**B. Omba kwa Ajili ya Kanisa la Mungu**

Tumia dakika chache mkiomba pamoja kama kundi kwa kila moja ya maeneo haya:

1. Omba kwa Ajili ya Umoja
2. Omba kwa Ajili ya Upendo wa Kristo
3. Omba kwa Ajili ya Utii

C. Omba **kwa Ajili ya watenda Kazi Wengi kwa Mavuno ya Mungu** yote hapa na ulimwenguni kote.

**D. Omba kwa Ajili ya Wapanda Kanisa**

Ombea kwa majina kwa hao miongoni mwenu na wengine ambao unajua kuwa wanapanda makanisa mapya.

**E. Ombea Siasa, Jamii, na Viongozi wa Dini**

Gawanyika katika makundi madogo tena na omba kwa ajili ya serikali yenu na majina ya viongozi wengine, mkiuliza kwamba Mungu aweze kuwatumia kuweka mazingira mazuri kwa ajili ya kuhubiri injili.

**F. Omba kwa Ajili ya Taifa Lako na Mataifa ya Ulimwengu**

Funga kongamano hili la maombi kwa kuchukua mda uliobaki kuomba kama kundi moja kwa ajili ya wokovu wa watu wenu, na pia kwa watu wa makundi mengine katika nchi yako na ulimwenguni. Taja kila moja maalumu na kwa jina kadiri Mungu anavyowaleta kwenye akili yenu.

# Uongozi – Azimio la Mafunzo 6

## Uongozi wa Kitumishi

**I. Uongozi wa Kidunia**

| Katika makundi madogo, jadili yafuatayo: (Dakika 15) |
|---|

Fikiria kiongozi wa kidunia unayemjua vema. Kwa kiwango gani kiongozi huyu anafata dhana zifuatazo:

48. Huwezi kuwatumaini watu kufanya yale unayotaka wafanye.
49. Kama unawatumaini wengine kupita, watachukulia manufaa kwako.
50. Viongozi wanajitwalia madaraka kwa kuzingatia nafasi zao au kwa hadhi zao.
51. Watu watafanya unachowataka kufanya wanapokuwa wamevutiwa na malipo, kutishika kwa adhabu.
52. Viongozi wanatakiwa waepuke mawasiliano ya karibu na wafuasi wao, au wafuasi wao watawaona wao kama dhaifu. Unakubaliana na mojawapo ya maelezo haya? Kwa nini na kwa nini siyo?

A. Jinsi gani unafikiri utumishi na uongozi vinaweza kwenda pamoja?

B. Ni kanuni zipi za mvuto wa kikristo na uongozi zinapatikana katika mistari hapo chini?

53. Watu wameumbwa kwa mfano wa mungu na kwa hiyo kuwa na thamani halisi **(Mwa 1:27-28).**
54. Watu wanavutiwa kutenda kwa ubora kwa kutambua kuwa kila kitu kitafanyika kwa utukufu wa Mungu (**Col 3:23).**
55. Watu hawatakua na kuendelea mpaka waaminiwe na kupewa uhuru wa yote kufanikiwa na kushindwa.
56. Kiongozi anateuliwa na Mungu na kuchukua madaraka kutoka kwake **(Rom 13:1).**
57. Viongozi wenye mafanikio wanawaona wenzao kama marafiki, na siyo kama wa chini, na kuzungumza nao kwa roho ya uwazi na unyenyekevu (**Yn 15:15).**

| Katika makundi madogo, jadili yafuatayo: (Dakika 15) |
|---|

Fikiria kiongozi wa kanisa unayemjua vema. Bila kumulinganisha mtu, jadili jinsi tabia yake kama kiongozi inavyooana na kanuni.

Ni nini matokeo ya uongozi wa kanisa ambao unatumia kanuni kama ilivyolinganishwa na huo uwsiotumia kanuni?

**III. Mafundisho ya Agano Jipya Juu ya Uongozi wa Kitumishi**

**A. Mfano na Mafundisho ya Yesu (Mat 20:25-28, Flp 2:1-11, Yohana 15:15)**

**B. Mfano na Mafundishi ya Paulo (1 The 2:6-9, 5:14, Rum 15:1, Gal 6:1-2)**

**C. Mfano na Mafundisho ya Petro (1 Pet 5:1-4)**

IV. Hadhi ya tabia za kiongozi mtumishi: **Kila mwanafunzi atajipima mwenyewe kutoka kweye 1 mpaka 5 na 1 ikionyesha maelezo hayaendani naye kabisa na 5 ikionyesha inaendana naye sana.**

58. Kiongozi mtumishi anatunza na kujenga umoja (Efe 4:3). Anaepuka mabishano yasiyo ya lazima juu ya umilikaji wa mali au ngome.
59. Viongozi watumishi hawatishwi na uwezo na makamilisho ya wengine. Badala yake, wanatambua thamani ya uwezo huu na kuutumia kufaulu malengo ya kikundi.

60. Kiongozi mtumishi ni “mjenzi” wa wengine. Kiongozi mtumishi anafanya kazi kuwatia moyo na kuwainua wengine kwa kila njia inayowezekana. Wanashangilia mafanikio ya wengine, bila kujali ni madogo kiasi gani.
61. Viongozi watumishi ni wa mstari wa mbele kusogeza maswala mbele, wakati wakitunza upole na kuwafikiria wengine.
62. Kiongozi mtumishi anawazungumza wengine vizuri kila wakati.
63. Kiongozi mtumishi anatafuta kujenga msingi mpana wa viongozi kuongoza pamoja naye.
64. Viongozi watumishi wanatambua na kutumia mamlaka inavyopaswa (kinafasi, kimahusiano, kiuzoefu, kibinafsi, kiroho).
65. Kiongozi mtumishi hajipatii umaarufu, kufaa, sifa kutokana na nafasi anayoshikilia.
66. Kiongozi mtumishi hafanyi maamzi kutokana na maendeleo yake, kusonga mbele, faraja. Kuzidi kwa mamlaka au nafasi kwa gharama ya hao anaotumikia.
67. Kujitoa kwa kiongozi mtumishi kwa wafuasi wake kunasonga mbele, huduma yao, na kuongezeka kwao ni ufunguo wa kuonyesha upendo wake.
68. Kiongozi mtumishi anawaendeleza viongozi wenzake, ili kutoa msingi imara wa uongozi kwa makanisa mapya yanayozaa.

# Uongozi – Azimio la Mafunzo 7

Nguvu za Uongozi

Ni kwa nini baadhi ya viongozi wanashindwa na wengine wanafaulu? Inawezekana kabisa kuelezea aina ya kiongozi wa kijamii atakayekuwa mfanisi katika hali zote na katika tamaduni zote? Tunaweza kufanya maelezo ya ujasiri kama vile “kiongozi kawaida lazima…?” Kwa nini baadhi ya viongozi wanazidi katika baadhi ya hali na kushindwa katika nyingine?

**I. Tabia za Kiongozi**

- **A.** Kiongozi wa watu **—tabia ni nyeti kwa kiongozi? Kwa nini?**
- B. Jinsi gani kiongozi anajilinganisha kwenye kundi—kwa “kuwaambia” “kushawishi” “kushaulisha” “kushiriki na wengine,” “kugawa?” Ni lipi kati ya haya unaridhika unapojilinganisha na hao unaowaongoza? Kwa nini? Ni nini matokeo ya mitindo hii kwa hao unaowaongoza?
- C. Kuelewa kwa kazi kwa kiongozi**—Jinsi gani unavyofanya maamzi ni kiasi gani ungejua kuhusu kazi zinazofanywa na wajumbe wa kundi lako? Jib: Jua vya kutosha kwa heshima lakini si kila kitu.**

**II. Tabia za Kikundi**

- A. **Ujuzi wa wajumbe wa kundi na uwezo—**maisha ya kiroho na tabia, uinjilisti, ufuasishaji, na kujenga mahusiano ni nyeti kwa mpanda kanisa. Moja ni muhimu zaidi kuliko yaliyobaki? Kundi unalofanya nalo kazi lina uzoefu, linahitaji mafunzo, wako tayari kutolewa kwa huduma nyingine, na kufahamu vipawa vyao vya kiroho?
- B. **Kujitoa kwa wajumbe wa kundi kwenye kazi—**Ajira au familia vinaingilia? Wajumbe wa kundi lako wamejitoa?
- **C. Mahusiano kati ya wajumbe—**Jinsi gani unashughulika na migogoro na wengine? Jinsi gani unachukulia migogoro na kundi lako?

**III. Asili ya kazi**

Wajumbe wa kundi lako wako wazi kabisa juu ya asili ya kazi ya upandaji kanisa?
Unakazia kupita juu ya kazi na kidogo sana juu ya mahusiano ya kundi?

Maswali ya kutafakari,marudio na matumizi

69. Ni vigezo gani vitatu vikuu vinavyoathiri mafanikio ya uongozi?
70. Ni mtindo upi halisi zaidi wa uongozi wa serikali katika nchi yako?
71. Ni mtindo upi halisi zaidi wa uongozi kwenye makanisa yako?
72. Ni mtindo upi wa uongozi ulitumiwa na viongozi hao wakristo ambao wamekuwa na mguso zaidi wa kuonekana kwako wakati wa nyuma?

**UTEKELEZAJI WA AZIMIO**

Andika matokeo ya vigezo kadhaa kwenye hali ya uongozi wako kwa kujibu maswali yafuatayo. Mpatie matokeo haya mshauri wako na jadili pamoja naye kabla ya kipindi cha mafunzo yajayo.

1) Jielezee mwenyewe kama kiongozi

73. Ni mtindo upi wa uongozi unatumia zaidi?
74. Ni vipingamizi vipi unavyoviona mwenyewe unavyo? Nini unachoweza kufanya kufidia kweye vipingamizi hivi?

2) Elezea kundi lako

75. Elezea ujuzi na uwezo wao.
76. Ni kiwango gani chao kwenye kujitoa kwenye kazi?
77. Kuna aina yoyote na migogoro kati yao ambayo inahitaji kushughulikiwa?

3) Elezea kazi yako.

78. Unapanda kanisa miongoni mwa watu wanaopinga au wanaokubali?
79. Wewe au wajumbe wa kundi lako ni "wa kuja" au wageni miongoni mwa watu hawa?
80. Kuna hali halisi ya uchumi inayofanya juhudi za upandaji kanisa kuwa ngumu?
81. Una habari za kutosha kuhusu mandhali yako? Wewe na kundi lako mnaelewa kazi yenu?
82. Una mpango wazi na mkakati ambao unapeleka matokeo ya utafiti wako kwenye wajibu?
83. Kuna nguvu za kiroho zisizo za kawaida ambazo lazima zikabiliwe?
84. Kuna msukumo wowote wa kisiasa ambao unaathiri hali?
85. Una rasilimali zinazohitajika kukamilisha kazi?
86. Ni kwa njia zipi Mungu amekutayarisha wewe na kundi lako kwa kazi hii?

4) Suluhu

87. Kama matokeo ya ulichojifunza, nini unahitaji kukazania?
88. Ni mtindo upi wa uongozi unaweza kuwa wa ufanisi zaidi kwenye hali yako, na kwa nini?

# Uongozi – Azimio la Mafunzo 8

## Mitindo ya Mwingiliano

**I. Mitindo Minne ya Mwingiliano**

**A. Mtendaji-** "Chukua hatua na ibuka na changamoto ya kuleta mabadiliko kufanya huduma yenye ufanisi zaidi."

Watendaji wanakuwa watu wenye uwezo, wanaoweza kukubali changamoto na kutatua matatizo kwa njia ya haraka na ya ufanisi. Ni watu wa utekelezaji na wanaweza kutegemewa kufanya mambo kufanyika. Watendaji hawaogopi kuchukua hatari; wakati mwingine wanachukua kazi nyingi zaidi na wanaweza kuonekana kutokuwa wavumilivu kunapokuwa hakuna maendeleo wakati huo. Mfano: Paulo **(Flp 4:13)**

**B. Mvutiaji**- "Kuvutia na kugusa wengine kufanya kazi pamoja kupata matokeo muhimu"

Wavutiaji ni watu wanaotarajia na wenye shauku ambao ni wazuri katika kuhusiana na wengine. Mara nyingi ni makini sana na wanaweza kuelewa mawazo na uwezekano katika namna inayowavuta wengine kushiriki. Kawaida yao kuwa na msisimko juu ya vitu vipya inaweza kuwawia vigumu kwao kufatilia baadhi ya kazi. Mfano: Petro **(Mt 14:28,16:16)**

C. **Mchezaji wa Timu**- "Shirikiana kiutayari na wengine kufanya maono na mipango" Timu ya mchezo inaunga mkono, watu wenye fahari walio na hisia nzito kwenye mahitaji ya wengine. Wanaweza kuhesabika kuchukua kazi kama zilivyogawiwa na viongozi na

hawatakwaza hao waliojitoa kwa ajili yao. Timu ya mchezo inaweza isifanye kazi vizuri peke yake kwa kuwa wakati mwingine wanakosa uanzilishi wa kipekee. Mfano: **Barnabas (Mdo 15:37-39)**

D. **Anayefikiri-** "Aliyevutika kuchukua maono na kupanga kwa mchanganuo safi na kwa uangalifu" Wanaofikiri ni waaminifu, watu wenye mpangilio walio na wanaokamata mambo kwa wingi. Wanaweza kutegemewa kufuatwa kwenye miradi ambayo wengine wanaona kuwa ya kutatanisha. Wanaofikiri wanatiwa changamoto na mabadiliko yasiyotarajiwa na kutaka kung'ang'ania yanayoonekana kutokueleweka. Mfano: Luka **(Luka 1:1-4)**

**Katika mitindo hii minne, ni upi unakuelezea vema_____,wa pili _____, wa tatu ____, wa mwisho___?**

**II. Mtendaji:**

| | |
|---|---|
| ***Anatamani hali zinazoruhusu:***<br>Uhuru, madaraka, mchanganyiko, kazi ngumu, nafasi za kuendelea, kutia moyo mmoja mmoja<br><br>***Hao walio sawa wanaweza kukuona kama:***<br>Mdanganyifu, unayejitegemea, Mfanisi, mwenye kutenda | ***Anaitikia vema kwa wengine ambao:***<br>Hutoa majibu ya moja kwa moja, hung'ang'ania kwenye biashara, hukazia maana, hutoa msukumo<br>***Hao waliotofauti wanaweza kukuona kama:***<br>Mkorofi, anayelazimisha, anayemiliki, mkali, mgumu |

**BADHI YA HATUA ZA UTEKELEZAJI**

89. Jifunza kusikiliza, kuwa mvumilivu
90. Kutoa amri kidogo
91. Endeleza kujali watu zaidi
92. Kuwa wa kuingilika zaidi na kusaidia watu
93. Elezea kwa nini vitu viko kama vilivyo

III. Mvutiaji

| | |
|---|---|
| ***Anatamani hali zinazoruhusu:***<br>Fahari, urafiki wa kimahusiano, uhuru kutokana na kusimamia mambo mengi, nafasi ya kuvutia na kusaidia wengine , mtoaji wa mawazo kiuhuru | ***Anaitikia vema kwa wengine ambao:***<br>Ni marafiki na huru, kutoa sifa na kukubalika, kutafuta kushiriki kijamii |
| ***Hao walio sawa wanaweza kukuona kama:***<br>Anayeamsha, mwenye shauku, mwigizaji, mtu mchangamfu | ***Hao walio tofauti wanaweza kukuona kama:***<br>Anayechangamshwa, majivuno, mkasilikaji, muonevu, mzungumzaji |

## BAADHI YA HATUA ZA UTEKELEZAJI

94. Uwe mwenye haraka kidogo—tathimini mawazo yako
95. Uwe wa –kuangalia matokeo zaidi
96. Tawala matendo na hisia
97. Kazania zaidi mambo/ukweli
98. Punguza, sikiliza, usiseme sana

**IV. Timu ya Mchezo**

| | |
|---|---|
| ***Anatamani hali zinazoruhusu:***<br>Uchaguzi wa kazi moja pekee, Kujihusisha na kundi, kuanzisha mtindo wa kazi, usalama, malengo wazi na mgao wa kazi | ***Anaitikia vema kwa wengine ambao:***<br>Hutumika kama marafiki, wanaruhuru mda wa kuzoea mabadiliko, wanaruhusu uhuru wa kufanya kazi katika mda wako,wanatoa msaada |
| ***Hao walio sawa wanaweza kukuona kama:***<br>Mwenye kutia moyo, utayari, wa kutegemeka, wa | ***Hao waliotofauti wanaweza kukuona kama:*** |

| | |
|---|---|
| kutegemewa | Mthibishaji, asiye stadi, mtegemezi, mzito, mnyamavu |

**BAADHI YA HATUA ZA UTEKELEZAJI**

99. Uwe mwepesi kidogo kwa yale wanayofikiria wengine
100. Uwe mnyoofu zaidi
101. Uwe na kuhusika zaidi na kazi yenyewe
102. Kutana na makabiliano na uwe mwamuzi zaidi
103. Jifunze kusema hapana
104. Fanya mengi kuanzisha utekelezaji

IV. Mwenye Fikara

| | |
|---|---|
| ***Anatamani hali zinazoruhusu:***<br>Uchaguzi wa kazi moja, Uangalifu, Upangaji, ulinzi, uimara, matatizo kidogo ya kushindwa | ***Anaitikia vema kwa wengine ambao:***<br>Hutoa hakikisho tena, anga la usaidizi, kupambanua njia na viwango |
| ***Hao walio sawa wanaweza kukuona kama:***<br><br>Mkamilifu, shupavu, wa utaratibu, kutokuwa na mzaha | ***Hao waliotofauti wanaweza kukuona kama:***<br>Mpinzani, mwenye vitu, mpekuzi, si mdanganyaji, mwenye maadili |

**BAADHI YA HATUA ZA UTEKELEZAJI**

105. Kukazania kufanya mambo yaliyo sahihi—siyo tu katika kufanya vitu kiusahihi
106. Anaitikia haraka zaidi
107. Anaanza kutumaini fikira na kukalia kidogo ukweli
108. Kuwa tayari kuchukua matatizo
109. Kuwa wazi zaidi na rahisi
110. Usiogope kuanzisha mahusiano

Matokeo haya yanakuelezea wewe? Unaweza kutaka kumshirikisha matokeo mwenzi wako au watu wengine wanaokujua vema kuona kama wanaweza kuainisha matokeo haya. Kumbuka kwamba mitindo haiendani na watu kikamilifu. Unaweza kukuta kwamba huendani kabisa na moja kati ya mitindo hii minne. Kwa watu wengi katika makundi mawili ambayo wamepa alama za juu watawekea kivuri chepesi kwenye mitindo yao.
Chukua mda fulani kushirikisha uliyojifunza kwa wafunzwa wenzio kuhusu wewe mwenyewe kufikia hatua hii. Katika vikundi vidogo, jibu maswali yafuatayo:

111. Ni mazingira gani unayopendelea kufanyia kazi?
112. Ni watu wa aina gani ambao unaitikia kwao zaidi?
113. Elezea mazingira yako halisi unayofanya kazi. Jinsi gani yanafanana na mapendeleo yao au kutofanana?
114. Umekuwa na ugumu katika kugusa watu ambao unahisi mitindo yao ni tofauti na yako mwenyewe?
115. Ni nini ulichojifunza kuhusu wewe mwenyewe ambacho hukujua kabla?
116. Ni hatua zipi unazoweza kuchukua ili kuwa mfanisi zaidi kwa watu wanaokuzunguka? Unahitaji kuwa muwazi zaidi? Unahitaji kusikiliza zaidi? Unahitaji kuwa mchangamfu zaidi?

Kwa kila moja ya makundi manne ya watu, yanaelezea uwezo na udhaifu kwa misingi ya utaratibu wa upandaji kanisa.

117. Jinsi gani watendaji wanavyokabili kazi ya upandaji kanisa? Ni nini uwezo wao na udhaifu?
118. Jinsi gani watia moyo wanavyokabili kazi ya upandaji kanisa? Ni nini uwezo wao na udhaifu?
119. Jinsi gani wachezaji wanavyokabili kazi ya upandaji kanisa? Ni nini uwezo wao na udhaifu?
120. Jinsi gani wanaofikiri wanavyokabili kazi ya upandaji kanisa? Ni nini uwezo wao na udhaifu?

**Utekezaji wa Azimio**

121. F Kama njia ya kuelewa vitengo hivi vinne, chukua watu watano unaowajua kutoka kwenye mzunguko wa marafiki zako na kimya kimya wachunguze katika hali tofauti tofauti na kisiri nukuru matendo yao au maelezo yanayochanganua mtindo wao wa mwingiliano.

122. Fikiria "hatua za utekelezaji" ambazo zinafatana na kila mtindo. Tambua miwili ambayo kwa uangalifu utaifanyia kazi kabla ya kipindi kinachofata cha mafunzo. Shirikisha hili kwa mshauri wako, na muulize mshauri kukupatia matokeo juu ya jinsi unavyofanya.

# Uongozi – Azimio la Mafunzo 9

## Hitaji la Uongozi

**I. Ni aina Gani ya Uongozi Kanisa Linahitaji?**

**A. Viongozi wa Vikundi Vidogo au Vikundi Kiini – Wafanya Majaribio (Mdo 2:46-47)**

**B. Viongozi wa Kanisa la Mtaa—Waandaaji (2 Tim 2:2)**

**C. Viongozi wa kanisa la Eneo—Wahamasishaji (1 The 3:2, Mdo 14:23)**

**D. Viongozi wa Kanisa wa Kitaifa—Wenye Fikara (Mdo 15:6-11)**

Jinsi gani ngazi hizi nne za uongozi wa kanisa zinalingana na huo unaoufahamu?

**II. Ni Viongozi wangapi kanisa Linahitaji?**

**A. Piramidi—**Uongozi wa kanisa ni kama piramidi ikiwa na viongozi wachache wanaohitajika katika ngazi ya kitaifa na wengi kwenye vikundi kiini na ngazi ya kanisa.

**B. "Kanauni ya Yethro'—Kut 18,** Kwa kufanya hesabu, Yethro alishauri 131 au asilimia 13.1 ya shirika wanatakiwa wawe viongozi. Una asilimia 15 au zaidi ya watu wako wanaoongoza?

Kufuatana na 'kanuni ya Yethro' ni viongozi wangapi wanahitajika katika jengo lako la kanisa? Ni wangapi ulio nao kwa sasa?

**III. Wapi Tunawapata Viongozi Hawa?**

Umekuwa na ugumu wa kupata viongozi unaohitaji? Kama ni hivyo, Kwa nini? Nini unachoweza Kufanya Juu ya hili?

Maswali ya kutafakari, marudio na matumizi

123. Watu wangapi katika kanisa lako wanatenda katika ngazi fulani ya uongozi?

124. Ni nini hitaji lako kuu katika huduma yako kwa kipindi hiki?

125. Nini unaweza kufanya katika kanisa lako kufunza viongozi wa kikundi kiini na kikundi kidogo?

126. Nani ni viongozi katika eneo lako? Wapi na jinsi gani wamefunzwa?

**UTEKELEZAJI WA AZIMIO**

Jifunze vipindi vya mafunzo na hitaji la uongozi katika eneo lako. Ni mafunzo yapi yanapatikana kwa kila ngazi ya uongozi? Jinsi gani unaweza kufaidika kutoka kwenye vyanzo hivi katika jengo la kanisa lako? Shirikisha matokeo yako kwa mshauri wako.

# Uongozi – Azimio la Mafunzo 10

## Kufunza Viongozi Wapya

Kwa nini maendeleo ya uongozi ni muhimu?

**I. Mifano ya Kibiblia ya Kuzidishwa kwa Uongozi**

A. **Ni nini uhusiano wa** Musa na Yoshua **unatufundisha kuhusu uongozi?** (Kut 17:9-14, 24:12-13, 33:7-11, Hes 14:6-9, Kum 31:7, 34:9)
B. **Ni nini mistari hii inatufundisha kuhusu uongozi wa** Yesu? (Yohana 1:35-51, Mat 10, 17:14-21)
**C. Elezea uongozi wa** Paulo. (2Tim 1:3, 2:2, Mdo 14:21-24, Gal 4:15, Flp 2:22-24)

Jinsi gani ulifunzwa kama kiongozi? Elezea shughuli za kujenga zilizokusaidia kuendeleza uwezo wako wa uongozi.

Ni vizazi vingapi vya uongozi vilivyoelezewa katika **2 Timotheo 2:2?**

Jinsi gani **Mathayo 4:19** inafanana na 2 Timotheo 2:2?

II. Makusudio ya Mafunzo

**Kati ya vigezo vifuatavyo vya mafunzo, ni kati ya kipi viongozi wako wana hitaji kuu zaidi? Vipawa vya kiroho, uwezo, uchukuliaji fulani, mahitaji ya huduma, uzoefu, na hadhi.**

**III. Hatua Tano za Kufundisha Viongozi Wapya**

**A. Hatua 1: "Ninaifanya"**
**B. Hatua 2: "Ninaifanya; Unaangalia"**
**C. Hatua 3: "Tunafanya Pamoja"**
**D. Hatua 4: "Unaifanya; Ninaangalia"**
**E. Hatua 5: "Unaifanya"**

Maswali ya kutafakari, marudio na matumizi

Kwa nini maendeleo ya uongozi ni muhimu?

Jinsi gani ulivyofunzwa kama kiongozi? Elezea shughuli za kujenga zilizokusaidia kuendeleza uwezo wako wa uongozi

**Utekelezaji wa Azimio**

Chukua kazi nzuri unayojua kuifanya vema kama vile kuendesha gari. Kupika chapati, au kujenga stuli ya mbao. Mfundishe mwingine kuifanya kwa kutumia hatua 5 zilizoelezewa katika somo hili. Elezea matokeo yako kwa mkufunzi au mshauri wako.

# Vikundi Kiini – Azimio la Mafunzo 10

## Majadiliano ya Maswali na Matatizo ya Kikundi Kiini

Somo hili limeandaliwa kwa ajili ya kutoa mda wa majadiliano ya mwingiliano kati ya wafunzwa. Jukumu lako ni moja la mwezeshaji, au msuluhishi, kati ya wafunzwa. Utahitaji kuwauliza wafunzwa matatizo yao au maswali. Usitoe majibu au mapendekezo wewe mwenyewe—ruhusu majibu kutoka katikati ya kikundi, kama inawezekana. Katika tukio lisilotarajiwa kwamba hakuna mmoja wa wafunzwa aliye na maswali wala matatizo, kuna baadhi ya maswali yaliyoshauriwa ya kawaida yaliyotolewa katika somo. Jaribu kutumia uzoefu wa wafunzwa kujibu maswali na matatizo yaliyotolewa wakati wa mda wa somo hili.
Sisitizia kwamba wafunzwa wanahitaji kufikiri juu ya suluhu au mapendekezo ambayo yamejadiliwa na kuonyesha jinsi yanavyoweza kutumika kwenye makundi yao. Watie moyo kuandika njia maalumu za kuonekana ambazo watatumia kutatua baadhi ya matatizo kwenye makundi yao wenyewe.

**I. Uhalisi wa Huduma ya Kikundi Kiini**

Max amekuwa akiongoza kikundi kiini kwa zaidi ya miezi mitatu. Ingawa watu sita wanakuja mara moja moja kwenye mikutano ya kikundi kiini, hawaonekani kukua sana katika imani yao, kikundi hakionyeshi haja yoyote ya kufikia watu wanaowazunguka. Wanaonekana wako tayari kukutana kila wiki, kuzungumuzia matatizo yao, na kujifunza Biblia kidogo. Max anaendelea kuchanganyikiwa zaidi na zaidi, na hajui nini la kufanya kitofauti ili kuwasaidia wajumbe wa kikundi chake kuwa wakomavu kiroho zaidi.

**II. Maswali na Matatizo**

Ni nini maswali na matatizo uliyonayo na kikundi kiini chako?

Orodha hapo chini inaweza kutumika katika tukio ambapo wafunzwa wanakuwa hawana maswali zaidi na matatizo ya kujadili.

Kuna yeyote aliye na tatizo lolote kati ya yafuatayo?

Kikundi kiini hakikui kiroho.

Kiongozi hawezi kupata kiongozi mwanafunzi.

Kikundi kiini hakitaki kuogezeka chenyewe.

Kikundi kiini hakiwezi kupata sehemu nzuri ya kukutania
Kikundi kiini hakikui kiidadi.
Baadhi ya migogoro inakuwepo kati ya wawili au zaidi wa wajumbe wa kikundi, na kiongozi anaonekana hawezi kulitatua hilo.

**III. Suluhu**

Kila kikundi kiini ni tofauti, na kila hali ya tatizo ina tabia ya kipekee. Hata hivyo, mara nyingi kuna kanuni za kawaida zinazoendana au sababu ya matatizo. Kila kiongozi wa kikundi kiini antakiwa kusikiliza kwa uangalifu kwenye mapendekezo au utatuzi uliotolewa wakati wa mda wa majadiliano wa somo hili. Kama inawezekana, anatakiwa afikirie jinsi ya kutumia kanuni za utatuzi uliotolewa kwenye kikundi kiini chake mwenyewe kama anakutana na tatizo lile lile.

**Masweali ya kutafakari, marudio na matumizi**

Ni tatizo lipi ni kubwa au udhia kwenye kikundi kiini chako? Suluhu na mapendekezo yaliyotolewa wakati wa mda huu wa darasa unaoweza kutumia kusaidia kutatua tatizo hili?

Unafahamu viongozi wengine wa kikundi kiini ambao hawakuwa katika darasa hili lakini ambao wanaweza kufaidi kutoka kwenye mda huu wa majadiliano? Jinsi gani unaweza kuwatia moyo na kushirikishana baadhi ya vitu ulivyojifunza?

Nani unayeweza kumzungumzia matatizo yanayoendela au yajayo katika vikundi kiini?

**Utekelezaji wa Azimio**

Andika matatizo makuu matatu unayokutana nayo kwenye kikundi kiini chako.

Kutokana na majadiliano ya leo, andika angalau suluhu mbili zinazowezekana kwa kila moja ya matatizo.

Omba kwa ajili ya hekima katika kuweka utatuzi ambao umemaliza kuandika. Panga kuyaweka mapema iwezekanavyo.

# Vikundi Kiini – Azimio la Mafunzo 11

## Kuzidisha kwa Kikundi Kiini

**I. Lengo la Kuzidisha—**Kuzidisha kuna maanisha nini kwa kikundi kiini chako?

**II. Utaratibu wa Kuzidisha "kikawaida"**

A. **Kuzidisha Kibaolojia**

Chagua watu wawili kutoka katika darasa lako kuja mbele ya darasa. Muulize mtu wa "kwanza" kuchagua mtu mmoja kutoka kwa wajumbe wa darasa jingine kusimama naye (kila mjumbe wa darasa anawakilisha kikundi kiini). Muulize mtu wa "pili" kuchagua mtu mmoja kutoka kwenye darasa na kusimama naye. Katika awamu nyingine, muulize mtu wa "kwanza" kuleta mtu mwingine zaidi mbele. Kisha muulize mtu wa "pili" na yule anayesimama naye kila mmoja kuchagua mtu mmoja wa kuungana nao (kwa hiyo kundi hili linaongezeka kwa wawili). Endeleza hili mpaka darasa zima linakuwa kati ya moja ya makundi mawili. "Kundi la pili" litakuwa kubwa zaidi kwa sababu limekua kwa kuzidisha – kwa kila awamu, kila mjumbe wa kundi hili ameleta mbele mtu mwingine. Kundi la "kwanza" litakuwa limeleta mbele ya darasa mtu mpya mmoja tu kwa kila awamu. Jadili jinsi kuwa na viongozi wa kila kundi jipya bado linaanzisha kundi jingine jipya la kikundi kiini (KUZIDISHA) ni kuzuri zaidi kuliko kuwa tu na kiongozi wa kikundi kiini cha mwanzo kuanzisha makundi machache (KUONGEZA).

B. **vishada vya Asili**—katika kugawanyika katika vikundi kiini viwili, fikiria urafiki kati kati ya kundi lililopo. Tambua jinsi watu kiasili wanavyojigawa katika vijikundi mnapounda makundi madogo zaidi ya majadiliano.

Unaweza kuona jinsi inavyowezekana kuweka kikundi kiini katika vishada? Hili linaweza kuwa msaada katika kuanzisha vikundi kiini vipya? Inaweza kuwa msaada katika kuainisha viongozi wanafunzi maarufu?

**III. Hatua katika Kuzidisha**

Kuandaa Kwa Ajili ya Kuzidisha kwa Kikundi Kiini

1. Kuendelea kutoa maono ya kugawanyika mbeleni kuwa mawili (weka tarehe iliyopangwa)
   Tia moyo kufikia nje kwa wasioamini
   Anzisha ufuasishaji kati ya waumini
   Mshauri kiongozi mwanafunzi.
2. Uwekaji wa Kuzidisha kwa Kikundi Kiini
   Jadili mabadiliko yanayokuja
   Onyesha nani ataongoza kundi lipi
   Amua nani atakuwa katika kundi lipi
   Chagua eneo la mkutano
   Endelea kumshauri kiongozi mwanafunzi baada ya kuzidisha
   Fanya tarehe ya mwisho ya kikundi cha mwanzo kuwa ya kusherehekea

**III. Vizuizi Kwenye Kuzidisha**

Kwa kila tatizo hapo chini, waulize darasa kutoa suluhu lao. Kisha soma mapendekezo yaliyotolewa.

| **Tatizo** | **Mapendekezo** |
|---|---|
| Kundi halielewi umuhimu wa kuzidisha. | • Kiongozi wa kikundi kiini lazima asitoe tu maono ya kuzidisha, lakini lazima pia aeleze kwa nini kuzidisha ni muhimu hivyo. Wajumbewa kikundi kiini lazima waelewe ni faida zipi zipo kwa ajili ya kundi na kwenye kuendeleza ufalme wa Mungu. |
| Kundi linaelewe hitaji la kuzidi, lakini wameridhika na mmoja kwa mwingine na hawataki kugawanyika. | • Omba kwamba Roho Mtakatifu atakupa hekima katika kulielewa kundi lako na hali yako ya kipekee.<br>• Kazia umuhimu wa kuzidisha na elezea kwamba ni hatua inayofata katika mwendelezo wa asili wa maisha ya kundi.<br>• Toa kielelezo cha jinsi gani kuzidisha kumekuwa utii kwenye amri ya Mungu ya "kwenda na kufanya wanafunzi" katika Mt. 28:19. Kupitia kuzidisha, kikundi chako kiini kina wajibu muhimu na bayana katika kusaidia kutimiza Utume Mkuu.<br>• Omba kwa ajili ya kugawa kundi katika mipaka ya asili, ukitumia sura ya vishada. |
| Hakuna kiongozi mwanafunzi. | • Kwanza, kiongozi wa kikundi kiini lazima atumie mda katika maombi, akimuonmba Roho Mtakatifu kumpa hekima juu ya nani wa kuchagua. Kisha, kimakusudi anatakiwa afanye uamzi huu na kuanza kufuasa na kushauri mwanafunzi.<br>• Tumia vishada katika kikundi kiini chako kuweza kuainisha kiasili viongozi wanaoibuka. Omba kwa ajili ya watu hawa kama viongozi mashuhuri wanafunzi kwa ajili ya kundi jipya.<br>• Katika mipaka ya kuchagua kiongozi mwanafunzi, fanya marudio ya Somo la Kikundi Kiini katika Mwongozi wa 3, "Kuwafunza Viongozi Wapya wa Kikundi Kiini" |
| Kuna kutokuelewana nani aenda na kundi lipi. | • Kama kundi lako lina vishada kadhaa, fikiria kutumia kishada kimoja au zaidi kuanza kundi jipya. Fikiria mipaka ya mahusiano ya asili kwenye kundi.<br>• Muombe kila mjumbe wa kundi kuomba na kumuomba Roho Mtakatifu kuliweka wazi kwake juu ya kundi lipi la kuweza kujiunga.<br>• Endesha majadiliano wazi ya kweli kwenye mkutano wa kikundi kiini kutafuta sababu ya kukosekana kwa umoja kwenye uamzi huo. |

**Maswali ya kutafakari, marudio na matumizi**
Jinsi gani kuzidisha katika vikundi kiini kunasaida kuendeleza kueneza harakati za upandaji wa kanisa?

Nini ni "vishada vya asili" katika kikundi kiini? Jinsi gani vinaweza kutumika kusaida kundi kuhamia kwenye ngazi ya kuzidisha? Nini kinaweza kutokea kundi linapokuwa tayari kuzidi na wajumbe wa kundi lake wamegawanyika bila utaratibu, pasipo na kufikiria mahusiano katika kundi?

Jinsi gani vishada vinaweza kutumia kusaidia kugundua viongozi mashuhuri wa vikundi kiini?

Ni vizuizi vipi vya kawaida kwenye kuzidisha katika kikundi kiini? Jinsi gani vinaweza kushindwa?

**Utekelezaji wa Azimio**

- Vishada katika kikundi kiini wakati mwingine vitaibuka kiasili tu, Kama vikundi vyako havina tayari vishada ndani yake, fikiria kuvitumia wakati wa sehemu tofauti za mkutano wa kikundi kiini. Unaona faida yoyote ya kutumia vishada katika makundi yako?
- Anza kufikira nini kinatakiwa kitokee katika kila moja ya makundi yako ili kufikia lengo la kuzidisha. Andika vitu vitano ambavyo utafanya katika miezi mitatu ijayo ili kuyasogeza makundi yako karibu na kwenye kuzidisha.
- Fikira juu ya vizuizi mashuhuri kwenye kuzidisha katika kila moja ya makundi yako. Nini unachoweza kufanya kabla ya mda kuvishinda na kuepuka matatizo unapokuwa mda wa kuzidisha?
- Anzisha mpango wa kuzidisha katika makundi yako. Hakikisha unawaweka viongozi wako wanafunzi kwenye utaratibu huu ili kwamba nao waweze kuandaliwa kupanga kwa ajili ya kuzidisha kwenye makundi yao. Omba kwa ajili ya kuzidisha na weka pamoja na tarehe ya kuzidisha katika mpango wako kwa kila kundi. Tafuta mtu fulani atakayekuwajibisha katika uwekaji wa mpango huu wa kuzidisha.

WANAFUNZI WOTE WAPANDA KANISA LAZIMA WALETE "AZIMIO LA UFUASISHAJI LILILOKAMILIKA" (KUTOKA ZIADA 5A, MWONGOZO WA TATU) KWENYE KIPINDI KINACHOFATA CHA UFUASISHAJI.

# Ufuasishaji – Azimio la Mafunzo 6

## **Warsha ya Ufuasishaji:** Majadiliano ya Maswala ya kivitendo Yanayoendana na Ufuasishaji

Unda vibao vya matangazo au mashine ya kuonyeshea maandishi ubaoni ya Azimio la Kufuasa (kutoka Ziada 5A, Mwongozo wa Tatu) la kukamilisha wakati wa majadiliano ya kundi kubwa. Hili linaweza kuhitajika kama majadiliano ya kundi dogo hayawezekani kwa sababu ya kumaliza vibaya kazi iliyokuwa imetolewa. Ni ya lazima kwamba wafunzwa wanafanyia kazi utaratibu na kufikiria maswala na mfuatano wa kufanya ufuasishaji. Ili kufanya matumizi mazuri ya mda uliotolewa kwa ajili ya kipindi hiki katika kufanya ufuasishaji, ni muhimu kwamba washiriki wanahamia kwa haraka kwenye makundi madogo ya watu 5 mpaka 8. Wakilisha maswali au yaweke ubaoni.

**I. Majadiliano ya Kikundi Kidogo( Dakika 30)**
Umekuta zoezi hili la "Azimio la Kufuasa" kivitendo likifaa kutumika katika huduma yako? Jinsi gani?
Jinsi gani umeonyesha utaratibu ambao ungetumia kugusia maswala?
Ni vitu gani vya ufatiliaji (ujuzi sura, au thamani) unavyoamini lazima viwemo katika miezi ya kwanza ya maisha ya mkristo? Kwa nini haya ni muhimu sana? Jinsi gani unaweza ______ (kuchukua kitu kimoja) ambacho kinaweza kuendelezwa zaidi katika maisha ya muumini au kanisa?
Jinsi gani wewe binafsi ulishawishiwa na umuhimu wa ______ (swala/ukweli/ujuzi au wazo)?
Ni mifumo ipi ambayo unaridhika nayo zaidi?
Umejaribu kuwianisha mifumo ili kwamba mmoja au miwili isitumike zaidi au kuachwa?
Unafanya nini kueneza kazi ya kufanya ufuasishaji mahali ulipo? Jinsi gani unaandaa "wafuasishaji"?
Nini utafanya wiki ijayo kuwasogeza wanafunzi mbele kwenye imani yao, tumaini na upendo?

**II. Warsha ya Kufuasa (Dakika 20 kwa darasa zima)**

Elezea tukio, mkasa au shughuli ambayo ulikuwa umehusika mwanzoni mwa maisha yako ya ukristo ambayo bila mashaka ilikusaida kuendelea katika kutembea kwako na Kristo.

Ni kipande kipi cha ukweli unachoweza kurithisha kwa hao wanaoanza kufanya wanafunzi?

**Utekelezaji wa Azimio**

Katika mwanga wa majadiliano wakati wa warsha hii, fanya marudio na tathimini mpango wa ufuasishaji ulioandaa baada ya mafunzo ya Mwongozo wa Tatu kwa kila mtu unayemfuasa katika huduma yako ya upandaji kanisa. Fanya mabadiliko yoyote ya lazima kwenye mipango yako kufuatana na ulichojifunza wakati wa warsha hii. Kumbuka kwamba mipango uliyounda siyo ya kitakwimu—itabadilika na inatakiwa ibadilike kulingana na mda na ukuaji katika sehemu ya wanafunzi wako. Kwa vipindi fanya marudio na rekebisha azimio la kufuasa ulilo nalo kwa kila mwanafunzi wako. Endelea kufikiria kufuasa kama njia ya kuzaliana mwenyewe katika maisha ya wengine na kuzidisha wafanyakazi wanaoweza kufikia kijiji chenu, wilaya, miji na nchi kwa ajili ya Kristo.

# Uwakili – Azimio la Mafunzo 1

## Utangulizi kwenye Uwakili

Ni vitu gani ambavyo Mungu amekupatia? (Viorodheshe ubaoni)

**I. Uwakili ni nini?**

Ni nini neno uwakili, linachomaanisha kwako? Ni nini kinakuja akilini mwako unaposikia neno hili?

**II. Kwa nini Kuzungumzia Uwakili?** Maswala mawili?

A. **Swala la Uaminifu**

Kuwa wakili mwema, ni nini unachotakiwa kuamini?

B. Swala la Thamani

**Yesu aliposema, "Palipo na mali zako ndipo moyo wako utakapokuwa pia," Alimaanisha nini?**

Ni vitu gani unathamini zaidi?
Jinsi gani unaweza kutoa kila moja ya vitu hivi kwa Mungu?
Jinsi gani tunaweza kumtumikia Mungu kila siku?
Fikiria mtu fualani ambaye ni jirani yako. Jinsi gani unaweza kumuhudumia mtu huyo vema?
Ni mtu gani Mungu amemuweka chini ya uangalizi wako? Jinsi gani unaweza kutawala rasilimali zako vema (fedha, mda, uangalizi, n.k.) kumuhudumia mtu huyo?

**III. Kanuni za uwakili katika Biblia**

**A. Nani alikuwa Wakili katika Agano Jipya? (Luka 12:42, 16:1-3, 1 Kor 4:1)**

B. **Uwakili katika Mifano**

1. Wakili Mwema ni Mwaminifu (**Luka 12:42-48)**
2. Wakili mwelevu anatumia nafasi yake kuandaa kwa ajili ya mbeleni (**Luka 16:1-12)**
3. Mawakili Watatathiminiwa Kufuatana na Uwezo Wao (**Mat 25:14-30)**

**C. Hesabu**

Ni kwa nani tunatoa hesabu yetu ya uwakili? **(Rum 14:12)** Ni nini tunachowajibika kwacho? (**2 Kor 5:10**)

IV. **Uwakili wetu** - Tu mawakili juu ya nini?

A. Fedha Zetu
B. Mda Wetu **(Efe 5:15-17, 2:10)**
C. Mali Zetu
D. Miili yetu **(1 Kor 6:19)**
E. Familia Zetu
**F.** Huduma Zetu **(1 Pet 4:10)**

- Ni eneo lipi ni gumu zaidi kutawala? Kwa nini?
- Una tabia kama za mtu anayempenda Mungu na wengine? (Mt 22:37-39) Namna unavyotumia mda wako, mali, mwili, familia, huduma, n.k. vinakubaliana na hili?
- Ni rasilimali zipi Mungu amekupatia? Ziorodheshe.
- Masikini anaweza kumtolea Mungu hasa? Anatakiwa? Kwa kiasi gani?
- Jinsi gani thamani ilivyo muhimu kwenye majadiliano ya uwakili?

- Ni yupi ni mfano muhimu zaidi wa uwakili kwa watu kwenye kikundi kiini chako?

# Uwakili – Azimio la Mafunzo 2

## Uwakili wa Hazina

Jaribu kuepuka mjadala uliochemshwa kwenye swala la utoaji wa zaka. Wazo kuu la somo hili ni kwamba tunawajibika kutumia pesa kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Kazania katika swala hilo, ambalo linaendana bila kujali anachoamini mtu mwingine kuhusu utoaji wa zaka

**I. Kuipeleleza Biblia**

A. Utoaji zaka katika sheria ya **Agano la Kale**– **Law. 27:30-32; Mal. 3:8-12**
B. **Sadaka ya kujitolea** kwa ajili ya Hema – **Kut 25:1-8**
C. **Kielezo cha Daudi cha kutoa** kwa ajili ya jengo la Hekalu – **1Nya 29:1-20**
**D. Kutoa nje ya Umasikini-- Luka 21:1-4**
**E.** Ufadhili kwa **Viongozi wa kanisa la Agano la Kale – 1Kor 9:4-14; 1Tim 5:18**
F. **Ukusanyaji kwa ajili ya Watakatifu wa Yerusalemu – 1Kor 16:1-2; 2 Kor 8:1-6**

**II. Utoaji wa Binafsi**

Kanuni zifuatazo zinaelekeza utoaji kwa waumini:

127. Kila muumini anatakiwa atoe.
128. Utoaji wetu unatakiwa uwe unaendana na kipato chetu, zote tasilimu na zisizo tasilimu. Fikiria kama Mungu amefanya kipato chako kulingana na utoaji wako!
129. Tunatakiwa kutoa hata katika umasikini wetu.
130. Tunatakiwa tutoe kwa ukarimu na kwa sababu tunapenda kufanya hivyo—siyo kwa sababu mtu anatulazimisha. Utoaji lazima utokane na utayari wa moyo ili kumpendeza Mungu.
131. Tunatakiwa tutoe zaidi ya tunavyoweza (tukimutumaini Mungu).
132. Utoaji wetu wa fedha unatakiwa ufate kujitoa kwetu wenyewe kwa Mungu. Utoaji ni kuonyesha kujitoa kwetu kwa Mungu.

Katika makundi madogo, jadili kanuni kwa kutumia maswali yafuatayo: (Dakika 15-20)

- Kuna waumini ambao hawakuweza kutoa kwa Bwana kwa sababu ya umasikini wao?
- Kama kipato cha watu hapa kilikuwa sawa na utoaji wao hii itamaanisha nini kwa kipato katika mkoa huu?
- Kwa nini muumini atoe kwa Bwana
- Ni nini unachofikiri juu ya wazo kwamba tunatakiwa kutoa zaidi ya tuwezavyo, tukimutumaini Mungu?
- Kuna chochote cha kupata kutokana na utoaji kifedha tunapokuwa hatujajitoa wenyewe kwa Mungu?
- Umeona Mungu akionyesha upendo wake kwa kutoa kwako kwa njia ya kushangaza?
- Ni nini **1 Fal. 17:7-16** inashauri kwako kuhusu utoaji wa uaminifu?
- Ni nini kanuni kuu za utoaji katika **2 Kor. 9:6-11**?

**III. Hazina za Kanisa la Mtaa**

A. **Makanisa Yanayojisaidia**

Ni nini faida kwa kanisa mpya kwa kujisaida lenyewe?

**B. Kutunza Fundi za Kanisa**

1. Fundisha utaratibu wa utoaji
2. Anzisha mfumo unaokubalika kwa gharama zilizokadiriwa za matumizi na bajeti iliyowekwa
3. Funza na toa mhasibu wa Kanisa-mfumo wa ukusanyaji na usambazaji wa hazina unatakiwa uwe na: watu kadhaa,upangaji kimaombi, uwajibikaji, ukusanyaji wa mara moja moja, utunzaji wa kumbukumbu, na utoaji wa taarifa wa mara kwa mara.

**IV. Utoaji fedha na harakati za Upandakji Kanisa**

133. Uko tayari kutoa zaidi ya uwezo wako, kama wamasedonia? (jibu la pekee tu)
134. Nini wakristo wapya wanatakiwa wafundishwe kuhusiana na utoaji?

135. Unaonyesha kiasi chako cha zaka kufuatana na kipato chako tasilimu tu, au vile vile na vyanzo vingine ambavyo Mungu amekubariki navyo?

136. Jinsi gani unaweza kuelezea utoaji kwa asiye mkristo anayefikiri kwamba makanisa yanaomba pesa tu?

137. Ni matokeo yapi mafungu ya nje yaliyo nayo kwa kanisa la mtaa?

**Action Plan**

Ordhesha mapato yako kutoka katika vyanzo vyote (yakiwemo na yasiyo tasilimu) na utoaji wako kwa wiki au mwezi. Hili ni kati yako na Mungu. Piga hesabu ni asilimia ngapi umempa. Unapendezwa na hili? Anapendezwa? Gawanya jumla ya matoleo ya kanisa lako kwa mwezi kwa idadi ya watu wazima waliowakilishwa kupata wastani wa utoaji kila mwezi kwa watu wazima. Zidisha tarakimu hizo kwa kumi kuona ni kiasi gani kila mtu mzima atakuwa nacho kuishi kila mwezi kama kweli matoleo yao yamewakilisha zaka. Unafikiri kanisa lako linaendeleaje? Wanahitaji maelekezo zaidi kwenye eneo hili? Kama ni hivyo, anzisha mpango wa kuwafundisha. Kumbuka kwamba kusudi la hili ni kuwasaidia waelewe uwakili, na siyo kutaka kutunga sheria ya kutaka utoaji ambayo italazimisha. Mungu anawapenda hao wanaotoa kwa uhuru.

# Uwakili – Azimio la Mafunzo 3

## Matumizi ya Mda

| |
|---|
| Inapendekezwa sana kwamba mkufunzi anaanza kujiandaa kwa ajili ya somo hili vya kutosha kabla ili kuipitia sehemu ya "Uwekaji wa Kimazoezi' mwenyewe. Kwa kifupi somo hili litachukua zaidi kwenye maana kama mkufunzi ana uzoefu binafsi wa kimazoezi na zoezi hili. Chukua mda kushirikisha uzoefu wako wa mafanikio/kushindwa katika kuweka muhutasari na kuainisha ratiba, vile vile na upangaji wa malengo yako, kujumlisha ratiba mpya ya kila siku ambayo inatokana na kufanyia kazi zoezi hili. Kadiri utakavyolifanya zaidi somo hili kuwa la binafsi ndivyo litakavyokuwa na mguso zaidi kwa hao unaowafunza. |

Utunzaji wa mda kikamilifu kunaweza kukusaidia kutawala mda wako badala ya mda kukutawala.

**I. Anzisha Vipao Mbele – Kujifunza jinsi ya kutunza mda**

- **A.** Ni **Kanuni Zipi za Kibiblia za Kutunza Mda** Unazoweza **k**upata katika mistari hii? **(Zab 24:1, Yos 24:15, Efe 5:15-17, 1 Pet 4:10, Omb 3:1-8)**
- B. Ni baadhi ya vitu gani vinatakiwa kuwa **kipao mbele kwa mpanda kanisa? (1 Tim 3:4-5, Tit 1:6, Efe 4:11-13, Mat 14:23, 28:19-20)**
- C. Ni kipi kati ya hivi ni kipaombele cha juu? Cha pili? Cha tatu? Elezea?

**II. Uwekaji kivitendo** (zoezi)

- A. Weka Kitabu cha matumizi ya Mda Uliopo – Kipekee, andaa kalenda ya wiki moja ikiwa na safu za siku za wiki na mihimili kwa saa za siku. Kwa wiki iliyopita, kumbuka na andika jinsi ulivyotumia kila saa ya wiki.
- B. Kufuatana na kalenda yako, ainisha maeneo makuu ambayo umetumia mda wako na mda kiasi gani umetumia kwa kila moja.

Nyumbulisha Matumizi ya Mda wako

138. Ni shughuli zipi unafanya kwa kurudia rudia?

139. Unatoa kipao mbele kwenye maeneo muhimu zaidi ya maisha yako?

140. Kuna kuingilia kunakoendelea kwa mda uliopotea?

141. Ni mabadiliko yapi maalumu unayotaka kufanya kwenye ratiba yako?

142. Je munyumbulisho wa matumizi ya mda wako unaonyesha vipao mbele hivi? Ni marekebisho yapi ungependa kuweka?

- C. Panga kwa wiki yako ijayo, ukionyesha siku na mda utakaofanya shughuli tofauti tofauti za maisha yako.

Uwe mwangalifu kutoa kisasi cha mda unaofaa kwa vitu hivyo ambavyo ni muhimu zaidi.

143. Soma **Luka 4:42-44, 6:12-19,9:14-21,11:1-13.** Tambua vipao mbela vya Mary na Martha. Jinsi gani mistari hii inaendana na somo hili? Ni yupi kati ya watu hawa unafanana naye zaidi?

144. Soma **Luka 4,6,9,11.** Tambua jinsi Yesu alivyotenga mda wa kuomba. Unafanya hili vile vile? Unaomba pamoja na mwenzi wako mara moja moja kuhusiana na maisha yako na huduma?

145. Kusoma kwa uangalifu kwa **Luka 9:51-62** kunaonyesha kwamba Yesu alikuwa na kazi fulani ambazo alitakiwa kuzikamilisha kwa mda wa kipindi fulani. Nini ilikuwa kazi hiyo? Umuhimu wa kazi hii ulikuwa na matokeo yoyote juu ya uhusiano wake na watu? Unafikiri kwamba kimakusudi alipanga kwa ajili ya mda wa ziada kwenye kazi hii ili kwamba aweze kuendelea kukazania kwenye mahusiano?

146. Soma **Kutoka 18** na tambua jinsi Musa alivyotatua tatizo la matumizi ya mda wake.

147. Soma mfano wa talanta unaopatikana katika **Mathayo 25:14-30.** Badilisha neno "talanta" kwa neno "miaka" na jina lako kwa jina la mtumishi wa kwanza aliyepokea talanta tano. Umepata miaka mitano kutoka kwa Bwana. Shirikisha ambavyo umewekeza katika mda wa Mungu ambao anakusifu na hatimaye kumuletea utukufu.

**Utekelezaji wa Azimio**

Soma kitabu cha Nehemia na angalia matukio ambapo Nehemia alionyesha hali yoyote ya matumizi ya mda ambayo yamezungumziwa katika somo hili.

# Uwakili – Azimio la Mafunzo 4

## Utaratibu wa Upangaji Kimkakati

I. Nini Maana ya Upangaji Kimkakati? **Jib**: **Ni utaratibu wa kuhakikisha kwamba watu, huduma, shughuli, na rasilimali vinatumika kuridhisha na kwa ufanisi kuhamia kwenye mwelekeo na kupata matokeo kwenye "Z."**

II. Hatua Katika Utaratibu wa Kupanga Kimkakati

| |
|---|
| Fanya darasa lote kufanyia kazi kuazimia kimkakatia kuanzisha kanisa lao mpya. Utaongeza maswali unapoendelea na zoezi hili. Maswali hapo chini yanaweza pia kutumika. |

**A. Hatua 1: Omba**

Ni vitu gani utahusisha katika maombi yako kwa ajili ya kanisa mpya?
Ni sifa na shukurani zipi ambazo unaweza kutoa?
Ni maombezi gani unaweza kufanya

**B. Hatua 2: Andika au Fanya Marudio ya Maelezo Yako ya Kusudi**

Kwa nini kanisa hili mpya liwepo?
Andika maelezo ya kusudi kwa sentensi moja
Maelezo haya yanaonyesha sababu yote ya kuanzisha kanisa mpya hapa?

**C. Hatua 3: Onyesha Thamani ya Kati na Utofauti**

Ni thamani zipi za kati ni msingi wa kuanzishwa kwa kanisa mpya?
Ni utofauti gani ni msingi wa kuanzishwa kwa kanisa mpya?
Thamani hizi zinaonyesha thamani kibiblia?
Kuna hao ambao wangependa kuongeza, kufuta, au kubadilisha maelezo ya thamani au utofauti?

**D. Hatua 4: Tambua Makusudio Yako**

Ni vitu gani tungeweza kufanya kama tungechukua mkakati huu?
Ni nini kikuu kinachosukuma huduma hii?
Ni nini mwelekeo kwa ujumla ambao timu itaelekeza juhudi zake?
Kwenye orodha ya makusudi chini, ni ipi tungehusiha kwa azimio hili?

148. Kutafiti eneo linalolengwa na watu

149. Hamasisha maombi kwa ajili ya upandaji kanisa

150. Injilisha

151. Funza na shauri viongozi kwa makanisa yanayoibuka

152. Funza na shauri wapanda kanisa

153. Endeleza vikundi kiini vinavyozaliana

154. Hamasisha makanisa mengine kwenye eneo kwa ajili ya upandaji kanisa

**E. Hatua 5: Weka malengo**

Kama zoezi tu, ainisha malengo mawili ambayo timu lazima iweke.
Tathimini malengo haya kwa misingi ya tabia hapo chini:

155. **Kwango cha Mda**. Kiwango cha mda maalumu wa kumaliza. MFANO: Kufikia MWISHONI MWA MWEZA WA SITA...

156. **Kuweza Kumalizika**. Mfanye mtu "kujikunjua" ili kuweza kumaliza kazi lakini inawezekana. MFANO: ANDAA MASOMO MATATU YA KUJIFUNZA KWA KUFATA NENO...

157. **Kupimika**. Weka pamoja na njia za kupimia endapo au la limefikiwa. KWA MFANO: KUONGOZA MAFUNZO YALIYOANDALIWA KATIKA KIKUNDI KIINI CHANGU...

158. **Lugha Wazi**. Lugha wazi, na makini kuwasilisha kazi zinazohitajika kukamilika.

**Mfano wa Lengo:** Mwishoni mwa mwezi wa sita nitaandaa na kuongoza mfuatano wa masomo matatu ya kujifunza kwa kufuata neno kwenye kikundi kiini changu juu ya kisa cha "Utume Mkuu na Upandaji kanisa katika mji wetu."

159. Nini tofauti kati ya upangaji kimkakati na kupangilia vema?

160. Unaweza kufikiri maeneo mengine ya maisha ambapo upangaji kimkakati unaweza kutumika?

161. Ni mifano ipi mingine ya maandiko, au kutoka katika maisha yako mwenyewe, ambapo umeona upangaji kiufanisi ukipelekea kwenye matokeo yenye ufanisi?

162. Jinsi gani unaweza kuitikia kwenye maelezo, "Mazao ya malengo yasiyo dhahiri, kwa hali ya juu, yana matokeo yasiyo dhahiri"?

163. Ni kwa njia zipi watu katika utamaduni wako wanachangia mawazo kutatua matatizo?

**Utekelezaji wa Azimio**

Fanya upangaji wa kimkakati pamoja na timu yako au uongozi wa kanisa lako linaloibuka. Uwe tayari kushirikisha mpango wako wa kimkakati kwenye kipindi kijacho cha mafunzo.

# Uwakili – Azimio la Mafunzo 5

## Warsha ya Utaratibu wa Upangaji Kimkakati

Jipange katika makundi ya watu wanne au watano kila moja na fanya kazi kana kwamba ni timu ya upandaji kanisa. Jitwalie kuwa mmeshakuwa na maelezo ya kusudi la huduma na thamani ya kiini na utofauti.

Kama timu mumeweka makusudio ya huduma kuwa na siku za mapumziko kwenda kufundisha vijana. Kazi sasa ni kuanzisha aina zifuatazo za malengo kama kielelezo cha tabia zilizofundishwa katika masomo yaliyopita.

Anzisha lengo la jumla kwa ajili ya mafunzo ya siku za mapumziko.

Anzisha lengo kwa ajili ya shughuli maalumu wakati wa mafunzo.

Uwe na uhakika kuyaangalia malengo yako dhidi ya tabia zilizotolewa kwenye somo la mwisho kuhakikisha zinafikia sifa za malengo mazuri.

Una dakika thelathini za kufanyia kazi shughuli hii. Mwishoni mwa mda huu tutaruhusu kila kundi kushirikisha malengo yake kwa ajili ya kutazama upya na kutathiminiwa na darasa.

# Familia – Azimio la Mafunzo 1

## Jukumu la Kibiblia katika Familia

**I. Wenzi waliooana (1 Tim 3:5)**

A. **Kanuni tatu Zinazoelekeza**

1. **Mme na Mke** Wana thamani sawa.
   Kutoka **Gal 3:28** tunafahamu kuwa Mungu ameumba mme na mke wakiwa na haki sawa.

2. **Mme na mke** wanatakiwa kutegemeana.
   Katika **1 Kor 11:11**, tunaona kwamba Mungu ameumba mme na mke kutegemeana. (Kuishi na kupendana na kusifiana mmoja kwa mwingine.)

3. **Kuna** utaratibu wa kuwajibika katika **familia.**
   **1 Kor 11:3**) Mungu ameumba utaratibu wa kuwajibika katika familia. Mungu ni kichwa cha Kristo, Ambaye ni kchwa cha mwanaume, ambaye ni kchwa cha mke.

Ina maana gani kwamba mme na mke wanatakiwa kutegemeana? Jinsi gani hili ni tofauti na kutegemea na kutoka kujitegemea?

Elezea mme na me ambao ni mfano wa kutegemeana.

**II. Wajibu wa Mme**

A. **Kuwa Kichwa cha Mke: (Waefeso 5:23)**

Kama mme anamuongoza mke kama Kristo anavyoongoza kanisa, jinsi gani mme ataenenda? Kujitoa mwenyewe ni sehemu ya uongozi wa mme?

Ni nini baadhi ya mifano ya wanaume wanaojitoa kwa wake zao?

**B. Kutunza Mahitaji ya kati ya Mke (Efe 5:25-29, 1 Tim 5:8, 1 Pet 3:7)**

Ni upi mfano bora zaidi unaojua ambao mme alimtunza mke?

**C. Kufanya Kazi za Baba (Efe 6:4, De 6:7, Mit 19:18, 22:6, 23:13-14, 29:17).**

**III. Wajibu wa Mke**

**A. Msaidizi-Mwa -2:18**

**B. Anayeunga Mkono-1 Pet 3:2**

**C. Mtiifu-1 Pet 3:1**

**D. Msimamizi –Mit. 31:11**

**E. Mama-Tit. 2:4**

Unafikiri majukumu yaliyoelezewa katika sehemu hii ya somo yanaheshimika na kuthaminiwa kwa mke?

Majukumu haya yanamuweka mke katika nafasi ya chini kiroho machoni pa Mungu? Katika macho ya ulimwengu?

**IV. Wajibu wa Watoto**

**A. Kuwatii Wazazi wao katika Bwana—Efe 6:1**

B. **Kuwaheshimu Baba na Mama—Efe 6:2-3, Kum 5:16**

C. Kama ni mtu bachela, jinsi gani somo linaweza kuwa la faida kwako na huduma yako?

D. Kama umeoa, unaweza kusema kwamba ndoa yako inaonyesha kioo cha sura ya Mungu kwa kuonyesha umoja?

164. Unapata umwandani katika ndoa yako? Inaonekana je?

165. Ni vigezo vipi katika jamii na katika ndoa vinafanya ugumu leo wa kuwa mwenzi mfanisi? Ni mahangaiko yapi makubwa katika kuwa wenzi wazuri?

166. Ni vigezo vipi katika jamii na katika kanisa vinavyofanya vigumu kuishi kama bachela leo? Ni mahangaiko yapi katika kuwa bachela?

**UTEKELEZAJI WA AZIMIO**

167. Soma 1 Petro 3:8-12. Tabia ya ubinafsi inaharibu umojao. Kwa kulifikiria hili, soma kwa mara nyingine kifungu hapo juu na kisha orodhesha vitu unavyotakiwa kufanya wakati mwenzi wako anapokuwa mbinafsi.

168. Uongozi wa kitumishi wa mme ndiyo kitu pekee kinachomfanya mke kuweza kutii. Mme wa kutendewa anafanya utiifu kutowezekana na mwanaume anayetawala anafanya utiifu kutovumilika. Uongozi wa kitumishi, kwa upande mwingine, unafanya kutii kuwa furaha. Kwa mwanga wa mawazo haya, jibu maswali yafuatayo:
   - Jinsi gani kuwa kwako kiongozi mtumishi kutagusa uwezo wa mke wako kuwa mtiifu?
   - Jinsi gani anaitikia katika maeneo mengine kama ungekuwa zaidi kiongozi mtumishi?
   - Je Biblia inafundisha kitu chochote kuhusu kwa nani wanawake bachela wanatakiwa wamtii? Ni mipaka ipi unayoweza kupata?

169. Katika barua yake kwa kanisa la Filipi, Paulo aligusia swala la umoja miongoni mwa wakristo. Soma Wafilipi 2:1-4 na kisha fikiria jinsi mstari 2 unavyoelezea kupata umoja kwenye mahusiano. Jinsi gani unaweza kutumia kanuni hizi katika maisha yako ya familia, iwe katika ndoa au kwenye mahusiano mengine ya familia?

170. Kama wapanda kanisa mtakuwa na nafasi nyingi kutoa ushauri wa kibiblia kwa wasioamini na wanaoamini waliopata shida kutokana na ndoa zilizoshindwa au ambao kwa wakati huo wanakutana na kutokuwa na umoja katika ndoa zao. Vile vile, utakuwa na nafasi ya kutoa ushauri kwa wanaume na wanawake wanaotaka kuoana. Anzisha majadiliano ya kundi dogo na wanaume wasiooa na wanawake wa umri wako wanaotaka kuoana mbeleni. Waongoze katika kugundua vipande vya kibiblia vilivyojadiliwa katika somo hili na fanyia kwa vitendo vipande hivi

# Familia – Azimio la Mafunzo 2

## Kulea

Je njia wazazi wanayojilinganisha kwa watoto wao inaonyeshwa na jinsi wanavyojilinganisha kwenye kanisa **(1 Tim. 3:4-5)?** Kwa jinsi gani?

**I. Baadhi ya Uchunguzi wa awali**

A. **Hakuna hakika**

Wengine wanabisha kwamba **Mit. 22:6** inatoa kanuni badala ya ahadi inayohakikisha. Unafikiria nini?

**B. Hakuna Mtoto Aliye kamili**

Unaweza ukafikiria "tu aliye kimili"

Kwa nini hakuna mtoto aliye kamili?

**C. Hakuna Mzazi Aliye Kamili**

Ni nini **1 Yohana 1:8-10** inachofanya kwa kutokuwa kamili kwetu kama wazazi?

Dhambi zetu na kukosekana kwa ukaribu kwa Mungu ni mzizi wa kushindwa kwetu kama wazazi?

**II. Baadhi ya Kanuni za Kibiblia**

Katika makundi madogo, jadili maandiko chini kwa misingi ya kile tunachoweza kujifunza kutoka kwake kuhusu kuwa wazazi:

**A. Eleleza Upendo na Utii kwa Bwana (Kut. 6:4-9,17)**

**B. Waelekeze Watoto wako Kutunza Njia ya Bwana (Mwa. 18:19)**

C. **Usighadhibishe Watoto Wako (Efe 6:4)**

171. Ni baadhi ya njia zipi za kivitendo unazoweza kufanya upendo na utii mtindo wa maisha kwa Bwana nyumbani kwako?

172. Ni baadhi ya njia zipi za kivitendo unazoweza kuona kama malezi yako yanafanyika nje ya upendo? Nini unachofikiria kizuizi kikuu kwa aina hiyo ya malezi?

173. Ni vitu vipi vya kivitendo unavyoweza kufanya mda was sala kwa familia kuwa wa kufurahiwa na watoto?

**Utekelezaji wa Azimio**


Orodhesha baadhi ya tabia unazopenda watoto wako kuwa nazo kiroho, kijamii, kiakili na kimwili wanapofikia umri wa miaka 18. Kisha andika jina la kila mtoto kwenye karatasi tofauti. Andika unachofanya au unachotaka kufanya kumsaidia mtoto kupata kila moja ya tabia hizi.

# Maazimio ya Mafunzo ya Omega Mwongozo wa Tano

## Maono ya KUM – Azimio la Mafunzo 13

### **Maono na Kupiga darubini:** Kuichukua Injili Ulimwenguni

**Mdo 1:8** (Jadili Mchoro na Jedwali hapo Chini)




| MATENDO 1:8: | "Yerusalemu" | "Yudea" | "na Samaria" | Miisho ya dunia |
|---|---|---|---|---|
| Maana | mji wa mtaa | mkoa | Eneo linalopakana | ulimwengu |
| Vidokezo vya Matendo | Matendo 1-8 (Mdo 5:28) | Matendo 8-12 (Mdo 8:5) | | Matendo 13-28 (Rum 15:19) |
| Mifano ya kibiblia | "Wathethalonike" 1 The1:6 | "Masedonia" 1 The1:7 | "na Akia" 1 The1:7 | "kila mahali" 1 The1:8 |

**I. Tafsiri ya maono na Kupiga darubini** (kupiga darubini inamaanisha kuuingia ulimwengu kwa ngazi nyingi)

Jinsi Gani Utume Mkuu Ulinganishwe na Kupiga Darubini?

Unakubaliana kwamba darubini ingekuwa na ngazi nne?

**II. Kuangalia kwa Maono ya mavuno ya Mungu (Mat 9:38)**

Kwa nini mtu aseme kuwa Pentekositi lilikuwa kanisa la kwanza la Agano Jipya kupandwa? Unakubaliana?

Unapoangalia nje katika shamba lako mwenyewe la mavuno, unaona nini? Liko wapi? Nani anafanya kazi? Kazi ni nini?

**III. Kupiga Darubini kwa Mavuno ya Mungu (**kadiri darubini inavyosogea, tunakazia kwa vitu vya mbali

zaidi)

**A. Sehemu 1: Huduma ya Ndani**

Unakubali maono ya kanisa linalokubali kila mmoja katika jiji lako au mji?

**B. Sehemu 2: Huduma ya Kimkoa**

Kutoka katika mfano wa Brazili, jinsi gani unaweza kutathimini ufikiaji nje wa kimishenari kimkoa wa makanisa katika nchi yako?

**Mfano**

Huko Brazili kwa zaidi ya kipindi cha miaka 20 kanisa moja lilijaza eneo la kijografia kwa makusanyiko 200. Mmishenari ambaye makanisa haya yalituma kwenda Albania alikuwa akifundisha juu ya kuzidisha makanisa kwa wapanda kanisa pale na alisema, "Ukuaji wa kanisa letu ulikuwa wa polepole ukilinganishwa na mwingine, lakini hata hivyo, tunapopanda kanisa mpya mara moja ambalo kanisa binti limepanga kupanda makanisa binti mengine upesi iwezekanavyo. Makanisa yetu yanajua kusudi lao ni kupanda makanisa mapya kutokea mwanzoni." Ni aina hii ya kufikiria na kusudi linaloweza kuhamasisha makanisa kutokea mwanzoni mwake kuwa na akili ya huduma kwenye kusanyiko lao wenyewe na zaidi.

Nini kinaweza kufanyika kukuza ngazi ya kufikia kwa umishenari katika eneo lako?

**C. Sehemu 3: Huduma ya Mwingiliano wa tamaduni**

Kuna hitaji hapa la kufikia nje kwa kabila au kundi la watu?

**D. Sehemu 4: Huduma ya Kimataifa**

Kutoka kwenye mfano wa Luis Bush, jinsi gani ungetathimini ufikiaji nje wa kimishenari wa ulimwengu wa makanisa katika nchi yako?

Luis Bush (aliyeendesha harakati za Latino ya Amerika za makanisa kutuma wamishenari), na wengine walisafiri Latino ya Amerika yote wakitangaza maono ya umisheri kama sehemu ya harakati za COMIBAM (kifupi cha, Shirika la Amerika la Ibero katika misheni). Kilio kilitoka nje, "Latino ya Amerika, kutokea umishenarini kwenda nguvu ya umishenari!" Wakati huo, nchi za Latino ya Amerika zilikuwa zikipita katika wakati mgumu kiuchumi na wengi hawakweza kuona jinsi ambavyo ingewezekana kutuma wamishenari nchi zingine kama walikuwa wakihangaika kifedha. Luis alitumia mfano wa Ibrahimu, ambaye mwili wake ulikuwa mzuri kama wa aliyekufa lakini imani yake ilikuwa hai. Ilikuwa imani yake ambayo ilileta ahadi ya kijana wake. Kwa njia hii alilinganisha kukosekana kwa fedha na mwili wa Ibrahimu akisema, "Katika Latino ya Amerika hatuna pesa- LAKINI TUNA IMANI!" Kanisa hadi kanisa walikubali wito wa umishenari na tangu COMIBAM katika 1987, maelfu ya wamishenari wametumwa na makanisa ya Latino ya Amerika. Wamekuwa na imani na Mungu ametoa fedha!

Nini kinaweza kufanyika kukuza ngazi ya ufikiaji kwa umishenari kwa ulimwengu?

**IV. Nguvu ya Kiroho na Mamlaka**

Wapi tunapata haki na nguvu kufikia nje kwa ulimwengu? **Mat 28:18-19, Mdo 1:8**

Nini vizuizi kwenye maono na jinsi gani unaweza kuvishinda?

Jinsi gani unaweza kuhamasisha maono na kupiga darubini katika makanisa yako mapya?

Kwa nini kanisa moja halitoshi sana kufikia mji wote kwa ajili ya Kristo?

Jinsi gani darubini yako ni pana? Darubini ya kanisa lako? Kwa nini?

### UTEKELEZAJI WA AZIMIO

Kwa kutumia darubini iliyoonyeshwa katika kielelezo 13.2, anza kushirikisha maono yako kwa kanisa (ma) kuhusu kufikia nje zaidi na zaidi kwa injili.

Angalia kwenye darubini katika kielelezo 13.3 chini. Kwa kila sehemu ya darubini, andika ni nini "Yerusalemu" yako, Yudea, Samaria na miisho ya dunia." Ni katika sehemu ipi kanisa lako linafanya kazi kijuhudi? Kama kuna sehemu ya darubini ambayo kanisa lako mpya halijahusika, nini unachoweza kufanya kuhamasisha hilo?

# Maono ya KUM—Azimio la Mafunzo 14

## Kuhamasisha

**I. Kuhamasisha ni Nini? Kuhamasisha ni Pamoja na:**

A. **Maono ya Pamoja ("Z")**

Mkufunzi: Leta darasani maelezo ambayo unaonyesha au kuanzisha maono ya kanisa ambayo yanazalisha kuhamasisha. Yashirkishe kwa darasa.

Andika maelezo ambayo yanaweza kuwakilisha maono ya kanisa lako katika kutimiza Utume Mkuu?

**B. Mafunzo**

Ni aina gani ya mafunzo watu wako wanahitaji kushirkisha imani yao?

**C. Rasilimali**

Ni rasilimali gani zinahitajika kuhamasisha kanisa? Jinsi gani zinaweza kupatikana?

**D. Kuweka Kimkakati** –Ni wapi Mungu anakutaka kutenda? Epuka kufuatisha.

Maswali yafuatayo yatatumika kuonyesha jinsi ufahamu wa watu darasani unaweza kusaidia kuainisha maeneo ya mahitaji.

Ni wapi katika mkoa wako unafikiri unahitaji zaidi makanisa mapya? Kuna yeyote anayejua huduma ya kanisa ambayo tayari inatimiza hitaji pale? Ni taarifa zipi kupita hizo zinazojulikana kwa wajumbe wa darasa hili zinaweza kufikiriwa ili kuonyesha wapi kazi inahitajika?

**II. Kwa Nini Waumini wahamasishwe? (Yohana 17:1-21)**

Kuna sababu gani kwa waumini na makanisa kuhamasishwa?

**III. Mifano ya Kibiblia ya Wahamasishaji**

**A. Nehemia (Neh 1:2-4, 2:7-9, 4:22-23)**

**B. Barnabas (Mdo 4:36-37, 9:26-31, 13:1-3)**

Unafanyia kazi vipawa vyako vya kiroho kwa shauku kama alivyofanya Barnabas?

**C. Paulo (Rum 15:25-27, 1 Cor 1:4-9, Rum 15:14)**

Nini yalikuwa maono ya watu hao watatu hapo juu na nani walimuhamasisha?

**IV. Ni nini Tabia za Wahamasishaji Wafanisi?**

**A. Maono**

**B. Imani na Kutia Moyo**

**C. Mguso**

Kufuatana na tabia hapo juu, unamjua yeyote ambaye angeweza kuwa muhamasishaji mfanisi? Kama ni hivyo, mwelezee mtu huyo.

**V. Mifano ya Kuhamasisha**

**A. Maombi ya Umoja**

Mfano: Kila wiki katika mkutano wa maombi, mtu mmoja angeweza kushirikisha taarifa ndogo kuhusu nchi maalumu au kundi la watu na wanaweza kutumia mda kuombea injili kupenya kwenye mioyo na akili za watu hao. Wangeweza kuomba kwa ajili ya wamishenari kutumwa sehemu hizi kwa watu wasiofikiwa na kwa makanisa kupandwa miongoni mwao. Kundi hili la maombi linaombea kwamba Bwana angeweza kutuma kutoka wajumbe wa kanisa lao timu ya kupanda kanisa kufanya kazi miongoni mwa kundi la watu wasiofikiwa. Walipoomba kwa ajili ya makundi ya watu wasiofikiwa, Bwana alilipa kundi hili mzigo maalumu kwa watu wa Kezaki wa Asia ya Kati. Kati kati ya mda wa kipindi cha miaka

miwili, wajumbe watatu wa kikundi hicho cha maombi waligeuka kuwa wamishenari huko Kezaki. Wajumbe wa kusanyiko kisha waliririthi watu wa Kezaki kama mkazo maalumu wa kufikia na kuanza kutuma timu za mda mfupi za wafanya kazi madaktari, wafanya kazi wa ujenzi, wafanyakazi wa watoto, wanamziki na wafanya biashara Kazakstani. Hatimaye, kanisa lilituma timu ya upandaji kanisa kufanya kazi Kazakstani ya magharibi. Kundi la maombi la mwanzo limeshayeyuka na kundi kubwa la watu sasa linakutana kila mwezi kuomba kwa ajili ya watu wa Kazaki.

Ni masomo yapi muhimu kutoka katika mfano huu ambayo unaweza kujifunza na kutumia katika huduma yako?

**B. Shule ya Jumapili/Vipindi vya watoto**

Mfano wa hili ulitokea mwaka 1992. Kikundi cha maigizo kutoka Uholanzi kilikuja Hungari kusaidia timu ya uinjilisti wa mda mfupi waliokuwa wanasaidia kanisa la Baptisti kwa uinjilisti. Kwenye timu ya uinjilisti kulikuwa na wanafunzi wawili kutoka kwenye chuo cha mageuzi cha walimu waliokamata maono ya kuanzisha kundi lao la maigizo. Walifundisha wengine saba na kuanza kuigiza katika makanisa yao. Kupitia huduma yao watu kadhaa waliokoka na kujiunga na kikundi. Katima miaka mitatu iliyofata, 20 walifundishwa na kushiriki kwenye kikundi cha maigizo. Wote hawa 20 sasa ni wajumbe hai wa makanisa ya mtaa na watano wanahusika katika kazi ya umishenari kikamilifu.

Ni masomo yapi muhimu kutoka katika mfano huu ambayo unaweza kujifunza na kutumia katika huduma yako?

**C. Kuhamasisha Watu Wazima**

Kanisa moja la mtaa lilimsaidia mkimbizi mmoja wa Kambodia kutafuta nyumba, vifaa vya ndani, na kazi. Mkambodia alipouliza alipe kwa ajili ya wema wao, kanisa lilisema, “njoo kwenye ibada yetu.” Mkambodia alikwenda, lakini kulikuwa na tatizo—kutokujua lugha, kwa upole alikaa kwenye viti, bila kuelewa chochote. Katika kuitikia kwenye tatizo hili, kanisa lilianda tafsri ya wakati uleule ili kwamba mkambodia aweze kushiriki kwenye ibada. Wanaoongea kivitenamu, kichina, kisipanishi pia waliomba na wakapata tafsiri. Wakati viziwi walipohudhuria ibada kanisa liliandaa kutafsiri kwa lugha ya vitendo. Kupitia mwingiliano wa watu wa tamaduni kadhaa, wajumbe wa kusanyiko walipata moyo kwa ulimwengu. Leo, kanisa hili limetuma zaidi ya familia zaidi ya ishirini kwenye msaada wao wa kifedha!

Nini kimefanya hili kama mfano wa kuridhisha wa kuhamasisha?

Ni vitu gani vya kuhamasisha kila mfano unaeleleza?

Jinsi gani unaweza kusaidia kanisa lako kuhamasisha kuendeleza injili – kuzaliana kwa upandaji makanisa mapya?

Kwa nini kuhamasisha ni muhimu?

Unamjua yeyote anayetaka kumtumikia Bwana ambaye anaweza kuhamasishwa?

Unamjua yeyote anayeweza kuwa muhamishaji mfanisi?

Ni baadhi ya njia zipi zingine maalumu ambazo unaweza kusaidia kuhamasisha watu katika kanisa lako kwenye uinjilisti na upandaji kanisa?

Ni sifa zipi za muhamasishaji unazokamilisha vema? Ni ipi ni ngumu zaidi kwako?

Jinsi gani unaweza kuhamasisha kanisa lako kuendeleza injili, kuzaliana kwa kupanda makanisa mapya?

**UTEKELEZAJI WA AZIMIO**

Anza kumtumikia Mungu katika kujaliwa kwako vipawa kuelekea kuendeleza injili.

Muulize Mungu kuweka yeyote katika moyo wako anayetaka kumtumikia Bwana na anza kufanya nao urafiki na kuwahamasisha.

Orodhesha hatua tatu unazoweza kuchukua kwenye kuhamasisha kanisa lako kwa ajili ya uinjilisti na upandaji kanisa.

# Maono ya KUM – Azimio la Mafunzo 15

## Hatua Inayofata: Upandaji Makanisa Zaidi

Somo hili ni bora likifundishwa kama kipindi cha majadiliano. Shirikisha kutoka katika uzoefu wako jinsi ulivyokabidhi huduma kwenye kanisa lililopandwa. Ruhusu wafunzwa kuuliza maswali na kushirikisha yanayowatinga wanayokabiliana nayo katika hali yao ya huduma.

**I. Mzunguko wa Upandaji kanisa** (rejea Mwongozo wa Kwanza)

**II. Jukumu la Kanisa Mpya: Upandaji Makanisa Binti**

A. **Kutunza maono Hai (Mdo 19:10, Gal 2:7-8, Rum 11:13) –** Ni eneo lipi Mungu anakuitia kulifikia?

B. Jinsi gani kanisa linajiandaa **Kutuma Timu ya Upandaji kanisa?** Jib:

1. Kuliombea na kuombea hao Mungu anaowaita
2. Kuonyesha wapi pa kuwatuma?
3. Kuhamasisha rasilimali
4. Kuifunza Timu

Katika makundi madogo, jadili maswali yafuatayo: (dakika 20)

1. Ni eneo lipi Mungu amekuita kulifikia?
2. Ni aina gani ya makundi ya watu wanaoishi katika eneo hilo lazima wafikiwe kwa injili?
3. Ni hatua ipi inayofata katika kanisa lako mpya inayotimiza Utume Mkuu?
4. Kama vikundi kiini vinazidi, unaweza kuanzisha kanisa jipya kutoka katika moja ya vikundi kiini vyako vyenye nguvu?

**III. Jukumu la Timu ya Mwanzo ya Upandaji Kanisa**: Kuanza Upya—Upandaji Makanisa Mapya

A. Timu ya Upandaji kanisa iendelee?

B. Timu ya Upandaji Kanisa Ibakie Kuchunga kanisa Mpya Lililopandwa?

C. Timu ya Upandaji Kanisa Inakuwa Timu ya Kuwezesha?

Katika makundi madogo, jadili maswali yafuatayo:

Ni nafasi ipi katika kazi ya upandaji kanisa utaweza kuchukua?

Je kanisa unalopanda lina maono ya kanisa binti? Kama siyo, ni hatua zipi utachukua kupitisha maono hayo?

Elezea tofauti kati ya mpanda kanisa wa kitume/mvumbuzi na mchunguji kwa kuangalia wito na kujaliwa vipawa.

Ni kujitoa gani utatakiwa kufanya kuona makanisa yameanzishwa?

Jinsi gani unaweza kusaidia wengine au katika utumaji wa kanisa lako au katika kanisa mpya kuwa wapanda kanisa?

**UTEKELEZAJI WA AZIMIO**

Pamoja na timu yako ya upandaji kanisa na mshauri, omba na fikiria nini itakuwa hatua yako inayofata katika huduma.

Gundua mmoja au wawili wapanda kanisa maarufu katika kanisa lako mpya lililopandwa. Tumia mda kuzungumza nao kuhusu maono yao na kuwashauri katika maandalizi ya kazi ya upandaji kanisa kama sehemu ya timu ya upandaji kanisa.

# Kanisa – Azimio la Mafunzo 15

## **Malezi ya kanisa:** Toba na Kurejeshwa

Ni nini mashauri ya malezi ya kanisa au taratibu ambazo unazifahamu—haya yanaweza kutoka katika kanisa lolote, hayaendani na kanisa?

Malezi ya kanisa ni ya kibiblia?

Ni nini malezi ya kanisa?

Ni nini hatua za kibiblia kanisa lazima zichukue katika kuonya wajumbe?

Ni nini malengo ya malezi ya kanisa?

**I. Kanuni za Kibiblia za Malezi ya Kanisa**

A. Malezi ya Kanisa ni Agizo la Kibiblia **(1Kor 5)**

Ni nini maelekezo ya jinsi ya kushughulika na kaka aliyehusika kuvunja maadili kingono yaliyotolewa katika moja ya mistari hii? (**1 Kor. 5:2, 5, 11, 13)**

B. Malezi ya kanisa Lazima Yafate Hatua fulani (**Mat 18:15-22)**

Ni nini taratibu za kushughulika na kaka aliye dhambini kufuatana na **Mat. 18:15,16,17**?

C. Kurejezwa kwa kaka anayetubu. Ni Lengo la Malezi ya Kanisa **(2 Kor 2:5-8)**

Nini tunachofanya wakati kaka anapotubu kama ilivyoonyeshwa katika **2 Kor. 2:7, 8**?

Katika makundi madogo, jadili maswali kwa michanganuo chini.

**II. Michanganuo**

A. Mchanganuo wa Kwanza

Geoge ni kijana tu aliyempenda Bwana na kijuhudi alikuwa akimtumikia kama kiongozi wa vijana katika kanisa lake na kiongozi wa kujifunza Biblia kiuinjilisti kwenye ujirani wake. Kanisa lake, mara ushuhuda wa juhudi wa kufikia nje kwenye jumuia, hivi karibuni umeshuka kutoka wajumbe 200 mpaka 30. Akiwa amesumbuliwa na hili, alianza kuuliza maswali.

Wazee walikwazwa na kumtaka akutane nao. Bila kupata nafasi ya kuelezea yanayomsumbua, aliamriwa asiulize maswali mengine zaidi na wasijadili hilo zaidi na mtu yeyote. Zaidi ya hayo, aliambiwa hataongoza tena vijana hata vikundi vidogo.

Akijisikia kwamba wazee hawakufanya haki katika matakwa yao, George aliendeleza kikundi chake kidogo. Wazee walimwamuru kukutana na kanisa lote na aliwekwa nje ya kanisa. Barua zilitumwa kwa viongozi wa kanisa katika eneo wakimlaumu kwa kuasi na kutotii mamlaka.

Kuuliza kwa Goerge ilikuwa dhambi?

Kuitikia kwa wazee kwenye kuuliza kwake kulikuwa sahihi?

Jinsi gani ambavyo wangelichukulia hili kwa njia ya kibiblia zaidi?

B. Mchanganuo wa Pili

Samweli alikuwa mzee wa kanisa katika kanisa lake. Alikuwa na tabia isiyofaa ya kuwaendea wanawake kanisani, mengi yake yakiwa ya kuwadharirisha. Ingawa hakuwa anajisikia hatia ya uzinzi, wazee wengine walijisikia kwamba vitendo vyake havikuwa vya kufaa kwa mzee. Walipomtia changamoto, alitubu dhambi yake kwa kanisa zima na alitolewa kwenye uongozi. Hakukuwa na jaribio lililofanywa la kumrejesha.

Wazee wengine walikuwa sawa kumtia changamoto Samweli kwa matendo yake? Kwa misingi ipi?

Walikuwa sahihi kumuondoa kwenye uongozi?

Ni mpango upi wa kurujesha ambao wangetakiwa kuwa nao?

C. Mchanganuo wa Tatu

Jemusi alikuwa mchungaji aliyeshukuriwa sana na kanisa lake. Ilipotambulika kwamba binti yake ambaye hajaolewa alikuwa na mimba, viongozi waligawanyika kuhusu uamzi gani wangechukua. Baadhi walisema haikuwa dhambi yake; alikuwa tayari anaugua kutokana na kuaibishwa pia na kumfikiria binti yake na kwa hiyo alitakiwa kuchukuliwa kwa neema. Wengine walisema kwamba hakuwa anatimiza matakwa ya kibiblia kwa mzee kutawala nyumba yake na kwa hiyo alitakiwa kuonywa. Lakini kwa kuwa hawakuwa na wa kushika nafasi yake na kwa sababu alikuwa anapendwa na watu, waliamua kutokufanya chochote.

Wazee walikuwa sawa kutolijali tatizo?

Jinsi gani mabavyo wangeitikia kwenye tatizo hili yote kwa neema na ukweli?

III. Suluhu

Malezi ya kanisa si ya kibiblia tu lakini ni sehemu ya lazima katika maisha ya kanisa. Sababu ya hili siyo ya kuadhibu, lakini kurejesha afya ya kiroho kwa mtu pekee na kanisa la mtaa. Kila kanisa la mtaa linatakiwa kimaombi na kiuangalifu kuanzisha sheria ya maonyo.

**Utekelezaji wa Azimio**

Soma 1 Wakorintho 11:29-32 na jibu maswali haya:

1. Kwa nini kulikuwa na wadhaifu na wagonjwa miongoni mwa waumini?
2. Nini ilikuwa adhabu ya mwisho?
3. Kwa nini Bwana anawaonya watoto wake?

Soma Wagalatia 6:1-5 na jibu maswali haya:

1. Nini baadhi ya sifa Paulo anazoorodhesha za kumurejeza ndugu?
2. Nini "sheria ya Kristo" ambayo Paulo anataja?
3. Jinsi gani sheria hizi zinatakiwa zitumike katika kumrejeza ndugu?

Na timu yako, anzisha sheria ya malezi ya kanisa kwa kanisa lako mpya.

# Kanisa – Azimio la Mafunzo 16

## **Ibada ya Umoja kwenye kanisa la Mtaa:** Mfumo na kazi katika Kuabudu

1. Ni mifumo ipi ya kuabudu uliyokutana nayo na unajisikiaje kuhusu kuitumia mifumo hii?
2. Ni kwa kiasi gani kushirki kwa kusanyiko kulikuwepo kwenye mifumo hii?
3. Fikiria baadhi ya mchanganyiko wa ibada ya kuabudu uliyoona. Fikiria kilichotokea katika ibada hizi – aina ya mziki, maombi, kuhubiri, kusoma maandiko, matukio maalumu, n.k. Ni kwa njia zipi ibada hizo zilisaidia au kukurudisha nyuma katika kumwabudu Mungu?

I. **Ni nini Baadhi** ya kazi za Kuabudu?

**A.** Kumpa Mungu **Utukufu Shukurani? (Zab 71:8; 107:32, 97:12, Mdo 2:47, Uf 7:12)**

**B.** Tunaweza **Kuabudu na Tusimuhudumie Mungu?** (**2 Nya 33:16, Mat 4:10, Uf 7:15, 12:1)**

C. Ni nini ilikuwa **mtazamo wa Yesu Juu ya Kuabudu**? (**Yohana 4:19-26)**

| Pia katika makundi madogo, jadili maswali hapo chini (Dakika 30) |
|---|

**II. Jinsi Gani Tunaonyesha Mifumo Inayofaa ya Kuabudu?**

Ni vigezo vipi unatakiwa kufikiria unapopanga ibada yako ya ushirika ya kuabudu?
Jinsi gani unaweza kuonyesha imani yako kwa Mungu katika kuabudu?
Jinsi gani unaweza kuonyesha hisia na kujisikia kwa uhusiano wako kwa Bwana katika kuabudu?

**III. Kuabudu Pamoja na Upandaji kanisa**

**Nani ni watazamaji wa kuabudu kwa kusanyiko?**

Kuabudu kimsingi kumekusudiwa kuwavuta wenye dhambi kwa Mungu?

Kwa nini ni muhimu kwa watu wa Mungu Kukusanyika pamoja kwa ajili ya kuabudu pamoja? Ni nini dhumuni la Kuabudu pamoja?

Ni baadhi ya sababu zipi "zinazovuta" ibada ya kuabudu kuchangia kwenye ukuaji? Ni nini asili ya "ibada ya kuabudu inayosisimua?

Ina maana gani kumwabudu Bwana katika kutanda kwa utukufu wake**? (1Nya 16:29).**

Kulingana na kanisa lako au dhehebu, kazi ya kuinama chini na kupiga magoti au mifumo au kuabudu? **(Zab 95:6).** Kama ni mfumo, kazi ni ipi?

Kulingana na kanisa lako au dhehebu kuinua mikono ni katika kazi ya kuabudu au mfumo? **(1Tim 2:8).** Kama ni mfumo, Ni ipi ni kazi?

**UTEKELEZAJI WA AZIMIO**

Fanya mafunzo ya kuabudu kwa kufata katika Ufunuo 4:8-11 na 5:9-14. Uwe na hakika kujibu maswali ya "nani", "Nini", "Lini", "Wapi", "kwa Nini" na Jinsi gani?"

Fanya orodha ya uchunguzi wa njia ambazo watu wengi katika eneno lako linalolengwa zaidi kiasili wanaonyesha upendo, furaha na uhusiano wa ndani.

Fikiria jengo lako jipya la kanisa. Ni ipi kati ya mifumo hii inafaa kuonyesha kuabudu kwa Mungu katika ibada yako ya pamoja ya kuabudu? Ni mifumo ipi kutoka katika kawaida ya kidhehebu amabayo inaweza kufaa pia? Ni upi unaweza ukawa haufai kwa kundi la watu wako wanaolengwa? Jadili uliyopata na mkufunzi wako au mshauri

# Kanisa – Azimio la Mafunzo 17

## **Jinsi ya Kuongoza Ibada ya Pamoja:** Kupanga na Kuandaa Ibada ya Kuabudu

Muombe kiongozi yeyote wa ibada mwenye uzoefu kwenye mafunzo ashirikishe jinsi wanavyoongoza ibada. Kama inawezekana, karibisha viongozi wenye uzoefu kutoka nje ya mafunzo kuja na kushirikisha wafunzwa jinsi wanavyofanya kazi na wachungaji kwenye makanisa yao na jinsi gani wanapanga na kuandaa kwa ajili ya ibada ya kuabudu. Katika makundi madogo, jadili maswali hapo chini:

Fikiria viongozi wafanisi zaidi uliowahi kuwajua. Jinsi gani unaweza kumtathimini mtu huyu kwa misingi ya hadhi hizi: Anayeabudu, mwenye uwezo wa mziki, mwenye kuwa macho kiroho, mwenye utu mwema, mwenye uwezo wa kuongoza wengine katika kuabudu?

Kuna vielezo vya kuonyesha (mf. shairi. Maigizo, kushika jukumu, dansi, kusoma Biblia kimsisimko, shuhuda na yanayofanana na hayo) yaliyotumika mara kwa mara katika utamaduni wako ambayo yanaweza kushirikishwa kwenye ibada yako ya kuabudu. Jinsi gani unavyoweza kutumia miundo ya kuonyesha katika ibada ya kuabudu?

Kwa nini ni muhimu kuchukua mda kupanga kwa ajili ya ibada ya kuabudu?

Nini linatakiwa liwe jukumu la mchungaji katika kupanga ibada ya kuabudu? Nini linatakiwa liwe jukumu la kiongozi wa kuabudu?

Elezea mtiririko wa ibada ya kuabudu ambayo ilileta maana kwako hasa hasa? Ni mambo yapi katika ibada yalikuwa na ufanisi zaidi? Nini unachoweza kujifunza kutoka katika ibada hii cha kukusaidia katika upangaji wa ibada ya kuabudu kwenye kanisa lako lililopandwa?

**Zoezi katika Kupanga Ibada ya Kuabudu**

Hatua zifuatazo zinaweza kukusaidia kupata uzoefu katika upangaji wa ibada ya kuabudu na timu yako ya upandaji kanisa. Katika darasa lako la mafunzo, gawanyika katika makundi madogo. Jadili kila moja ya hatua zifuatazo na tumia karatasi ya mfano wake kupanga ibada. Shirikisha mpango wako wa ibada na makundi mengine.

**A. Hatua 1: Chagua Kisa**

Nini kitakuwa kisa cha ibada ya kuabudu? Mda mwingi wazo kuu la mahubiri linafaa kwenye hitaji hili. Kwa mfano, katika somo la mahubiri katika mafunzo haya umeandaa mahubiri kwenye fungu la Waefeso 5:15-21. wazo kuu la fungu hili ni: "Mungu anatutaka tujazwe na Roho kwa sababu ni busara na inaletea maisha yenye furaha." Kisha kwa hiyo kisa cha ibada ya kuabudu kinaweza kuwa: "*Ujazwe na Roho.*" Kama siku hii ni siku maalumu, jumapili ya pentekosti, Krismas, Pasaka, kisa chako pengine kinakuwa kama vichwa hivyo.

**B. Hatua 2: Chagua Nyimbo/Mziki na Matukio Maalumu**

Ni nyimbo zipi na sifa utatumia katika ibada ya kuabudu? Chagua zile ambazo zinaendana na kisa na ambazo ni za kisasa na za kimapokeo. Pia, Uwe na uhakika kuwa mapigo ya mziki yametofautiana—yote yakionyesha kusherehekea na fikira. Utakuwa na mziki wowote maalumu, kama vile sauti au solo ya vyombo? Kutakuwa na maigizo yanayoelezea sura ya mahubiri? Utakuwa na ushuhuda wowote? Uwe na hakika shuhuda unazochagua zinaendana na kisa.

**C. Hatua 3: Weka Mtiririko wa Ibada ya Kuabudu**

Uwe na mda halisi wa kuanza na kumaliza. Husisha kila sura ya ibada ya kuabudu—nyimbo, mahubiri, matukio maalumu, maombi, kusoma Biblia, n.k. kielelezo 17.1 kina mfano wa karatasi ya upangaji wa

ibada ambayo unaweza kutumia au kuirekebisha kuweka mtiririko wa ibada. Karatasi hii ya kupanga kisha inaweza kutumika na kiongozi wa kuabudu na mchungaji kama marejeo ya kuongoza halisi kwa ibada.

**D. Hatua 4: Orodhesha Vyombo Vinavyotakiwa**

Tengeneza orodha ya vyombo utakavyohitaji kwenye ibada ya kuabudu, kama vile vitabu vya nyimbo au karatasi za nyimbo, kifaa chochote maalumu cha kuigizia, n.k. Onyesha nani atawajibika kukusanya na kuandaa vyombo kabla na wakati wa ibada.

**E. Hatua 5: Onyesha tarehe za Kufanya Mazoezi ya Nyimbo**

Amua lini utafanyia mazoezi ya ibada ya kuabudu. Uwe na hakika kwamba wahusika wote wanatambulishwa na kuweza kuhudhuria mazoezi ya kuimba.

**F. Hatua 6: Chukua Mda Kuomba Kwa Ajili ya Ibada ya Kuabudu**

Muombe Mungu kuongoza na kuelekeza ibada ya kuabudu. Omba kwa ajili ya mioyo ya watu kutayarishwa kumwabudu Bwana. Omba kwa ajili ya wasioamini wanaoweza kuhudhuria kwamba mioyo yao iweze kufunguka kwa ajili ya Bwana. Baadhi ya makanisa wana timu za maombi zinazoombea ibada ya kuabudu wakati ikiwa inaendelea. Makanisa mengine yana makundi ya kuomba wanaokuja kanisani asubuhi sana na kuchukua mda kuomba kwa ajili ya ibada na kimya kimya kuomba kwa ajili ya hao wanaoingia sehemu ya kuabudia.

**G. Hatua 7: Tathimini Ibada ya Kuabudu**

Baada ya ibada chukua mda kuitathimni. Mtiririko ulikuwaje na anga la kuabudu? Nini kinahitaji kubadilishwa? Nini kitumike tena? Mungu amekutana na kusanyiko lako kwa namna ya ajabu? Kulikuwa na watu hasa walioguswa wakati wa ibada ya kuabudu? Kulikuwa na yeyote aliyeokoka? Shirikisha unachojifunza kutoka kwenye tathimini yako kwenda kwenye ibada ijayo ya kuabudu.

**UTEKELEZAJI WA AZIMIO**

Panga na andaa ibada ya kuabudu. Baada ya ibada, tathimini ufanisi wake. Nini kilifanya kazi? Nini unachiohitaji kubadili? Shirikisha matokeo haya kwa mkufunzi wako au mshauri.

Kama ikiwezekana, tembelea makanisa mengine kwenye au karibu na eneo lako unalolenga. Chunguza ibada ya kuabudu na tambua mifumo ya kuabudu. Nini unachoweza kujifunza kutoka kwenye uchunguzi wako cha kutumia katika jengo lako mwenyewe la kanisa?

# Kanisa – Azimio la Mafunzo 18

## Kanisa la Mtaa na Mwili Mkubwa wa Kristo

Kufanya kazi Pamoja katika Ushirika

**I. Mchanganuo wa Ushirikiano**

Ni nini mistari hii inatuambia kuhusu mtazamo wa kibiblia wa ushirikiano katika mwili wa Kristo? **(Yohana 17:20-21, Efe 4:3-6, Gal 3:26-28)**

Unakubali kwamba ushirikiano wa makanisa ya kiinjili unahitajika kukamilisha Utume Mkuu kikamilifu katika nchi yako?

Kwa nini mara nyingi kunakosekana ushirikiano miongoni mwa makanisa?

**II. Ngazi za Kujitolea katika Ushirikiano**

A. **Ngazi 1: Kutokujua (Hakuna Ushirika**—Kutokujua huduma nyingine zenye imani sawa na maono
B. **Ngazi 2: Kufahamu**—kuwatambua wengine na kuanzisha hisia ya jumuia
C. **Ngazi 3: Kushaurisha**—makundi yanakutana mara moja moja kujulishana na kuombeana
D. **Ngazi 4: Ushirikiano au Mtandao**—Shirika la kushirikishana habari na miradi ya pamoja.
E. **Ngazi 5: Ushiriki au ushirika**—Ungana kuendesha kituo cha mafunzo ya au shule ya Biblia ya mwingiliano wa madhehebu.

Ni kiwango gani cha kujitolea katika ushirikiano katika mkoa wako?

**III. Sifa Kumi za Ushirikiano Wenya Ufanisi**

1 **Ushirikiano wenye ufanisi unajengwa kwenye kuaminiana, uwazi na kujali kwa wote.**
Ushirikiano ni zaidi ya ulinganifu, upangaji, mikakati na maarifa.

2 **Ushirika wa kudumu unahitaji mwezeshaji au mpangaji**
Huyu ni yule ambaye kwa ridhaa amepewa jukumu la kuleta ushirikiano kwenye kuishi na kutunza moto ukiwaka.

3 **Ushirikiano wenye Ufanisi unaanza ili kukamilisha maono maalumu au kazi.**
Ushirikiano wenye mafanikio unakazia kwa kile (makusudio) badala ya jinsi gani (muundo). Mfumo kawaida unafata kazi.

4 **Ushirikiano wenye ufanisi unaanza kwa kugundua mahitaji miongoni mwa watu wanaofikiwa na kuhudumiwa.**
Hawaanzi kwa kuanza kuandika maelezo ya kawaida ya kitheolojia. Kutokana na mahitaji haya, vipao mbele vya ufalme, vizuizi vya kufanikiwa kiroho, na rasilimali zilizopo au zinazohitajika, vipao mbele vinavyotarajiwa kwa utendaji lazima vichujwe na kukubaliwa.

5 **Ushirikiano ni utaratibu, siyo tukio.**
Kuanza, upelelezi na hatua ya kujengea ushirikiano mara nyingi inachukua mda mrefu. Hata mkutano wa kupelelezea wa mapema zaidi unaweza kuua uwezekano wa ushirikiano. Hatimaye, kuaminiwa kwa mtu kunatakiwa na hilo linachukua mda mrefu kujenga.

6 **Ushirikiano hata unatia changamoto zaidi kutunza kuliko kuanzisha.**
Kuhakikisha kuwa maono yanabakia kuwa hai, mkazo wazi, mawasiliano mazuri, na matokeo ya kutimiza yanachukua mkazo mkubwa na kujitolea kwa mda mrefu.

7 **Ushirikiano wenye ufanisi unajengwa na huduma ya washiriki wenye kutambulika wazi na maono.**
Washiriki wote wanatakiwa kuwa na maelezo wazi ya misheni yao na kuishi kwao kwa hiyo. Vinginevyo, hawataelewa kamwe jinsi "wanavyofaa humo." Kuchangia kwenye picha kwa ujumla, au kufaidika kutoka kwenye juhudi za pamoja.

8 **Ushirikiano wenye ufanisi unatambua, hata kusherehekea, tofauti katika historia zao za ushiriki, maono na uhudumu.** Lakini hatimaye, ushirikiano lazima ukalie kile walichonacho kwa pamoja, kama maono na thamani, na makusudio ya huduma, badala ya tofauti zao.

9 **Ushirikiano wenye ufanisi unakaa umekazia kwenye hatima ya malengo na maono.**
Hawakatishwi na uhitaji wa utendaji wa siku kwa siku. Mara nyingi ni rahisi kukazia kwenye "njia" badala ya kwenye "mwisho."

10 **Ushirikiano wenye ufanisi unatarajia matatizo na kupanga mapema kwa ajili yake.**
Muwe na hakika utaratibu umejengwa kwenye ushirikiano kwa ajili ya kushughulika na mabadiliko, uwezekano, kukatishwa tamaa, wajibu usiokamilishwa, na kwa kifupi yasiyotarajiwa.

Tambua: "Sifa Kumi" zilizotolewa kutoka kwenye ujumbe na Phil Butler wa mwingiliano wa maendeleo

| Katika makundi madogo, jadili maswali yafuatayo: (Dakika 30) |
|---|

Tathimini mkoa wako kwa misingi ya "hadhi za Ushirika Wenye Ufanisi.
Ni kwa njia zipi unaweza kuanza kuanzisha ushirikiano na kujenga imani na waumini katika makundi mengine katika eneo lako?
Ni njia zipi maalumu ambazo wapanda kanisa kutoka katika madhehebu tofauti kwenye mji wanaweza kufaidi kutoka kwenye ushirika kwenye kuzidisha makanisa?
Ni upi mtazamo wa Mungu wa mashindano kati ya makundi ya kikristo ya kiinjili?
Jinsi gani wakiinjili wahusiane na wajumuia zisizo za kiinjili katika maeneo yao, hasa hasa makanisa yaliyoanzishwa kama vile Orthodox na Romani Katoliki.

## UTEKELEZAJI WA AZIMIO

Fikiria ni makanisa yapi au mawakala katika eneo lako wanaofaa katika mzunguko wako (kanisa lako), mzunguko wa pili (makundi mengine ya kiinjili), wa tatu (makundi yasiyo ya kiinjili).
Fanya marudio ya utafiti (kupima ramani kiroho) kwenye eneo lako na orodhesha makanisa au huduma zilizo hai pale.

Fanya mawasiliano ya binafsi na viongozi wa makundi katika mzunguko wa kwanza na wa pili na anza kuanzisha uhusiano nao. Anza kuwauliza nini maono yao kwa ajili ya eneo.

Fikiria kuvurumisha ushauri, mtandao, au ushirikiano unaokazia kwenye kueneza eneo lako kwa makanisa.

# Tabia ya Kiroho – Azimio la Mafunzo 14

## **Huduma ya Upatanisho:** Kutatua Migogoro

**I. Mawazo ya Awali Kuhusu Utatuzi wa Migogoro (Gal 5:15)**

A. **Migogoro haiepukiki kwa sababu ya Kutokuwa kamili Kwetu**—Ni nini **Yakobo 3:2** inasema kinahitajika ili kuwa bila migogoro?

B. **Ugumu wa Kukabili—(Efe 4:25-29) –** Ni nini ufunguo katika kuchukulia migogoro?

C. **Matokeo ya kuepuka Kutatua Migogoro—**Ni nini kinatokea tunapoepuka kushughulikia migogoro?

Katika Makundi madogo, jadili maswali yafuatayo yanayoshuhulika na kichwa hapo juu: (dakika 15)

1. Kukosekana kwa ukamilifu kwa mtu kunapelekea nini zaidi katika migogoro?
2. Ni nini sabau za kushindwa kukabili mtu ambaye una mgogoro naye?
3. Ni nini matokeo ya kuepuka migogoro kila mfano hapo chini umeeleza?

**Mfano #1**

Mtu katika kanisa lako mpya ana baadhi ya tabia ambazo si rahisi kuishi nazo. Anajaribu kupita katika kanisa lote akijaribu kufanya urafiki bila kuwa na mafanikio. Hatimaye, anajua kuwa hatakiwi na pengine kusimama kushiriki katika kanisa au kuhamia jingine.

**Mfano #2**

Mwanamke katika kanisa ana tatizo la kiusafi. Alitaka mtu wa kuongea naye kuhusu hili. Wakati hao wa kanisani kwake mwishoni walipomkabili, ilikuwa ngumu na kulikuwa na hatari iliyokuwepo katika kulifanya hilo. Mwanamke angekuwa na hasira sana na kuaibika vibaya sana. Lakini lilifanyika kwa upendo na aliweza kulichukua. Upendo ulimaanisha kukabili mwanamke huyu ili kumsaidia, siyo kumsukumia mbali.

Jinsi gani unaweza kumkabiri mtu katika kila moja ya mifano hii? Jinsi gani mfano wa kwanza unaendana na **Mat. 5:40-41, 44**?

**II. Utatuzi wa Migogoro ni swala la Injili**

Injili Inatuweka **Huru Kushughulika na Migogoro**

Kama tunakubaliana na maelezo kwamba "Yesu ndiye anayetoa haki na sifa," kwa nini bado tuna hofu ya kutokuwa sahihi, kushindwa mapambano, kukataliwa, wengine watafikiria nini, au watakavyofanya wengine?

Ni lazima kujikumbusha nafasi yetu ndani ya Kristo hofu inapokuja? Kwa nini?

**Injili inatoa** Kipande cha Kutatua Migogoro (Efe 2:11-16, Plp 2:2-8, 1 Pet 3:18)

Ingekuwaje kama tungechukua tabia ya Kristo ya kutoa haki yake kwa wengine?

Unaweza kufikiria mfano ambapo tabia ya unyenyekevu ilitatua mgogoro?

**III. Mafundisho ya Agano Jipya Juu ya Kutatua Migogoro**

**A. Mat 18:15-17—**Ni kanuni zipi za utatuzi wa mgogoro ziko kwenye mistari hii? Tambua kuwa mfano wa kondoo aliyepotea unaendendeleza fungu hili na mfano wa mtumishi asiye na rehema unafata maelekezo haya juu ya mgogoro. Unafikiri mandhali haya yanasemaje kuhusu mistari ya 15-17?

**B.** 2 Kor 5:17-21**—Ina mana gani kuwa balozi wa Kristo katika huduma ya upatanishi?**

**IV. Kuwapenda wengine—(Rum 12:14-21)** Ni nini tunatakiwa tufanye kwa hao wanaotupinga?

**V. Msaada wa Kivitendo kwa Utatuzi wa Mgogoro**

A. Jinsi ya **Kuendea Mgogoro ?** Jib: (1) Tambua nia yako binafsi, (2) Usidhani tu kuwa unaelewa hali yote, (3) Ona jinsi ulivyoumiza mwingine, na (4) Anza kwa kutia moyo

B. Jinsi unavyoweza Kuchukua **upinzani kutoa kwa Wengine?** Jib: (1) Kuliangalia kimakusudio, (2) Kwanza hakikisha usahihi wa upinzani, (3) Ona udhaifu kweli au dhambi na tubu.

Toa mifano ya mgogoro. Jinsi gani mawazo juu ya "usaidizi kivitendo" hapo juu unahusika kwenye mifano hii?

Kwa nini watu wanasita kukabili wengine?

Lini kukabiliwa na mtu mwingine kumekuwa baraka hasa?

Ni kwa njia zipi inaweza kuwa sumu kuepuka kukabili kaka au dada katika Kristo kuhusu kikwazo?

Ni vitu gani vingine unaweza kufanya kuweka kukabili kuwa rahisi kuchukua?

**UTEKELEZAJI WA AZIMIO**

Zoezi lifuatalo litakusaidia kufanya mazoezi ya utatuzi wa mgogoro katika mahusiano yako binafsi:
Fanya marudio ya mahusiano yako na ona kama kuna watu ambao umekwaza—au waliokwaza na wewe.
Tambua mzizi inayosababisha migogoro—na shughulika na swala la mzizi.
Ongea na mtu na tafuta kupatana na utatuzi kwenye mgogoro wenu..

# Tabia ya kiroho – Azimio la Mafunzo 15

## **Unyoofu wa Maadili ya Wapanda kanisa:** Kushughulika na Fedha, Jinsia na Uwezo

Ni kielelezo gani unachojua kutoka kwenye maandiko au kutoka kwenye uzoefu wako ambacho kinaonyesha unyoofu wa maadili?

**I. Matatu yanayopendwa: Fedha, Jinsia na uwezo**

A. **Mali-**Ni tahadhari gani tunakuta katika maandiko haya?—**Mwa 1:28-30, 1 Tim 6:10**
Ni tabia zipi zimeshauriwa na maandiko?—**Mat 4:1-11, 1 Tim 5:8, Luka 18:18-30**

B. **Usafi kijinsia-**Ni tahadhari gani tunakuta katika maandiko haya?—**1 Kor 5:10, Efe 5:3**
Ni tabia zipi zinashauriwa na maandiko?—**Mwa 39.**

C. **Mamlaka na Uwezo-**Ni tahadhari gani tunakuta katika maandiko haya?—**Marko 10:42**
Ni tabia zipi zinashauriwa na maandiko?—**Mark 10:43-45**

| Katika makundi madogo, jadili maswali yafuatayo: (Dakika 15) |
|---|

1. Labda mtu fulani amekupa wewe na familia yako zawadi isiyo na masharti inayolingana na mshahara wa mwaka mmoja. Ni jinsi gani utaamua matumizi ambayo ungezitumia fedha? Jinsi gani wazo la "mahali mioyo yetu ilipo ndipo mali zetu zitakapokuwa" linagusa uamzi wetu? Jinsi gani kutambua kuwa "Kila tulichonacho ni cha Mungu" kunagusa uamzi wako?
2. Nini ulichojifunza kuwa muhimu katika kuepuka ushawishi wa tamaa?
3. Jinsi gani kiongozi anaweza kujua lini anapokuwa anatumia mamlaka na uwezo kwa kujipatia mwenyewe na ufahari?
4. Baadhi ya viongozi wa kikristo wamekuja kuona wafuasi wao kama watoto na wao wenyewe kwa namna fulani kama viumbe vya hali ya juu? Ni nini hatari katika hili? Ni nini matumizi ya uwezo yanayofaa?

**II. Kanuni za Ujumla za Unyoofu wa Maadili**
**Shinda Majaribu—Ebr 4:15; Kuwajibika**—Omb **4:9-10; Mkazo wa Juu—Ebr 12:2; Huduma ya Undani—Ebr 12:14-15; Tumaini la juu—Ebr 12:28**

III. Ni nini F**aida za Unyoofu wa Maadili?** Jib: maisha ya amani, maisha yenye maadili, kuheshimiwa na wafuasi, na Urithi wa hakika.

**IV. Unyoofu wa Maadili Unaweza kuwa wa Gharama—Mwa 39:12-20**

| Katika makundi madogo, jadili maswali yafuatayo: (Dakika 15) |
|---|

1. Ni nini unachoweza kusema kwa mtu anayesema kwamba atafurahia mara moja uhusiano wa jinsia ili kuiondoa nje ya mawazo yake na haja?
2. Ni nini unachoweza kusema kwa mtu anayesema kwamba anahitaji kuwa na uhusiano wa jinsia kwa sababu inasaidia afya yake na kustawi?
3. Ni kweli kwamba mtu anayekosa maadili ya kijinsia haamini kwamba tunda la Roho (upendo, furaha, amani, n.k.) linarutubisha maisha sana kuliko kujifurahisha kwa tamaa?

Jinsi gani kushindwa kisiri katika unyoofu wa maadili kunagusa huduma ya jumuia? Vipi kuhusu kufahamu kisiri dhambi ya mtumishi mwingine?

Kama watu wakishindwa katika eneo moja kuna uwezekano wa kushindwa kwenye eneo jingine? Jinsi gani kipande cha nguvu cha Kimungu katika eneo moja kinasaidia kuhakikisha unyoofu katika maeneo mengine?

Kutunza maadili mema kunakuwa rahisi kadiri unavyokaa mda mrefu katika huduma?

Jinsi gani uwajibikaji imara kwa waumini wengine unasaidia kuendeleza na kutunza unyoofu wa maadili?

Wakati jamii ikisisitizia kubadili sheria kuhusu unyoofu wa tabia inayofaa, nini tunachoweza kufanya ili kufanya mapatano yanayoendelezwa ya wakristo kuelekea kuwa na thamani kidogo?

Kimsingi tumeligusia tatizo la fedha, jinsia ana madaraka. Fikiria na jadili uwezekano unaoendana kati ya haya na maeneo mengine ya unyoofu wa maadili: ukweli, uaminifu, uwiano, huruma, umoja, kujilinda, furaha, uaminifu, na ustahimilivu.

**UTEKELEZAJI WA AZIMIO**

Muulize mwenzi wako/au rafiki mmoja au wawili wa karibu, "Ni eneo lipi moja la unyoofu wa maadili wengine wanaouchunguza mara chache katika maisha yangu?"

Kufuatana na ulichojifunza, (AU kufuatana na kile Mungu anachokuongoza baada ya kuuliza kwa uaminifu sehemu yako) omba na panga kwa ajili ya mkakati mfupi ambao ni pamoja na malezi maalumu kuimarisha kile ambacho kinatambulika kidogo cha tabia yako. Pengine hili linaweza kuwa eneo la kushindwa kwako, lakini halitakiwi; badala yake inaweza kuwa moja ya unayofanya kisiri ambayo hayajawavuta wengine bado.

Malizia mkakati wako angalau wakati wa wiki mbili. Hili halihitaji kuwa la utata, lakini linatakiwa kuwa imara.

Toa taarifa kwa mwenzi (kama umeoa) na angalau kwa rafiki mmoja au wawili ya ulichofanya na ulichojifunza kwenye utaratibu.

Fanya yote hapo juu kati kati ya miezi miwili ya hasa hasa ulipojifunza somo hili

# Maombi – Azimio la Mafunzo 10

## Kuwezesha Maombi kwa Harakati za Upandaji Kanisa

Kuwasaidia Wengine Kuomba kwa Ajili ya Kueneza Upandaji Kanisa

Ni hatua zipi unaweza kuchukua kusaidia kuhamasisha maombi katika dhehebu lako, mkoa, au taifa? Unafahamu rasilimali zozote au habari za mawasiliano kuhusiana na harakati za maombi zinazotokea katika mji wako, mkoa au nchi?
**I. Utafiti** unaweza kusema ni nini kimefanyika kwa sasa katika maombi katika eneo lako.
**II. Utupaji maono** –Ni nini Mungu anataka katika mkoa na taifa letu? Jinsi gani haja yake inaweza kutumiwa kuongoza utekelezaji wetu? Ni nafasi ipi maombi yanashika katika kazi hii?

| Katika makundi madogo, jadili maswali yafuatayo: (Dakika 25) |
|---|

1. Ni uzoefu gani binafsi umekuwa nao katika kuhamasisha maombi au kueneza upandaji kanisa?
2. Unajua mitandao yoyote ya kitaifa, kimkoa au jiji ya maombi?
3. Ni kwa njia zipi nzuri umetunza mawasiliano mazuri kati ya timu yako ya maombi na huduma yako ya upandaji kanisa?
4. Unajua mtandao wowote wa kitaifa au kieneo au kimji?
5. Ni kwa njia zipi ambazo umetunza mawasiliano mazuri kati ya timu yako ya maombi na huduma yako ya upandaji kanisa
6. Katika darasa chukua mda kujadili jinsi nyie kama wapanda kanisa mnaweza kushirikisha maono kwa kueneza upandaji kanisa na maombi kwa makanisa mengine na kati kati ya dhehebu lako.

7. Umewahi kuhudhuria maombi ya kujirudia au kusanyiko la maombi? Ilikuwaje? Jinsi gani unaweza kupanga kusanyiko la maombi katika jiji lako au mji?
8. Ni nini mapenzi ya Mungu kuhusiana na maombi katika maisha yako? Maombi, kama kipao mbele, swala ambalo si la kutokujadiliana kwa viongozi?
9. Kwa nini maombi siyo sehemu nyeti sana ya maisha yetu na huduma?

**III. Funza na Andaa** Watu **Kuomba** kwa Ajili ya Kueneza Upandaji Kanisa

Njia za Kutia Moyo Maombi

Maombi ya Utatu ( kuomba katika kundi la watatu)

Maombi ya kutembea katika eneo la mkazo

Kuanzisha timu ya msaada wa maombi kwa juhudi za upandaji kanisa

Vita vya Kiroho

Kushirikisha habari kati ya makundi ya maombi na uinjilisti na juhudi za upandaji kanisa

Kongamano la Maombi

Siku ya Maombi Kitaifa

Kuomba na Kufunga

**IV. Tafuta na Weka Mtandao wa Viongozi wa Maombi**

**Tabia za Viongozi wa Maombi**

| | |
|---|---|
| Tabia ya utiifu na unyenyekevu | Sifa njema |
| Wawezeshaji wazuri wa mikutano ya maombi | Siyo mwenye porojo |
| Waliojitoa kwa nguvu kwa Kristo | Kuwa na uwiano mzuri kihisia |
| Mwaminifu katika malezi ya kiroho | Anaelewa upandaji kanisa |
| Uhusiano mzuri na watu | Mpangiliaji kati ya kundi la maombi |

Ni kwa njia zipi nzuri umetunza mawasiliano mazuri kati ya timu yako ya maombi na huduma yako ya upandaji kanisa?

Katika darasa chukua mda kujadili jinsi nyie kama wapanda kanisa mnaweza kushirikisha maono kwa kueneza upandaji kanisa na maombi kwa makanisa mengine na kati kati ya dhehebu lako.

Umewahi kuhudhuria maombi ya kujirudia au kusanyiko la maombi? Ilikuwaje? Jinsi gani unaweza kupanga kusanyiko la maombi katika jiji lako au mji?

Ni nini mapenzi ya Mungu kuhusiana na maombi katika maisha yako? Maombi, kama kipao mbele, swala ambalo si la kutokujadiliana kwa viongozi?

Kwa nini maombi siyo sehemu nyeti sana ya maisha yetu na huduma?

**UTEKELEZAJI WA AZIMIO**

Fanya marudio ya sura mbali mbali za maombi ya kuhamasisha kwa kueneza upandaji kanisa. Amua ni katika hatua zipi unaweza kuchukua kusaidia kuhamasisha maombi kwa ajili ya jiji lako, mkoa, au nchi.

# Maombi – Azimio la Mafunzo 11,12

## Kongamano la Maombi: Kumshukuru Mungu kwa Uaminifu Wake

(Panga somo hili kwa kipindi cha saa mbili)

Panga kiuangalifu kuufanya mda wa kutia moyo, baraka na kusherehekea. Chagua watu wawili au wanne wa kushirikisha jinsi Bwana alivyobariki juhudi zao za upandaji kanisa. Kisha gawanyika katika makundi madogo kuwapa watu mda zaidi wa kushirikisha. Mwishoni, kutaneni tena kwa mada wa sifa na kuabudu.
Uwe na ramani ya nchi na orodha ya makundi ya watu wasiofikiwa kuitumia wakati wa maombi ya pamoja. Tumia historia ya ukristo katika nchi yako kama chanzo cha kichwa
Tambua: Zaburi 67 ni zaburi bora kutumia kama kisa cha maombi haya ya pamoja

**I. Mtukuze Mungu kwa Kuwa Mungu Mwaminifu--** Imba pamoja idadi ya nyimbo au pambio ambazo zinakazia kwenye kutoa shukurani kwa Mungu kwa ajili ya uaminifu wake.Waulize wafunzwa kufikiria sehemu yoyote ndogo ya maandiko ambayo yanahusiana na uaminifu wa Mungu, na kuyasoma kwenye kundi yanapokuja akilini.

**II. Kumbuka Baraka zilizopita za Bwana**

**A. Kwa kila mmoja Wetu Pekee**

Shirikisha ushuhuda mdogo wa jinsi Bwana alivyofanya kazi katika wokovu wako binafsi na ukuaji.

B. **Kwa Familia Zetu**

Shirikisha shuhuda za kazi ya Mungu katika familia yako.

**C. Katika Huduma Yako ya Upandaji Kanisa**

Uwe na watu binafsi watatu au wanne wa kushirikisha kundi lote njia ambazo walimuona Bwana akibariki huduma yao ya upandaji kanisa au masomo ambayo Bwana aliwafundisha wakati wa mzunguko wa mafunzo.

Katika makundi madogo, ruhusu kila mmoja anayetaka kushirikisha baraka kutoka kwa Bwana.

**D. Kwa Kanisa katika Taifa Lako**

Somo la Kanisa la 18, "Historia ya Ukristo katika___," Linajadili msingi wa ukristo katika nchi yako.Tumia hili kama kiongozi kwenye maombi.

Mshukuru Mungu kwa wamishenari wa kwanza walioleta injili katika nchi yako.

Mshukuru Mungu kwa kuandaa mioyo ya waumini wa kwanza kupokea injili.

Mshukuru Mungu kwa wafia dini—hao waliokufa kwa ajili ya imani yao nchini kwako.

Mshukuru kwa ajili ya wamishenari ambao wametumwa nje kutoka nchini mwako kwenda sehemu nyingine za ulimwengu.

Msifu Mungu kwa Uchungaji wake wa kanisa katika historia.

Mshukuru Mungu kwa Ajili Yake, Kwa baraka zake zilizopita, kwa baraka zake zijazo.

**V. Omba kwa Ajili ya Kazi Inayoendelea ya Upandaji Kanisa**

Katika makundi madogo, wafanye wafunzwa waombe kwa ajili ya kila mmoja wapo. Kuomba kwa ajili ya kuendelea kwa ufalme wa Mungu kwenye jiji na mikoa ambapo wapanda kanisa wanafanya kazi. Omba kwa ajili ya amani na ujasiri wa kutangaza injili.

Kwenye kundi kubwa, omba kwa ajili ya taifa lote. Muombe Mungu kwa ajili ya ukuaji ulioendelezwa na upanuzi wa ufalme wake kupenye sehemu zote za taifa. Omba kwamba injili itapenya kwa makundi ya watu wasiofikiwa. Tumia ramani ya nchi na orodha ya makundi ya watu wasiofikiwa kusaidia mda huu wa maombi.

**IV. Sherehekea Wema wa Bwana katika Wimbo na Kuabudu**

# Uongozi – Azimio la Mafunzo 11

## Kuwatoa Viongozi

**I. wapanda Kanisa lazima Watoe Wengine Kwenye Huduma**

**A. Mfano wa Yohana Mbatizaji (Marko 1:5, Yohana 1:35-36)**

Gawanyika katika makundi madogo. Mmoja katika kundi atasoma **Yohana 3:22-30.**

Ni tatizo gani liliwaudhi wanafunzi wa Yohana katika mstari wa 26?

Kwa nini unadhani walikuwa wamesumbuka?

Jinsi gani unafikiri walitarajia Yohana kuitikia? Kwa nini?

Ni neno gani Yohana anatumia katika mstari wa 29 kuelezea tabia yake kuhusu hali hii?

Unafikiria nini kuhusu ufupisho wa Yohana katika mstari wa 30? Alikuwa na moyo mweupe? Ni aina gani ya hisia unadhani alijisikia alipofanya maelezo hayo?

Jinsi gani kuitikia kwa Yohana ni sawa au tofauti kutoka kwenye tabia ya kawaidia ya viongozi wakristo ambao umewajua wakati huduma ya mtu fulani ilipoanza kuzidi zao?

**B. Mfano wa Paulo**

Baada ya majadiliano haya, kundi litasoma **Flp 1:15-18** na kujadili maswali saba yafuatayo.

Elezea aina mbili za mahubiri ambayo wengine walikuwa wakifanya wakati Paulo akiwa gerezani, kufuatana na mstari wa 15-17. Unajisikiaje kuhusu aina hizi za huduma? Kwa nini?

Nini kilikuwa kitu muhimu sana kwa Paulo, kufuatana na mstari wa18?

Nini Paulo alichofanya kwenye kuhubiri kutoka katika nia ya kweli?

Nini Paulo alichofanya kuhubiri kutoka kwenye nia ya uongo?

Unafikiri nia zilikuwa muhimu kwa Paulo?

Jinsi gani unadhani Paulo aliweza kuitikia kwa njia hii?

Nini utakachofanya wakati mtu mwingine akihubiri injili kwa njia ambayo hukubaliani nayo, au unapokuwa na maswali juu ya nia zao?

Jinsi gani Paulo angetumia mda mfupi wa kufundisha viongozi, na kisha kuendelea na kuwaacha wakiwa wasimamizi? Hakuwa ameogopa kwamba wangefanya kitu fulani kimakosa?

**II. Mtatizo ya Kutoa**

A. Kuogopa kwamba Kiongozi Atafanya K**azi Nzuri**

Hili linaweza kuwa tatizo kwa mpanda kanisa katika mkoa huu? Kwa nini?

Kuogopa kwamba Kiongozi Atafanya kazi Mbaya

Ni nini ufunguo wa kushinda wasi wasi huu?

**III. Kanuni za Kutoa**

A. Anzisha na Tunza Uhusiano wa Ndani**--1The 2:8, 2Tim 3:10**

B. Hakikisha Viongozi Wajao **Wanaendelea Kumiliki Maono**

**C. Usisubiri Sana Kuachilia**

D. **Tarajia Makosa -Mt 17:19-21**

**E. Mtumaini Mungu Kutenda Kupitia Wengine -Yohana 14:12**

**F. Epuka Kujitenga**

Katika makundi madogo, jadili maswali hapo chini yanayoshughulika na swala la Daudi na Samweli (Dakika 20)

Daudi ni mpanda kanisa mpya Nakuru. Alifanya kazi katika jumuia yake kuanzisha kikundi kiini na kulisha ukuaji wake. Alipata mtu aliyemfanya kiongozi wake msaidizi, Samweli. Daudi na Samweli mara walichukua uongozi katika kuanzisha kikundi kiini cha pili. Sasa, Daudi anajaribu kuamua kama ni mda wa kutoa uongozi wa kikundi hiki cha pili chote kwa samweli.

Ni swali gani Daudi anatakiwa kujiuliza mwenyewe kumuongoza katika kutumia kila moja ya kanuni sita?

Kwa nini kuachilia ni muhimu sana?

Wangapi katika kanisa lako wana wajibika na huduma?

Kwa mda gani mtume Paulo kawaida alifanya kazi na waumini kabla hajahama na kuwaamini kuendeleza kazi ya kanisa mpya?

Nini kinatokea wakati kanisa lako mama linapokataa kuachilia viongozi wapya kwenye huduma mpya?

## Utekelezaji wa Azimio

Wakati gani na jinsi gani unapanga juu ya kuachilia kiongozi mwanafunzi? Unamuona akichukua baadhi ya majukumu yako ya zamani, au wakiendeleza huduma zao? Fanya mpango, na anza kufanya kazi kuelekea kuwaachilia kufikia umaarufu wao.

# Vikundi Kiini – Azimio la Mafunzo 12

### Viini Vinavyoenea Kupitia Makanisa ya Mtaa

I. Tathimini—**Vikundi Kiini ni Sahihi kwa kanisa lako?**

A. **Maono--** Ni maono yapi waliyonayo viongozi kwa ajili ya kanisa? Inawezekana kwamba vikundi kiini vitumike kusaidia na kutia moyo maono? Kwa kudhania kuwa uinjilisti na ukuaji unatokea katika makundi, jinsi gani makundi yanayozaliana yanaweza kutumia katika mkakati wa huduma kwa ujumla.

B. **Kujitolea**-- Viongozi wako tayari kujitolea kwenye msisitizo huu kwenye huduma ya vikundi?

C. **Huduma Zilizopo**-- Kuna maeneo yenye migogoro maarufu? Kati ya huduma zilizopo na vikundi kiini? Baadhi ya huduma zilizopo zitahitaji kubadilishwa au kuondolewa kama makundi yanatumika?

D. **Mapokeo dhidi ya Mawazo**—kanuni inayotumika ya kufanyia uinjilisti wa mahusiano katika makundi kuwa kitu kigumu kwa baadhi ya wajumbe wa kanisa kukikubali?

E**. Mahali**-- Kwa kudhani kuwa makundi yanakua na kuzidi, wapi kundi jipya litakutana?

F. **Uongozi—**Kutafuta viongozi wa kiini itakuwa vigumu katika kanisa lako? Watahitaji mafunzo? Kuna aliye tayari kuwa mshauri wa viongozi wa vikundi kiini na aliye tayari kukutana na viongozi angalau mara moja kwa mwezi, vile vile na kutoa mafunzo yanayoendelea na kutia moyo?

**II. Upangaji na Uwekaji-Viongozi wa kanisa wanatakiwa kufata hatua hizi kutumia vikundi kiini**

A. **Hatua 1 –** Anzisha Maono ya Huduma Ambayo ni pamoja na Vikundi Kiini
B. **Hatua 2 –Anza Kushirikisha Maono na Kusanyiko**
C. **Hatua 3 –Chagua Viongozi na Wafunze**
D. **Hatua 4 –Anzisha Vikundi Kiini Vipya**
E. **Hatua 5 –Toa Tathimi Inayoendelea na Marekebisho Kwenye Huduma ya Kikundi Kiini**

Kwa kufikiria faida zote za vikundi kiini kweye maeneo ya ushirika, kufuasa, uinjilisti na maendeleo ya uongozi, kwa nini kila kanisa lisitumie vikundi kiini?

Ngoja tudhani kwamba kanisa limeamua kuanza kutumia vikundi kiini. Jinsi gani unaweza kuepuka "ushindani" kati ya huduma zilizopo za ufuasishaji na uinjilisti na huduma hizi sawa kwenye vikundi kiini?

Kwa nini ni muhimu kuwa na mshauri kwa viongozi wa vikundi kiini katika kanisa? Nini wajibu na majukumu yake?

Kwa nini "uongozi" wa kikundi kiini unatakiwa kuanzishwa miongoni mwa viongozi wa vikundi kiini wajao katika kanisa kabla kikundi kiini chochote kuanzishwa? Ni nini faida za kuwa na uongozi wa kanisa uliohusika katika huu "uongozi" wa kiini?

Ni nini lengo la jumla la kutumia vikundi kiini katika mfumo wa kanisa lililopo?

**UTEKELEZAJI WA AZIMIO**

Fikiria kuhusu kanisa unalidhania kuwa kanisa lako la "nyumbani". Ni nini maono ya kanisa? Ni malengo yapi lililo nayo? Inaweza ikawezekana kutumia vikundi kiini kusaidia kufikia malengo haya?

Katika kanisa hili hili, nini matatizo au ugumu ungeweza kuwepo kama vikundi kiini vingetumika?

Anzisha mpango mfupi, ulioandikwa kwa kutumia vikundi kiini katika kanisa hili (au katika kanisa lolote ambalo unalijua). Jinsi gani unaweza kuweka mpango huu?

Fikiria makanisa unayoyajua ambayo yangefaidi kutoka katika huduma ya vikundi kiini. Jinsi gani unaweza kuyaendea kuhusu kutumia vikundi kiini kuimarisha kanisa na kulisaidia kufikia malengo yake? Unaweza ukawa tayari kuyasaidia kuanzisha huduma ya kikundi kiini katika kanisa? Lipe hili uangalizi wa makini na maombi.

# Vikundi Kiini – Azimio la Mafunzo 13

## **Kusimamia Viini:** Uangalizi na Kupangilia Kwa Ajili ya Viongozi wa Kikundi Kiini

Jiunde katika makundi madogo na jibu maswali hapo chini kwa kutumia mchanganuo wa Petro, Sandra na Michael kama mandhali. .

Timu ya wamishenari wawili (Petro, Sandra and Michael) wamekuwa wakifanya kazi katika jiji lenye karibu watu 35,000 kwa miaka mitatu iliyopita. Wote wameanzisha vikundi kiini kadhaa, na baadhi ya vikundi hivi vimeongezeka mara kadhaa zaidi. Kama mtu angeangalia kwenye idadi ya watu wanaokutana na idiadi ya watu waliookoka, ingeweza kuonekana kwamba huduma yao imekuwa na mafanikio hata hivyo.

Kwa jinsi hiyo, vikundi vinaendelea kukua na kuzidi, Petro, Sandra and Michael wanachanganyikiwa zaidi na zaidi. Kila mmoja wao amekuwa na matatizo na maswali katika kujaribu kuanzisha kiongozi mwanafunzi mpya, na hakuna mmoja wa kuendea kwa ajili ya ushauri. Wote wana kazi nyingi ambazo hata inakuwa mara chache kuonana wao kwa wao. Na inaonekana kana kwamba wote wamechukuliwa katika huduma zao tofauti. Wakati Petro, Sandra and Michael walipoanza kufanya kazi kwenye jiji, Petro alikuwa

na maono ya kuanzisha makanisa kadhaa kwa kutumia vikundi kiini. Hivi karibuni, ingawa, kila mmoja ana kazi nyingi na kikundi chake mwenyewe kiasi kwamba hakuna mmoja anayezungumzia hilo tena

Kile ambacho Petro, Sandra and Michael hawajui ni kwamba vingi kati ya vikundi kiini kadhaa vipya vinakutana na matatizo ambayo baadhi ya viongozi wenye uzoefu zaidi wangeweza kusaidia, lakini hakuna aliyewaambia au kuwapa msaada. Vikundi viwili kati yake vinapanga kuendesha kufikia nje kiuinjilisti kwenye eneo hilo hilo la jiji, wakati eneo kubwa la mji linabakia kutokuwa na aina yoyote ya ushuhuda kwa ajili ya Kristo. Petro anafurahi kuwa viini vinaendelea kukua na kuzidi, lakini inaonekana kwake kwamba kwa jinsi fulani wanaweza kukamilisha zaidi kama wangepata njia ya kufanya kazi kwa umoja na ya mmoja kwa mwingine.

Ambacho Petro hatambui katika muonekano huo ni kwamba kuna sura ya kiuongozi ambayo inakosekana kutoka kwenye huduma yake ya kikundi kiini. Mtu fulani anahitajika kutoa usimamizi kwa ajili ya viini ili kupanga na kupangilia juhudi zao wanapokuwa wakifikia nje kwenye jiji lao.

Ni sura zipi za usimamizi zinaweza kuwa za kutumika zaidi: Upangiliaji, Kuelekeza, Uwajibikaji, au Unyoofu?
Ni kazi ipi ya muundo wa kiusimamizi unaonekana kuhitajika zaidi: matatizo kwenye kundi, ukuaji binafsi wa kiroho, kuendeleza viongozi wanafunzi, upangaji na uwajibikaji, ujuzi wa kivitendo wa huduma, kutia moyo, na maombi?
Mwangalizi anaweza kuhitajika katika hali hii?

**I. Usimamizi wa Vikundi Kiini**


A. Ni **Sababu ipi ya Kuhitaji Msimamizi?** Jib: (1) Kupangilia shughuli, (2) **Kuelekeza** katika matatizo na ugumu, (3) Kushikilia **uwajibikaji** wa viongozi wa viongozi wa kikundi kiini, na (4) **Unyoofu** kwenye Neno la Mungu.

**II. Muundo wa Kiusimamizi kwa Vielezo Tofauti** vya Huduma ya Kikundi Kiini

**A. Kielezo 1: Vikundi Viini Vinavyoanzisha kanisa la Mapokeo kwa Viini**

**Kielelezo 13.2 Viini Vinavyoanzisha kanisa**

**Kielelezo 13.2 Viini Vinaanzisha Kanisa**





Katika hali hii, kikundi kimoja au zaidi ya vikundi kiini vya awali vinakua na kuongezeka mara dufu mpaka vinapokuwa vinaweza kuanzisha kanisa mpya la mapokeo. Katika hali hii, muundo wa kiusimamizi utahitajika mda mrefu kabla kanisa halijaanzishwa. Mtindo huu utahitaji angalau mpangaji mmoja kuanagalia huduma ya kila kiini pekee na kuwasaidia viongozi kupanga juhudi za kuanzisha kanisa mpya.

**B. Mtindo 2: Kanisa Lililopo Linaanza Kutumia Vikundi Kiini**

**Kielelezo 13.3 Viini Vilivyoongezwa Kwenye kanisa**

Kanisa lililopo kuanza vikundi kiini kwa ajili ya ushirika, uinjilisti, na ufuasishaji. Kikufanana, muundo wa kiusimamizi katika hali hii unatumia viongozi wa kanisa waliopo kutimiza wajibu wa mpangaji na mwangalizi.


**Kielelezo 13.3 Viini Vinaongezwa Kwenye Kanisa**




## C. Kielezo 3: Vikundi Kiini ambavyo Vinaanzisha kanisa la Kikundi Kiini

Kanisa lina mkusanyiko wa viini vyenyewe, na kazi zote za kanisa zinatokea katika kila kiini, ikiwepo ubatizo na meza ya Bwana. Viini vinakutana pamoja mara moja moja kwa ajili ya mkutano wa kusherehea. Huu ni mda wa kutia moyo, ushirika, kuabudu na/au mafundisho.

**Figure 13.4 Cells Start a Cell Church**





Mara nyingi, muundo wa kiusimamizi kwa kanisa la kikundi kiini ni rahisi na wa kimadaraja. Kila vikundi kiini vitano, vina mpangaji na kuna mwangalizi kwa kila wapangaji watano

### C. Mtindo 4: Vikundi Kiini Kadhaa Vinakua, Vinazidi na "kulisha" Makanisa ya Mtaa Yaliyopo Kielelezo 13. 5 Viini Vinalisha Makanisa

Vikundi kiini vinaweza kujenga na kuimarisha makanisa ya mtaa yaliyopo ambayo katika mda yataanzisha makanisa binti mapya. Katika hali hii, moja ya viongozi wa kikundi kiini anaweza kushika wajibu wa mpangaji, ili kusaidia kupanga juhudi za vikundi kujenga makanisa kwenye eneo hilo.

**Kielelezo 13.5 Viini Vinalisha Makanisa**




**Ni nini uwezo na udhaifu wa kila moja ya kielezo cha huduma ya kikundi kiini?**
Kama ilikuwa uchague moja ya vielezo hivi kwa hali yako ya kanisa, ingekuwa kipi na kwa nini?

Elezea hitaji la baadhi ya mahitaji ya muundo wa kiusimamizi unapofanya kazi na huduma ya kikundi kiini. Kwa nini usiviache viini kufanya vyovyote wanavyotaka? Ni faida zipi za kuwa na kuwepo kwa muundo wa kiusimamizi?

Kwa maneno yako mwenyewe, kwa kifupi elezea kazi za kiuongozi ambazo zinatakiwa zitokee kwenye huduma yoyote inayoendelea ya kikundi kiini.

Kama kwa sasa unajihusisha katika huduma ya vikundi kiini na hakuna mmoja bado anayeshikilia wajibu wa mpangaji, nani unaweza kumwendea kuhusu kuwa mpangaji? Unaweza kujifikiria kushika wajibu huu wakati fulani mbeleni?

Inawezekana kwa wapangaji na waangalizi kuendelea kuwa viongozi wa vikundi kiini?

**UTEKELEZAJI WA AZIMIO**

Halafu, anzisha mpango rahisi wa aina ya muundo wa kiusimamizi ambao ni wa lazima katika mandhali ya huduma ya kikundi kiini chako maalumu. Fikiria juu ya vichwa utakavyoweza kutumia kwenye wajibu wa mpangaji na mwangalizi. Hata kama una vikundi kiini kadhaa wakati huo, nani wanaoweza kushika wajibu wa mpangaji kwa vikundi hivi? Roho Mtakatifu anavyoendelea kufanya kazi na kundi lako linakua na kuzidi, jinsi gani utaamua nani watakuwa wapangaji na waangalizi wa mbeleni? Wapi watatoka, na aina gani ya mafunzo au uzoefu watahitaji ili kuwaandaa kwa aina hii ya huduma? Ni aina gani ya muundo wa kiusimamizi unaohitaji kutunza na kuchochea ukuaji na haja za Mungu kuona ikitokea katika vikundi kiini vyako? Ni aina gani ya muundo wa kiusimamizi utaendana vema zaidi na mtindo wa huduma unayofanya nayo kazi? Chora katika mpango wako mchoro wa mtindo unaotumia na jinsi muundo wa kiusimamizi uliochagua unafaa katika mtindo huu.

Fanya marudio ya mpango wako kwa ajili ya muundo wa kiusimamizi na mshauri wako au na mkufunzi wa somo hili.

# Kuhubiri – Azimio la Mafunzo 1

## **Kuhubili Kibiblia I:** Kuuelewa Ujumbe

Ni nini kusudi la jumla la ujumbe wa kibiblia-yaani, unapofundisha ujumbe wa kibiblia au kuhubiri, ni nini matokeo yunayotakiwa kwa hao wanaousikiliza?

Ni vigezo gani vitatu ambavyo vinagusa endapo au la kama makusudio haya yatapatikana? Jib: (1) Ujumbe, (2) Watazamaji na (3) msemaji.

**I. Kujifunza Biblia Kwa Kufata Neno—Msingi Imara**

Ni njia ipi bora kuhakikisha kwamba tunatoa ujumbe wa Mungu na siyo mawazo yetu wenyewe?

**II. Wazo Kuu la Ujumbe**

Ni nini mhubiri mfanisi anachojenga ujumbe kuzunguka kwacho?

Ni nini katika ujumbe kinaunga mkono kisa moja kwa moja au si moja kwa moja?

**A. Weka Wazi Wazo Kuu (Kisa)**

Inasaidia mara nyingi kueleza wazo la kati la ujumbe kwa kuainisha vitu viwili muhimu: Kichwa na Ujazo.

Ina maana gani kwa kichwa cha ujumbe?

Ina maana gani kwa ujazo wa ujumbe?

Weka mchoro ufuatao ubaoni na wanafunzi wapanda kanisa waujaze.

| Aya | Kichwa | Ujazo | Wazo Kuu |
|---|---|---|---|
| **Yohana 3:17** | | | |
| **Zaburi 23:1** | | | |
| **Zaburi 67:1** | | | |
| **Rum. 5:8** | | | |

**B. Amua Kusudi la Ujumbe**

Kama umegundua mwitikio au utekelezaji ambao unaamini Bwana anataka kutoka kwenye fungu, Umegundua ____________________. Jib. Kusudi la ujumbe.

**III. Muundo wa Ujumbe**

**A. Utangulizi**

Ni nini makusudi matatu ya utangulizi wa mahubiri? Jib. Kusalimisha usikivu wa wasikilizaji, Kutoa kichwa cha mahubiri, Kuhusisha kichwa na mahitaji wanayojisikia wasikilizaji.

**B. Mwili**

Ni nini mwili wa mahubiri. Jib.Yaliyomo au mwili.

Moyo wa ujumbe unatakiwa utoke ______________. Kwa nini? Jib. Neno

**C. Suluhu**

Ni nini suluhu la ujumbe linachofanya? Jib. Kuweka kwa ufupi na kuita kwa ajili ya kuitikia na kujitoa.

Ni nini vipengele vya suluhu? Jib. Ufupisho au nukuru ambazo zinaleta pamoja wazo kuu; swali; maombi; na/au mwelekeo maalumu au rufaa kwenye utekelezaji.

**D. Vielelezo**

Ni nini kusudi la kutumia vielelezo? Jib. Kufanya wazo kueleweka zaidi au kuwa katika mkazo. Kielelezo kizuri kinatakiwa kitumike wakati wote mda unaporuhusu?

1. **Vielelezo vya Kibiblia**
   Ni vielelezo gani Yesu alitumia?
   Ni nini aina ya vielelezo vya kibiblia?
2. **Aina za vielelezo visivyo vya kibiblia**
   Ni nini baadhi ya vielelezo visivyo vya kibiblia? Jib. Matukio ya sasa, ya kihistoria, ya nyumba na uchunguzi wa asili, uzoefu binafsi, au maisha ya kila siku.
3. **Masomo ya Kitu**

Ni somo lipi la kitu  la ufanisi umesoma juu yake, kusikia kutoka kwa wengine au kutumia?

**IV. Aina za Ujumbe**

A. Wa Kuelekeza-**Unatoa ukweli na mafundisho ya kujulisha**
Unaelezea mahubiri ya kuelekeza.

B. Kiibada –**unatafuta mwitikio wa kiroho**
Ni nini kusudi la ujumbe wa kiibada?

C. Kimasimulizi- **unajengwa juu ya masimulizi**
Ni nini baadhi ya ujumbe wa kimasimulizi katika Biblia?

D. Kikuuliza-**unajibu maswali ya ufunguo**
Elezea mahubiri ya kikuuliza yanakuwaje? Kama umewahi kusikia mmoja, elezea juu yake.

Kimzunguko au kimstari-**kimstari unakwenda wazo hadi wazi, kimzunguko unarudi kwenye wazo kuu kwa kujirudia.**

**Jumbe nyingi ulizowahi kusikia zaidi ni za kimzungukoo au kimstari? Elezea kwa nini unasema hili.**

Fikiria kuhusu mmoja wa wahubiri bora uliowahi kusikia. Nini tabia ya mtindo wa kuhubiri kwao au yaliyomo yaliyofanya kuwa ya ufanisi? Watu waliitikiaje kwenye mahubiri yao?

Kwa nini mahubiri yatokane na kujifunza Biblia kwa kufata neno?

Nini kazi ya mahubiri kibiblia? Kuna mifumo tofauti ya kukamilisha kazi hii?

**UTEKELEZAJI WA AZIMIO**

Chagua moja ya kitabu cha injili, na unapokuwa unakisoma, fanya orodha ya vielelezo au somo la kitu unaloona limetumika.

Chukua chumba katika kota yako au nyumba na angalia kuzunguka ndani yake vitu ambavyo vinaweza kuwa vya masono ya vitu vya ukweli wa kiroho. Uwe mbunifu. Chunguza hata vitu rahisi vinavyoweza kuelezea kwa nguvu mawazo magumu ya kibiblia.

# Kuhubiri – Azimio la Mafunzo 2

## **Kuhubiri Kibiblia II:** Kuelewa wasikilizaji

**I. Mahubiri ya Agani Jipya**

A. **Kuhubiri kwa Yesu**
Jinsi gani ujumbe wa Yesu ulitofautiana wakati wasikilizaji walipokuwa Mafarisayo ikilinganishwa na walipokuwa wanafunzi?
Ni nini **Mathayo 13:10-15** inatuambia kuhusu kurithi kwa Yesu kwa wasikilizaji?

**B. Kuhubiri kwa Petro**
**Linganisha** Matendo 2:17-21 na Matendo 10:34-35. **Jinsi gani ujumbe wa Petro kwa Wayahudi unatofautiana** na wa kwa Mataifa?

**C. Kuhubiri kwa  Paulo**

Jinsi gani ujumbe wa Paulo kwa Wayahudi wanaoamini unatofautiana na mahubiri kwa wasoamini Mataifa kama ilivyoonyeshwa katika mchoro 2.1? Kwa nini?

**Mchoro 2.1 Mahubiri ya Paulo**

| *Aya* | *Wasikilizaji* | *Utangulizi* | *Ujumbe* |
|---|---|---|---|
| Mdo 13:16-41 | Wayahudi wasioamini Pisidian Antiokia | • Historia ya zamani ya Waisraeli na nukuru za Agano la Kale | • Hitaji la toba<br>• Kristo |
| Mdoa 17:22-31 | Mataifa wasioamini huko Atheni | • Madhabahu yao ya ndani | • Kuwepo wakati wote kwa Mungu<br>• Kufufuka kwa Kristo |
| Mdo 20:18-35 | Wazee wa kanisa la Waefeso huko Mileto | • Maisha ya Paulo miongoni mwao | • Haja ya Paulo ya kuhudumu<br>• Wajibu wao kwenye kundi |
| Mdo 22:1-21 | Mob Myahudi asiyeamini huko Yerusalemu | • Historia ya Paulo kama Mfarisayo na mtesaji wa kanisa | • Kukata shauri kwa Paulo (ushuhuda)<br>• Misheni ya Paulo kwa Mataifa. |
| Mdo 26:2-23 | Mfalme Myahudi asiyeamini herodi Agripa huko Kaisaria | • Shukurani kwa Agripa<br>• Maisha ya Paulo yaliyopita | • Maisha ya Paulo ya nyuma<br>• Kukata shauri kwa Paulo<br>• Msamaha kupitia Kristo |

Mchoro 2.1 **II. Kukusudia kwa Wasikilizaji wako wanaolengwa**

A. Ni nini baadhi ya **tabia muhimu za wasikilizaji?** Jib. Umri, ngazi ya kiroho, elimu, mapendeleo, historia ya kibiblia, historia ya kidini, hali ya familia, ajira na kijinsia.

> Katika makundi madogo, jadili watazamaji halisi wa kikundi kiini au makanisa ya wajumbe wa kundi kwa misingi ya tabia zilizoorodheshwa hapo juu. Kisha wafanye wajadili mahitaji ya wasikilizaji hawa.

**B. Ni nini Mahitaji ya Wasikilizaji—1 Kor 3:2**

Ni nini baadhi ya mafungu ya maandiko ambayo yanazungumzia vema mahitaji ya waumini?
Ni baadhi ya vifungu gani ambavyo vinagusia mahitaji ya wasikilizaji mchanganyiko?
Ni baadhi ya vifungu vipi vinagusia mahitaji ya wasioamini?

**III. Kusaidia Wasikilizaji Kugundua**

Kwa nini tujisumbue kuhubiri?
Kwa nini tusiwape tu Biblia na kuwaacha kuisoma?

Jinsi gani unafikiri Paulo alivyolichukulia swala la miungu katika kifungu cha Matendo 17:16-34? Jinsi gani ungekuwa umetoa ujumbe huo katika hali inayofanana?

Ni njia ipi ni bora ‘kuwianisha mlo’ kwenye ujumbe kwa ajili ya kundi mchanganyiko?

Vitu gani unafikiri ni ‘nyama’ na vitu gani ni ‘maziwa’?

**UTEKELEZAJI WA AZIMIO**

Soma nyuma kwenye orodha za tabia kwenye sehemu ya 11. A. kisha tathimini kundi unalohudumu. Andika maelezo mafupi kufupisha kila maana kadiri inavyohusiana na kundi lako. Kuna tabia nyingine muhimu unayohitaji kuongeza kwenye orodha kuweza kueleza vya kutosha wasikilizaji wako? Nini unachohitaji bado kuendelea kujifunza kuhusu wao ili kuhubiri kwa namna ambayo inakidhi mahitaji yao?

Inayofata, tathimini moja ya ujumbe ambao umehubiri hivi karibuni, au ulioandaa kuhubiri hivi karibuni. Unaendana na kundi hili? Kwa nini na kwa nini siyo? Jinsi gani unaweza kuurekebisha kuufanya kuendana zaidi, wa kuvutia na kutumika?

# Kuhubiri – Azimio la Mafunzo 3

## **Kuhubiri Kibiblia III:** Kujielewa Mwenyewe

Ni kwa njia zipi mzungumzaji anagusa kupokea kwetu kwa ujumbe?

**I. Maswala ya Kiroho**

**A. Kwa wewe Mwenyewe**

Jinsi gani unaweza kujua lini huwi "wewe mwenyewe?"

Unakuta kuitikia kwa Mungu kwa Musa katika **Kut 4:10-12** kuwa msaada kwako?

**B. Toa umakini katika kutembea kwako na Bwana**

Jinsi gani unaweza kutumia **1 Tim. 4:16** kwenye kuhubiri kwako?

Ni nini tunaweza kujifunza kutoka **Matendo 4:13** kuhusu kilicho muhimu kwa muhubiri?

**II. Maswala ya Kihisia**

**A. Hofu ya Kuongea kwa Umati**

| |
|---|
| Katika makundi madogo, jadili swala lifuatalo na maswali: (Dakika 15) |

Yohana anahofu mbaya sana ya kuongea mbele ya kundi. Kabla hajaanza kuzungumza anakuwa na wasi wasi. Baada ya dakika chache za kuongea mdomo wake unakauka na mikono yake inakuwa baridi na kutoa jasho. Ameshaambiwa kwamba kwa uzoefu hili litapungua. Hata hivyo, hajaona kupungua baada ya mahubiri kadhaa.

Ni nini kinaweza kuwa sababu ya hofu ya Yohana?

Ni baadhi ya vitu gani ungeweza kumshauri Yohana kupunguza hofu yake?

Ni nini anachoweza kufanya kuepuka mkazo ambao hofu inazalisha?

**B. Kiburi (1 Tim 3:6)**

Ni hatari ipi ya mzungumzaji aliye na kiburi? Jinsi gani kiburi kinajionyesha chenyewe kwa mzungumzaji?

**III. Maswala ya Kimwili**

A. **Sauti**—(1) ukubwa, (2) Kusikika kwa sauti (3) Matamshi, (4) Wepesi na Uharaka, (5) Rithisha Sauti Yako Kwenye Kusikika kwenye Chumba. Ni ipi kati ya tabia hizi za sauti unaiona kuwa ngumu zaidi? Na ipi ni muhimu zaidi?

**B.** Muonekano**—(1)Uvaaji, (2) Mkao, (3) Ishara**

Ni ipi kati ya tabia hizi za muonekano unakuta ni vigumu kuifanya vema? Na ipi muhimu zaidi?

**C. Usomaji Kiufafanuzi**

Elewa fungu kwanza. Angalia kusudi lake. Kamata hisia za masimulizi au mwandishi.

Kama zoezi la pekee, "Fikiria msemaji mfanisi wa umma uliyewahi kumsikia.

Mpe kiwango mtu huyo kama dhahili, nzuri, inatosha au hafifu kwa misingi ya kila moja ya vitu kwenye "sauti" na Muonekano"

Kulikuwa na maeneo ya "sauti" au "Muonekano" ya msemaji mfanisi uliyemuwekea kiwango ambayo yamemfanya mfanisi hasa hasa? Yalikuwa nini na kwa nini yalikuwa ya ufanisi?

**UTEKELEZAJI WA AZIMIO**

Uwe na rafiki atumie kanda ya kurekodia (au video ya kamera, kama una moja) kukurekodi unapotoa ujumbe. Kisha unapokuwa unarudia kanda, tathimini matumizi yako ya sauti kufuatana na kubadilika badilika kulikotolewa katika somo hili. Kama unatumia video, jifunze muonekano wako na lugha ya mwili vile vile. Kama una kanda tu muombe rafiki yako anayerekodi aangalie vitu hivi na kukutathimini.

# Familia – Azimio la Mafunzo 3

## Huduma kwa Familia : Warsha

Mifano iliyotolewa hapa inatumika mara chache kusisimua majadiliano juu ya hitaji la kutafuta uwiano kati ya huduma ya mpanda kanisa na ndoa na familia. Tafadhali jisikie huru kutumia mifano yako mwenyewe na maswali ya majadiliano lakini hakikisha majadiliano yako yanagusia kwenye maswala kama vile uongozi wa kitumishi, utatuzi wa migogoro, kufanya majadiliano sahihi nyumbani, njia zinazofaa za kuonyesha upendo kwa mwenzi wa mtu, kukubali udhaifu wa mwenzi wako na uwezo, n.k. Kiuangalifu jiandae kwa ajili ya kipindi hiki kwa kusoma muonekano wa mambo na kisha anzisha mda wa somo lako kufuatana na maswala ambayo yanasumbua wafunzwa wako. Mfuatano wa mambo na maswali yaliyotolewa yanaweza au yasiweze kutosha kukidhi mahitaji ya mandhali yako maalumu. Katika hali hii, jisikie huru kuanzisha mifano yako mwenyewe na maswali.

Gawanyika katika makundi madogo mwanzoni mwa mda wa somo. Kila kundi linatakiwa kuwa na kundi moja tu la Muonekano wa mambo.

Pata kanuni za kibiblia ambazo zingeweza kutumika kwenye hali.

Wakati wa mwisho wa mda wa kikundi kidogo, kila mmoja akusanyike kama kundi moja kubwa na kila kundi litoe liliyopata.

I**. Muonekano wa Kwanza—James na Luba**

Akiwa ametikiswa na kuyumba yumba kwa treni, James alipumzika chini kwa kukaribisha usingizi wa usiku. Wakati zimekuwa siku tano za kazi nyingi wakati wa semini ya mafunzo, alikuwa ametiwa moyo na kile alichokuwa amejifunza na ushirika wa wengine walio na haja sawa naye: kuanzisha makanisa mapya. Kumekuwa na umoja wakati wa semina. Kila mmoja alielewa mahangaiko yake na kusumbuliwa kwa kuwa wote walikuwa katika hatua ya awali ya kuanzisha makanisa. Mda wao wa maombi ulikuwa wa kiibada na kuwezeshwa.

James alipochukuliwa na usingizi, akinuia kuendelea kwa huduma yake ya upandaji kanisa, alijisikia amani safi na hisia zilizorejezwa za kuwepo kwa nguvu ya Mungu katika maisha yake. Asingesubiri mawazo yake mapya na timu yake ya upandaji kanisa na kuanza kuyaweka katika huduma yake.

Luba, karibia katika mda sawa ambao James alikuwa amechukuliwa na usingizi, alikuwa kati kati ya msiba mkuu wa familia nyingi tangu kuondoka kwa James. Alipowafungia yeye na mtoto mdogo wa James (mtoto wa kike wa miezi 8) alijisikia kuwa na wazimu. Homa ya mafua ikawa imewapiga watoto wote watatu kwa siku mbili zilizopita na sasa mtoto Katiya alikuwa na homa kali na amekuwa akitapika. Luba alikuwa amechoshwa. Kuendelea kwa hitaji la watoto wake na kusafisha kusikoisha kwa uchafu unaotokana na homa ya mafua kulikuwa kumemfikisha mwisho wa nguvu zake kimwili.

Lakini homa ilikuwa ya mwisho katika matatizo kadhaa tangu James alipoondoka. Tofauti na kazi za ziada ambazo zililetwa na kuondoka kwake, Friji yao ilikuwa imeharibika na kuvuja kwa dari kulikuwa kumeharibu baadhi ya ukuta wa sebureni wakati wa mvua kubwa ya mwisho.

Wakiwa wameishi katika mji huu mgeni kwa miezi michache, hakuwa na wa kukimbilia au hata kuongea naye. Alikuwa akikutarajia kurudi kwa James. Msaada wake ungekubaliwa, lakini hata zaidi ya hilo alitaka kuzungumza na mtu kuhusu mizigo ya moyo wake na nafsi inayohusiana na kuishi eneo la porini mbali na familia yake na marafiki na mtindo rahisi wa maisha.

James na Luba waliposalimiana katika mlango wa mbele walikuwa wamefurahi sana kuonana. Hakuweza kusubiri kuzungumzia kuhusu matukio ya wiki iyopita lakini kulikuwa na matatizo ya ghafla ambayo yalihitaji usikivu wa James.

MASWALI YA KUFIKIRIA

1. Ni vitu gani vya mara moja ambavyo James angefanya kufanya hali kuwa bora?
2. Jinsi gani James ataitikia kwenye hali anayokuta nyumbani?
3. Tafadhali eleza unachofikiri James atataka kuzungumzia wakati yeye na Luba watakapokaa chini kwa ajili ya mazungumzo.
4. Ni aina ani ya mzigo Luba anaweza akawa anabeba ambayo alitaka kushirikisha mtu mwingine?
5. Huduma ya James inamtaka kuwa mbali na nyumbani mara kwa mara- wakati mwingine kwa mda wa wiki nzima. Jinsi gani anaweza kuzuia kutokea kwingine kwa kuchosha kama huko?
6. Jinsi gani anaweza kumtia moyo kujiona mwenyewe kama mshiriki wake katika huduma?
7. Jinsi gani mpanda kanisa mwenye familia anavyoonyesha mda kiasi gani anahitaji kutunza/kuweka pembeni kwa ajili ya kuangalia mahitaji ya familia yake?

**II. Muonekano wa Pili—Anjurea na Robert**

Anjurea alikuwa akifurahia kuhusu baba mchanga ambaye mme wake, Robert, alikuwa ndiyo amemuongoza kwa Bwana. Alikuwa na furaha sana kwa ajili ya Robert kwa sababu alikuwa akitumiwa sana na Bwana. Katika miezi sita iliyopita kanisa mpya lilikuwa limekua kutoka familia ya wenzi mpaka familia 15. walikuwa wametiwa moyo katika huduma hii lakini Anjurea alikuwa bado na usumbufu unaojirudia na fikira. Alikuwa amemwambia Robert juu ya hitaji lake la kuzungumza lakini ilionekana kana kwamba alikuwa na kazi nyingi sana mara zote na huduma yake kiasi kwamba hawakupata mda wa kuzungumza. Alirudi nyumbani kila jioni akiwa amechelewa sana na kuchoka sana. Alisema kuwa wangeongea wakati ambao atakuwa na usikivu, lakini tena alikuwa akiamka na kutoka nje ya nyumba asubuhi sana kwenda kwenye mikutano fulani au kuzungumza na mkata shauri mpya au kufundisha darasa katika moja ya mkutano wa vikundi kiini kwenye ujirani wao. Tofauti ya usumbufu wa awali, alikuwa anaanza kujisikia wivu. Huduma hii ya upandaji kanisa ilikuwa inageuka kumeza upendo wote wa Robert ambao ulikuwa ukichukua nafasi yake katika maisha yake. Alikuwa akijisikia vitu ambavyo hakutaka kujisikia. Alitaka kuwa msaada kwa Robert na huduma yake. Huko kulikuwa kujitoa kwake kwa Bwana na kwa mme wake. Lakini alijisikia kuachwa sana. Huu ulikuwa mji ambao haukuwa na kanisa kabla yao kuja na mpaka hivi karibuni kulikuwa hakuna waumini. Sasa kulikuwa na badhi ya wanawake waliokata shauri waliokuwa wakifuashwa lakini kamwe wasingeweza kuelewa maisha yake kama mke wa mchungaji. Alitaka kujisikia kana kwamba ni sehemu ya mchango kwa huduma ya Robert, lakini mpaka kufikia hatua hii hakuwa amehusishwa na hakuwa ameombwa kuhusika. Atafanya nini kumfanya Robert kupunguza vya kutosha kuzungumzia mizigo hii moyoni mwake?

MASWALI YA KUFIKIRIA

1. Kutoka katika ukweli wa hadithi inaonekana kwamba Robert alikuwa akiwasiliana na Anjurea juu ya mahitaji yake kama mke na mama?
2. Unafikiri Robert alikuwa akimuhusisha Anjurea katika huduma yake ya upandaji kanisa? Kulikuwa na ushirikiano na umoja katika maisha yao?
3. Katika njia zipi Robert anashindwa kama mme?
4. Ni ushauri gani wa vitendo unaoweza kushauri ambao unaweza kumsaidia Robert kuwa mzuri katika kuwasiliana na mke wake?
5. Nini unachoweza kusema kuhusiana na “uiwiano” katika ndoa hii?
6. Jinsi gani Robert anaacha nje Waefeso 5:25-26?
7. Jinsi gani Robert anaweza kumhusisha Anjurea kiufanisi katika huduma yake?